**12 MEI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 12 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa 19 Kikao cha 22 leo tarehe 12 Mei, 2025.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja

na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 274

**Kuwakwamua Kimaisha Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanajikwamua kimaisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Patrobas Katambi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha watu wenye ulemavu kujikwamua kimaisha, Serikali imeendelea kuandaa na kutekeleza mikakati, mipango, programu na miradi mbalimbali kwa kuzingatia sera na sheria zinazohusu masuala ya watu wenye ulemavu kama ifuatavyo:-

(i) Programu ya Ukuzaji Ujuzi iliyoanza kutekelezwa mwaka 2016;

(ii) Mikopo ya 10% isiyokuwa na riba inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo watu wenye ulemavu wametengewa asilimia mbili.

(iii) Utekelezaji wa takwa la Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura 183 la kutenga asilimia ya ajira kwa waajiri wenye watumishi kuanzia 20 na kuendelea kwa ajili ya waombaji wenye ulemavu.

(iv) Utekelezaji wa takwa la Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 la kutenga 30% ya zabuni za umma kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

(v) Utekelezaji wa Mkakati wa Teknolojia Saidizi wa Mwaka 2024 - 2027;

(vi) Utekelezaji na Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu Wenye Ulemavu *(Albinism)* wa Mwaka 2024 – 2029; na

(vii) Utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali na ile ya kibajeti kama vile Mwongozo wa Teknolojia Saidizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu hayo mazuri ambayo amenipa, moja ya sababu ya baadhi ya watu wenye ulemavu kutokuwa na uchumi imara ni upatikanaji wa elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunajua hali zao zilivyo na wanapata adha sana kwenye ada wakiwa vyuoni, shuleni na halikadhalika wakiwa kwenye elimu ya juu; kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa ruzuku. Swali la

kwanza; je, kwa nini Serikali isiwapatie ruzuku hawa watu wenye ulemavu wakiwa masomoni ili waweze kupata elimu vizuri na baadaye wajikwamue kimaisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kumekuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano kwa kutumia lugha za alama kwa hawa watu wenye ulemavu wakienda kupata mahitaji katika jamii, kwamba wengi wanashindwa kuwaelewa hawa watu wenye ulemavu na baadaye hatimaye wanaweza kuajiri watu ili waweze kuwasaidia; ambapo inakuwa ni adha kubwa kwao. Je, Serikali haioni haja Wizara yao pamoja na Wizara ya Elimu wakashirikiana pamoja ili waweze kufundisha lugha ya alama kwa walimu wote na wanafunzi wote ili waweze kupata hiyo elimu ya lugha ya alama ili wale watu wenye ulemavu wanapochanganyika na jamii waweze kupata mambo ambayo yatakayowasaidia kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimia Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tendega, kama alivyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa Tendega kwamba, watu wenye ulemavu, ambao mimi ni wajomba zangu, wanapata changamoto kubwa sana hasa kwenye masuala ya elimu. Hata hivyo, zingatio hilo lilionwa na Mheshimiwa Rais alipokutana nao Chamwino – Dodoma, mwezi Machi, 2022 na walieleza moja ya changamoto ilikuwa ni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais yalitolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Mojawapo ilikuwa ni kuhakikisha miundombinu rafiki inakuwepo kwenye maeneo yote ya utoaji elimu ikiwemo shule, utoaji wa vifaa saidizi na vifaa mwendo. Vilevile, Mheshimiwa Rais aliongeza bajeti ya kusaidia watu wenye ulemavu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika hatua nyingine tuliamua kuunda Mfuko

Maalum wa Watu Wenye Ulemavu na kufungua akaunti maalum kupitia *BOT* ambayo tayari kwa mwaka huu fedha imeshawekwa shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuwasaidia kwenye mambo ya elimu na uwezeshaji kwa ujumla, ikiwa ni sambamba na na kuwatengenezea mazingira mengine ya uwezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Mfuko wa *TASAF* unazingatia watu wenye ulemavu, Mfuko wa 10% zile zinazotoewa na halmashauri unazingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. Vilevile, kipengele cha ajira kuna mwongozo wa asilimia tatu ya ajira zote zinazotolewa nchini. Pia, hata wanapokwenda kwenye ushindani wa kielimu au wa ajira kuna upendeleo maalum ambao unatolewa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, ikiwa ni sambamba na kufungua shule zilizokuwa zimefungwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimia Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kutengeneza shule ambazo zitasaidia. Ukiacha elimu ya juu pia zipo za elimu ya kati, ufundi na za marekebisho. Pale Sabasaba – Singida tayari imekwishakufunguliwa; Lwanzali – Tabora (Mtapika) linaendelea kujengwa; Milongo – Mwanza na Yombo – Dar es Salaam. Zote hizi ni za elimu jumuishi kwa ajili ya kuweza kuwasaidia watu wenye ulemavu ili kujipatia elimu na kuweza kusaidiwa. Thamani yake ni zaidi ya shilingi bilioni tatu ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa. Pia bilioni 3.6 nyingine Mheshimiwa Rais ameitoa kwa ajili ya kufungua shule na vyuo vingine kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili la swali la Mheshimiwa Mbunge Mama Tendega ni kuhusu lugha za alama. Kupitia Bunge lako Tukufu na niwambie Watanzania, Mheshimiwa Mbunge ambaye ameuliza swali na wajomba zangu; habari njema ni kwamba, tayari tumekwishaanza kufanya mabadiliko ya mitaala, ukiacha hata mtaala rasmi kupitia Wizara ya Elimu. Tunataka sasa lugha ya alama iwe ya watu wote kwa sababu wanahitaji msaada na wanajumuika na jamii kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumeanza kwenye televisheni yetu ya Taifa unaona kuna mtu anatafsiri habari kwa

lugha ya alama kwenye Bunge lako Tukufu na kwenye shughuli za kitaifa ambazo zimekuwa zikifanyika tumeweka zingatio hilo. Kwa hiyo, nikijbu swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tuko tayari kuweza kuhakikisha mazingatio haya yanakuwepo na wajomba zangu hawa watu wenye ulemavu tunazingatia haki zao kwa sababu hujafa hujaumbika na sisi wote ni waja wa Mwenyezi Mungu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Fatma Taufiq.

Na. 275

**Vitendo vya Ukatili kwa Wafanyakazi wa Majumbani**

**MHE. FATMA HASSAN TAUFIQ K.n.y. MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa Wafanyakazi wa Majumbani unaozidi kukithiri kwenye Jamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, lililoulizwa na Mheshimiwa Taufiq. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kulinda haki za wafanyakazi wote nchini wakiwemo wafanyakazi wa nyumbani. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuridhia Mkataba wa *ILO (International Labor Organization),* Na. 189 kuhusu Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani. Baada ya hatua hiyo kukamilika Serikali kwa kushirikiana na wadau

itaandaa kanuni mahususi kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura 366 ambayo imeweka katazo kuhusu unyanyasaji wa aina zote katika maeneo yote ya kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Taufiq.

**MHE. FATMA H. TAUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na kuwa Serikali imesema italeta mkataba huo, imekuwa ni muda mrefu sana. Je, Serikali inaji-*commit* vipi kuleta mkataba huu *C189* ili kuweza kuwalinda wafanyakazi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; baadhi ya wafanyakazi wa ndani ni watoto ambao wako chini ya miaka 18. Hawa wako katika hatari kubwa sana ya kufanyiwa ukatili. Je, Serikali haioni kwamba imefikiwa wakati sasa wa kupata data kamili ili kuweza kuwanusuru watoto hawa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu hapa kama Mheshimiwa Taufiq alivyouliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Maryam. Ni kweli kama Serikali tunatambua kwamba kuna manyanyaso makubwa sana wafanyakazi wa ndani wanayapata na hasa ni kwa sababu makubaliano ya kikazi yanakuwa hayajajengewa msingi wa kisheria. Hata wakati mwingine imesababisha kufanya kazi kwa wafanyakazi ambao wako chini ya umri unaotakiwa kwa mujibu wa sheria hata ile Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo pia, wapo wapo wafanyakazi ambao wamekuwa wakinyanyaswa, wakipewa ujauzito na wakati mwingine wakinyimwa chakula na kunyanyaswa kwa sababu hii ni kazi pekee ambayo unakula kazini na unalala kazini; lakini pia ni kazi ambayo ni kubwa sana kwa sababu malezi yote ya watoto kwa Taifa kwa sehemu kubwa yamekuwa yakichangiwa na wafanyakazi wa ndani. Siku hizi

familia watu wamekuwa *busy*, wazazi wanawaachia majukumu wafanyakazi wa ndani wa kike au wa kiume na matokeo yake hata ule mmomonyoko wa maadili unaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, kwamba kumekuwa na hizi changamoto, tumeamua na tumedhamiria kuhakikisha kuwa mkataba huo Serikali inausaini; na tumekwishafika kwenye hatua kubwa. Hatua ya kwanza ya ngazi ya Wizara, hatua ya pili kupitia kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri kupitia *committee* ya watendaji (wataalam) na tunasubiri hatua nyingine ambazo ni za kumalizia. Kwa sababu tunatambua kwamba kwenye eneo hili wapo wafanyakazi ambao si tu wa kike peke yake, hata wa kiume wamekuwa wakinyanyasika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia hata kabla hatujasaini sheria hii kuomba sisi wazazi wa kike na wa kiume kutokukaimisha majukumu yote pia hata kwa wafanyakazi hawa wa ndani. Kwa sababu kuna wakati wanakaimisha majukumu ya kufua nguo za baba, kufanya kila kitu na chakula. Matokeo yake hatimaye kuna kazi ambazo hazikaimishwi watoto hawa wamekuwa wakijikaimisha au wazazi kulazimisha na inaleta migogoro ya kindoa wakati mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia haya tunataka tuone kwamba, hata mafunzo ya wafanyakazi wa ndani yazingatiwe. Tuwe na mafunzo maalum na wakiajiriwa tujue umri, anakotoka na stahiki zake nyingine za afya na usalama mahali pa kazi, muda wa kazi; kwa sababu wengine wanafanya kazi muda wote, hata usiku wa manane anaamshwa afanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuliangalia hili kwa uchungu mkubwa alionao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekwishakutoa maagizo mahususi; na maelekeo ya utekelezaji Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishatupatia na hivi karibuni mkataba huu tutamalizana nao. Mheshimiwa Waziri wangu Ridhiwani Kikwete anafahamu kwamba mkataba huu umeshafikia hatua nzuri na yeye ananiona anatikisa kichwa hapo.

Kwa hiyo, jambo hili tumelipokea kama Serikali na tutalifanyia kazi haraka sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa. Ninaona Mheshimiwa Waziri anataka kusimama, Mheshimiwa Ridhiwani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ninataka niyaunge mkono na ni maelezo ya kweli, ninataka kuongeza katika lile eneo la ahadi ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ametuelekeza sisi kama Wizara na katika utaratibu ambao unaweza kuwa ni mpya kabisa katika maelekezo ya Mheshimiwa Rais, ameelekeza Wizara na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ikutane pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza leo hii kazi hiyo ya kukutana kwa Wizara na *Cabinet* ya *Secretariat* inakamilika leo. Kwa hiyo, ninataka nilihakikishie Bunge lako kwamba tuko katika hatua nzuri; na sasa hivi ni kupeleka kwenye *Cabinet* ili baada ya hapo tuweze kuleta mbele ya Bunge lako kwa ajili ya kupitia mkataba huo. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Patrobas Katambi, kwa majibu hayo ambayo ninamini yataleta faraja kwa wazazi nchini na ninawashukuru sana pia kwa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge, ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, badala ya kuanza na Ofisi ya Rais tunaanza na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Na. 286

**Huduma za Utengamao kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS** aliuliza:-

Je, kwa kiasi gani huduma za utengamao zinazotolewa na Wizara ya Afya zinasaidia watu wenye ulemavu kumudu maisha na kuleta maendeleo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tiba za utengamao *(rehabilitation)* ni muhimu kwa watu wenye ulemavu, kwani zinawasaidia kurejesha au kuboresha uwezo wao wa kujitegemea, kuishi kwa furaha na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Maswali ya nyongeza ni mawili, tafadhali ninaomba leo Mheshimiwa Waziri ayajibu vizuri. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha huduma hizi zinatolewa katika hospitali za mikoa na kuhakikisha wataalam wanaongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya huduma hizi unazozisema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya mama yangu Dkt. Thea na nimhakikishie kwamba nitayajibu vizuri kabisa kama ambavyo tumekuwa

tukiyajibu hata yaliyopita. Kwanza, nimwambie kwamba tunachokufanya ili kuhakikisha kwamba huduma hizi zinakwenda kwenye hospitali za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie, kwamba kwenye hospitali za mikoa kuna huduma hizi; kwa kweli kama anavyosema, kwamba inahitaji kuboreshwa na kufanywa ya kisasa zaidi, ambapo sasa hivi ndiyo tumeelekeza fedha ili kuhakikisha kunakuwepo na kitengo maalum na idara maalum ambayo inahudumia masuala kama hayo. Kwa hiyo, hilo tunalizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu suala la hospitali zetu za mikoa, pia kwenye hospitali za wilaya. *Issue* hapa, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameshatoa fedha kwa ajili ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* hapa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa fedha kwa ajili ya eneo hilo ila sasa tunapambana na *issue* ya wataalam kwa sababu uzalishaji wa wataalam ni mdogo. Kwa hiyo, tunakosa wataalam wa kuweza kwenda kila wilaya, lakini kwa kweli ni eneo la kipaumbele na ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, nimwombe dada yangu kama anaweza akarudia swali lake la pili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, jaribu kulifupisha swali la pili ili alielewe vizuri.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya huduma hizo za utengemao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unajua kiasi; kama hujui unaweza kumwandikia kwa maandishi baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba,

kwa kweli fedha zimetengwa, lakini siwezi kumwambia *specifically* ni kiasi gani lakini ipo kwenye mpango. Kama alisikia bajeti ya mwaka jana hii bajeti tunayoitekeleza sasa katika vipaumbele 10 ambavyo vilitajwa na Wizara ya Afya, ninafikiri kipaumbele cha sita au cha saba ni suala la utengamao ni eneo ambalo limezingatiwa, likiwekwa pamoja na afya ya akili ambayo inaenda kwa pamoja.  Kwa hiyo, imewekwa kama kipaumbele lakini fedha zimetengwa na mkakati na maelekezo mahususi ya Rais kwa ajili ya kuwekea uzito eneo hilo yapo tayari na yanatekelezeka.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Afya, Dkt. Godwin Mollel kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kwa niaba ya Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 276

**Hitaji la Magari ya Wagonjwa Vituo vya Ilamba Ndogo na Mwasengela - Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka magari ya wagonjwa katika Vituo vya Afya Iramba Ndogo na Mwasengela - Meatu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya za dharura na rufaa kwa kununua magari ya wagonjwa na kuyapeleka katika vituo vya huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, halmashauri ya Wilaya ya Meatu imepokea magari matatu ya kubebea wagonjwa na kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Meatu, ambapo magari mawili ya kubebea wagonjwa ya Kituo cha Afya Iramba Ndogo na Kituo cha Afya Mwasengela yameachwa katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu kwa muda na pindi majengo ya kutolea huduma za upasuaji wa dharura yatakapokamilika magari hayo yatapelekwa kwenye vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninapenda kuishukuru Serikali kwa kupeleka magari hayo katika hivyo vituo vya afya vya Wilaya ya Meatu, lakini magari hayo kweli hayajapelekwa. Kama alivyojibu Waziri kwamba mpaka wamalize miundombinu ya upasuaji ndiyo magari hayo yapelekwe. Swali la kwanza; kuna wagonjwa wengine wanaohangaika katika vituo hivyo vya afya na magari ni tatizo sana. Je, ni lini sasa Serikali itasema magari hayo yapelekwe kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; sambamba na hilo kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hasa madaktari katika hivyo Vituo vya Afya Mwasengela na Iramba Ndogo. Hakuna kabisa watumishi wa afya. Ni wawili tu walioko katika hivyo vituo vya afya na vituo hivyo, kwa mfano Iramba Ndogo ina wakazi 72,000 na Mwasengela inahudumia kata sita ambazo zina watu 62,000 na bado madaktari ni tatizo. Je, ni lini Serikali itapeleka hao wauguzi na madaktari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Minza Mjika kwa maswali yake mawili ambayo yanalenga kuhakikisha kwamba huduma za afya zinaimarika na hasa katika mkoa na jimbo analotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba, magari haya matatu ya kubebea wagonjwa tayari yameshafikishwa katika Wilaya ya Meatu na ni suala la muda tu pale vituo hivi vya afya vitakapokuwa vimekamilika na vimeanza kutoa huduma za rufaa, basi magari haya yatapelekwa kwenye vituo hivyo vya afya kwa ajili ya kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na watumishi, katika kazi mojawapo kubwa sana ambayo inafanyika na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha sekta ya afya na hasa afya msingi inaimarika ni pamoja na kuajiri watumishi na kuwapanga katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma ya afya ili huduma bora za afya ziweze kupatikana. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Minza sauti yake Serikali imesikia na katika hizi ajira mpya za watumishi wa kada ya afya ninaomba nimhakikishie kwamba tutaweka kipaumbele katika kupanga watumishi wa kada ya afya katika vituo hivi vya afya vya Iramba Ndogo pamoja na Mwasengela. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini.

Na. 277

**Kumaliza Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Bunda imeanza ujenzi wa hospitali ya halmashauri mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Serikali ilipeleka shilingi milioni 500 ambazo zimetumika kujenga jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* na jengo la maabara. Aidha, jengo la wagonjwa wa nje limekamilika na linatoa huduma na jengo la maabara lipo hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2022 hadi 2024/2025, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 1.45 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi lenye huduma za upasuaji wa dharura, jengo la upasuaji wagonjwa wa kawaida, wodi mbili za upasuaji, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la kufulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhia dawa, jengo la mionzi pamoja na kukamilisha ujenzi wa majengo ya awali katika hospitali ya Mji Bunda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Mwaka wa fedha wa Serikali ulioisha Serikali ilileta shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali hiyo. Baada ya mwaka wa fedha kuisha halmashauri ikawa imetumia zaidi ya shilingi milioni 150 katika hizo shilingi milioni 800. Shilingi milioni 650 ikarudi Serikalini. Je, ni lini sasa Serikali itarudisha hizi fedha shilingi 650 ili ziende kutusaidia kukamilisha hospitali hii ya Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Robert Maboto kwa swali lake lenye lengo la kuhakikisha kwamba sekta ya afya na hasa afya msingi katika Jimbo lake inaimarika. Ninaomba nimhakikishie kwamba kila mwaka wa bajeti Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ikiwemo miundombinu ikiwemo miundombinu ya Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie kiwango hicho cha fedha alichokitaja ni taratibu tu za Kiserikali, lakini ile fedha ilishatengwa na itafika katika hospitali hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaendeleza ujenzi. Kwa hiyo, nitazungumza na Mheshimiwa Mbunge kuona kwamba wamekwama wapi lakini ni taratibu tu za Kiserikali za kuhakikisha kwamba fedha hiyo baada ya kuwa imevuka mwaka kuna utaratibu wa kuiombea na inaweza ikatumwa katika halmashauri kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Mheshimiwa Hassan Kungu atafuatia.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, Kituo cha Afya cha Buswelu kina jengo moja tu la *OPD* na hakijakamilika mpaka leo. Sambamba na hilo, Kituo cha Afya Sangabuye ambacho ni cha mwaka 1974 mpaka leo miundombinu yake haijakamilika. Je, ni lini vituo hivi miundombinu yake itakamilishwa ili watu waweze kupata huduma kwa uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwa swali lake zuri linalolenga kuimarisha sekta ya afya msingi hususan kwenye Jimbo lake. Ninaomba nimtaarifu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne imefanya uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 1.29 katika kuimarisha miundombinu katika sekta hii ya afya msingi. Pia, katika

kipindi cha miaka hiyo minne ujenzi wa vituo vya afya 367 umefanyika ikiwemo pia na ukarabati wa hospitali na vituo ambavyo ni vya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea na jitihada hizo na itafika katika vituo vya afya hivi viwili alivyovitaja, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inavikamilisha na vinaweza kutoa huduma ya afya iliyo bora kwa wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Kungu na Mheshimiwa George Malima niliwaona.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ilitupatia fedha kiasi cha shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Tarafa ya Nampungu na majengo yalikwishakamilika kwa muda mrefu sana na ujenzi ule haujaendelea. Je, ni lini Serikali itatupatia shilingi milioni 250 za awamu ya pili ili kukamilisha Kituo cha Afya kile na kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya afya kwenda Hospitali ya Wilaya ya Tunduru?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kungu kwa swali lake hili linalolenga kuimarisha huduma za afya msingi katika Jimbo lake. Serikali imekuwa ikiimarisha miundombinu katika sekta hii ya afya na imekuwa ikifanya hivyo kwa kutenga fedha kila mwaka wa bajeti kujenga miundombinu kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari katika kituo cha afya alichokitaja shilingi milioni 250 ililetwa kwa ajili ya majengo ya awali. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali inaleta fedha iliyosalia kwa ajili ya kuendelea na awamu nyingine ya kukamilisha majengo yale ili kituo hiki cha afya kiweze kutoa

huduma bora kwa wananchi; na wananchi wasipate adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Iwondo kilichoko Jimbo la Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa George Malima kwa swali hili ambalo linalenga kuhakikisha na kupaza sauti na kuona kwamba huduma za afya msingi zinaimarika katika jimbo lake. Ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana wa kuendelea kuimarisha miundombinu katika sekta hii muhimu kabisa ya afya msingi. Katika jimbo lake fedha italetwa kwa ajili ya kukamilisha kituo hiki cha afya alichokitaja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge. Kwa niaba anauliza nani? Mheshimiwa Mkundi kwa niaba.

Na. 278

**Huduma ya Maji Shule za Sekondari na Msingi Nchini**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafikisha huduma za maji safi na salama katika shule zote za msingi na sekondari nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya Elimu Msingi Mwaka 2024 inaonesha kuwa shule 5,311 za sekondari zina vyanzo vya maji vya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 2,960, shule zenye maji ya visima ni 1,217 na wanaovuna maji ya mvua ni shule 1,134. Aidha, shule 20,509 za msingi zina vyanzo vya maji ya uhakika ambapo shule zenye maji ya bomba ni 10,965, maji ya visima ni shule 4,966 na shule zinazovuna maji ya mvua ni 4,578.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya Serikali ya kufikisha huduma za maji safi na salama katika shule za msingi na sekondari nchini ni pamoja na:-

Kuhakikisha kuwa ujenzi wa shule mpya unajumuisha fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji inayohusisha kuvuna maji ya mvua; kuunganishwa na mifumo ya mamlaka za maji na kuchimba visima; Ujenzi wa miundombinu ya vyoo unajumuisha fedha ya ujenzi wa miundombinu ya maji tiririka; na kutumia sehemu ya fedha ya ruzuku ya uendeshaji wa shule kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha shule zinakuwa na huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na majibu ya Serikali, lakini ninaomba mkakati huo uzingatiwe kwa sababu katika miradi inayoendelea sasa shule nyingi hazijatengewa mifumo hiyo ya kupata maji hasa eneo la Ukerewe. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri ninaamini umelipokea. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba, ahsante sana kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, swali la Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge wa Mpendae litaulizwa na Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 279

**Changamoto Zinazoikabili *NEMC***

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kutatua changamoto za *NEMC* hususan za kibajeti ili iweze kushughulikia athari zitokanazo na uchafuzi wa mazingira nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Ili kukabiliana na changamoto hizi hususani changamoto za kibajeti, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo:-

Kufanya mapitio ya Kanuni za Ada na Tozo za mwaka 2021 na kuongeza vyanzo vipya vya mapato na viwango vya tozo kwa miradi mikubwa ambayo shughuli zake zina athari kubwa kwenye mazingira; Kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa matumizi ya Kanuni mpya ya Ada na Tozo ya Mwaka 2024; Kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato *(online billing system)* ambayo inarahisisha ukusanyaji wa ada kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza; na Kuboresha kanzidata ya miradi yote inayotakiwa kulipa ada na tozo za Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukamilisha mchakato wa kuifanya *NEMC* kuwa Mamlaka ili kuipa nguvu ya

kisheria *(Legal Mandate)* ya kusimamia majukumu yake ipasavyo na hivyo kujiwezesha kimapato; kufanya kaguzi za kimazingira katika miradi mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu na kuhimiza ulipaji wa ada na tozo za mazingira; na kuongeza idadi ya watumishi na kuanzisha Ofisi za Kanda ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwafikia wadau wengi kwa muda mfupi katika maeneo mbalimbali nchini. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili. Swali la kwanza; je, ni lini sasa mchakato wa *NEMC* kuwa *NEMA* utakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa vyeti vya tathmini na ukaguzi kutoka *NEMC? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza mchakato wa kutoa *NEMC* kuipeleka kwenye *NEMA;* hii ni kwa sababu tumeona kweli kuna baadhi ya mapungufu ambayo sisi kama *NEMC* tunatakiwa tuyarekebishe. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba kuna baadhi ya makusanyo na baadhi ya mapato mengine ambayo hayo tunahisi yanawezekana yakawa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchakato wa kuifanya *NEMC* kuwa *NEMA* kwa maana ya kuipa mamlaka na nguvu, huo mchakato umeshaanza na niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwamba mchakato huu unaendelea kwa sababu unapita kwenye hatua mbalimbali uakapokuwa tayari tutauleta hapa kwa ajili ya kuujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mipango mbalimbali ambayo tumeipanga. Ni kweli zinatokea changamoto ndogondogo za upatikanaji wa vyeti, lakini nikwambie katika hili Mheshimiwa, Mameneja wetu wa Kanda, *NEMC* na Mkurugenzi wote wanafanya kazi kubwa na nzuri katika hili jambo kubwa la upatikanaji wa hizi *certificate* za tathmini na za ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka nichukue fursa hii niwapongeze sana wafanyakazi wote wa *NEMC:* Mkurugenzi na Mameneja wa Kanda kwa kazi kubwa wa wanayoifanya ya kuharakisha upatikanaji wa *certificate* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinajitokeza, kwanza ni changamoto ya mifumo. Inafika wakati mifumo inakuwa inasumbua kwa hiyo kidogo inavuta muda. Changamoto nyingine ni kutokuwa na vigezo kwa baadhi ya miradi. Hatuwezi kutoa *certificate* kwa mradi ambao haujakidhi na haujatimiza vigezo. Hii ni kwa sababu ya kulinda mazingira na afya za wananchi, lakini zaidi taarifa za wataalam elekezi zinachelewa kuja kwetu. Tunawasajili wenyewe, lakini wawekezaji wakiwapa kazi ya kuandaa taarifa kuleta kwetu zinakuwa zinachelewa, mwisho wa siku mteja ama mwekezaji anakuwa anachelewesha katika upatikanaji wa *certificate*. Kwa hiyo, niwaombe tu wawekezaji wote wanapokuja kwetu wahakikishe kwamba tayari wameshakamilisha baadhi ya taratibu na vigezo ili tufanye haraka ya hivyo. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ussi Pondeza nilikuona.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, kutokana na uchache wa mameneja wa kanda kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri, sasa Serikali haioni haja kuwapa uwezo Mameneja wa Mikoa ili nao waweze kufanya shughuli ileile ambayo inafanywa na Mameneja wa Kanda ili kufanya zoezi lipate unafuu na liwe la haraka zaidi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza. Nitumie fursa hii kwanza, nimpongeze sana kwa kazi kubwa anayoifanya hasa katika suala la hili la mazingira, amekuwa akishiriki kwenye *program* mbalimbali za uhifadhi hasa kule Zanzibar na maeneo mengine ya mikoa ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapo katikati tulikuwa tuna changamoto ya uhaba wa Meneja wa kanda wa *NEMC,* lakini hapa karibuni tulifanya mabadiliko kidogo. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa tulikuwa tuna mtu mmoja, Mheshimiwa Kayombo ndiyo meneja alikuwa kule. Tumeanza kugawa baadhi ya mikoa kwa maana kwamba, Mkoa kama wa Mara na mikoa mingine ya Katavi, tumeipunguza tumewapatia baadhi ya Meneja wengine wapya kwa ajili ya kusukuma hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii niwapongeze sana Mameneja kwa kazi kubwa wanayoifanya ingawaje na uchache ambao wako nao. Tunao maafisa wetu viungo ukiacha Meneje wa Kanda ambao na wao wanaongeza kasi ya suala zima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira hasa kwenye miradi mikubwa ikiwemo viwanda, migodi, majengo makubwa na miradi mingine ya uhifadhi wa vyanzo vya maji. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Kavejuru Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nipongeze Serikali kwa michakato inayoendelea ya kuibadili *NEMC* kuwa mamlaka. Je, ni lini Muswada wa Sheria wa kubadili Baraza la Mazingira kuwa mamlaka utauleta humu Bungeni?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba,

mchakato wowote wa mabadiliko ya sheria unapita hatua kwa hatua. Na tunafahamu mchakato huwa unakuja kwa sababu moja ni hiyo mahitaji kwamba, tunataka sasa tutoke katika hali hii tuende katika hali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Ofisi ya Makamu wa Rais, hatua ya kwanza tayari tumeianza. Sasa tunasubiri hatua nyingine kutoka kwa mamlaka zenye uwezo zaidi pale zitakapofika. Wakati huo tumeshakuwa tayari kwamba sheria itakuja hapa na itajadiliwa. Wananchi wataona kazi kubwa inayofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Taasisi ya Baraza la *NEMC,* na itakwenda kuwa mamlaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere nilikuona.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kutokana na tishio la *climate change* nchi nyingi duniani kwa mfano Brazil, Marekani na maeneo mengine wana Wizara ya Mazingira maalum. Suala hili limekuwa zito sana kwenye nchi yetu. Ni lini Wizara ya Mazingira itaanzishwa ili wataalam walioko kwenye maeneo mbalimbali wapewe nafasi ya kutumikia Wizara hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la uanzishwaji wa Wizara ni jambo la kimamlaka zaidi. Kwa hiyo, nimuombe tu awe na subira mamlaka bila shaka itakuwa imemsikia itaona namna ya kufanya kwenye hili. Nakushuru ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Khamis kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Nishati Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe Mbunge wa Kibiti aulize swali lake.

Na. 280

**Tatizo la Kukatika Umeme Jimbo la Kibiti**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua tatizo la kukatika kwa umeme katika Jimbo la Kibiti?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* inatekeleza mikakati mbalimbali ya matengenezo na ukarabati wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme katika Wilaya ya Kibiti ili kuondokana na tatizo la kukatika kwa umeme kunakotokana na uchakavu wa miundombinu hiyo. Mikakati hiyo ni kubadili nyanya za umeme kwa kuweka zenye uwezo mkubwa, kubadili nguzo za umeme na kuweka za zege, kubadili *Pin insulators* na kuweka mpya, na kufunga vidhibiti matatizo (kwenye line zenye urefu wa zaidi ya kilometa 50. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina mambo mawili; kwanza, pongezi kwa Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo Daktari Samia Suluhu Hassan ameweza kuifanya na kutendea haki wananchi wa Jimbo la Kibiti hususan wale wanaoishi katika maeneo ya Delta Kata ya Kiungoroni, Mapaloni, Mbuchi, Msala kule kote kumepelekwa umeme takribani shilingi bilioni 3.8 tunashukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa Serikali ilishatenga eneo pale kwenye Kata ya Ruwaruke Kijiji cha Lungungu kujenga *substation* ili kupunguza tatizo la

kukatikakatika umeme. Sasa ni lini Serikali wataanza kufanya ujenzi huo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze amekuwa akifatilia jambo hili mara kwa mara. Pia tunashukuru kwa pongezi ambazo amezitoa kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lake la kujenga Kituo cha Kupoza Umeme katika eneo la Lungungu ni kweli na sisi tulishafika katika eneo hilo na tulishafanya *design* na michoro ipo tayari. Ni kwamba tu Kituo cha Kupoza Umeme cha Lungungu lazima kilishwe na Kituo cha Kupoza Umeme cha Msifuni. Kwa hiyo, kwa sasa hivi ujenzi wa Kituo cha Umeme pale Msifuni kinaendelea Mkandarasi ni mzuri sana *TIBEA* na tuna uhakika atamaliza kazi kwa wakati. Akishamaliza pale tutajenga laini ya kutoka 400 *kv* mpaka 33 *kv*, msongo wa kilovoti 33 mpaka Lungungu kwa ajili ya kuweza kujenga kituo kidogo cha kupoza pale umeme ili wananchi wa Kibiti na wenyewe waendelee kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira, mikakati imeanza kupitia kituo cha kupoza umeme kikubwa cha Misifuni ambacho kitaenda kulisha Lungungu pale ambapo mradi utakamilika basi tutajenga na hicho Kituo kidogo cha Kupoza Umeme Lungungu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaban Shekilindi nilikuona.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, transfoma iliyopelekwa na Mkandarasi katika Kijiji cha Kigulunde Kata ya Ngwelo iliungua na ninavyosema sasa hivi ni miezi minne hawapati huduma. Je, nini kauli ya Serikali ya kumtaka Mkandarasi yule kupeleka transfoma nyingine ili wananchi wangu waondokane na adha wanayoendelea kuipata sasa? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe pole Mheshimiwa Shekilindi na wananchi wa Kijiji hiki cha Kigulunde kwa changamoto ambayo wameipokea. Ninaomba nikitoka hapa nifuatilie ili tuhakikishe kwamba tatizo hilo linatatuliwa na wananchi wake wa Kijiji cha Kigulunde waendelee kunufaika na upatikanaji wa umeme katika kijiji hicho. Kwa hiyo, nikitoka hapa Mheshimiwa Mbunge nitafuatilia tuweze kutatua changamoto hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo nilikuona.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Songwe kwa ujumla wake, umeme kwa sasa unakatikakatika mara kwa mara na wachimbaji wadogo wa Saza, Makangorosi, Chunya, Mbangala, Patamela wanapata hasara sana kwa ajili ya mota zao zinaharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunashukuru sana Serikali kwa kuleta umeme vijiji vyote vya Wilaya ya Songwe, lakini kwa kweli tatizo kubwa ni kukatikakatika kwa umeme hasa kwenye viwanda vidogo vya makarasha. Nini kauli ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake na kwa kweli amekuwa akifuatilia mara kwa mara kuweza kuona namna ya kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Songwe. Serikali kupitia Wizara ya Nishati tunatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme katika Mikoa ya Songwe hadi kufika katika Mkoa wa Rukwa kwa maana ya kupeleka gridi katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu tunajenga vituo vya kupoza umeme maeneo mbalimbali ikiwemo, katika Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, mradi huu unaendelea na mkandarasi kwa kweli ana-*speed* nzuri sana. Tuombe watuvumilie, tutakapokamilisha kujenga Kituo cha Kupoza Umeme pale Songwe, basi tutakuwa tumeimarisha hali ya

upatikanaji wa umeme pale na wananchi hususan hawa ambao wapo katika machimbo, wachimbaji wadogo wa madini na wenyewe wataweza kunufaika kwa sababu umeme utaendelea kuwa wa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mradi unaendelea na uko hatua nzuri, tuwaombe wananchi wa Songwe kupitia Mheshimiwa Mulugo waendelee kutuvumilia wakati Mkandarasi yuko *site* na atamaliza. Tulikubaliana mpaka Mei, 2026 lakini kwa kasi ya Mkandarasi huyu tuna uhakika ataweza kusogeza muda nyuma kidogo ili wananchi hawa waendelee kunufaika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Kapinga na Naibu Waziri, Wizara ya Nishati kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 281

**Upanuzi wa Mradi wa Maji Makonde**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini ukarabati na upanuzi wa Mradi wa Maji Makonde utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Makonde kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28 kwa gharama ya shilingi bilioni 84.7. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu vitatu vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 26 kwa siku, ujenzi wa matanki manne yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 13 na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 37% ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025 na kunufaisha wananchi waishio kwenye Wilaya za Newala, Tandahimba pamoja na Mji wa Nyanyamba.

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali. Kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha nyingi na kuokoa Mradi wa Makonde ambao kwa miaka mingi ulikuwa haujatekelezwa, kwa hiyo ninaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa Mkandarasi ambaye anaendelea na ujenzi wa mradi anafanya kazi kwa kusuasua kwa changamoto ambazo Serikali inazifahamu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitatua hizi changamoto ili Mkandarasi wetu aendelee na kazi yake? Ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye upande wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, kuna mradi mdogo umesanifiwa kwa ajili ya kutoa maji Kijiji cha Nyundo na kupeleka Kata ya Nima, Hinju na Njengwa. Je, mradi huo mdogo umefikia katika hatua gani ya utekelezaji? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii pia kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Chikota kwa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maji, bajeti ambayo imevunja rekodi kwa kipindi cha kwanza kwa ongezeko la 31%. Hii inaonesha namna gani *commitment* ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi kupata huduma ya maji safi na salama. Waswahili wanasema mwenye haki akitawala nchi hujaa neema na kwa

hakika kwa bajeti hii kwa kweli tunaenda kuona miradi mingi ikitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chikota natambua Mradi huu ambao unaenda Newala- Tandahimba- Nanyamba kwa Mheshimiwa Maimuna, Mheshimiwa Mkuchika, Mheshimiwa Katani pamoja na wewe mwenyewe ni jicho la Serikali kuona wananchi wa maeneo haya Mradi huu wa Makonde unaenda kukamilishwa na waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mdogo ambao umesanifiwa Mheshimiwa Mbunge amesema, tunafahamu dhamira yake na anapenda sana kuona wananchi wake wakinufaika; huu Mradi unaitwa Nyundo – Lipwidi. Kutakuwa na tenki litakalojengwa pale Nyundo, lakini utaweza kuhudumia vijiji takribani 11. Vilevile unaenda kwenye Kata za Njengwa, Mnina pamoja Hinju zile kata zote tatu kwa umoja wake kutakuwa na vijiji 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mradi huu tayari umesanifiwa, bilioni 14 zinakadiriwa kuhitajika na tumeshaanza mchakato wa manunuzi tuko kwenye *prequalification* na baada ya hapo tunaomba kibali Wizara ya Fedha wakishatoa tutatangaza ili kumpata Mkandarasi ili mradi huu uweze kukamilika na bahati nzuri umeingizwa kwenye bajeti ya mwaka huu 2025/2026. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mradi huu utaenda kutekelezwa vizuri na utakamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda nimekuona.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nina swali tu la nyongeza kwamba, wakati tunasubiri mradi huu mkubwa wa Makonde kuendelea kukamilishwa au kuendelea kwenye ujenzi wake. Upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, ile miradi midogo ya visima ambavyo vimechimbwa kule katika kila jimbo vitaanza kutoa huduma na wananchi wakawa wanatumia hayo maji kwa uhakika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la mama yangu Maimuna, Mbunge wa Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana mama yangu kwa kuendelea kuwapigania wananchi na kuhakikisha kwamba, anaiishi kwa vitendo falsafa ya Daktari Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani kwa yeye kuendelea kuwa kisemeo kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba, programu ya visima 900 ni programu ambayo Daktari Samia Suluhu Hassan alilitazama hilo na kuona kwamba kuna miradi mingi mikubwa inayoendelea lakini kuna miradi midogo midogo pia. Tukaona kwamba, miradi hii ya visima ndiyo mkombozi wakati miradi mikubwa ikiwa inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa muktadha huo nikuhakikishie kwamba mradi wa visima 900 tumeshajiwekea *deadline* mpaka tarehe 25 Juni visima vyote viwe vimeshaanza kutoa huduma kwa wananchi wote. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma, nimekuona Mheshimiwa Amar, Mheshimiwa Kilave.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi mkubwa wa maji wa Kiwira ambao unasubiriwa kwa hamu kubwa na wananchi wa Mbeya Jiji na wananchi wengi sana wa Mji wa Mbalizi. Mradi huo unasubiriwa kwa hamu hasa wanawake wa maeneo hayo wanapata shida sana kutafuta maji. Je, huo mradi mpaka sasa hivi umefikiwa asilimia ngapi? Wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanataka kujua. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la dada yangu. Ni ndani ya mwezi mmoja ameliuliza hili swali mara ya pili leo nadhani hii ni dhamira yake ya moja kwa moja. Huu mradi unawasaidia Wanambeya, Mbeya Mjini pamoja na kwenye Jimbo la Mheshimiwa Spika. Tunatambua umuhimu wa namna gani maji ni msingi wa uchumi wa nchi yetu, tunatambua kwamba maji ni uhai na pia tunafahamu kwamba, maji yakishakuwepo basi kuna adha ambazo zitakuwa zimeondoshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mradi unaendelea kutekelezwa. Majibu ya wiki iliyopita hayawezi kuendana na leo kwa sababu tayari mradi unaendelea kwenye *progress* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu kwamba mradi huo unaenda vizuri sana kulingana na makubaliano yaliyopo kwenye mkataba na hata mpaka itakapofikia mwisho wa mkataba mradi huo utakuwa umekamilika na wananchi watapata. Kama akihitaji taarifa za takwimu halisi tukitoka hapa nitaweza kuwasiliana na waliopo *site* ili waweze kutupatia takwimu halisi kwa ajili ya wananchi wake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar nilikuja, Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mjitahidi kuuliza maswali mafupi ya Kibunge.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari kufanya tathmini kwenye Wilaya ya Nyang'hwale ili kuweza kupunguza gharama ya bei ya maji kutoka 2000 na kuwa 1500?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mbunge wa Nyang'hwale. Ni kweli Serikali iko tayari, lakini utayari wa Serikali pia unaendana na aina ya huduma inayotolewa. Kama maji ni maji mserereko gharama haiwezi kufanana tunapotumia nguvu ya *solar* na

vilevile kama maji yanasukumwa kwa pampu ambazo zinatumia umeme wa *TANESCO* gharama yake pia haiwezi kufanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini itakapofanyika tutaweza kuangalia *production cost* na ndio inaenda kutoa majibu kwamba, maji yauzwe kwa kiasi gani. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri huo Serikali tumeupokea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy nilikuona.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanatemeke tunashukuru sana kwa maji ambayo yanaendelea kuwekwa, lakini kuna namna ambayo ya kulipa jinsi ya kuvuta maji kuja kwenye nyumba zetu. Sisi kama Wanatemeke tunatamani kufanya mkataba kati ya wizara na mwananchi mmoja mmoja kwa bei ilivyo kubwa ili tuweze kulipa kidogo kidogo na watukate kwenye bili. Je, wako tayari kufanya mikataba hiyo na sisi Wanatemeke? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge mahiri kabisa wa Temeke, mwanamama ambaye anaendelea kuwapambania wananchi wake wa Temeke na hakika naamini kabisa kwamba, Novemba atarudi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo sisi Serikali daima tumekubali kushirikisha wadau mbalimbali kupokea ushauri na hili nalo ni jambo la msingi sana ambao ni ushauri mzuri ambao tunaupokea, lakini lazima tufanya tathmini tuangalie faida na hasara ya kufanya hivyo na tukiona kwamba, faida ni kubwa kwa maslahi ya wananchi wetu Serikali iko tayari kushirikiana nawe ili kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ambayo inaonekana ni tatizo katika eneo lao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Esther nimewaona.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Lindi zawadi mliyotupa ya kutuchimbia visima vitano, vitano kila jimbo maana yake majimbo yote ya Mkoa wa Lindi visima vimechimbwa isipokuwa Jimbo la Lindi Mjini bado visima vitano havijachimbwa na tulielekeza kupeleka katika maeneo ambayo wana uhitaji mkubwa wa maji. Sasa ningependa kujua ni lini watakuja kukamilisha mchakato wa kuchimba visima vitano katika Jimbo la Lindi Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba nilipokee na tukaone ni nini kimesababisha mpaka sasa Lindi Mjini hawajapata maji, japo hapo awali tulikuwa tumepanga visima hivi vinapelekwa katika Majimbo ya Vijijini ambayo kimkakati ni kuhakikisha kwamba tunaondoa ile *gap* ya upatikanaji wa huduma ya maji kati ya mjini na vijijini kwa sababu tunaamini mjini kuna miradi mikubwa ambayo inaendelea kutekelezwa ambapo hawatohitaji visima. Kwa hiyo, nitaenda kulitazama kwa kina na nitamshirikisha Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuelewa kwamba ni nini kinaendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wanawake wa Mkoa wa Simiyu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa shilingi bilioni 440 kwa ajili ya Mradi wa Ziwa Victoria. Wakati mradi huo ukiendelea sasa, Kata ya Budekwa na Kata ya Busilili Wilaya ya Maswa kuna shida sana ya maji. Je, ni lini Serikali itachimba visima virefu katika kata hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge mahiri wa Mkoa wa Simiyu. Kazi anayoifanya sisi Wanasimiyu tunaifahamu na hakika katika mradi huu ni baadhi ya kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge ameshiriki kuhakikisha kwamba mradi huu unapatikana na unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa takribani shilingi bilioni 440 kwa awamu ya kwanza kutoka Nyashimo – Bariadi – Itilima inapita kuanzia kwa Mheshimiwa Simon Songe inaenda Bariadi, inaenda Itilima kwa Mheshimiwa Njalu Silanga. Awamu ya pili tumeishatangaza *tender* ambapo unaanza kutoka Maswa kwenda upande wa Meatu napo huko kote ni kwa ajili ya neema ambayo Mheshimiwa Rais ameendelea kuiweka kwa Wanasimiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mradi huu utakapopita kwa Sera yetu ya Maji, bomba kubwa likipita kilometa 13 kushoto, kilometa 13 kulia vijiji vyote na maeneo yote yanaweza kupata huduma hiyo ya maji safi na salama. Kwa hiyo nimtoe hofu dada yangu vijiji hivyo na kata hizo iwapo zitakuwa nje ya *range* hiyo ambayo tumeiweka basi Serikali iko tayari kwenda kuchimba visima ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 282

**Kukamilisha Miradi ya Maji Uvinza**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE K.n.y. MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji ya Rukoma na Mwakizega – Uvinza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mwakizega uliopo Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma. Kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 300,000, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 21.5 sanjari na ujenzi wa vituo 46 vya kuchotea maji. Mradi huo umefikia wastani wa 85% na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kunufaisha zaidi ya wananchi 20,348 waishio katika vijiji vya Mwakizega pamoja na Kabeba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani *(UNICEF)* itakarabati miundombinu chakavu ya Mradi wa Maji wa Rukoma pamoja na kuongeza wingi wa maji kwa kufanya upanuzi wa kutoa maji Kijiji cha Lagosa kwenda Rukoma kupitia Skimu ya Maji ya Buhingu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Jimbo la Kigoma Kusini kwa eneo kubwa limepakana na Ziwa Tanganyika, lakini pia na Mto Malagarasi. Vipo vijiji ambavyo vimepakana kabisa na Ziwa Tanganyika, wananchi wanakwenda kuchota maji kwa kutumia ndoo kwenye Ziwa Tanganyika, lakini havina maji. Ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha vijiji hivyo vinavyopakana na Ziwa Tanganyika vinapatiwa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; katika Halmashauri ya *Kasulu DC* Kata ya Muzye lilijengwa tenki linalohifadhi maji kiasi cha lita 250 lakini mpaka sasa hakuna mabomba yanayopelekwa pale kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji. Je, ni lini Serikali itapeleka Mkandarasi ipeleke na mabomba

ili kumaliza tatizo kusudi wananchi waondokane na tatizo la maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Wanakigoma. Mheshimiwa Rais katika bajeti ya 2024/2025 ambayo inahitimishwa mwezi ujao, takribani shilingi bilioni 13.9 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma na zaidi ya miradi 37 imetekelezwa katika Mkoa wa Kigoma kwa kipindi cha 2024/2025. Hii ni dalili tosha kabisa kwamba Mheshimiwa Rais yupo *committed* sana kuhakikisha kwamba Wanakigoma wanapata suluhisho la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Ziwa Tanganyika, chanzo cha uhakika cha maji katika Mkoa wa Kigoma, Rukwa pamoja na Katavi ni Ziwa Tanganyika. Pia, hata uchakataji wa maji mpaka yamfikie mtumiaji ambao ni wenye gharama nafuu zaidi ni Ziwa Tanganyika na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameshairidhia na akatoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza kufanya *study,* wataalam wetu wanapita huko kuanzia Katavi, Rukwa pamoja na Kigoma ili tuone namna gani tutajenga mradi mkubwa wa kimkakati wa kuhakikisha kwamba wananchi wanaoishi katika maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Tanganyika waanze kuwa wanufaika wa kwanza wa kupata huduma ya maji safi na salama kabla hatujayapeleka maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu, Serikali ipo kazini inafanya kazi nzuri kabisa na kwa bajeti hii ya shilingi trilioni 1.016 mliyoipitisha siku ya Ijumaa hakuna ambalo litashindikana. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, vijiji hivi vitakuwa sehemu ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo la pili, tumeshajenga tenki na sasa yamebaki mabomba. Nimhakikishie kwamba hatuwezi kujenga tenki halafu tukaacha kupeleka mabomba kwa sababu maji lazima yapitie kwenye mabomba ili yawafikie watumiaji. Ninalichukua kwa uzito stahiki, nitaenda kulifanyia kazi na nitampa mrejesho wa nini tunaenda kukifanya. Lengo wananchi wetu na wananchi ambao Mbunge anawapambania wapate huduma ya maji safi na salama. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuchimba visima 12 katika Jimbo la Mbulu Mjini na hadi sasa visima sita bado havijakamilika na hata tukitangaza mara kadhaa Wakandarasi huwa hawaombi. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha walau wakandarasi wanalipwa ili waweze kuomba kazi pale inapotangazwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa changamoto hizi tunakutana nazo na kuna maeneo ambayo mfano hata Singida tumekutana na wakandarasi akapatikana wa kwanza akafanya akashindwa, akaja wa pili akashindwa. Ni uwezo tofauti wa kifedha wa kuhimili kuwa na vifaa na mashine za nguvu ambazo zinaweza kuhimili maeneo mbalimbali. Kwa hiyo tunatambua kabisa kwamba maeneo hayo mara nyingine tunachimba hata maji hatupati lakini kuna maeneo ambayo unapata, lakini inahitaji vifaa ambavyo vina gharama kubwa zaidi, lakini unaenda kutekeleza mradi wenye gharama ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hapa ndiyo kumekuwa na changamoto kubwa. Sasa Serikali ndiyo maana ikaona kwamba tutanunua mitambo yetu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

atanunua mitambo 25 ya kuchimbia visima hivyo, lakini bado tunapitia changamoto mbalimbali. Serikali imeshaanza kuangalia kutumia vyanzo vingine ili kusogeza maji katika maeneo ambayo sasa tumeshindwa kuchimba kisima. Lengo kubwa ni kwamba wananchi wanahitaji huduma ya maji safi na salama. Nimtoe hofu maeneo hayo tutayafikishia maji na kwa Serikali hii maji yatafika katika eneo hilo na wananchi wa Mbunge watapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 283

**Ujenzi wa Bandari Kavu Katika Mji wa Tunduma**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali imetoa fedha kiasi gani za ujenzi wa Bandari Kavu katika Mji wa Tunduma ambayo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo. Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi kwa Niaba ya Wizara ya Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari *(TPA)* imeainisha eneo lenye ukubwa wa ekari 1,600 katika Kijiji cha Mpemba Mkoani Songwe litakalotumika kujenga Bandari Kavu ambayo itahudumia maeneo ya mipakani ikiwemo Tunduma. Kwa sasa hatua iliyofikiwa ni taratibu za utwaaji wa ardhi ili kuruhusu mipango ya ujenzi wa bandari hiyo hivyo, gharama halisi zitajulikana baadaye, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaishukuru Serikali kwa kulipa fidia kwa wananchi, lakini ninataka kufahamu, ni lini hasa Serikali imepanga kuanza ujenzi wa hii Bandari Kavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba mbili; sambamba na ujenzi wa Bandari Kavu, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha unaboresha Reli ya *TAZARA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tunakamilisha taratibu zote za kutwaa lile eneo. Taratibu zikishakamilika sasa kujua tarehe ni lini itategemea na mchakato utakavyokuwa umekamilika lakini azma ya Serikali ni kuanza ujenzi haraka kadri Serikali itakavyokuwa imekamilisha utwaaji wa hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunajua kwamba Bandari Kavu hiyo inajengwa kwa sababu ya kuunganisha hiyo Bandari Kavu na Bandari ya Dar es Salaam kupitia Reli ya *TAZARA*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hata katika ziara aliyofanya Mheshimiwa Rais kwenda China, tayari kuna makubaliano maalum ya kuhakikisha kwamba Reli ya *TAZARA* inafanyiwa ukarabati mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika hata katika bajeti itakayokuja ya Uchukuzi, Waheshimiwa Wabunge watapata bahati ya kuisikia, lakini mpango wa Serikali ni kuifanyia ukarabati mkubwa ili irudi kwenye hali yake ya ubora na ndiyo, maana Serikali imeamua kuwekeza vikubwa katika hiyo Bandari Kavu ya Mpemba ambayo iko mpakani kabisa mwa nchi yetu na nchi

ambazo tunafanya nazo biashara ikiwepo ya Malawi, Zambia, *DRC* mpaka Zimbabwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali juu ya Ujenzi wa Bandari Kavu katika Mkoa wa Tabora? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari Kavu ni kusogeza huduma za bandari kwenda sehemu za nchi kavu. Kwa sasa tuna bandari ambayo inafanya kazi eneo la katikati ambalo ni Isaka, lakini kwa upande wa Mkoa wa Tabora tathmini lazima ifanyike. Kwa sababu *MGR* ipo (hiyo Reli ya Kati ya Zamani) lakini pia hii Reli ya *SGR*. Kwa hiyo lazima tathmini ifanyike kuonekana kwamba kuna umuhimu wa kujenga Bandari Kavu katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 284

**Kipaumbele kwa Wanawake Katika Miradi ya Usafirishaji**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, kuna sera za Vipaumbele kwa ajili ya wanawake wajasiriamali katika miradi ya serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Uchukuzi ya Mwaka 2003 imetoa kipaumbele cha kutambua na kutatua changamoto

mbalimbali za wanawake katika kuleta usawa katika jamii. Kwa kupitia Miradi ya Usafirishaji inayotekelezwa na Serikali, wanawake wajasiriamali wamepewa nafasi za kuwezeshwa kufanya biashara katika Vituo vya Reli ya SGR Dar es Salaam – Dodoma. Pia, vituo vya mabasi ya Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Arusha na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wajasiriamali ambao ni madereva wa vyombo vya usafiri wanatoa huduma za usafiri katika vituo hivyo na maeneo ambayo miradi ya Serikali inaendelea kutekelezwa ambapo wamethibitishwa na kusajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni hatua gani mahususi ambazo Serikali imezifanya kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanahusika moja kwa moja katika miradi ya uchukuzi hususan kwenye ununuzi wa magari na zabuni za usafiri wa umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; mikakati gani maalum ambayo Serikali imejiwekea kuhakikisha wanawake wajasiriamali wanaweza kupata fursa za kiuchumi katika miradi ya usafirishaji hasa kwa kuwapa semina? Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi; kwanza Sera ipo ya kuhakikisha kwamba wanawake wanapewa kipaumbele katika shughuli za miradi mbalimbali ya kufanya shughuli zao katika Sekta ya Uchukuzi. Ndiyo maana kama nilivyosema sasa hivi katika miradi ambayo tumeweka ipo

miradi ambayo imetengwa kwamba hii lazima itashughulikiwa na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo miradi iliyotengwa bado pia wanashindanishwa katika miradi yote ya kawaida. Kwa hiyo kwa sababu Sera ipo na miradi hiyo tumeshatenga pia nafasi zao, kwa hiyo, hiyo ndiyo mikakati ya Serikali. Sera ipo, lakini pia Wabunge wakienda sasa hivi kwenye miradi ambayo tunatekeleza na hasa ya *SGR* wapo wanawake wengi ambao wanaendesha shughuli zao kwa sababu ya hiyo Sera, lakini ni pamoja na nafasi ambayo Serikali imetoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi, tunakushukuru sana.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 285

**Kuzungusha Uzio kwenye Hifadhi za Taifa**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka uzio katika Hifadhi za Taifa ili kunusuru maisha ya wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi imejenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 33 kwa gharama ya dola za Kimarekani 330,000 katika mpaka wa Pori la Akiba la Ikorongo na Vijiji sita vinavyopakana na Pori hilo ambavyo ni Mbilikili, Bonchugu, Rwamchanga, Kazi, Miseke na *Park Nyigoti* katika Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile uzio wenye urefu wa kilometa 12 wenye thamani ya dola za Kimarekani 88,971.24 katika ushoroba wa Mwinihana – Magombera iliyopo Udzungwa na uzio wenye urefu wa kilometa 16 wenye thamani ya dola za Marekani 371,696 kwenye mipaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Vijiji vya Mang'ola juu, Oldeani, Mtaa wa Kambi ya Nyoka na Mtaa wa Tloma Wilayani Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, licha ya kujitokeza kwa uhitaji wa uwepo wa uzio katika maeneo yote ya Hifadhi nchini, tafiti za kisayansi zinaelekeza kutofanya hivyo kwa kuwa kutasababisha kuvurugika kwa mwingiliano uliopo wa wanyamapori kwenye mifumo yao ya kiikolojia hali itakayoathiri mienendo, tabia na athari kwenye mtiririko wa vinasaba vya wanyamapori na hivyo kuathiri uzalianaji na ukuaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Serikali inaendelea kufanya tafiti na tathmini ya kina ili kuona uwezekano wa kuweka uzio kwa baadhi ya maeneo ya hifadhi hapa nchini ambayo yameathiriwa sana na wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo maeneo ya Bagamoyo, Mikumi, Kagera, Mkomazi na eneo la kutokea Pori la Akiba la Ikorongo kuelekea Tabora B na kutokea Pori la Akiba la Grumeti kuelekea Ndabaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali kwa kuwa maeneo yote yaliyotajwa hapo katika majibu ya Serikali hakuna maeneo ambayo yametaja Jimbo la Bunda, ninaomba kuwauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa Vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Mugeta, Kyandege, na Tingirima vimeathirika sana na uharibifu wa wanyamapori na mazao yao yameathirika sana; je, ni lini sasa Serikali itaweza uzio katika vijiji hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa uharibifu umekuwa mkubwa sana na madai ya fidia ya kifuta machozi na kifuta jasho yamekuwa mengi sana katika Vijiji vya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Kyandege, Tingirima na Mugeta; ni lini sasa Serikali italipa kifuta machozi kwa wadai wa maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja yapo katika Mpango wa Serikali wa kuweka uzio katia ukanda huu. Zoezi hilo la kuweka uzio wa umeme lilikuwa limegawanyika katika mafungu matatu. Tumefanya utekelezaji katika fungu la kwanza, tulipokuwa tunataka kufanya uwekaji umeme katika fungu la pili kukatokea baadhi ya malalamiko kwa sababu, uzio ule ulikuwa unapita kwenye maeneo ambayo ni maeneo ya malisho ya wananchi. Kwa hiyo, inaonekana ni busara tusitishe kwanza zoezi hilo iundwe timu ya pamoja ambayo itafanya kazi ya kujenga uelewa wa pamoja vilevile kupitia maeneo haya, ili kuweka makubaliano na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hii inatoa wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya TAMISEMI na Uongozi wa Mkoa na Wilaya katika maeneo haya. Timu hii imeanza kufanya kazi, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Tukikamilisha jambo hili tutaelekea awamu ya pili na ya tatu, ambayo itagusa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ulipaji wa fidia. Tathmini imekwishafanyika kwa baadhi ya maeneo, ambayo taarifa zao zimefika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hili linafanyiwa kazi, tunawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, ili kuona jinsi ambavyo malipo haya yanaweza kufanyika hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Norah Mzeru.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kutokana na tembo hao kuwa tishio kwa wananchi. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha haitetereki kwa namna yoyote juu ya usalama na amani wa nchi yetu tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2025? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo; usalama wa Watanzania ni kipaumbele chetu namba moja. Pamoja na kwamba, tunayo changamoyo hii, lakini Serikali imejizatiti kuhakikisha kwamba, maisha ya Watanzania yanalindwa kwa gharama yoyote ile. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tumejipanga vizuri, tutahakikisha tunalinda maisha ya watu wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita nimekuona, Mheshimiwa Waitara pia.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa miezi minne sasa tembo wameua wananchi zaidi ya wanne Kiteto, hata jana. Sasa ni lini utatuletea kikosi na helkopta kwa haraka sana, ili kuwafukuza wanyamapori warudi kwenye maeneo ya hifadhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Olelekaita, kama ifuatavyo; ni kweli, tumekuwa na changamoto hii kwenye eneo la jimbo lake, amewasiliana na mimi kwa karibu na jana tulikuwa na mawasiliano. Hivi ninavyozungumza kikosi kipo njiani kuelekea kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara. Mheshimiwa Mtaturu nimekuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tunao mgogoro wa kati ya Wananchi wa Tarime Vijijini, Kata za Nyanungu, Goloma na Kwihancha na Hifadhi ya Serengeti. Mgogoro huo bado upo kwenye *process,* haujakamilika utatuzi wake. Mheshimiwa Waziri, kule wananchi wangu wa Nyanungu, Kwihancha na Karakatonga pale, wanapoenda kunywesha ng'ombe kwenye vyanzo mbalimbali vilivyo mpakani, ngo'mbe wanakamatwa, kutaifishwa na kupigwa faini kubwa. Serikali ipo tayari kuruhusu wananchi wangu waendelee kunywesha ng'ombe kwenye vyanzo vya maji vilivyopo sasa mpaka hapo mtakapochimba malambo, ili malambo yale wayatumie badala ya kwenda kugombana na wahifadhi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mwita Waitara, kama ifuatavyo; zuio la kwenda kwenye maeneo haya ni kwa sababu kubwa ya uhifadhi na vilevile usalama wa nchi yetu. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, mara baada ya *session* hii ya asubuhi tukae, ili tuweze kutafuta suluhu ya pamoja ya jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu. Mheshimiwa Maimuna Pathan nimekuona.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali, katika Jimbo la Singida Mashariki tulipata uvamizi wa wanyama tembo, Mheshimiwa Naibu Waziri unajua, Waziri alifika na hatua ilichukuliwa kubwa ya kuleta kikosi. Miezi mitatu imepita sasa wale tembo wamerudi tena upya katika Kijiji cha Mkiwa na kusababisha usumbufu mkubwa. Ni nini hatua ya Serikali katika kupata suluhu ya kudumu ya hawa wanyama tembo wakakae kwenye hifadhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu, kama ifuatavyo; ni kweli zimefanyika jitihada, lakini tembo wamerudi tena. Niwaelekeze wahifadhi wetu wapeleke kikosi kwa haraka, cha ndege nyuki, kwenda kudhibiti hali hiyo na baada ya hapo tuone njia nyingine mbadala ambazo tunaweza kuzitumia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali haioni haja ya kuchukua wazo lile ambalo nimekuwa nikililililia mara nyingi sana kuhusu kuweka uzio wa *solar electric fence*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuweka *solar electric fence,* wapi?

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo ambayo yanazungukwa na Hifadhi za Taifa za Mbunga za Wanyama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna, kama ifuatavyo; kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi, Serikali kwa sasa inafanya jambo hilo la kuweka uzio kwenye baadhi ya hifadhi, lakini utafiti wa kisanyansi umeonesha kwamba, hatuwezi kuweka uzio kwenye hifadhi zetu zote. Tunachofanya sasa ni kufanya utafiti wa kina kwenye maeneo ambayo yamepata athari kubwa ya wanyama hawa, ili tuweze kuona ni jinsi gani tunaweza kuyanusuru maeneo haya kwa kuyawekea uzio wa umeme.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan kitandula, Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 287

**Kukomesha Wizi wa Mitandao Kupitia *Sim Banking***

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakomesha wizi wa mtandao kupitia *Sim Banking* na ni wahalifu wangapi wamekamatwa na hatua gani zimechukuliwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imeendelea kukua kwa kasi hapa nchini na duniani kwa ujumla na kusababisha kuimarika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Miongoni mwa maeneo yaliyofaidika ni pamoja na huduma za fedha. Kwa mujibu wa takwimu za *TCRA* za robo ya tatu ya huu mwaka wa fedha 2024/2025, idadi ya laini za simu imefikia milioni 90.4 na utumiaji wa *internet* umefikia milioni 49.3. Mafanikio haya yamekuja na fursa na changamoto mbalimbali, ikiwemo wizi wa mitandaoni ukihusisha pia, *Sim Banking* ambapo watumiaji wa huduma za mawasiliano wamekuwa wakifanyiwa hadaa na kujikuta wametapeliwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizi Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Mawasiliano Nchini imeendelea kuelimisha umma kuhusiana na masuala mbalimbali ya usalama mtandaoni kwa kupitia kampeni mbalimbali, ikiwemo Kampeni ya SITAPELIKI pamoja na NIRAHISI SANA, ili kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu namna bora na salama ya kutumia mitandao, ikiwemo utunzaji wa nywila, kuwa na nywila imara

katika programu mbalimbali za kifedha na zile za matumizi mengine. Aidha, kwa upande mwingine Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kujiimarisha katika aina hizi mbaya za uhalifu na tayari hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kwa wahalifu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri, ambayo yametoa faida kwa jamii. Nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, mitandao inasaidia kupata mawasiliano ya haraka, lakini utakuta pia, inakera katika taarifa hizo za haraka kwa sababu, unaweza ukaletewa jambo kila ukikaa linarudia hilohilo. Je, kama hilo jambo mie sitaki lirejee tena kwenye simu yangu nifanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti swali la pili. Unasema kwamba, wahalifu wanachukuliwa hatua. Hatua gani kwa sababu, taarifa zake wananchi hawazipati. Uzuri wa taarifa na hatua kwamba, mzitangaze, ili tujue mtu fulani kafanya kitu fulani, kachukuliwa hatua fulani. Je, hizi taarifa tutazipata vipi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipokee pongezi zako Mheshimiwa Fakharia, lakini kwenye suala la *messages* zinajirudia rudia; *messages* zinapojirudiarudia, elimu tunayoendelea kuitoa kwa wananchi ni tunaomba sana, kwa kutumia Bunge lako Tukufu, wananchi wote lazima wawe kwanza na mawasiliano na watu wanaowafahamu na kama unapata *message* ya mtu, ambaye humfahamu ni vyema ukapuuza. Usipende kufanyia kazi *message* ambayo mtu humfahamu. Watu wengi wanaotapeliwa ni wale wanaojihusisha na kusikiliza mtu ambaye hamfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unaambiwa unatakiwa kupata milioni sita, tuma namba hii, jibu swali hili. Usipende fedha za kirahisi kwa sababu, pamoja na changamoto za ugumu wa maisha hakuna fedha ya rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupata vitu vya kirahisi, kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge hapa, wengi tumetapeliwa kwa kudhania kwamba, tuna majiko ya gesi ambayo utapatiwa, kuna watu fulani wanataka wakupatie majiko ya gesi. Sasa wewe kwa nini ujihusishe na mtu ambaye humfahamu! Unamtuamia mtu 400,000 ili usafirishiwe majiko ambayo hayapo kwenye utaratibu rasmi. Kwa hiyo, wito wangu kwa wananchi wote ni kuona kwamba, kila mmoja ahakikishe anawasiliana na mtu anayemfahamu na kama humfahamu ninakushauri upuuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa na sisi, kama Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kupitia Taasisi yetu ya *TCRA*. Kazi kubwa tunayoifanya ni kutambua, kupitia mitambo tuliyonayo. Tukishatambua, tunawakabidhi wenzetu wa Jeshi la Polisi, wao sasa wanafanya taratibu zao za Kisheria, kadiri ambavyo nchi yetu inaendeshwa Kisheria. Wengi wameshafikishwa Mahakamani na wameshafungiwa hizo *line,* nyingi sana zimeshafungiwa, na hawa wanaochipukia, sisi kama Serikali tutaendelea kuwafanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid Ali na Mheshimiwa Esther Matiko, nimewaona.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, malalamiko mengi ya wizi mitandaoni yanaelekezwa kwenye Jeshi la Polisi. Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia *access (database)* ya moja kwa moja, ili tukio lolote la kihalifu linapotokea waweze kuchukua hatua za haraka zaidi? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza, Jeshi la Polisi kupata *access;* ninachoweza kusema ni sisi, kama Serikali, Jeshi la Polisi siyo kwamba, halina *access,* lakini Serikali inafanya kazi kama timu moja. Kwa hiyo, wao wanafanya kwenye sehemu yao na sisi kama *TCRA* kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na yenyewe pia, inafanya sehemu yao**.** Tutaendelea kuboresha Jeshi la Polisi katika kuhakikisha kwamba, mifumo inakuwa mizuri zaidi ya ambavyo ipo sasa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia wizi wa kimtandao umetamalaki, siyo tu kwenye *Sim Banking* na mengine. Kwa mfano, Naibu Waziri amejibu hapa kwamba, ni watu kutokujua; mtu ana-*hack* namba yangu mathalani na imetokea mara nyingi. Mtu ana-*hack* namba yako na anawasiliana na watu mbalimbali akiomba fedha. Namba inajitokeza ni ya Esther Matiko mtu anayeombwa fedha au hitaji fulani anajuaje kwamba, ni mtu tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilitoa hatamu ya usajili wa *line,* lakini tunaona zinasajiliwa mpaka mtaani, watu wanapita wanasajili. Unakuta mimi Esther Matiko nina *line* ya watu tofauti, ninaweza kuwa na *line* ya Bhoke na nani! Mtu au mimi Esther Matiko ninamiliki *line* za watu wengine tofauti. Haya yote yanasababisha kuendelea kuwepo na huu wizi wa kimtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mtu anapigiwa simu na *Vodacom,* mathalan wa kijijini kabisa, anaambiwa fuata maelekezo haya, ili tuweze kukusaidia. Mtu anajitolea, anapigiwa simu anatoa maelezo hayo, kumbe yule ni tapeli. Baada ya hapo anakuwa amesha-*hack* kila kitu anaanza kukuibia fedha zilizokuwa kwenye simu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali ione hiki kitu na watu wanatoa taarifa, lakini stahiki hazichukuliwi. Ione kwamba, hili ni Janga la Kitaifa, muweze kudhibiti. Watanzania wa kawaida

wanatapeliwa fedha nyingi sana, siyo hii waliyosema Wabunge hapa, Watanzania wanatapeliwa milioni. Serikali ichukue hatua stahiki kudhibiti hili. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, huo ni ushauri Mheshimiwa Waziri. Siyo ushauri mbaya, ninafikiri Serikali imesikia.

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Maryprisca Mahundi, kwa kujibu maswali hayo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Dkt. Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, aulize swali lake.

Na. 288

**Kukamilika kwa Ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali – Misenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Katoma – Bukwali yenye urefu wa kilometa 35 utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza maandalizi, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Katoma – Bukwali, yenye urefu wa kilometa 35, kwa kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hiyo ilianza Machi 2024 na inatarajiwa kukamilika Septemba 2025. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha, kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nichukue fursa hii

kuipongeza Serikali ya Dkt. Samia kwa jinsi ambavyo nimekuwa nikipaza sauti juu ya barabara hii na sasa tunaona imefikia hatua kubwa ya kuiweka kwenye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ili tuweze kupata bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Katika majibu ya swali la msingi ni kwamba, barabara hiyo upembuzi utaisha Septemba, 2025. swali la kwanza; je, sasa Serikali haioni haja ya kuweka kwenye bajeti, angalau baada ya Septemba tuweze kupata kiasi cha fedha ianze kujengwa kwa kiwango cha lami tukisubiri mwaka wa fedha mwingine unaofuata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Barabara nyingine ya Omushenyi – Bugandika – Kitobo – Buyango – Ruzinga na yenyewe ni barabara ambayo inahudumiwa na *TANROADS*. Je, ni lini barabara hiyo na yenyewe itawekwa katika utaratibu wa usanifu na upembuzi yakinifu ili na yenyewe ianze kujengwa katika kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa, ambayo anaifanya hadi barabara hii imeingia kwenye utaratibu wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kama tulivyosema kwenye jibu la msingi, usanifu utakamilika mwaka huu 2025, mwezi Septemba na kwa taratibu zetu ni kwamba, bajeti tumeshaipitisha, kwa ajili ya usanifu. Pia, tunaamini kwamba, kwa kuwa, tutakuwa tumekamilisha, basi katika mwaka unaofuata itaingizwa kwenye mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu, tutakuwa tayari tumeshakamilisha usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii Barabara ya pili, ambayo anasema inaanza Omushenye kwenda Ruzinga, ni barabara ambayo pia, tunaihudumia, lakini ni Barabara ya Mkoa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakachokifanya kwa sasa ni kwamba, tutahakikisha inapitika kipindi chote cha mwaka, lakini tayari tukiwa tunafikiria kuiweka kwenye maandalizi ya kuifanyia pia, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa mwaka wa fedha utakaofuata. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Mtwara Vijijini linapakana na Nchi ya Msumbiji na tuna barabara zetu za ulinzi. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha barabara hizi muhimu za ulinzi zinajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna barabara ndefu sana, ambayo inaambaa ambaa na Mto Ruvuma, tayari tumeshaanza, ili ipitike muda wote. Barabara ambayo ipo chini, lakini tumeanza kujenga madaraja makubwa karibu yote kuhakikisha kwamba, inapitika kwa sababu, kipindi cha masika huwa inashindwa kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, na hata katika Sera yetu ya Ujenzi, ni kwamba moja ya kipaumbele ni kujenga hizi barabara za za mipakani, kuziimarisha, ikiwa ni pamoja na kuzijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, wakati tunaimarisha kuijenga na kujenga madaraja, tayari tuna mpango wa kutaka kuanza kuijenga yote kwa kiwango cha lami, lakini kwanza tuhakikishe kwamba inapitika muda wote wa mwaka, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, nimekuona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa ujenzi wa Daraja la Rau ulifungua ile barabara na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo alipokuja Mheshimiwa Rais, je, ni lini sasa ile Barabara ya Rau – Shimbwe, Rau – Kishumundu ambako ndiyo wengi mnaifahamu sana Kishumundu, pia na barabara ile ya *Old Moshi* Magharibi na *Old Moshi* Mashariki zitapata ujenzi wa lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nijibu maswali yake kuhusu barabara hizo mbili. Ni kweli, kwanza ni maombi ya mkoa, lakini pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatafuta fedha kuhakikisha kwamba barabara hiyo tunaijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, nilikuona.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Mtwara Mjini linapakana na eneo moja linaloitwa *Mnazi Bay* kwenye visima vya gesi, je, ni lini Serikali itatuwekea lami kutoka Mtwara Mjini mpaka kwenye visima hivi vya gesi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia vizuri. Mtwara kwenda eneo lipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, naomba urudie kwa umakini.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vya gesi viko eneo la Mnazi Bay, Msimbati. Barabara ambayo inakwenda kwenye visima vya gesi ni mbaya na siyo nzuri. Je, ni lini Serikali itatupelekea barabara ya lami kule kwenye visima vya gesi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa maana ya ubaya na isiyopitika, kwanza ninatoa maelekezo kabisa kwa Meneja wa Mkoa wa Mtwara kuhakikisha kwamba barabara hii ambayo inakwenda kwenye maeneo ya kimkakati inatengenezwa na kupitika kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo kwenye mipango yetu

kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari ilishafanyiwa usanifu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia mwisho kwa siku ya leo. Sasa hivi ni wakati wa matangazo, nitaanza na tangazo la wageni.

Kuna wageni ambao wapo asubuhi hii leo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika; tuna wageni 69 wa Mheshimiwa Spika ambao ni wananchama wa Shirika Lisilo la Kiserikali la *Mama na Mwana Care* kutoka Kijitonyama Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Jiang Alipo. Haya, karibuni sana katika Bunge letu. Hawa wenzetu ni kutoka *Mama na Mwana Care*. *(Makofi)*

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Shirika Lisilo la Kiserikali la *Lions Club International*. Kuna Ndugu Habil Khanbai ambaye ni *District Governor,* karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Manish Dhaji Chavda, *First Vice District Governor*; Ndugu Muslm Bharwani, *Second District Governor*, karibu; Ndugu Bhavika Sajan, *Third Vice District Governor*; Ndugu Abidhussein Nurbhai, mwakilishi wa *Run Society Marathon*; Ndugu Hasnain Hirani; Ndugu Shabbir Khanbhai, na Ndugu Zinat Wal Mohamed, ambao wote ni Makatibu wa CCM Kata ya Kisutu. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine 32 wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Taasisi ya *Charity Event Group* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wageni wetu hao kutoka *Charity Event Group* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 31 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sanyansi na Teknolojia. Tunaye Profesa Carolyne Nombo, Katibu Mkuu; tunaye Profesa Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu; Naibu Katibu Mkuu; Tunaye Dkt.

Wilson Mahera, Naibu Katibu Mkuu Elimu; tunaye Dkt. Lyabwene Mtahabwa, Kamishna wa Elimu; tunaye Balozi Mwanaidi Maajar, Mwenyekiti wa Bodi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Dkt. Leonard Akwilapo, Mwenyekiti wa Tume ya Vyuo vikuu *(TCU)* na Mamlaka ya Elimu Tanzania, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunaye Ndugu Bernadetha Ndunguru, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Profesa Hamisi Dihenga, Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Mheshimiwa Fadhili Maganya, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, karibu sana Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi Tanzania, ambao ni wadau wa elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kuna Ndugu Ali Issa, huyu ni Naibu Katibu Mkuu Jumuiya ya Wazazi Taifa kutoka Zanzibar. Karibu sana Naibu Katibu Mkuu wetu kutoka Ofisi ya Wazazi Zanzibar. Ndugu Anthony Tesha, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rombo, karibu sana Mwenyekiti wetu wa CCM kutoka Rombo; Ndugu Masoud Melimeli, Katibu wa CCM Wilaya ya Rombo, karibu sana Katibu wetu wa CCM kutoka Rombo. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Themistockles, Katibu Mwenezi CCM Wilaya ya Rombo, karibuni sana; tunaye *Sister* Mary Veneranda, Mganga Mkuu *Ngoyoni Hospital*, *Sister Mary* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye *Sister* ambaye ni Dkt. Daria Mushi, Mganga Mkuu *Uhuru Hospital* Rombo, Shehe Mlewa Kimwaga, Shekhe wa Mkoa wa Kilimanjaro; Ndg. Saadi Abdala Saadi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya BAKWATA Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Dkt. Aikande Kwayu, Katibu wa Kamati ya Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu; Profesa Makenya Maboko, Mwenyekiti wa Kamati ya Maboresho ya Mitaala;

Profesa Chambi Machage Mjumbe wa Kamati ya Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, karibu sana. *(Makofi)*

Vilevile tunaye Profesa Joseph Semboja Mwenyekiti wa Kamati ya Mapitio ya Sera; Dkt. Pendo Mkenda mtoto wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana mtoto wetu; Ndugu Vincent Laswai kaka wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana kaka yetu. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sanyansi na Teknolojia, Ndugu Momahed Faki, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mafia, Mkoa wa Pwani, karibu sana Mwenyekiti wetu kutoka Mafia. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa Ujenzi ambao ni familia ya Sheikh Twalib Ahmed Abdallah, ambaye ni Mkurugenzi wa Jumuiya ya Maridhiano ya Amani Kitengo cha Dini kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer* Andrew Mathew Kundo ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ambaye ni mdogo wake kutoka Nyamagana, Mkoa wa Mwanza, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza ambaye ni mtoto wake kutoka Zanzibar, karibu sana mtoto wetu kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula ambaye ni rafiki yake, Balozi wa Utalii kutoka Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni wadogo zake wawili kutoka Mkoa wa Dodoma;

Margreth na Farida; na wameandamana au wameongozwa na Ndugu Evelyne Mwakaje, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ambao pia ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni wapigakura wake kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, ni wadau wa Asasi za Elimu na Hakielimu kwa watu wenye ulemavu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wadau wa *Redcross* kutoka Moshi Mjini, wakiongozwa na Ndugu Doreen Lyatonga Mrema, mke wa Marehemu Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 60 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni wanafunzi 55 na wafanyakazi watano wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Iringa. *(Makofi)*

Wageni wengine tulionao leo ni wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tuna wanafunzi 80 na walimu sita wa Shule ya Sekondari Umonga kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Umonga Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Pia tuna Umoja wa Wenyeviti wa CCM Kata 21 kutoka Wilaya za Dodoma, karibuni sana Umoja huu wa Wenyeviti wa CCM kutoka hapa Wilaya za Dodoma. *(Makofi)*

Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, leo tuna Hoja za Serikali kutoka Wizara ya Elimu, Sanyansi, na Teknolojia. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia ili aweze kuwasilisha Hoja za Serikali kwenye bajeti ya fedha 2025/2026. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla sijasoma muhtasari wa bajeti yangu, hotuba yote iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni, na Michezo iliyochambua na kutoa ushauri wa makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia na Fungu 18 – Tume ya Taifa *UNESCO*. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Fungu 48 na Fungu 18 – Tume ya Taifa *UNESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia na Tume ya Taifa ya *UNESCO* kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, msiba uliotokea tarehe 7 Mei, 2025 Jijini Dar es Salaam. Vilevile, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa msiba huu mzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Ukanda wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, natoa pole kwa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Tabitha Siwale aliyewahi kuwa Waziri wa Elimu katika Taifa letu na ambaye ndiye mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kuteuliwa kuwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutoa pole kwa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, ambaye pamoja na nafasi nyingi ambazo amewahi kuzishika na kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu, aliwahi pia kuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni mwaka 1993 – 1994. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Wabunge wenzangu, viongozi wa Chama na Serikali, wananchi na watumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kujumuika nami katika kipindi kigumu cha kumpoteza mama yangu mpendwa Bi. Sekunda Nemes Massawe (Mama Mkenda), tarehe 30 Januari, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na dhamira yake ya dhati ya kusimamia mageuzi makubwa

katika mfumo wetu wa elimu kama alivyoahidi katika hotuba aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maono na dhamira hiyo imewezesha kuandaa na kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, inayolenga kuongeza ubora wa elimu yetu na kumwezesha Mtanzania kupata ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya rasilimawatu ya nchi na soko la ajira la ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba kutumia fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupendekezwa na Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais kupitia Chama hicho Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongea Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kupitia Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu. Aidha, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kupendekezwa kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi, ushauri wao na miongozo yao ambayo imetusaidia sana katika utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi kwa Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natumia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge hili ambao kwanza ni wewe Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Jimbo la Madaba, na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini wao katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana mimi pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Omari Juma Kipanga kusimamia na kuongoza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo; na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao katika kuisimamia na kuishauri Wizara katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2025/2026. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati yametusaidia sana katika maandalizi ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiahidi Kamati kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano, kupokea maoni na ushauri wao na kufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya sekta yote ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Nombo na watendaji wote wa Wizara kwa utumishi wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Rombo kwa ushirikiano wanaonipa katika jitihada za kuleta maendeleo ya jimbo letu. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiananao katika kuleta maendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu, hasa mke wangu mpendwa Beatrice kwa kunitia moyo na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa uwezo wangu wote niliojaaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 na Fungu 18 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,968,212,534,000 kwa ajili ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa ni ongezeko la shilingi shilingi 619,649,159,000 sawa na ongezeko la 31% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2021/2022 na ambapo shilingi 637,287,706,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 1,328,042,674,000 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia Tume ya Taifa *UNESCO* Fungu 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 2,882,154,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha shilingi 1,319,040,000 za mshahara na shilingi 1,563,114,000 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi 677,299,142,174.83. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2024 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 479,770,873,713.48 sawa na 71% ya makadirio. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla

ya shilingi 637,287,706,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo, matumizi ya mishahara ni shilingi 585,225,031,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025 Wizara imepokea jumla ya shilingi 501,689,846,848.61 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kupitia Fungu 46 sawa na 79% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO*, Fungu 18 Wizara imepokea jumla ya shilingi 2,440,900,854.22 sawa na 85% ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imetekeleza vipaumbele vitano kwa lengo la kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu pamoja na matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo: kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya elimu ufundi stadi, yaani amali za kihandisi na amali zisizo za kihandisi; kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu; kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na kuendeleza utafiti matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 01 Februari, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inayolenga kutoa elimu inayozingatia ujuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira na kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kutekeleza kwa ufanisi, sera na mitaala iliyoboreshwa Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, mikutano na majukwaa mbalimbali. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa walimu ikiwepo utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa walimu

70,657 ikilinganishwa na walimu 1,250 waliyopata mafunzo katika mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imetoa mafunzo kwa wadhibiti ubora wa shule 611 ikilinganisha na wadhibiti ubora wa shule 368 waliyopata mafunzo mwaka 2021/2022. Vilevile, Serikali imetoa mafunzo kwa maafisa elimu kata 403, wakufunzi wa vyuo vya ualimu 70, watumishi wa vyuo vya ualimu 120, wakuu wa vyuo 35, na walimu wakuu 9,020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sera na mitaala inayoboreshwa, Serikali imeanza mapitio ya Sheria ya Elimu Sura ya 353 ili kuendana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023 ambapo maoni ya wadau mbalimbali wa elimu kuhusu sheria husika yameendelea kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhuisha na kuandaa miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini ili kuendana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 kwa kutoa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Amali katika Shule za Sekondari wa mwaka 2025; Mwongozo wa Mafunzo ya Amali kwa Wanafunzi wenyewe Mahitaji Maalumu wa mwaka 2025; Mwongozo wa Matumizi ya *Braille* wa mwaka 2025; na Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijiti katika elimu wa mwaka 2024/2025 hadi 2029/2030 sambamba na miongozo minne kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huo kama ifuatavyo: Mwongozo wa Ujumuishi wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijiti katika Shule na Vyuo vya Ualimu 2025; Mwongozo wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijiti katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 2025; Mwongozo wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijiti katika Vyuo Vikuu 2025; na Mwongozo wa Matumizi ya Akili Unde *(Artificial Intelligence)* katika Elimu 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za elimu ni nyenzo muhimu katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, kufanya tafiti na kutoa maamuzi mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeunganisha mifumo ya takwimu za elimu na kuwa na mfumo mmoja wa sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa mfumo wa takwimu kwa sekta ya elimu utakaowezesha upatikanaji wa takwimu zote za sekta kupitia mfumo huu. Aidha, mfumo huu utakuwa na uwezo wa kupokea takwimu mbalimbali zinazohusiana na elimu kutoka katika mifumo mengine ya Serikali ikiwemo *NIDA, RITA,* Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa mipango madhubuti ni muhimu katika kuendeleza maendeleo ya sekta ya elimu. Kwa msingi huo, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu *(Education Sector Development Plan - ESDP)* wa 2025/2026 hadi 2029/2030 ambao utawezesha utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kisekta ikiwemo utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo. Vilevile, imekamilisha mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi unaotoa mwelekeo wa uhamasishaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya amali katika shule zetu za sekondari ni nyenzo muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa ufundi na ujasiriamali kwa lengo la kumudu maisha yao, kushindana katika soko la ajira na kuchangia maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Serikali imewezesha ujenzi wa shule mpya 103 za sekondari za amali ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kukamilika kwa shule hizo kutawezesha kuongezeka kwa idadi ya shule za amali za sekondari kutoka shule tisa hadi kufikia shule 112 za sekondari za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada za kuongeza shule za sekondari za amali nchini, Serikali imeendelea

kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi hadi kufikia wanafunzi 199,118 kwa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na wanafunzi 161,750,000 waliyodahiliwa katika mwaka wa 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 37,368,000 sawa na 23%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la udahili wa wanafunzi linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya elimu ya ufundi hadi kufikia vyuo 512 kwa mwaka 2024/2025 kutoka vyuo vya ufundi 441 mwaka 2021/2022. Halikadhalika Serikali imedahili wanafunzi 11,232 katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi *(VETA)* katika mwaka wa masomo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya *VETA* imefikia wanafunzi 58,912 ambapo kati yao wanafunzi wa kozi za muda mrefu ni 24,670 na wanafunzi wa kozi za muda mfupi ni 34,242. Ongezeko la wanafunzi linatokana na ongezeko la vyuo vya *VETA* kutoka 810 mwaka 2021/2022 hadi kufikia vyuo 905 mwaka 2024/2025. Vilevile, imedahili wanafunzi 391 katika Chuo cha Ualimu cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro *(MVTTC)* ili kuongeza idadi ya walimu wa elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa kitaifa kwa kuhakikisha kuwa kila wilaya na mkoa unakuwa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi, ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imeendelea na ujenzi wa vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi wa vyuo 63 umefikia wastani wa 45%; Chuo cha Mkoa wa Songwe 40%; na chuo cha Wilaya ya Chamwino kimefikia 88%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha na kuongeza miundombinu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya nyongeza katika vyuo 10 vya mafunzo ya ufundi stadi vya Ndulage Muleba, Ileje Isongele, Newala Kitangali, Ngorongoro Samunge, Goloa Babati, Urambo Chekeleni, Kasulu Nyamidaho, Mabalanga Kilindi, Nkasi Palamawe na Kanadi Itilima, ambapo utekelezaji wa ujenzi umefikia wastani wa 82%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Kigamboni, Kihonda, Nyamidaho, Urambo, Morogoro, Arusha, Karagwe, Busokelo, Makete na Namtumbo, ambapo ujenzi umefikia wastani wa 98.5%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa vitendo ni nyenzo ya kuandaa wahitimu wa vyuo vya elimu ya ufundi katika kupata uzoefu na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Hivyo, Serikali imeendelea kugharamia mafunzo kwa vitendo viwandani kwa wanafunzi 1,724 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambapo ni wanafunzi 551 na Chuo cha Ufundi Arusha 500 na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam wanafunzi 673.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka mifumo madhubuti ya ithibati na udhibiti ubora kwa lengo la kuhakikisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari za amali zinazingatia viwango vya ubora katika uendeshaji na utoaji wa mafunzo kwa kuidhinisha uanzishaji wa idara na programu 48 katika vyuo 18 ili kuendesha programu za tuzo za kitaifa za ufundi *(National Technical Award - NTA)* kwa bodi za masomo zilizosajiliwa. Vilevile, imehakiki mitaala 223 iliyoandaliwa na vyuo vya ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kwa wahitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 813 na muda mrefu kwa watumishi 99 katika ngazi za Shahada ya Uzamili na Shahada ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanaendana na mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ili kuhakikisha kila Mtanzania anapata fursa ya kujiendeleza katika ngazi hizo kwa kusajili, jumla ya shule 589 ambapo shule za awali pekee ni 24 na awali na msingi ni 344.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa mara ya kwanza Serikali ya Awamu ya Sita imetoa ufadhili kwa wanachuo 787 kusoma Stashahada ya Ualimu Elimu Maalum kwa lengo la kuongeza walimu wenye taaluma hiyo na kuboresha utendaji kazi ambapo wanufaika wanasoma katika Chuo cha Ualimu Kabanga, Mpwapwa na Patandi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imesajili wanachuo 15,583 katika vyuo vya ualimu ambapo mwaka wa kwanza wa wanafunzi 3,815, mwaka wa pili 9,977 na mwaka wa tatu 1,801. Aidha, Serikali imeendelea kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 10,010 kwa vyuo vya ualimu pamoja na kugharamia huduma ya chakula kwa wanafunzi 15,570 kwa vyuo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha elimu inatolewa katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya walimu inazingatia taratibu na miongozo iliyotolewa Serikali imeendelea na udhibiti ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza imefanya tathmini ya jumla katika asasi 7,499 kati ya 7,200 zilizolengwa zikiwemo za Serikali 6,434 na zisizo za Serikali 1,065 kwa mchanganuo ufuatao: shule za awali na msingi 6,458, shule za sekondari 1,016, vyuo vya ualimu 21, vituo vya elimu ya nje ya mfumo rasmi viwili na vyuo vya maendeleo ya wananchi viwili. Aidha, asasi hizo zilipewa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, imefanya tathmini ya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika asasi 1,126 zikiwemo shule za awali na msingi 866 na za sekondari 260. Aidha, maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini hiyo yameendelea kufanyiwa kazi kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utoaji wa elimu na imeandaa Mfumo wa Udhibiti Ubora wa Shule *(School Quality Assurance System)* unaopokea taarifa kutoka mifumo mingine, ikiwemo mfumo wa taarifa za shule *(School Information System)* ili kuwezesha uchakataji wa takwimu na kutoa taarifa kwa wadau kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo husika kwa wadhibiti ubora wa shule 102 na maafisa TEHAMA 88 kwa ngazi ya makao makuu ya wizara na halmashauri za wilaya 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kujenga uwezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika matumizi ya TEHAMA, Serikali imeanza majaribio ya utekelezaji wa mradi wa maabara ya TEHAMA inayotembea *(Digi Truck project)* katika mikoa mitano kupitia Kampuni ya *Huawei*. Mikoa iliyoanza majaribio ya utekelezaji wa mradi ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeandaa mpango wa majaribio ya teknolojia za darasa janja *(smart class)*, mfumo wa usimamizi na ujifunzaji na maabara ya mtandao na uigaji, teknolojia ya kufundishia kwa kuigiza uhalisia *(virtual and augmented reality)* na matumizi ya simu janja na vishikwambi kwa lengo la kuzibadilisha teknolojia hizo ili ziendane na mazingira ya Kitanzania na kutumika katika kujifunzia na kufundishia kwa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea kuibua vipaji vya waandishi wa kazi za fasihi ya Kitanzania kwa lengo la kukuza tabia ya kujisomea, kuhifadhi historia, amali na mitazamo bora ya Taifa letu la Tanzania kwa kupitia shindano la tatu la Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu ambapo jumla ya miswada 282 ya riwaya, hadithi za watoto, ushahiri na tamthilia vilipokelewa na kushindanishwa. Aidha, washindi wa kwanza hadi wa tatu walipata fedha taslimu pamoja na vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashindano ya Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yameendelea kuleta tija kwa Taifa kwa kuongeza machapisho ya kazi za Fasihi ya Kitanzania. Serikali imechapa na kusambaza katika shule za sekondari na msingi jumla ya nakala za vitabu 148,000 vilivyotokana na miswada ya washindi wa kwanza wa Shindano ya Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Waandishi Bunifu la tarehe 13 Aprili, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuhakikisha kuwa uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja unafikiwa kwa kuongeza idadi ya vitabu kwa wanafunzi wa elimu ya msingi, awali na sekondari pamoja na Kiongozi cha Mwalimu. Katika kutekeleza dhamira hiyo, Serikali kupitia taasisi ya elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imechapisha na kusambaza nakala 16,795,403 za vitabu vya kiada ngazi ya elimu ya awali na msingi katika mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na nakala za vitabu 12,197,434 vilivyochapishwa na kusambazwa mwaka 2021/2022;

(ii) Imechapisha na kusambaza nakala 9,902,102 za vitabu vya kiada elimu ya sekondari ngazi ya chini na juu katika mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na nakala za vitabu 5,206,800 vilivyochapishwa na kusambazwa mwaka 2021/2022; na

(iii) Imeandaa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa darasa la pili na la nne pamoja na *Braille* na Kiongozi cha Mwalimu darasa la pili na la nne na vitabu vya kiada na Kiongozi cha Mwalimu kidato cha kwanza na cha tano na imeendelea kuhamasisha wadau kuchangia upatikanaji wa vitabu vya kiada kupitia Kampeni ya Kitabu Kimoja Mwanafunzi Mmoja. Kampeni hii inafanyika kupitia njia mbalimbali ikiwemo matembezi ya hisani yaliyofanyika tarehe 7 Machi, 2025 ambapo jumla ya shilingi 1,178,163,533 zilikusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeandaa maudhui ya elimu ya sekondari kwa kuwekwa katika mfumo wa kidijiti ambapo maudhui hayo yanapatikana kwa matumizi ya wanafunzi na walimu kupitia Mfumo wa Mafunzo kwa Walimu na Wanafunzi *(Learning Management System - LMS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania limeendelea kuongeza usajili wa watahiniwa wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na sekondari ambapo katika mwaka 2024 watahiniwa 1,230,774 walisajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, sawa na ongezeko la asilimia nane.

Aidha, watahiniwa 529,329 walisajiliwa kufanya mtihani wa kidato cha nne katika mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia sita ikilinganishwa na mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, ufaulu wa wahitimu wa ngazi ya elimu msingi na sekondari umeendelea kuongezeka kila mwaka, ambapo ufaulu wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi katika mwaka 2024 umeongezeka hadi kufikia 80.87% ikilinganishwa na ufaulu wa 79.62% wa mwaka 2021/2022. Vilevile, ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne umepanda hadi kufikia 92.37% mwaka 2024/2025 ukilinganisha na ufaulu wa 87.3% wa mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kudahili wanafunzi na kutoa fursa za mafunzo kupitia programu mbalimbali za elimu ya watu wazima kwa lengo la kuchochea malengo endelevu ya kijamii na kiuchumi ambapo kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imedahili jumla ya wanafunzi 2,562, na katika programu mbalimbali za masomo ya elimu ya watu wazima;

(ii) Imeendelea kutoa mafunzo ya programu ya elimu ya watu wazima na mafunzo endelevu ya elimu ya watu wazima na maendeleo ya jamii kwa wanafunzi 792;

(iii) Imewezesha wanafunzi 6,998 kuendelea na masomo kwa njia mbadala ambapo kati yao wanaume ni 1,108 na wanawake ni 5,818; na

(iv) Imewezesha wanafunzi 6,000 walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali kuendelea na masomo katika vituo 191 vinavyotoa elimu kwa njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kutoa elimu jumuishi kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata vifaa na mahitaji yanayowezesha kujifunza kwa ufanisi. Katika kufikia lengo hilo Serikali imenunua na kusambaza viti mwendo 120, *computer* 35,

vishikwambi 45 na vinasa sauti vya kidijiti 48 kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 120 katika halmashauri ambazo zilibainika kuwa na wanafunzi wengi wenye ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imenunua na kusambaza *computer* mpakato, viti mwendo na vinasa sauti kwa wanafunzi 691 wanaosoma shule ya nyumbani katika shule 136 za msingi zilizobainika kuwa na upungufu wa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, imeendelea kuongeza fedha kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hadi kufikia shilingi bilioni 787.4 mwaka 2024/2025 kutoka shilingi bilioni 570 zilizotolewa mwaka 2021/2022. Ongezeko hili la bajeti limewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanufaika kutoka wanafunzi 177,925 mwaka 2021/2022 hadi wanafunzi 248,331 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la 39.6%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kutoa mikopo kwa ngazi ya elimu ya stashahada *(Diploma)* kwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 19.95 kwa wanafunzi 7,534 wa fani za sayansi na ufundi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikiwa ni ongezeko la 177.6% ikilinganishwa na wanafunzi 2,714 waliopata mikopo hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wenye thamani ya shilingi bilioni 7.29 kwa wanafunzi 646 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wanaoendelea wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia *SAMIA Scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ufadhili huo, Serikali kwa mara ya kwanza imeanza kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma shahada za juu katika sayansi na teknolojia ya nyuklia nje ya nchi kupitia tunachokiita SAMIA *Extended Scholarship* ambapo wanafunzi watano wamenufaika tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa lengo la kuongeza idadi ya wanufaika wapya na wanaoendelea ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya shilingi 161,287,805,492.00 zimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya taasisi za sayansi na teknolojia kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha na kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika taasisi hizo ikiwemo kukamilisha ujenzi wa jengo la Maabara Mtambuka la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan lenye maabara nane, madarasa nane yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,205 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo hilo lilizinduliwa Agosti 6, 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Kukamilisha ujenzi wa madarasa yenye ghorofa mbili na hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kiume katika Kituo cha Umahiri cha Ngozi cha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - Kampasi ya Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali, pia imeendelea na utekelezaji Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ili kuimarisha utoaji wa elimu ikiwemo ujenzi wa Kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kampasi ya Zanzibar – Buyu utekelezaji umefikia 50%, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Kagera 50%, Chuo Kikuu cha Sokoine Kampasi ya Katavi 15%; Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili Kampasi ya Kigoma 10%; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Kampasi ya Lindi 50%; Chuo Kikuu Ardhi Kampasi ya Mwanza 10%; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Kampasi ya Rukwa 87%; Chuo cha Ushirika Moshi Kampasi ya Shinyanga 46%; Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia Kampasi ya Tabora 10%; na

Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mkinga, Tanga 45%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za elimu ya juu zilizo nje ya nchi kwa lengo la kutoa fursa za masomo kwa Watanzania kupitia *scholarship* zinazotolewa na nchi rafiki kwa kutoa ufadhili kwa wanafunzi 181 kwenda nchi rafiki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urusi 90, Algeria 33, China 120, Hungary 20, Jumuiya ya Madola ya Uingereza watano na Mauritius wawili. Aidha, imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa afua za kuwezesha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika taasisi za elimu ya juu ni hatua muhimu katika kuhakikisha usawa katika utoaji wa elimu. Hii inahusisha kuweka mazingira ya kujifunzia ambayo yanawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kushiriki kikamilifu katika masomo yao na kufikia malengo yao ya kitaaluma. Ili kufanikisha hili, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imesambaza vifaa saidizi ikiwemo kompyuta mpakato 29, vishikwambi 45, vifaa vya usikivu 46, *digital voice recorder* 36, vitimwendo 15 na *binoculars* 10 katika taasisi saba za elimu ya juu. Aidha, imetoa miguu bandia kwa wanafunzi wanne wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na imetoa bajaji mbili, vifaa vya usikivu vitano, *voice recorder* moja, vishikwambi viwili kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; na

(ii) Imetoa mafunzo kuhusu elimu maalum na elimu jumuishi kwa washiriki 1,668 ikiwemo wanafunzi, wahadhiri na viongozi wa vyuo kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Taasisi ya Uhasibu *(TIA)*. Aidha, imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa

hosteli 147 wa vyuo vikuu 19 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuwabaini wanafunzi wenye mahitaji maalum na namna ya kuwapa huduma kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwaendeleza kitaaluma na kitaalamu wahadhiri na watumishi wa taasisi za elimu ya juu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 639 na mafunzo ya ngazi ya stashahada, shahada ya umahiri na shahada ya uzamivu kwa watumishi na wahadhiri 305.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti ili kukuza na kuendeleza maarifa, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kusaidia kutatua changamoto mbalimbali kwa kutoa vibali 489 kwa watafiti wa ndani na nje ya Tanzania wanaofanya tafiti katika nyanja za sayansi ya jamii, sayansi asilia, sayansi ya tiba na afya, kilimo na sayansi ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeanzisha dirisha la utoaji mikopo kwa watafiti na wabunifu kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia *(MTUSATE)* kwa kushirikiana na benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti 784 kupitia taasisi za elimu ya juu katika maeneo ya elimu, afya, mazingira, kilimo, utawala, ardhi, ujenzi, usanifu wa majengo, uchumi endelevu wa viwanda, mabadiliko ya tabia ya nchi na njia ya uvunaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezindua mfuko wa *SAMIA Innovation Fund* wenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 utakaotoa mikopo nafuu kwa wabunifu kwa lengo la kuendeleza na kubiasharisha ubunifu pamoja na kutoa fursa za ajira kwa Watanzania kupitia kazi za ubunifu. Mfuko ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imekamilisha Mkakati wa Kitaifa na Mpango wa Utekelezaji wa Kuhamasisha Ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi *(Diaspora)* 2024/2025 - 2029/2030 katika shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Sambamba na hatua hiyo, Serikali imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Ugharamiaji na Utoaji wa Motisha katika Masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa lengo la kuimarisha uwekezaji na hamasa kwa wadau katika masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa jamii ili kutatua changamoto mbalimbali kupitia taasisi za elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi kwa kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii ikiwemo kutoa mafunzo na ushauri wadau kwa 7,610 kuhusu uongozi, uchumi wa vyama, uandaaji wa mipango mikakati ya vyama, uwekezaji katika vyama na elimu ya fedha kwa vyama na mtu binafsi ili kuimarisha utekelezaji wa kazi za vyama vya ushirika kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, imetoa mafunzo, huduma za ugani na ushauri kwa jamii kwa wadau 1,572,390 ikiwemo wakulima, wafugaji, maafisa ugani, watafiti na wafanyakazi kutoka Serikalini na mashirika binafsi kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia, Serikali imepima uwepo wa mionzi kwenye jumla ya sampuli 26,349 za vyakula na mbolea kati ya sampuli 50,000 zilizolengwa. Kati ya hizo, sampuli 6,861 ziliingia nchini, sampuli 18,892 zilisafirishwa nje ya nchi, sampuli 496 zilikuwa za mbolea na tumbaku na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, matokeo ya upimaji yalionesha kuwa sampuli hizo hazikuwa na madhara yoyote yatokanayo na mionzi. Aidha, imesajili jumla ya vyanzo vipya vya mionzi 66 na hivyo kuwezesha nchi kuwa na jumla ya vyanzo vya mionzi 1,637 vilivyosajiliwa. Vilevile, imetoa vyeti 157 kwa waliokidhi vigezo vya kusimamia utoaji wa mionzi kwa watu (wagonjwa), ufungaji, matengenezo, na uendeshaji wa vifaa vya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18), Serikali kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO,* imeendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya Kimataifa kwa kuratibu uanzishaji wa Kamati ya Kitaifa ya Kumbukumbu za Urithi wa Nyaraka wa Dunia itakayosimamia uingizaji wa kumbukumbu za nyaraka za Tanzania katika mfumo wa kidijiti wa Kumbukumbu za Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tume imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa hifadhi hai pamoja na kuheshimu mipaka kati ya vijiji na hifadhi kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayopakana na Hifadhi Hai za Mazingira ambazo ni Jozan Chwaka Bay na Ziwa Manyara; Imeratibu mafunzo kwa vikosi vya ulinzi vinavyoshiriki operesheni za ulinzi wa amani katika Mataifa mbalimbali kwa lengo la kulinda nyara za kiutamaduni katika kipindi cha majanga ya kivita; na imetoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya majukwaa ya habari katika kufikisha ama kupokea taarifa lengwa kwa waandishi na wadau wa habari 200 katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia kwa Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imepanga kutekeleza vipaumbele vitano kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo na kutoa mafunzo;

(ii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali katika shule za sekondari na vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu;

(iv) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia upatikanaji wa maendeleo endelevu. Katika hili, juhudi zaidi zitatumika kupeleka vijana wa Kitanzania kusomea mambo ya sayansi ya nyuklia, mambo ya kompyuta na akiliunde kwenye vyuo bora vilivyo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wadau wa elimu na umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa kwa kutoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule, walimu wa shule za msingi na sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, maafisa elimu, wakufunzi, na wahadhiri wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na taasisi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itakamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ili iendane na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Aidha, itakamilisha mapitio ya sheria katika Taasisi ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Bodi ya Huduma ya Maktaba, Baraza la Taifa la Mitihani, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Taasisi ya Elimu Tanzania, Mamlaka ya Elimu Tanzania ili kuendana na sera pamoja na mikataba ya makubaliano ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakamilisha zana mbalimbali za utekelezaji wa sera ikiwemo Mwongozo wa Upimaji na Tathmini katika Elimu, Mfumo wa Taifa wa Upimaji na Tathmini katika Elimu na Mfumo wa Taifa wa Mitaala kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kuandaa na kuhuisha miongozo mbalimbali ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa kwa kuhuisha Mwongozo ya Uanzishaji na Usimamizi wa Programu ya Elimu ya Watu na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; na kuandaa mfumo wa Kitaifa wa kuwaendeleza

kitaalamu wakufunzi na wafanyakazi wasio wakufunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itaendelea kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa ushirikiano baina ya viwanda na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; mwongozo wa uanzishaji wa kampuni bunifu *(spin-off companies)* na vituo vya ubunifu wa teknolojia kwa taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi pamoja na taasisi za utafiti wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo endelevu ni muhimu katika kuendeleza taaluma na kuimarisha utendaji kazi wa walimu, wakufunzi, wadhibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu nchini. Kwa muktadha huo, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu 13,784, maafisa elimu 488, wadhibiti ubora 544, wakufunzi 100, wanafunzi 5,172 na walezi 100 wa skauti katika maeneo mbalimbali ikiwemo usawa wa kijinsia, masomo ya biashara na ufundi, ufundishaji wa elimu ya awali, utawala bora na menejimenti ya elimu, ushauri na unasihi, pamoja na utoaji wa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utoaji wa elimu ya amali katika shule za sekondari nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania itawezesha upanuzi wa shule 55 za sekondari kuwa sekondari za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha elimu ya amali inatolewa kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014, Toleo la 2023, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ualimu kwa kujenga miundombinu na kuweka vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida na Chuo cha Ualimu Mtwara Ufundi ili kuviwezesha vyuo hivyo kuwa vyuo vya mafunzo ya ualimu wa amali na vitakuwa ni Kampasi ya Chuo Kikuu cha Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya amali kwa kuendelea kukamilisha

na jenga miundombinu mbalimbali katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo stadi ikiwemo kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili Vyuo 64 vya Ufundi Stadi *(VETA)* vya Wilaya na Chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe. Pia kuanza ujenzi wa vyuo vitano vya ufundi *(Polytechnics college)* vitakavyojengwa katika Mkoa wa Rukwa, Kigoma, Mtwara, Morogoro na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia na kuendeleza elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini, Serikali itaendelea kuimarisha ithibati na udhibiti katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya maendeleo ya wananchi na sekondari za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa vifaa na zana vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuimarisha ufundishaji kwa kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya *VETA* 98, vyuo 54 vya Maendeleo vya Wananchi na Chuo cha Ufundi Dodoma, pamoja na kununua vifaa vya kisasa vitakavyotumika katika maabara ya udongo, maji na mimea kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo kwa vitendo, uzalishaji na ushauri wa kitaalam kupitia Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia itaendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Kituo cha Magonjwa ya Moyo, Mloganzila kwa kuongeza miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya awali ili kumwandaa mwanafunzi kujiunga na ngazi ya elimu ya msingi kulingana na miongozo na taratibu kwa kutoa elimu kwa wadau kuhusu kiunzi cha elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa za elimu ya

awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kusajili shule za msingi na sekondari takribani 785.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu bora ni muhimu katika kuboresha na kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi, sekondari na ualimu. Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendelea kuwezesha ujenzi wa madarasa 2,730 na mabweni 140 ili kuwezesha utekelezaji wa mpango wa elimu ya msingi ya lazima wa miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya udhibiti ubora wa elimu katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ni muhimu katika kuhakikisha elimu inayotolewa katika taasisi hizo inazingatia taratibu na miongozo inayotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za uthibiti ubora kwa kufanya tathmini ya jumla katika asasi 6,962 sekondari 1,260, vyuo vya ualimu 72, vyuo vya maendeleo ya wananchi 53, na vituo 50 vya elimu ya watu wazima na mafunzo nje ya mfumo rasmi kwa lengo la kubaini ubora, hali ya uandikishaji, ufundishaji, usimamizi na uongozi shuleni na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itakarabati miundombinu katika Ofisi za Udhibiti Ubora wa Shule za Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara, Bukoba, Ikungi, Halmashauri ya Mji Kasulu, Chalinze, Chato, Songea, Handeni, Nzega, Ileje, Longido, Mafia, Halmashauri ya Wilaya Morogoro na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutambua na kukuza kazi za uandishi bunifu ili kuendelea kuibua Waandishi wa Fasihi ya Kitanzania, kuongeza machapisho na kukuza tabia ya usomaji katika ngazi mbalimbali za elimu kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa lengo la kuwatambua na kuwazawadia waandishi mahiri wa kazi za fasihi; na kuendelea kuratibu Shindano la Uandishi wa Insha wa Nchi za Afrika Mashariki

na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu vya elimu awali, msingi, sekondari na ualimu ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Itachapa na kusambaza vitabu vya kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa elimu ya msingi darasa la tano, sekondari mkondo wa jumla kidato cha pili, sekondari mkondo wa amali kidato cha tatu na kidato cha sita kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) Itachapa na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo kwa shule 20,000 na vyuo vya ualimu 34; na vitabu 3,500,000 vya masomo ya ufundi, sayansi na hisabati kwa kidato cha kwanza, cha pili, cha nne na cha sita;

(iii) Itaendelea kuandaa maudhui ya kieletroniki kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na kuwajengea walimu uwezo wa kufundisha kwa kutumia teknolojia kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza fursa za elimu kupitia vituo mbalimbali vya utoaji wa elimu kwa njia mbadala kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutoa fursa za masomo ya kuwajengea ujuzi vijana walio nje ya shule kupitia Mpango wa Elimu Changamani *(IPOSA)* kutoka vijana 6,500 kwa mwaka 2024/2025 hadi vijana 22,500 kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, itaongeza fursa za utoaji wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 11,762 kwa mwaka 2024/2025 hadi 15,000 kwa mwaka 2025/2026 ili kuhakikisha kila mwanafunzi anakamilisha mzunguko wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 2,000 watakaosoma Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum na kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu ikiwa ni moja ya jitihada ya kuondoa vikwazo vya kimfumo kwa kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji, mafunzo, uandaaji wa miongozo kwa ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza utekelezaji na uendeshaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ili kuhakikisha walimu wanaohitimu katika vyuo vinavyotoa mafunzo ya elimu ya ualimu vinavyotambulika na Serikali, wanapata usajili utakaowawezesha kutambulika ndani na nje ya nchi pamoja na kuendeleza utaalamu wao. Aidha, bodi itawezesha usajili na uendelezaji wa walimu wote walioajiriwa katika shule za Serikali na zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaboresha miundombinu katika vyuo vya ualimu nchini kwa kuanza ujenzi wa nyumba tatu za wakufunzi katika Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa; itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa na Kleruu; ujenzi wa jengo la utawala katika vyuo vya ualimu Tarime, Kinampanda, Kitangali, Mpuguso, Shinyanga na Ndala na ujenzi wa miundombinu ya michezo katika Chuo cha Ualimu Dakawa na Butimba. Vilevile, itanunua na kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo 34 vya ualimu vya Serikali na itanunua na kusambaza vifaa vya maabara katika vyuo 13 vya ualimu vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa elimu jumuishi na elimu kwa watu wazima kwa lengo la kujenga uelewa kwa Watanzania kuhusu fursa mbalimbali za elimu zilizopo kwa makundi yote katika jamii kwa kutoa elimu kwa wadau kuhusu Mwongozo wa Ujumuishi wa Matumizi ya Kidijiti katika Shule na Vyuo vya Ualimu; na kuendelea kujenga uelewa kuhusu haki na wajibu wa watu wenye ulemavu kupitia Maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Suniani, Wiki

ya Viziwi, Siku ya Fimbo Nyeupe kwa Wasioona, na Siku ya Breli na wenye Ualbino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza fursa za elimu ya juu nchini kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Serikali itaendelea kuratibu udahili wa wanafunzi 150,000 kwa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kujiunga na programu mbalimbali za masomo katika vyuo vya elimu ya juu. Vilevile, itakagua na kutathmini ubora wa vyuo vikuu 25 na mitaala 60 inayofundishwa katika vyuo vikuu kwa lengo la kuhakiki ubora wake. Aidha, itakagua na kutathmini mitaala 60 inayofundishwa katika vyuo vikuu na kutoa ithibati ya chuo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekitii, vilevile Serikali itaendelea kutoa mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wenye sifa ili kuongeza fursa za elimu ya juu nchini kama ifuatavyo: -

(i) Itaongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu kutoka 245,314 mwaka 2024/2025 hadi wanafunzi 252,773 kwa mwaka 2025/26;

(ii) Itaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi 10,000 wa ngazi ya stashahada katika fani za kipaumbele ikiwemo Sayansi, Teknolojia, na Uhandisi;

(iii) Itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 2,630 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi kupitia *Samia Scholarship;* na

(iv) Itaendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu mitihani ya Kitaifa ya kidato cha sita na shahada za awali kupitia Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 210.2 kutoka sekta za umma, binafsi na zisizo rasmi kwa kuwatambua wanufaika wapya 40,000 na kufanya ukaguzi kwa

waajiri 8,000 kuhusu umuhimu wa utii wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kuendelea na ujenzi na ukarabati katika taasisi 19 za elimu ya juu zinazotekeleza mradi wa elimu wa juu kwa mageuzi ya kiuchumi. Miundombinu hiyo ni pamoja ujenzi wa kumbi za mihadhara, madarasa, hosteli na ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, itaendelea na ukamilishaji, ujenzi na ukarabarati wa miundombinu mbalimbali katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia ikiwemo kuendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa, kikanda na Kimataifa, Serikali itaendeleza elimu ya juu ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za Elimu ya Juu. Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kukuza na kubiasharisha Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali vilevile itatoa ufadhili kwa wanafunzi wawili, raia wa Oman, na wanafunzi watano raia wa Hungary kusoma katika vyuo vikuu vya hapa nchini kulingana na mikataba na utaratibu. Vilevile, itaratibu uhusiano wa kiutendaji kati ya taasisi 15 za elimu ya juu na sekta binafsi vikiwemo viwanda ili kuwezesha wanafunzi kupata nafasi za kujifunza kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu katika taasisi za elimu ya juu kwa kuwezesha ushiriki wa viongozi wa elimu 420, watumishi 30, wanafunzi wenye ulemavu 20 na wasio na ulemavu 370 kutoka taasisi 10 za elimu ya juu kushiriki kongamano kuhusu elimu jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha masuala mtambuka ikiwemo mazingira, masuala ya kijinsia na elimu ya afya katika taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo kuhusu masuala ya teknolojia ya nyuklia 2013 ili kubainisha hali halisi ya utekelezaji wa sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itaanzisha utekelezaji wa Mfuko wa *Samia Innovation Fund*, wenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 utakaotoa mikopo nafuu kwa wabunifu kwa lengo la kuendeleza na kubiasharisha ubunifu pamoja na kutoa fursa za ajira kwa Watanzania kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa mara ya kwanza, itatoa ufadhili kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika matokeo ya kidato cha sita kwenye mchepuo wa masomo ya sayansi ili waweze kujiunga na masomo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu mahiri duniani, kusomea taaluma za *data science* ikiwemo *artificial intelligence*, *machine learning* na sayansi za mwelekeo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu hiyo itaitwa *Samia Scholarship Extended for Data Science, Artificial Intelligence and Allied Sciences.* Lengo la programu hii ya *Samia Scholarship Extended* ni kutengeneza wataalamu mahiri katika masuala ya *data science* ili waweze kushindana na kufanya kazi popote duniani. Mkakati wa utekelezaji umegawanyika katika ngazi kuu tatu;

(i) Ngazi ya kwanza ni kuwajengea uwezo vijana waliomaliza kidato cha sita kupitia kambi maalum *(Preparatory Camp)* ili kuwaandaa kujiunga na vyuo vikuu mahiri duniani katika taaluma za *Data Science* kwa kupewa mafunzo na wataalamu wabobezi kutoka Sekta Binafsi na wataalamu wazawa wanaoishi nje ya nchi;

(ii) Ngazi ya pili ni kuwawezesha vijana (waliopitia kambini) kupata udahili katika vyuo vikuu mbalimbali duniani na kuwasaidia kutafuta *scholarship* katika sehemu mbalimbali; na

(iii) Ngazi ya tatu ni kutoa ufadhili kwa vijana wenye Shahada ya Kwanza kwenda kuongeza ubobezi kupitia Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na *Indian Institute of Science and Technology* kampasi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza nia ya kuongeza wataalamu wabobezi katika nyanja ya sayansi na teknolojia ya nyuklia, Serikali kupitia *SAMIA Extended Scholarship* itaendelea kutoa ufadhili kwa Watanzania wenye ufaulu wa juu katika fani za Sayansi na Teknolojia ya Nyuklia kwa ngazi ya shahada ya kwanza ili kuweza kujiunga na masomo ya shahada za juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye shukrani. Naomba nitoe shukrani kwa taasisi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani kwa Mheshimiwa QS Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Ignatius Nombo; Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Daniel Mushi na Dkt. Wilson Mahera kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, ninaomba kutoa shukrani zangu kwa Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Cuba, Ethiopia, Finland,

Hungary, India, Israel, Italia, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi. Aidha, ninatambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na *Aga Khan Education Services,* Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Christian Social Services Commission (CSSC), Comprehensive Nuclear–Test - Ban Treaty Organisation (CTBTO),* na *DAAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni *Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO), Global Partnership for Education (GPE), Human Development Innovation Fund (HDIF), Inter University Council for East Africa (IUCEA), International Atomic Energy Agency (IAEA), Japan International Cooperation Agency (JICA),* Jumuiya ya Madola, *Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), na Plan International.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni *Swedish International Development Agency (SIDA), Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO) na United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,436,428,405,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 688,614,234,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo shilingi

635,249,992,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 53,364,242,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na shilingi 1,747,814,171,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi 1,186,987,965,000 ni fedha za ndani na shilingi 560,826,206,000 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 3,240,288,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi 1,538,096,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 1,702,192,000.

Mheshimiwa Mwenyekitii, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya shilingi 2,439,668,693,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Dhima**

Dhima ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujiendeleza kielimu ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

Majukumu ya Wizara. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu nchini kwa kuandaa Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali kutoka ngazi ya Elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika nyanja mbalimbali ikiwemo biashara, viwanda, kilimo na maisha ya kila siku. Wizara pia ina wajibu wa kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Elimu ya Ualimu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, na Elimu ya Juu. Vilevile, Wizara ina jukumu la kusimamia mafungu mawili ambayo ni Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia) na Fungu 18 (Tume ya Taifa ya UNESCO).

Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yameainishwa katika Hati Idhini iliyotolewa tarehe 7 Mei, 2021 (GN No. 385) na marekebisho yaliyotolewa tarehe 24 Januari, 2022 (GN No. 57B) ambapo Wizara imeelekezwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) kutunga na kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo na Ujuzi;
(ii) kusimamia maendeleo ya Elimumsingi;
(iii) kusimamia ithibati ya Elimu ya Ualimu na maendeleo ya viwango vya elimu ya ualimu;
(iv) kusimamia maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;
(v) kusimamia maendeleo ya Elimu ya Juu;
(vi) kubaini na kuendeleza vipaji;
(vii) kusimamia utoaji wa elimu ya maendeleo kwa wananchi;
(viii) kusimamia Mfumo wa Tuzo wa Taifa;
(ix) kusimamia ubainishaji na uendelezaji wa ujuzi unaohitajika;
(x) kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule;
(xi) kusimamia huduma ya uchapaji wa nyaraka za elimu;
(xii) kuhamasisha matumizi ya Sayansi, Uhandisi, Teknolojia na Hisabati;

(xiii) kuendeleza utaalamu asilia katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;
(xiv) kusimamia masuala ya Tume ya Taifa ya UNESCO;
(xv) kusimamia masuala ya utafiti na maendeleo katika Sayansi na Teknolojia;
(xvi) kuimarisha utendaji na maendeleo ya rasilimaliwatu katika Wizara; na
(xvii) kusimamia Idara, Mashirika, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

## A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, Baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua na kutoa ushauri wa makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa mwaka wa fedha 2024/25. Pia, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26 ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 Tume ya Taifa ya UNESCO.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2025/26.

### Salamu za Pole

3. Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyekuwa Makamu wa Kwanza

wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea tarehe 7 Mei, 2025 jijini Dar es Salaam. Vilevile, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa msiba huu mzito.

4. Mheshimiwa Spika, pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Ukanda wa Afrika.

5. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninatoa pole kwa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Tabitha Siwale, aliyewahi kuwa Waziri wa Elimu katika Taifa letu na ambaye ndiye mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania kuteuliwa kuwa waziri. Pia, ninaomba kutoa pole kwa familia na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Profesa Philemon Sarungi, ambaye pamoja na nafasi nyingi ambazo amewahi kushika na kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu, aliyewahi pia kuwa Waziri wa Elimu na Utamduni mwaka 1993 hadi 1994.

6. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, wabunge wenzangu, viongozi wa Chama na Serikali, wananchi na watumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kujumuika nami katika kipindi kigumu cha kumpoteza mama yangu mpendwa Bi. Sekunda Nemes Massawe (Mama Mkenda) tarehe 30 Januari, 2025.

Ninawaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina!

**Pongezi na Shukrani**

7. Mheshimiwa Spika kwa namna ya pekee, ninaomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na dhamira yake ya dhati ya kusimamia mageuzi makubwa katika mfumo wetu wa elimu kama alivyoahidi katika hotuba aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021. Maono na dhamira hiyo

imewezesha kuandaa na kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inayolenga kuongeza ubora wa elimu yetu na kumwezesha Mtanzania kupata ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya rasilimawatu ya nchi na soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

8. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninaomba kutumia fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupendekezwa na mkutano mkuu maalum wa Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea pekee wa Urais katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka 2025.

9. Mheshimiwa Spika, nampongeza pia, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza kupitia Chama cha Mapinduzi. Aidha, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kupendekezwa kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi wa urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

10. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi, ushauri wao na miongozo yao ambayo imetusaidia sana katika utendaji wetu.

11. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.) Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, ninatumia nafasi hii kuwapongeza wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Jimbo la

Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kwa umakini wao katika kuliongoza bunge letu Tukufu.

12. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana mimi pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Omary Juma Kipanga (Mb) kuisimamia na kuiongoza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

13. Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao katika kuisimamia na kuishauri Wizara katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2025/26. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati yametusaidia sana katika maandalizi ya bajeti ya Wizara. Napenda kuiahidi Kamati kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano, kupokea maoni na ushauri wao na kufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya Sekta yetu ya elimu.

14. Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu Mkuu, Profesa Carolyne Nombo na watendaji wote wa Wizara kwa utumishi wao mzuri.

15. Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Rombo kwa ushirikiano wanaonipa katika jitihada za kuleta maendeleo ya jimbo letu. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Aidha, kwa namna ya pekee ninapenda kuishukuru familia yangu hasa mke wangu mpendwa Beatrice kwa kunitia moyo na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa uwezo wangu wote niliojaliwa.

16. Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa nitoe taarifa ya utelekezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia FUNGU 46 na FUNGU 18 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

17. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/25 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi 1,968,212,534,000.00 kwa ajili ya FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa ni ongezeko la Shilingi 619,649,159,000.00 sawa na asilimia 31 ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi 1,348,563,375,000.00 kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo Shilingi 637,287,706,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,328,042,674,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 2,882,154,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha Shilingi 1,319,040,000.00 za Mishahara na Shilingi 1,563,114,000.00 za Matumizi Mengineyo.

### Ukusanyaji wa Maduhuli

18. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/25 Wizara kupitia FUNGU 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya Shilingi 677,299,142,074.83 ambapo kiasi cha Shilingi 9,700,537,000.00 kilipangwa kukusanywa na Idara na Vitengo vya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Shilingi 667,598,605,074.83 kilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni ada, kodi za nyumba, malipo ya ushauri elekezi, huduma za Uthibiti Ubora wa Shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

19. Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi 479,720,873,713.48 sawa na asilimia 71 ya makadirio ambapo, Shilingi 7,752,078,366.57 zimekusanywa na Idara na Vitengo vya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Shilingi 471,968,795,346.91 zimekusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Matumizi ya Kawaida**

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2024/25, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 637,287,706,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya mishahara ni Shilingi 585,225,031,000.00 ambapo idara na vitengo vya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni Shilingi 100,231,467,000.00 na Shilingi 484,993,564,000.00 kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Matumizi Mengineyo Shilingi 52,062,675,000.00 ambapo idara na vitengo ni Shilingi 36,208,567,352.00 na Taasisi ni Shilingi 15,854,107,648.00.

21. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025, Wizara imepokea Jumla ya Shilingi 501,689,846,848.61 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46 sawa na asilimia 79 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 2,440,900,854.22 sawa na asilimia 85 ya fedha ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

**Miradi ya Maendeleo**

22. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,328,042,674,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni Shilingi 1,033,393,669,000.00 na fedha za nje ni Shilingi 294,649,005,000.00.

23. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 1,028,713,856,289.34 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 77 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo

Shilingi 747,517,536,002.84 ni fedha za ndani na Shilingi 281,196,320,286.50 ni fedha za nje.

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA FUNGU 46**

24. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imetekeleza vipaumbele vitano kwa lengo la kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu pamoja na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia maendeleo endelevu ya taifa.

25. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 ni kama vifuatavyo:

a) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo;
b) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali za kihandisi na amali zisizo za kihandisi);
c) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya msingi, sekondari na ualimu;
d) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na
e) kuendeleza tafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

**a. Utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Uandaaji wa Miongozo na Utoaji wa Mafunzo.**

26. Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Februari 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inayolenga kutoa elimu inayozingatia ujuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira na kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Aidha, ili kutekeleza kwa ufanisi sera na mitaala iliyoboreshwa, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, mikutano na majukwaa mbalimbali.

27. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa walimu ikiwemo utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa kwa walimu 70,657 (shule za msingi 3,403 na

sekondari 67,254) ikilinganishwa na walimu 1,250 wa shule za msingi na sekondari waliopata mafunzo mwaka 2021/22. Aidha, imetoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule 611 ikilinganishwa na wathibiti ubora wa shule 368 waliopata mafunzo mwaka 2021/22. Vilevile, Serikali imetoa mafunzo kwa maafisa elimu kata 403, wakufunzi wa vyuo vya ualimu 70, watumishi wa vyuo vya ualimu 120, wakuu wa vyuo 35 na walimu wakuu 9,020.

28. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sera na mitaala iliyoboreshwa, Serikali imeanza mapitio ya Sheria ya Elimu Sura ya 353 ili kuendana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 ambapo maoni ya wadau mbalimbali wa elimu kuhusu sheria husika yameendelea kukusanywa.

29. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya VETA, Sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na Sheria ya Mfuko wa Elimu (TEA). Aidha, Serikali imekamilisha taarifa ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba pamoja na mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 58 cha Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura ya 346 na kanuni ya 33 ya Kanuni za Vyuo Vikuu. Vilevile, imefanya marekebisho ya Sheria Ndogo za Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Marekebisho ya sheria hizo yanalenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sera na kuwezesha taasisi hizo kuendana na makubaliano ya kikanda na kimataifa.

30. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhuisha na kuandaa miongozo mbalimbali ya utoaji elimu na mafunzo nchini ili kuendana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imehuisha Mwongozo wa Taifa wa Tuzo na Sifa Linganifu za Kitaaluma (Tanzania Qualification Framework- TQF) utakaowezesha kubainisha vigezo, viwango vya sifa za elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali za elimu ndani na nje ya nchi;

(ii) imehuisha Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule wa Mwaka 2020 kwa kuweka utaratibu wa kuanzisha na kuendesha shule za amali pamoja na kuanza matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili wa shule;

(iii) imeandaa Mwongozo wa Utambuzi wa Vipawa na Vipaji wa Mwaka 2025 kwa lengo la kuwabaini na kuwaendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji katika shule za msingi na sekondari nchini;

(iv) imehuisha Mwongozo wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini wa Mwaka 2020 kwa kuongeza vipengele vinavyolenga kuimarisha ufanisi katika kuwaendeleza kitaaluma na kitaalamu walimu wa shule za sekondari;

(v) imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Elimu wa Mwaka 2024/25-2029/30 sambamba na miongozo minne (4) kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huo kama ifuatavyo: Mwongozo wa Ujumuishi wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Shule na Vyuo vya Ualimu 2025; Mwongozo wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 2025; Mwongozo wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Vyuo Vikuu 2025; na Mwongozo wa Matumizi ya Akili Unde (Artificial Intelligence) katika Elimu 2025;

(vi) imehuisha na kusambaza Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu na Jamii (MUKEJA) kwa kuongeza maudhui yanayozingatia ujuzi utakaowawezesha wahitimu kujiajiri au kuajiriwa;

(vii) imetoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Amali katika Shule za Sekondari wa Mwaka 2025 na Mwongozo wa Mafunzo ya Amali kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2025 ili kuhakikisha wahitimu wanakuwa na ujuzi, maarifa na stadi zitakazowawezesha kujitegemea na kuchangia maendeleo ya jamii;

(viii) imetoa Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma kwa Walimu na Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2025 unaotoa utaratibu wa namna ya kutoa huduma kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum kulingana na mahitaji yao;

(ix) imetoa Mwongozo wa Matumizi ya Breli wa Mwaka 2025 ili kuimarisha matumizi ya breli katika nyanja mbalimbali. Vilevile, imetoa Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2025 kwa lengo la kuhakikisha mfumo wa elimu unawajumuisha wanafunzi wote kwa kutoa fursa za ujifunzaji zinazokidhi mahitaji; na

(x) imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Tathmini ya Ujifunzaji kwa lengo la kurahisisha upimaji wa wanafunzi katika shule za msingi.

31. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha taarifa ya awali ya tathmini ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996 ili kuwezesha kuendelea na mapitio ya sera husika kwa lengo la kuandaa sera inayoakisi hali ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu hapa nchini.

32. Mheshimiwa Spika, takwimu za elimu ni nyenzo muhimu katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji, kufanya tafiti na kutoa maamuzi mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeunganisha mifumo ya takwimu za elimu na kuwa na mfumo mmoja wa sekta ya elimu. Aidha, imeendelea na ujenzi wa Mfumo wa Takwimu wa Sekta ya Elimu utakaowezesha upatikanaji wa takwimu zote za sekta kupitia mfumo huu. Aidha, mfumo huu utakuwa na uwezo wa kupokea takwimu mbalimbali zinazohusiana na elimu kutoka katika mifumo mingine ya Serikali ikiwemo NIDA, RITA, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Idara ya Uhamiaji na OR–TAMISEMI.

33. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa mipango madhubuti ni muhimu katika maendeleo ya sekta ya elimu, kwa msingi huo Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Education Sector Development Plan-ESDP) 2025/26 – 2029/30 ambao utawezesha utekelezaji wa mipango mbalimbali ya

kisekta ikiwemo utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo. Vilevile, imekamilisha mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi unaotoa mwelekeo wa kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali (Ufundi na Ufundi Stadi) katika shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi**

34. Mheshimiwa Spika, elimu ya amali katika shule zetu za sekondari ni nyenzo muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa ufundi na ujasiriamali kwa lengo la kumudu maisha yao, kushindana katika soko la ajira na kuchangia maendeleo ya Taifa. Kwa muktadha huo, Serikali imewezesha ujenzi wa shule mpya 103 za sekondari za amali ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya shule hizo, shule 29 ni za amali za kihandisi na shule 74 ni za amali zisizo za kihandisi. Kukamilika kwa shule hizo kutawezesha kuongezeka kwa idadi ya shule za amali za sekondari kutoka shule tisa (9) hadi shule 112 za sekondari za amali.

35. Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada za kuongeza shule za sekondari za amali nchini, Serikali imeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi hadi kufikia wanafunzi 199,118 kwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wanafunzi 161,750 waliodahiliwa kwa mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 37,368 sawa na asilimia 23. Ongezeko la udahili wa wanafunzi linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya elimu ya ufundi hadi kufikia vyuo 512 kwa mwaka 2024/25 kutoka vyuo ufundi 441 mwaka 2021/22.

36. Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Serikali imedahili wanafunzi 11,232 kati ya 15,150 walioomba kujiunga na mafunzo ya Ufundi Stadi katika mwaka wa masomo 2025. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi - VET imefikia wanafunzi 58,912 (wanawake 12,022 na wanaume 46,890) ambapo kati yao wanafunzi wa kozi za muda mrefu 24,670 (wanawake 8,450 na wanaume 16,220) na wa kozi za muda mfupi ni 34,242 (wanawake 3,572 na wanaume 30,670). Ongezeko la wanafunzi

linatokana na kuongezeka kwa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VET) kutoka 810 mwaka 2021/22 hadi kufikia Vyuo 905 mwaka 2024/25. Vilevile, imedahili wanafunzi 391 katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro – MVTTC ili kuongeza idadi ya walimu wa elimu ya ufundi.

37. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa kitaifa wa kuhakikisha kuwa kila wilaya na mkoa unakuwa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imeendelea na ujenzi wa vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi wa vyuo 63 umefikia wastani wa asilimia 45, chuo cha Mkoa wa Songwe asilimia 40 na chuo cha Chamwino kimefikia asilimia 88.

38. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha na kuongeza miundombinu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kama ifuatavyo:

(i) imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya nyongeza katika vyuo 10 vya mafunzo ya ufundi stadi (Ndolage - Muleba, Ileje - Isongele, Newala - Kitangali, Ngorongoro - Samunge, Golowa-Babati, Urambo - Chekereni, Kasulu-Nyamidaho, Mabalanga-Kilindi, Nkasi - Palamawe na Kanadi-Itilima) ambapo utekelezaji wa ujenzi umefikia wastani wa asilimia 82. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika chuo cha Kigamboni, Kihonda, Nyamidaho, Urambo, Morogoro, Arusha, Karagwe, Busokelo, Makete na Namtumbo ambapo ujenzi umefikia wastani wa asilimia 98.5;

(ii) imeendelea na ukarabati wa jengo la karakana ya umeme katika Chuo cha Ualimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi – Morogoro ambapo ukarabati umefikia asilimia 90;

(iii) imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kampasi ya Pemba ambapo ujenzi wa jengo la utawala umefikia asilimia 95 na ukumbi wa mikutano umefikia asilimia 50. Aidha, imeendelea na ujenzi wa hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi

768 kila moja katika Kampasi ya Karume – Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 52. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara utakaohudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja, katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Kivukoni ambapo ujenzi umefikia asilimia 42;

(iv) imekarabati mfumo wa maji taka, maji safi na umeme katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kivukoni kwenye majengo yafuatayo: mgahawa wa Mianzini, bweni la Azimio, maliwato ya nje ya jengo la Kizota, jengo namba 14, jengo la utamaduni, nyumba namba 13 eneo la maghorofani na jengo la utawala, jengo la "Vituo atamizi vya TEHAMA", jengo la Utamaduni, mabweni ya Mwongozo, Kizota na nyumba namba 11;

(v) imekamilisha ujenzi wa kituo cha afya katika chuo cha Ufundi Arusha ambacho kitatoa huduma kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii inayoizunguka chuo;

(vi) imeendelea na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa nguvu za maji katika kituo cha mafunzo ya nishati jadidifu Kikuletwa ambapo ujenzi umefikia asilimia 30. Mtambo huu unatarajiwa kuzalisha takribani 1.6MW kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, utafiti na kuunganishwa katika Gridi ya Taifa;

(vii) imekamilisha ukarabati wa jengo la mgahawa wa watumishi katika ofisi za Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi – NACTVET Kanda ya Mashariki – Dar es Salaam na kuhuisha mfumo wa Usimamizi wa Takwimu za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; na

(viii) imeendelea na ukamilishaji wa ofisi mbili za kanda za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizopo Tabora na Mbeya.

39. Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa vitendo ni nyenzo ya kuandaa wahitimu wa vyuo vya ufundi katika kupata uzoefu na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Hivyo, Serikali imeendelea

kugharimia mafunzo kwa vitendo viwandani kwa wanafunzi 551 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, wanafunzi 500 wa Chuo cha Ufundi Arusha na wanafunzi 673 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam.

40. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imewezesha upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi 15,000 wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 54, wanafunzi 850 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, wanafunzi 800 wa Chuo cha Ufundi Arusha na wanafunzi 761 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

41. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mifumo ya ithibati na uthibiti ubora kwa lengo la kuhakikisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari za amali zinazingatia viwango vya ubora katika uendeshaji na utoaji wa mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeidhinisha uanzishwaji wa idara na programu 48 katika vyuo 18 ili kuendesha programu za Tuzo za Kitaifa za Ufundi (National Technical Award-NTA) kwa bodi za masomo zilizosajiliwa;

(ii) imetoa Namba za Uhakiki wa Tuzo (AVN) 27,686 kwa lengo la kuimarisha uhakiki wa taarifa mbalimbali za wahitimu wa Stashahada wanaoendelea na elimu ya juu pamoja na kuviwezesha vyuo kuhakiki udahili unaofanywa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu - TCU;

(iii) imehakiki mitaala 223 iliyoandaliwa na vyuo vya ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kwa wahitimu; na

(iv) imefanya ulinganifu wa tuzo 243 ili kuthibiti viwango vya Elimu ya Ufundi nchini.

42. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 912 yakiwemo mafunzo ya muda mfupi

kwa watumishi 813 na muda mrefu kwa watumishi 99 katika ngazi ya Shahada ya uzamivu, uzamili na shahada ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanaendana na mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya teknolojia.

**c. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu**

43. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kwa kuwezesha ujenzi wa miundombinu kama ifuatayo: madarasa 334 (msingi 263 na sekondari 71), mabweni 239 kati ya 114 yaliyolengwa katika shule za sekondari, mabwalo saba (7); nyumba za walimu 63 katika shule za msingi, matundu ya vyoo 4,207 (msingi 3,799 na sekondari 408) kati ya 2,848 yaliyolengwa, matenki ya kuhifadhia maji 140 katika shule za msingi 139, vituo vya walimu 85 kati ya 300 vilivyolengwa na ukamilishaji wa mabweni 285 ya shule za sekondari.

44. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa za elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ili kuhakikisha kila mtanzania anapata fursa ya kujiendeleza katika ngazi hizo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya shule 589 kati ya 772 zilizolengwa ambapo shule za awali pekee 24 (zisizo za Serikali), awali na msingi 344 (Serikali 140 na zisizo za Serikali 204) na sekondari 219 (Serikali 100 na zisizo za Serikali 119) na vyuo vya ualimu viwili (cha Serikali 1 na kisicho cha Serikali 1);

(ii) imekamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa Uanzishaji na Usajili wa Shule (School Accreditation System – SAS) ambapo tangu Oktoba 2024 hadi Aprili, 2025 shule 395 (Serikali 201 na zisizo za Serikali 194) zimesajiliwa kupitia mfumo huo. Mfumo umeongeza ufanisi na kupunguza gharama kwa wadau kwa kurahisisha taratibu za usajili wa shule; na

(iii) imedahili na kusajili wanachuo wa vyuo vya ualimu 15,583 ambapo mwaka wa kwanza wamesajiliwa wanafunzi 3,815, mwaka wa pili 9,977 na mwaka wa tatu 1,801.

45. Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa mara ya kwanza Serikali ya Awamu ya Sita imetoa ufadhili kwa wanachuo 787 (wanawake 429 na wanaume 358) kusoma Stashahada ya Ualimu Elimu Maalum kwa lengo la kuongeza walimu wenye taaluma hiyo na kuboresha utendaji kazi ambapo wanufaika wanasoma katika Chuo cha Ualimu Kabanga, Mpwapwa na Patandi. Vilevile, Serikali imesajili wanachuo 15,583 katika vyuo vya ualimu ambapo mwaka wa kwanza wanafunzi 3,815, mwaka wa pili 9,977 na mwaka wa tatu 1,801. Aidha, Serikali imeendelea kugharimia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 10,010 wa vyuo vya ualimu pamoja na kugharimia huduma ya chakula kwa wanafunzi 15,570 katika vyuo husika.

46. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha elimu inayotolewa katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu inazingatia taratibu na miongozo inayotolewa, Serikali imeendelea kutekeleza kazi za uthibiti ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu kama ifuatavyo:

(i) imefanya tathmini ya jumla katika asasi 7,499 kati ya 7,200 zilizolengwa zikiwemo za Serikali 6,434 na zisizo za Serikali 1,065 kwa mchanganuo ufuatao: shule za awali na msingi 6,458; shule za sekondari 1,016; vyuo vya ualimu 21; vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi viwili (2); na vyuo vya maendeleo ya wananchi viwili (2). Tathmini hiyo ilifanyika katika nyanja zifuatazo: utekelezaji wa mtaala katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi; tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji; uongozi na usimamizi wa rasilimali; mazingira ya shule na mchango wake katika ustawi, afya na usalama; ushiriki wa jamii, nidhamu, maadili, utamaduni na uzalendo; matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha, Asasi hizo zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imefanya tathmini ya ufuatiliaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla katika asasi 1,126 kati ya 1,010

zilizolengwa (za Serikali 876 na zisizo za Serikali 250) zikiwemo shule za awali na msingi 866 na shule za Sekondari 260. Aidha, maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini hiyo yameendelea kufanyiwa kazi kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika utoaji wa Elimu; na

(iii) imeandaa Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule (School Quality Assurance System– SQAS) unaopokea taarifa kutoka mifumo mingine ikiwemo Mfumo wa Taarifa za Shule (School Information System – SIS) ili kuwezesha uchakataji wa takwimu na kutoa taarifa kwa wadau kwa wakati. Vilevile, imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo husika kwa wathibiti ubora wa shule 102 na maafisa TEHAMA 88 wa ngazi ya Makao Makuu ya Wizara na Halmashauri za wilaya 67.

47. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024-2034 kwa kukamilisha uwekaji wa nishati safi ya kupikia katika vyuo vya ualimu 11 ambavyo ni Nachingwea, Katoke, Kleruu, Tabora, Dakawa, Patandi, Mpwapwa, Sumbawanga, Mhonda, Kasulu na Monduli. Aidha, kwa sasa vyuo vyote 35 vya ualimu vinatumia nishati safi ya kupikia.

48. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kujenga uwezo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika matumizi ya TEHAMA, Serikali imeanza majaribio ya utekelezaji wa mradi wa maabara ya TEHAMA inayotembea (DigiTrack Project) katika mikoa mitano (5) kati ya 10 kupitia Kampuni ya HUAWEI. Mikoa iliyoanza majaribio ya utekelezaji wa mradi ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Singida. Vilevile, Serikali imeandaa mpango wa majaribio ya teknolojia za darasa janja (smart class), mfumo wa usimamizi na ujifunzaji, maabara za mtandao na uigaji, teknolojia ya kufundishia kwa kuigiza uhalisia (Virtual and Augmented Reality-VR/AR), matumizi ya simu janja na vishikwambi kwa lengo la kuzibadilisha teknolojia hizo ili ziendane na mazingira ya kitanzania na kutumika katika kujifunzia na kufundishia kwa shule za msingi na sekondari.

49. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha tabia ya usomaji kwa wanafunzi kwa kuendesha mashindano mbalimbali yanayolenga kuchochea ari ya usomaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha maandalizi ya shindano maalum la uandishi wa insha kwa wanafunzi katika nyanja za: Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujijenga Upya ili kuchochea uelewa wa fikra tunduizi kuhusu falsafa ya 4Rs ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(ii) imeratibu mashindano ya uandishi wa insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki – EAC kwa wanafunzi 595 wa shule za sekondari nchini ambapo washindi watano (5) walipatikana kwa ajili ya kushiriki mashindano ngazi ya kikanda. Lengo la mashindano hayo ni kukuza stadi na ujuzi wa uandishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Aidha, imeratibu uandishi wa insha ya SADC kwa wanafunzi 243 wa shule za sekondari ambapo washindi watatu (3) waliopatikana insha zao zimepelekwa kushindanishwa katika ngazi ya Kikanda.

50. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuibua vipaji vya waandishi wa kazi za fasihi ya kitanzania kwa lengo kukuza tabia ya kujisomea, kuhifadhi historia, amali na mitazamo bora ya Taifa la Tanzania kwa kupitia shindano la tatu la Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ambapo jumla ya miswada 282 ya riwaya, hadithi za watoto, ushairi na tamthiliya vilipokelewa na kushindanishwa. Aidha, mshindi wa kwanza hadi wa tatu walipata fedha tasilimu pamoja na vyeti.

51. Mheshimiwa Spika, mashindano ya Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu yameendelea kuleta tija kwa taifa kwa kuongeza machapisho ya kazi za fasihi ya Kitanzania ambapo, Serikali imechapa na kusambaza katika shule za sekondari na msingi jumla ya nakala za vitabu 148,000 (Riwaya 70,000, Ushairi 70,000 na Hadithi za watoto 8,000) vilivyotokana na miswada ya washindi wa kwanza wa shindano la Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu la tarehe 13 Aprili, 2023.

52. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuhakikisha kuwa uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja unafikiwa kwa kuongeza idadi ya vitabu kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari pamoja na kiongozi cha mwalimu. Katika kutekeleza dhamira hiyo, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imechapa na kusambaza nakala 16,795,403 za vitabu vya kiada ngazi ya elimu ya awali na msingi katika mwaka 2024/25 ikilinganishwa na nakala za vitabu 12,197,434 vilivyochapwa na kusambazwa mwaka 2021/22;

(ii) imechapa na kusambaza nakala 9,902,102 za vitabu vya kiada elimu ya sekondari ngazi ya chini na juu katika mwaka 2024/25 ikilinganishwa na nakala za vitabu 5,206,800 vilivyochapwa na kusambazwa mwaka 2021/22;

(iii) imeandaa na kusambaza vitabu vya kiada vya Maandishi yaliyokuzwa Darasa la II na IV pamoja na Breli na Kiongozi cha mwalimu Darasa la II na la IV na vitabu vya Kiada na Kiongozi cha Mwalimu Kidato cha 1 na cha 5; na

(iv) imeendelea kuhamasisha wadau kuchangia upatikanaji wa vitabu vya kiada kupitia kampeni ya Kitabu Kimoja Mwanafunzi Mmoja. Kampeni hii inafanyika kupitia njia mbalimbali ikiwemo matembezi ya hisani yaliyofanyika tarehe 7/03/2025 ambapo jumla ya Shilingi 1,178,163,533 zilikusanywa.

53. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeandaa maudhui ya elimu ya sekondari na kuwekwa katika mfumo wa kidijiti ambapo maudhui hayo yanapatikana kwa matumizi ya wanafunzi na walimu kupitia Mfumo wa Mafunzo kwa walimu na wanafunzi (Learning Management System).

54. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha maktaba za mkoa na wilaya ambapo imesambaza vifaa vya TEHAMA katika maktaba tisa (9) za mikoa minne (Tanga, Mara, Iringa na

Njombe) na wilaya tano (Pangani, Lushoto, Bagamoyo, Njombe na Kongwa).

55. Mheshimiwa Spika, Serikali, pia imeendelea kuboresha huduma za maktaba kwa kuandaa na kusambaza maudhui ya hadithi za habari 39 na picha 106 kupitia mitandao ya kijamii, tovuti na vyombo vya habari vya umma. Aidha, imesambaza vitabu 28,976 katika maktaba za mikoa, wilaya, na vitongoji pamoja na kukarabati Maktaba Kuu ya Taifa na vituo nane (8) vya maktaba katika Mkoa wa Mwanza, Shinyanga, Njombe, Singida, Mtwara, Tanga, Kilimanjaro na Kagera.

56. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania imeendelea kuongeza usajili wa watahiniwa wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na sekondari ambapo katika mwaka 2024, watahiniwa 1,230,774 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi sawa na ongezeko la asilimia 8 ikilinganishwa na watahiniwa 1,132,084 waliosajiliwa mwaka 2021. Aidha, watahiniwa 529,329 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne katika mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na watahiniwa 501,039 waliosajiliwa mwaka 2021.

57. Mheshimiwa Spika, halikadhalika, ufaulu wa wahitimu wa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari umeendelea kuongezeka kila mwaka, ambapo ufaulu wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi katika mwaka 2024 umeongezeka hadi kufikia asilimia 80.87 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 79.62 mwaka 2021/22. Vilevile, ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne umepanda hadi kufikia asilimia 92.37 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 87.30 mwaka 2021.

58. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,530,911 sawa na asilimia 93 ya watahiniwa 1,633,279 waliosajiliwa, ambapo watahiniwa 1,320,227 (wasichana 699,901 na wavulana 620,326) sawa na asilimia 86 walifaulu upimaji huo. Aidha, imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 805,091 sawa na asilimia 92 ya watahiniwa 879,291 waliosajiliwa, ambapo watahiniwa 684,779 (wasichana 369,825 na wavulana 314,954)

sawa na asilimia 85 walifaulu upimaji huo. Vilevile, imekamilisha usajili wa watahiniwa 126,953 kwa ajili ya Mtihani wa Kidato cha Sita na watahiniwa 10,725 wa Mtihani wa Ualimu ambayo itafanyika mwezi Mei, 2025.

59. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa elimu jumuishi na elimu kwa watu wazima kwa lengo la kujenga uelewa kwa watanzania kuhusu fursa mbalimbali za elimu zilizopo kwa makundi yote katika jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imefanya maadhimisho mbalimbali ya watu wenye ulemavu yakiwemo: Siku ya Viziwi Duniani ambayo yalifanyika tarehe 28/9/2024, Wiki ya Fimbo Nyeupe tarehe 21 - 25 Oktoba, 2024 na Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani tarehe 29/11/3/12/2024, kwa lengo la kujenga uelewa kwa jamii na wadau wa elimu kuhusu elimu jumuishi na kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) imefanya maadhimisho ya miaka 30 ya utekelezaji wa Elimu Jumuishi nchini kwa lengo la kuelezea mafanikio ya Serikali tangu mwaka 1994 na kutangaza fursa mbalimbali zilizopo kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji Maalum; na

(iii) imeratibu maadhimisho ya Siku ya Kisomo Kimataifa na Juma la Elimu ya Watu Wazima Kitaifa kuanzia tarehe 7 hadi 11 Oktoba, 2025 ambapo kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika Mkoani Tabora na kuhudhuriwa na washiriki takribani 500.

60. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fursa za mafunzo kwa walimu, wakuu wa shule, wathibiti ubora wa shule na maafisa elimu kata ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo usimamizi wa rasilimali, utawala bora, uthibiti ubora wa shule na utekelezaji wa sera na miongozo ya elimu ambapo kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa walimu 1,696 sawa na asilimia 92 ya walimu 1,843 waliolengwa katika kozi za Astashahada, Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu, na

Uthibiti Ubora wa Shule kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu katika Kampasi ya Bagamoyo, Mbeya na Mwanza; na

(ii) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu pamoja na Utawala Bora wa shule kwa walimu wakuu na Waratibu Elimu Kata 8,617 kutoka Mikoa 13 Tanzania Bara. Vilevile imetoa mafunzo kwa walimu wakuu na mameneja 141 wa shule zisizo za Serikali kuhusu uongozi na usimamizi wa elimu pamoja na utawala bora wa shule.

61. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kudahili wanafunzi na kutoa mafunzo kupitia programu mbalimbali za elimu ya watu wazima kwa lengo la kuchochea malengo endelevu ya kijamii na kiuchumi ambapo kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 2,562 (wanaume 638 na wanawake 1,924) katika programu mbalimbali za masomo ya elimu ya watu wazima;

(ii) imesajili wanafunzi 4,874 (wanaume 2,067 na wanawake 2,807) ambao wanaendelea na masomo katika ngazi mbalimbali hivyo kuvuka lengo la taasisi la kusajili wanafunzi 5,200 (wapya 1,500 na wanaoendelea na masomo 3,700);

(iii) imeendelea kutoa mafunzo ya programu za Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu na Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii kwa wanafunzi 792 (Astashahada 208, Stashahada 166 na Shahada 418);

(iv) imetoa mafunzo ya ana kwa ana kwa wanafunzi 5,271 kati ya 6,602 wanaojifunza kwa njia ya masafa katika mikoa ya Tanzania Bara; na

(v) imewezesha wanafunzi 6,998 kuendelea na masomo kwa njia mbadala ambapo kati yao wanaume ni 1,108 na wanawake ni 5,818. Vilevile, imewawezesha wanafunzi 6,000 walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali kuendelea na masomo katika vituo 191 vinavyotoa elimu kwa njia mbadala.

62. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kutoa elimu jumuishi kwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata vifaa na mahitaji yanayowawezesha kujifunza kwa ufanisi. Katika kufikia lengo hilo, Serikali imenunua na kusambaza vitimwendo 120, kompyuta 35, vishikwambi 45 na vinasa sauti vya kidigiti 48 kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 120 katika halmashauri ambazo zilibainika kuwa na wanafunzi wengi wenye ulemavu wa viungo. Vilevile, imenunua na kusambaza kompyuta mpakato, vitimwendo na vinasa sauti kwa wanafunzi 691 wanaosoma shule ya nyumbani katika shule 136 za msingi zilizobainika kuwa na upungufu wa vifaa.

## d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu

63. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeendelea kuongeza fedha kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hadi kufikia Shilingi bilioni 787.4 mwaka 2024/25 kutoka Shilingi bilioni 570 zilizotolewa mwaka 2021/22. Ongezeko hili la bajeti limewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanufaika kutoka wanafunzi 177,925 mwaka 2021/22 hadi wanafunzi 248,331 mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 39.6.

64. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kutoa mikopo kwa ngazi ya elimu ya stashahada (Diploma) kwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 19.95 kwa wanafunzi 7,534 wa fani za sayansi na ufundi kwa mwaka wa fedha 2024/25 ikiwa ni ongezeko la asilimia 177.6 ikilinganishwa na wanafunzi 2,714 waliopata mikopo hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wenye thamani ya Shilingi bilioni 7.29 kwa wanafunzi 646 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi wanaoendelea (shahada wa kwanza 674 na ngazi ya umahiri 80) wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia SAMIA Skolashipu.

65. Mheshimiwa Spika, sambamba na ufadhili huo, Serikali kwa mara ya kwanza imeanza kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa

Kitanzania wanaosoma shahada za juu katika sayansi na teknolojia ya nyuklia nje ya nchi kupitia SAMIA Extended Skolashipu ambapo wanafunzi watano (5) wamenufaika.

66. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa lengo la kuongeza idadi ya wanufaika wapya na wanaoendelea ambapo katika mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya Shilingi 161,287,805,492.00 zimekusanywa.

67. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika vyuo vikuu kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo la maabara mtambuka la Dkt. Samia Suluhu Hassan lenye maabara 8 na madarasa 8 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,205 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Jengo hilo lilizinduliwa Agosti 6, 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan;

(ii) imekamilisha ujenzi wa jengo la mihadhara lenye kumbi tisa (9) na ofisi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,800 kwa wakati mmoja. Vilevile, imenunua viti 1,548 ambavyo vimefungwa kwenye jengo jipya la mihadhara. Aidha, imeendelea na ujenzi wa majengo yafuatayo: maktaba ambapo ujenzi umefikia asilimia 72, jengo la TEHAMA asilimia 41, hosteli asilimia 41 na ukumbi wa mihadhara asilimia 33 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi;

(iii) imekamilisha ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Msingi ya Mazoezi Chang'ombe, maabara za Sayansi nne na darasa moja katika Shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika mafunzo kwa vitendo. Aidha, imekarabati mabweni matano na kumbi za mihadhara tatu na miundombinu saba ya TEHAMA;

(iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala lenye uwezo wa kuchukua watu 1,800 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu Mzumbe. Aidha, imeendelea kukamilisha jengo la upasuaji katika zahanati ya chuo kampasi kuu na upanuzi wa zahanati kampasi ya Mbeya. Vilevile, imekamilisha uchimbaji wa visima katika kampasi za Chuo Kikuu Mzumbe ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji chuoni;

(v) imeendelea na ujenzi wa jengo la maabara ya matumizi anuwai; jengo la studio; jengo la karakana na jengo la madarasa na ofisi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 6,135 na watumishi 73 kwa wakati mmoja katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu Ardhi ambapo ujenzi umefikia asilimia 86. Aidha, imekarabati madarasa 76, maabara mbili (2), hosteli tatu (3), nyumba tano (5) za watumishi katika Chuo Kikuu Ardhi. Vilevile, imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya TEHAMA ambapo ukarabati huo umefikia asilimia 60;

(vi) imeanza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la kituo cha wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5. Aidha, imeendelea na ujenzi wa maabara kuu ya kemikali katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 50;

(vii) imeanza ujenzi wa maabara katika ndaki ya sayansi asilia na hisabati ambapo ujenzi umefikia asilimia 26 na ujenzi wa madarasa katika ndaki ya sayansi ya ardhi na uhandisi ambapo ujenzi umefikia asilimia 42.8 katika Chuo Kikuu cha Dodoma;

(viii) imeendelea na ujenzi wa jengo la kitivo cha sayansi ya jamii na jengo la utafiti na uzamili ambapo ujenzi wa majengo hayo umefikia asilimia 30 kila moja katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam; na

(ix) imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Tume ya Vyuo Vikuu katika Jiji la Dodoma ili kusogeza huduma za tume karibu na wananchi ambapo ujenzi umefikia asilimia 29.

68. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya taasisi za sayansi na teknolojia kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa madarasa yenye ghorofa mbili (2) na hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kiume katika kituo cha umahiri cha ngozi cha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - Kampasi ya Mwanza. Aidha, imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la mihadhara, jengo la nishati mbadala, ujenzi wa mfumo wa maji taka, uzio wa eneo la kampasi, jengo la taaluma, hosteli za wanafunzi, jengo na miundombinu ya kuchakata bidhaa za ngozi kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) imekamilisha ujenzi wa jengo la taaluma na karakana katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - Kampasi ya Rukwa ili kuongeza uwezo wa kampasi kudahili wanafunzi wapatao 3,000. Aidha, imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya hosteli za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambapo ukarabati huo umefikia asilimia 99;

(iii) imeendelea na ujenzi wa jengo moja la taaluma, majengo mawili (2) ya karakana na jengo moja la kituo cha ubunifu na uhaulishaji wa teknolojia katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuongeza uwezo wa kampasi kudahili wanafunzi wapatao 15,000;

(iv) imeendelea na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ambapo ujenzi umefikia asilimia 74; na

(v) imeanza ujenzi wa majengo mawili (2) ambayo ni kituo cha kikanda cha umahiri katika TEHAMA na majengo ya hosteli katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kampasi kuu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 ambapo ujenzi umefikia asilimia 90. Vilevile imeanza ukarabati wa jengo la utawala na madarasa.

69. Mheshimiwa Spika, Serikali, pia imeendelea na utekelezaji Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ili kuimarisha utoaji wa elimu ikiwemo ujenzi wa kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi kama ifuatavyo: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Zanzibar – Buyu asilimia 50, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Kagera asilimia 50, Chuo cha Kilimo cha Sokoine kampasi ya Katavi asilimia 15; Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili kampasi ya Kigoma asilimia 10; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Lindi asilimia 50; Chuo Kikuu Ardhi kampasi ya Mwanza asilimia 10; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi ya Rukwa asilimia 87; Chuo cha Ushirika Moshi kampasi ya Shinyanga asilimia 46, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kampasi ya Tabora asilimia 10; na Chuo Kikuu cha Mzumbe kampasi ya Mkinga asilimia 45;

70. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango na mahitaji ya soko la ajira, Serikali imeendelea kusimamia na kuthibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu maombi 147,710 ya kujiunga na Elimu ya Juu kwa ngazi ya Shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu nchini kwa mwaka wa masomo 2024/25. Kati ya maombi hayo, waombaji 137,817 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 37,197 ikilinganishwa na wanafunzi 100,620 waliodahiliwa mwaka 2021/22;

(ii) imetathmini tuzo 3,021 kati ya 5,000 zilizolengwa kwa wanafunzi waliohitimu vyuo vikuu vya nje ya nchi na kutambua tuzo 2,516 (Cheti 9, Stashahada 152, Shahada 1,377, Post. Cert. 23, astashahada 3, uzamili 813 na uzamivu 139) sawa na asilimia 83 ambazo zimekidhi vigezo. Aidha, imeendelea na maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa kutathmini na kutambua tuzo za kigeni zilizotolewa katika vyuo vikuu nje ya nchi kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango, maamuzi ya kisera na kiutendaji;

(iii) imefanya kaguzi 22 kwa lengo la kuhakiki ubora wa elimu katika vyuo vikuu vifuatavyo: Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Tanzania (KIUT), Chuo Kikuu Mwanza (MzU), Chuo Kikuu Kishirikishi cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMCO), Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha (RUCU), Chuo Kikuu cha Jordan (JUCo), Chuo Kikuu cha Waislam cha Morogoro (MUM), Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Chuo Kikuu cha Mt. Yosefu Tanzania (SJUIT), Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait (SUMAIT), Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya (CUHAS), Chuo Kikuu Mzumbe (MU), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Mt. Augustino cha Tanzania (SAUT) Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mtakatifu Francis (SFUCHAS), Chuo Kikuu cha Kiislam cha Afrika Mashariki (IUEA)– Kigamboni, Chuo Kikuu cha Makumira (TUMA) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE);

(iv) imepokea na kutathmini programu 360 kutoka vyuo vikuu ambapo programu 257 zilipatiwa ithibati kama ifuatavyo: Astashahada 12, Shahada za Awali 53, Shahada ya Uzamili 188 na Shahada ya Uzamivu 4; na

(v) imefanya ukaguzi kwa mawakala saba (7) wanaohusika kupeleka wanafunzi kusoma katika vyuo vya nje ya nchi kwa lengo la kuwasajili au kuhuisha usajili. Taasisi hizo ni: EuroAsia Universities Limited, Worldwide Interconnection, UniAid Africa Limited, Lidege International Education Link, Raffles Global Education Services, Imperial Learning Solutions na Edukwanza consultants Limited ambapo walipatiwa leseni za kufanya kazi ya uwakala.

71. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi za elimu ya juu zilizo nje ya nchi kwa lengo la kutoa fursa za masomo kwa watanzania kupitia skolashipu zinazotolewa na nchi rafiki kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 181 kwenda nchi rafiki kama ifuatavyo: Urusi 90, Algeria 33, China 120, Hungary 20, Jumuiya ya Madola ya Uingereza watano (5) na Mauritius wawili (2). Aidha, imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(ii) imesaini hati ya makubaliano na Vignan Foundation for Science, Technology and Research (VFSTR) iliyopo nchini India mnamo tarehe 18 Julai, 2024.

Makubaliano hayo yatawezesha wanafunzi 100 wa kitanzania kwenda kusoma India katika fani za kipaumbele ambazo ni Kilimo, Afya, Uhandisi na TEHAMA kwa gharama nafuu.

72. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kufundisha wanyama (APOPO) hususan Panyabuku kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambapo jumla ya panya 100 wamefundishwa na kufuzu kisha kupelekwa Angola (13), Azerbaijan (11), Cambodia (58) na Ethiopia sita (6) kwa ajili kutambua mabomu yaliyotegwa ardhini pamoja na utambuzi wa vimelea vya kifua kikuu. Aidha, panya 12 wamepelekwa nchini Marekani kama panya wa maonesho (mabalozi) kwenye shamba la wanyama.

73. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo umeendelea kuijengea sifa na kuitangaza Tanzania Kimataifa ambapo panya wa Kitanzania ajulikanaye kwa jina la Ronin amevunja rekodi ya dunia kwa kutambua mabomu 109 yaliyotegwa ardhini nchini Cambodia akivunja rekodi ya panya wa Kitanzania Magawa ambaye alitambua mabomu 71 yaliyotengwa ardhini.

74. Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia ni muhimu katika maendeleo ya kitaaluma na kitaalamu. Mafunzo haya husaidia wanafunzi kupata ujuzi unaohitajika katika soko la ajira pamoja na kupata fursa ya kuhusianisha kazi na walichofundishwa vyuoni. Katika kufikia azma hii, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imenunua mtambo wa kuchimba visima vya maji (Well-drilling Rig) na vifaa vyake kwa ajili ya kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma shahada zinazohusiana na uhandisi wa rasilimali za maji katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo;

(ii) imeanzisha karakana ya bidhaa za nguo na ngozi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wanaosoma Shahada ya Sayansi za Kaya na Taaluma za Walaji kwa lengo la kuwapa uzoefu wa ubunifu, usanifu na utengenezaji wa nguo na bidhaa za ngozi, pamoja na kutoa huduma kwa jamii inayozunguka kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; na

(iii) imeratibu na kuwezesha mafunzo elekezi kwa wanafunzi 155 waliochaguliwa kushiriki katika programu ya ushirika wa kilimo ya miezi 11 nchini Israel kwa lengo la kuwajengea uwezo wa stadi za kilimo na kuwapa uzoefu wa mafunzo kwa vitendo, teknolojia na mbinu mbalimbali za kuimarisha kilimo.

75. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwaendeleza kitaaluma na kitaalamu wahadhiri na watumishi wa taasisi za elimu ya juu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 639 na mafunzo ya ngazi ya stashahada, shahada ya umahiri na shahada ya uzamivu kwa watumishi na wahadhiri 305.

76. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa afua za kuwezesha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika taasisi za elimu ya juu ni hatua muhimu katika kuhakikisha usawa katika utoaji wa elimu. Hii inahusisha kuweka mazingira ya kujifunzia ambayo yanawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kushiriki kikamilifu katika masomo yao na kufikia malengo yao ya kitaaluma. Ili kufanikisha hili, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imesambaza vifaa saidizi ikiwemo kompyuta mpakato 29, vishikwambi 45, vifaa vya usikivu 46, digital voice recorder 36, vitimwendo 15 na binoculars 10 katika taasisi saba (7) za elimu ya juu. Aidha, imetoa miguu bandia kwa wanafunzi wanne (4) wa

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na imetoa bajaji mbili (2), vifaa vya usikivu vitano (5), voice recorder moja (1), vishikwambi viwili (2) kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; na

(ii) imetoa mafunzo kuhusu elimu maalum na elimu jumuishi kwa washiriki 1,668 ikiwemo wanafunzi, wahadhiri na viongozi wa vyuo kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Taasisi ya Uhasibu (TIA). Aidha, imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa hosteli 147 wa vyuo vikuu 19 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuwabaini wanafunzi wenye mahitaji maalum na namna ya kuwapa huduma kulingana na mahitaji yao.

**e. Kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

77. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa nchi katika tafiti ili kukuza na kuendeleza maarifa, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kusaidia kutatua changamoto mbalimbali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imetoa vibali 489 kwa watafiti wa ndani na nje ya Tanzania wanaofanya tafiti katika nyanja za sayansi ya jamii, sayansi asilia, sayansi ya tiba na afya, kilimo na sayansi ya mifugo. Aidha, imeanzisha dirisha la utoaji mikopo kwa watafiti na wabunifu kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) kwa kushirikiana na benki ya CRDB;

(ii) imeendelea na miradi ya utafiti 784 kupitia taasisi za elimu ya juu katika maeneo ya elimu, afya, mazingira, kilimo, utawala, ardhi, ujenzi, usanifu wa majengo, uchumi endelevu wa viwanda, mabadiliko ya tabia ya nchi na njia ya uvunaji wa maji;

(iii) imeendelea kushirikiana na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti cha Sayansi ya Kilimo cha Japan kufanya tafiti kuhusu

teknolojia ya umwagiliaji mashamba ya mpunga katika maeneo yanayopata mvua au maji kidogo kupitia shamba la mafunzo ya umwagiliaji lililopo Oljoro. Utafiti wa uwiano wa maji katika skimu ya umwagiliaji iliyopo Magugu-Mkoa wa Manyara na utafiti juu ya uimarishaji wa kingo za majaruba ya mpunga kwa kutumia majani yanayotambaa katika shamba la majaribio lililopo Chuo cha Ufundi Arusha; na

(iv) imetoa mafunzo kuhusu dhana ya mali akili (Intellectual Property), uanzishaji wa vituo vya teknolojia, ithibati katika miundombinu ya utafiti na ubunifu pamoja na uwazi katika sayansi kwa viongozi na wataalam kutoka taasisi 18 za elimu ya juu na utafiti nchini ili kuongeza fursa za ubiasharishaji wa matokeo ya utafiti na ubunifu yanayozalishwa nchini.

78. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa machapisho ya utafiti kupitia taasisi za elimu ya juu, taasisi za sayansi na teknolojia, taasisi za utafiti na maendeleo na vyuo vya elimu ya ufundi kwa kutoa machapisho 832 kati ya 379 yaliyolengwa katika maeneo ya elimu, ushirika, afya, usimamizi na uendelezaji ardhi, mazingira, makazi, uongozi, ukulima na tabia ya nchi katika majarida mbalimbali ya kitaaluma ya ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza maarifa katika jamii na kutatua changamoto mbalimbali.

79. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza utafiti, ubunifu na ubiasharishaji wa teknolojia na aina nyingine za bidhaa zinazoibuliwa na kutambuliwa nchini, Serikali imebainisha maabara 10 ambazo zitajengewa uwezo na kupandishwa hadhi kuwa Maabara za Kitaifa za Rufaa za Utafiti na Ubunifu (National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories) ili kuongeza mchango wa utafiti na ubunifu katika uchumi wa viwanda. Maabara hizo zipo katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Mlingano Tanga, Taasisi ya Jiolojia Tanzania Dodoma, Taasisi ya Utafiti wa Tiba Kilimanjaro, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Mamlaka ya Viuatilifu na Afya ya Mimea Tanzania, Maabara ya Kitaifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi

Muhimbili, Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania na Kituo cha Jemolojia Tanzania.

80. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha mapendekezo kuhusu uanzishwaji wa Jukwaa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu baina ya Wizara za Kisekta (Inter-Ministerial STI Platform) ili kuimarisha uratibu sambamba na ufungamanishaji wa mipango, mikakati na juhudi nyingine za kuchochea mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, Serikali imeandaa Kongamano la eLearning Afrika lililofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 7 hadi 9 Mei, 2025 lililowaleta pamoja wadau kutoka nchi zaidi ya 65 za Afrika.

81. Mheshimiwa Spika, Vilevile, imewajengea uelewa wajumbe wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (Association of Local Authorities of Tanzania – ALAT) kuhusu uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa madawati ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kuimarisha ubainishaji wa bunifu na uwekezaji sambamba na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika ngazi ya halmashauri.

82. Mheshimiwa Spika, Serikali imezindua mfuko wa "SAMIA Innovation fund" wenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.3 utakaotoa mikopo nafuu kwa wabunifu kwa lengo la kuendeleza na kubiasharisha ubunifu pamoja na kutoa fursa za ajira kwa watanzania kupitia kazi za ubunifu. Mfuko ulizinduliwa na Mhe. Dkt. Dotto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

83. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imekamilisha Mkakati wa Kitaifa na Mpango wa Utekelezaji wa Kuhamasisha Ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) 2024/25 - 2029/30 katika shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu nchini. Sambamba na hatua hiyo, Serikali imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Ugharamiaji na Utoaji wa Motisha katika Masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa lengo la kuimarisha uwekezaji na hamasa kwa wadau katika masuala hayo.

84. Mheshimiwa Spika, Serikali, imeendelea kuhamasisha wasichana na wanawake kupenda fani na masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kwa kuandaa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi iliyoadhimishwa Dodoma tarehe 11 Februari, 2025 ambapo washiriki wapatao 2,000 walihudhuria.

85. Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kitaifa wa kurusha satelaiti katika anga za juu mzunguko wa chini (low earth orbit) kwa kusanifu satelaiti husika kwa kushirikiana na Kituo cha Anga za Juu - Japani (JAXA) kwa ajili ya matumizi ya utafiti na kusaidia uhifadhi wa mbuga za wanyama.

86. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa huduma kwa jamii ili kutatua changamoto mbalimbali kupitia taasisi za elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imehamasisha na kutoa mafunzo pamoja na ushauri kuhusu uongozi, uchumi wa vyama, uandaaji wa mipango mikakati ya vyama, uwekezaji katika vyama na elimu ya fedha kwa vyama na mtu binafsi kwa wadau 7,610 (wanaume 5,397 na wanawake 2,213) ili kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Aidha, imeendelea na utekelezaji wa kazi 10 za ushauri ambapo tatu (3) kati ya hizo zimekamilika na saba (7) zipo katika hatua mbalimbali za utekekezaj. Vilevile, imewajengea uwezo wanachama 216 kutoka Mkoa wa Tabora kuhusu utayarishaji wa taarifa za kifedha na mbinu bora za usimamizi wa fedha na biashara katika vyama vya ushirika na imetoa huduma za kijamii katika eneo la uchumi, elimu, sayansi na maendeleo ya jamii kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

(ii) imeendelea kutoa mafunzo, huduma za ugani na ushauri kwa jamii kwa wadau 1,572,390 ikiwemo wakulima, wafugaji, maafisa ugani, watafiti na wafanyakazi kutoka Serikalini na mashirika binafsi kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Aidha, imeendelea kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kupima jumla ya sampuli 1,704, kati ya hizo sampuli

1,253 za udongo, sampuli 297 za mimea, sampuli 8 za mbolea za viwandani, sampuli 135 za maji na sampuli 11 za mbolea ya mboji. Sampuli hizo zilitoka kwa wateja mbalimbali wakiwemo wakulima na watafiti;

(iii) imekamilisha jumla ya miradi 20 ya ushauri wa kitaalamu kupitia Ofisi ya Ushauri ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Aidha, imeendelea kutekeleza jumla ya miradi 51 ambayo imejikita katika usanifu majengo na usimamizi wa ujenzi, tathmini za athari za kijamii na mazingira na upimaji wa vifaa vya kujengea kama vile udongo na changarawe;

(iv) imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika maeneo yafuatayo: usanifu na usimamizi wa ukarabati wa maabara za sayansi, maktaba na maabara ya TEHAMA katika vyuo saba (7) vya Ualimu na ukarabati wa vyuo 20 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs); usanifu na usimamizi wa ujenzi wa vyuo vinne (4) vya VETA vya mikoa na vyuo vitatu (3) vya ualimu ambavyo ni Dakawa, Mhonda na Sumbawanga kupitia Chuo cha Ufundi Arusha; na

(v) imeendelea na utekelezaji wa miradi 53 ya kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kupitia Chuo Kikuu Ardhi kama ifuatavyo: usanifu na usimamizi wa ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) la ofisi za Mamlaka ya Tiba na Dawa Tanzania - Dodoma; usanifu na usimamizi wa ujenzi wa uwanja 'National Heroes Stadium' katika Mji wa Serikali Dodoma; usanifu na usimamizi wa ukarabati wa majengo ya biashara, nyumba ya uwekezaji, maisha house, NIC Kisutu, NIC Morogoro na kihonda appartments; Usanifu na usimamizi wa ujenzi wa karakana za TEMESA katika miji ya Dodoma na Geita; na usanifu wa jengo la ofisi na madarasa katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

87. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kudhibiti na kukuza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ujenzi wa maabara, ofisi na kinunurisho jumuishi (Mult Purpose Irradiator) katika eneo la Mbezi Msakuzi Dar

es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 41 ya Utekelezaji. Aidha, imekamilisha ujenzi wa ofisi na maabara za mionzi katika eneo la Nyegezi - Mwanza na Dunga Zuze – Zanzibar; na

(ii) imeshiriki katika Mkutano Mkuu wa 68 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 20 Septemba 2024 Jijini Vienna, Austria ambapo kupitia ushiriki huo, Tanzania imepata fursa ya kuwa sehemu ya miradi inayolenga kuongeza matumizi ya teknolojia ya nyuklia katika sekta ya afya, maji na kilimo ikiwemo mradi wa Atom for food.

88. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imepima uwepo wa mionzi kwenye jumla ya sampuli 26,349 za vyakula na mbolea kati ya sampuli 50,000 zilizolengwa. Kati ya hizo, sampuli 6,861 ziliiingia nchini, sampuli 18,892 zilisafirishwa nje ya nchi, sampuli 496 zilikuwa za mbolea na tumbaku na bidhaa zinginezo. Aidha, matokeo ya upimaji yalionesha kuwa sampuli hizo hazikuwa na madhara yoyote yatokanayo na mionzi;

(ii) imefanya upimaji wa uthibitisho wa ufanyaji kazi wa vifaa 62 ambapo vifaa 17 vilitoka Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania, Chrysos Corporation 12, Albizia Co Limited 2, Uganda 16, Tanzania Steel Pipe 2, PCS Energy Company 4, Stami Gold 1, Sunmaker 5, Aghakan health services 1 na Bulyankhulu goldmine 2;

(iii) imesajili jumla ya vyanzo vipya vya mionzi 66 na hivyo kuwezesha nchi kuwa na jumla ya vyanzo vya mionzi 1,637 vilivyosajiliwa;

(iv) imetoa vyeti 157 vya usajili kwa waliokidhi vigezo vya kusimamia utoaji wa mionzi kwa watu/wagonjwa, ufungaji, matengenezo, na uendeshaji wa vifaa vya mionzi;

(v) imetoa leseni 595 ikiwa ni sawa na asilimia 119 ya lengo ambapo orodha ya leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo; kumiliki

na kutumia vyanzo vya mionzi 493, kuingiza nchini vyanzo vya mionzi 67, utoaji wa vyanzo vya mionzi nje ya nchi 5, na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ndani ya nchi 30; na

(vi) imekagua jumla ya vituo 324 vinavyotumia vyanzo vya mionzi ikiwa ni sawa na asilimia 72 ya lengo la kukagua vituo 450, ambapo vituo 258 vilikuwa katika kanzidata na 66 vilikuwa vituo vipya.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

89. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, imeendelea kuratibu, kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu uanzishaji wa Kamati ya Kitaifa ya Kumbukumbu za Urithi wa Nyaraka wa Dunia itakayosimamia uingizaji wa kumbukumbu za nyaraka za Tanzania katika mfumo wa kidijiti wa Kumbukumbu za Urithi wa Dunia;

(ii) imetoa elimu kuhusu umuhimu wa hifadhi hai pamoja na kuheshimu mipaka kati ya vijiji na hifadhi kwa Wananchi wanaoishi maeneo yanayopakana na Hifadhi Hai za Mazingira ambazo ni Jozan Chwaka Bay na Ziwa Manyara;

(iii) imeratibu mafunzo kwa vikosi vya ulinzi vinavyoshiriki operesheni za ulinzi wa amani katika mataifa mbalimbali kwa lengo la kulinda nyara za kiutamaduni katika kipindi cha majanga ya kivita; na

(iv) imetoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya majukwaa ya habari katika kufikisha ama kupokea taarifa lengwa kwa waandishi na wadau wa habari 200 katika Mkoa wa Mwanza.

## C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 KWA FUNGU 46

90. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

(i) kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria na kuandaa miongozo ya utoaji wa elimu na mafunzo;

(ii) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali katika shule za sekondari na vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu;

iv) kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(v) kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia upatikanaji wa maendeleo endelevu. Katika hili, juhudi zaidi zitatumika kupeleka vijana wa Kitanzania kusomea mambo ya sayansi ya nyuklia, mambo ya kompyuta na akili-unde kwenye vyuo bora vilivyo nje ya nchi.

### a. Kuendelea na Utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria na Kuandaa Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo

91. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wadau wa elimu na umma kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa kwa kutoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule, walimu wa shule za msingi na sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, maafisa elimu, wakufunzi, na wahadhiri wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na taasisi za elimu ya juu.

92. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itakamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ili iendane na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023. Aidha, itakamilisha mapitio ya sheria katika taasisi ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Bodi ya Huduma ya Maktaba, Baraza la Taifa la Mitihani, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Taasisi ya Elimu Tanzania, Mamlaka ya Elimu Tanzania ili kuendana na sera pamoja na mikataba ya makubaliano ya kikanda na kimataifa.

93. Mheshimiwa Spika, Serikali itakamilisha zana mbalimbali za utekelezaji wa sera ikiwemo Mwongozo wa Upimaji na Tathmini katika Elimu, Mfumo wa Taifa wa Upimaji na Tathmini katika Elimu na Mfumo wa Taifa wa Mitaala kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa sera.

94. Mheshimiwa Spika, vilevile, itaendelea kuandaa na kuhuisha miongozo mbalimbali ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa na kusambaza mwongozo wa utekelezaji wa kiunzi cha mahitaji na usambazaji wa walimu ili kuimarisha msawazo wa walimu kulingana na mahitaji;

(ii) itaandaa mwongozo wa kitaifa wa kuwaendeleza kitaalamu wakufunzi na wafanyakazi wasio wakufunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) itaandaa mwongozo wa kitaifa wa ushirikiano baina ya viwanda na taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(iv) itaandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Utambuzi wa Ujuzi katika Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(v) itaandaa mwongozo wa kushughulikia masuala mtambuka katika taasisi 49 za elimu ya juu;

(vi) itaandaa mwongozo wa uanzishaji wa kampuni bunifu (spin-off companies) na vituo vya ubunifu wa teknolojia (TICs) kwa taasisi za elimu ya juu za umma na binafsi pamoja na taasisi za utafiti wa maendeleo (RDIs);

(vii) itahuisha miongozo na taratibu za udahili, upimaji na ithibati kwenye vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari na ufundi;

(viii) itahuisha mwongozo wa uanzishaji na usimamizi wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi;

(ix) itahuisha Mwongozo ya Uanzishaji na Usimamizi wa Programu ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; na

(x) itaandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Mwongozo wa Kutambua na Kuwaendeleza Wanafunzi wenye Vipaji na Vipawa.

**c. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Amali**

95. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utoaji wa elimu ya amali katika shule za sekondari nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania itawezesha upanuzi wa shule 55 za sekondari kuwa sekondari za amali.

96. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha elimu ya amali inatolewa kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014, Toleo la 2023, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya ualimu kwa kujenga miundombinu na kuweka vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida (K) na Chuo cha Ualimu Mtwara Ufundi (U) ili kuviwezesha vyuo hivyo kuwa vyuo vya mafunzo ya ualimu wa amali.

97. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuongeza fursa za mafunzo ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi

stadi) katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itasajili vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 100 ambapo vyuo vya elimu ya ufundi 30 (Technical Education Training Colleges) na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 70 (Vocational Education Training Centres), hivyo kuwa na jumla ya vyuo 504 vya elimu ya ufundi na vyuo 898 vya mafunzo ya ufundi stadi. Aidha, itasajili shule 100 za sekondari za ufundi;

(ii) itadahili wanafunzi 265,000 wa elimu ya ufundi na mafunzo na ufundi stadi ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi 190,000 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 75,000 sawa na ongezeko la asilimia 43 ikilinganishwa na udahili wa mwaka 2024/25; na

(iii) itatoa ithibati kwa vyuo 70 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi hivyo kuwa na jumla ya vyuo 370 vilivyopata ithibati ili kuthibiti ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivyo.

98. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya amali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya vyuo 64 vya ufundi stadi (VETA) vya wilaya na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe. Aidha, itaanza ujenzi wa vyuo vitano (5) vya ufundi (Polytechnics college) katika Mkoa wa Rukwa, Kigoma, Mtwara, Morogoro na Zanzibar;

(ii) itajenga hosteli tatu (3) katika vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali. Aidha, itakarabati miundombinu katika vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi;

(iii) itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma. Ujenzi huu utahusisha mabweni mawili (2) yenye

uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 kwa wakati mmoja, maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja, karakana mbili (2) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa wakati mmoja, ujenzi wa nyumba 10 za watumishi na ukuta kuzunguka chuo;

(iv) itaendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika Chuo cha Ufundi Arusha. Aidha, itakamilisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa vitendo na kufanya upanuzi wa maabara ya udongo ili kuongeza uwezo wa kuhudumia wanafunzi wengi zaidi kukabiliana na mahitaji katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(v) itaendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia na wanafunzi 1,536 (wanaume 768 na wanawake 768) katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume. Vilevile, itaanza ujenzi wa jengo la madarasa na ofisi za wafanyakazi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Karume. Aidha, itaendelea na ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi wa mihadhara katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Pemba;

(vi) itaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara utakaohudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kampasi ya Kivukoni; na

(vii) itaendelea na ujenzi wa ofisi ya makao makuu ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi - NACTVET ili kusogeza huduma za taasisi hizo katika Mji wa Serikali - Dodoma.

99. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kugharamia huduma ya chakula kwa wanafunzi 18,316 (Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya wanafunzi 800, Chuo cha Ufundi Arusha wanafunzi 790, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam wanafunzi 1,276, vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi wanafunzi 15,000 na

vyuo 10 vya Ufundi vya wanafunzi wenye mahitaji maalum wanafunzi 450). Vilevile itagharamia mafunzo kwa vitendo viwandani (Industrial Practical Training – IPT) kwa wanafunzi 2,085 (wanafunzi 873 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, wanafunzi 702 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na wanafunzi 510 wa Chuo cha Ufundi Arusha).

100. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuendeleza elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini, Serikali itaendelea kuimarisha ithibati na uthibiti katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi ili kusimamia ubora wa mafunzo ya amali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ili kuimarisha shughuli za uthibiti ubora wauendeshaji katika vyuo 504 vya elimu ya ufundi; vyuo 898 vya mafunzo ya ufundi stadi, vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi na shule za sekondari 131 zinazotoa elimu ya amali;

(ii) itahakiki mitaala 230 iliyokuzwa na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi soko la ajira;

(iii) itahuisha mfumo wa usajili na upimaji ili kujumuisha vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya maendeleo ya wananchi na shule za sekondari za ufundi; na

(iv) itaandaa miongozo 12 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs-ESPJ) katika taasisi zinazotekeleza maeneo ya vipaumbele.

101. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi ili Kuendana na Mahitaji ya Soko – Awamu ya Pili (Tanzania Education Labour Market Survey – TELMS II) utakaowezesha uanzishwaji wa vituo vya ujasiriamali, ubunifu na uhaulishwaji wa teknolojia. Aidha, vituo hivyo vitatoa mafunzo yatakayolenga kuendeleza na

kubiasharisha bidhaa zinazotokana na kazi za ubunifu katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar. Vilevile, itanunua vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo vifaa vya maabara na karakana za uhandisi katika taasisi hizo zinazotekeleza Mradi.

102. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Takwimu za Elimu ya Juu na Kati (Tertiary education Management Information System - TEMIS) ili uwezeshaji kufuatilia wahitimu wa elimu ya ualimu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu kwa lengo la kubaini uhusiano wa ujuzi waliopata wahitimu na soko la ajira.

103. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa vifaa na zana vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuimarisha ufundishaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya VETA 98, vyuo 54 vya Maendeleo vya Wananchi na Chuo cha Ufundi Dodoma;

(ii) itanunua vifaa vya kisasa vitakavyotumika katika maabara ya udongo, maji na mimea kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo kwa vitendo, uzalishaji na ushauri wa kitaalam kupitia Chuo cha Ufundi Arusha;

(iii) itanunua zana, vifaa na mashine katika kituo cha mafunzo Kikuletwa - Chuo cha Ufundi Arusha (ATC); na

(iv) itaendelea na ununuzi na kuweka vifaa tiba katika kituo cha afya katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa programu ya vifaa tiba na kutoa huduma za afya kwa wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo jirani.

104. Mheshimiwa Spika, Serikali pia itachapa na kusambaza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo

ya Ufundi Stadi, Kiunzi cha Ulinganifu wa Sifa za Kitaaluma na Mkakati wa Ugharamiaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

105. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwaendele kitaalamu na kitaaluma wakufunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya maendeleo ya wananchi pamoja na walimu wa shule za sekondari za amali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kwa walimu 1,000 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu tathmini ya mitaala ya umahiri (Competency Based Education and Training-CBET) ili kuwawezesha walimu kufundisha na kufanya tathmini ya wanafunzi kwa kuzingatia umahiri;

(ii) itatoa mafunzo kwa watumishi 26,000 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kuhusu mbinu za ufundishaji, upimaji na tathmini, pamoja na uthibiti na ithibati ya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; na

(iii) itatoa mafunzo kwa wahandisi watano (5) kutoka makao makuu ya Wizara na vyuo vya maendeleo ya wananchi katika utekelezaji wa uendeshaji wa shughuli za Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi kwa Ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi.

106. Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Kituo cha Magonjwa ya Moyo – Mloganzila kwa kuongeza miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji.

**d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu**

107. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu ya awali ili kumuandaa mwanafunzi kujiunga

na ngazi ya elimu ya msingi kulingana na miongozo na taratibu kwa kutoa elimu kwa wadau kuhusu kiunzi cha elimu ya awali.

108. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa za elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itasajili shule za msingi na sekondari takribani 785 ambapo awali pekee 32, awali na msingi 482 (Serikali 318 na zisizo za Serikali 164), sekondari 270 (Serikali 211 na zisizo za Serikali 59), chuo cha ualimu kimoja cha binafsi; na

(ii) itafanya ubainishaji wa shule 60 zenye walimu wa kigeni na kuhakiki sifa zao. Aidha, itafanya uhakiki katika shule 100 (msingi 60 na sekondari 40) zilizosajiliwa kwa masharti na kufanya ufuatiliaji katika shule 200 (msingi 100 na Sekondari 100) zilizosajiliwa kwa ajili ya kuhuisha usajili.

109. Mheshimiwa Spika, miundombinu bora ni muhimu katika kuboresha na kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi, sekondari na ualimu, kwa kutambua umuhimu huo Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu katika taasisi hizo kama ifuatavyo:

(i) itawezesha ujenzi wa madarasa 2,730 (shule za msingi 949 na sekondari 1,781) na mabweni 140 ili kuwezesha utekelezaji wa mpango wa elimu ya msingi ya lazima kwa miaka 10.

(ii) itakarabati nyumba 20 za walimu (vyuo vya ualimu 10 na vyuo vya maendeleo ya wananchi 10). Aidha, itakarabati baadhi ya majengo katika vyuo vya ualimu nane (8) ambavyo ni Ilonga, Nachingwea, Morogoro, Bustani, Korogwe, Tukuyu, Vikindu na Bunda. Vilevile, itaanza ujenzi wa nyumba tatu (3) za wakufunzi katika chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa;

(iii) itachimba visima nane (8) vya maji katika vyuo vya ualimu ambavyo ni Sumbawanga, Bunda, Shinyanga, Mpwapwa, Songea, Tabora, Mandaka na Tarime; na

(iv) itagharimia mafunzo kwa vitendo na huduma ya chakula kwa wanafunzi 15,750 wa vyuo 34 vya ualimu vya Serikali.

110. Mheshimiwa Spika, huduma ya uthibiti ubora wa elimu katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ni muhimu katika kuhakikisha elimu inayotolewa katika taasisi hizo inazingatia taratibu na miongozo inayotolewa na Wizara. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za uthibiti ubora kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 6,962 (shule za awali na msingi 5,527 sekondari 1,260, vyuo vya ualimu 72, vyuo vya maendeleo ya wananchi 53, na vituo 50 vya elimu ya watu wazima na mafunzo nje ya mfumo rasmi kwa lengo la kubaini ubora, hali ya uandikishaji, ufundishaji, usimamizi na uongozi shuleni na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo; na

(ii) itafanya ziara za ufuatiliaji kwa taasisi 1,260 (15%) zilizotembelewa katika tathmini ya jumla mwaka 2024/25 katika shule za awali na msingi 683, shule za sekondari 563, vyuo vya ualimu tisa (9) na vyuo vya maendeleo ya wananchi vitano (5) na kutoa ushauri kwa walimu wa masomo.

111. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha ofisi za uthibiti ubora wa shule ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wathibiti ubora wa shule kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itajenga na kukarabati miundombinu (ofisi na uzio) katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule zifuatazo; Ifakara, Bukoba, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Halmashauri ya Mji Kasulu, Chalinze, Chato, Songea, Handeni, Nzega, Ileje, Longido, Mafia, Halmshauri ya Wilaya Morogoro na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga; na

(ii) itanunua magari mawili (2) kwa ajili ya Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule za halmashauri ya Wilaya ya Karagwe na Nzega kwa lengo la kuwezesha Wathibiti Ubora wa Shule kuzifikia shule kwa ajili ya kufanya tathmini ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

112. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutambua na kukuza kazi za uandishi bunifu ili kuendelea kuibua waandishi wa fasihi ya kitanzania, kuongeza machapisho na kukuza tabia ya usomaji katika ngazi mbalimbali za elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa lengo la kuwatambua na kuwazawadia waandishi mahiri wa kazi za fasihi; na

(ii) itaendelea kuratibu shindano la uandishi wa insha kwa Nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari.

113. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu vya elimu awali, msingi, sekondari na ualimu ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa elimu ya msingi darasa la tano, sekondari mkondo wa jumla kidato cha pili, sekondari mkondo wa amali kidato cha tatu na kidato cha sita kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) itaandaa maudhui ya kieletroniki kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na kuwajengea walimu uwezo wa kufundisha kwa kutumia teknolojia kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia; Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu vya elimu awali, msingi, sekondari na ualimu ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(iii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa elimu ya msingi darasa la tano, sekondari mkondo wa jumla kidato cha pili, sekondari mkondo wa amali kidato cha tatu na kidato cha sita kwa ajili ya wanafunzi wenye

uoni hafifu na wasioona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(iv) itaandaa maudhui ya kieletroniki kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari na kuwajengea walimu uwezo wa kufundisha kwa kutumia teknolojia kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia;

(v) itachapa na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 kwa shule 20,000 na vyuo vya ualimu 34;

(vi) itachapa na kusambaza vitabu 3,500,000 vya masomo ya ufundi, sayansi na hisabati kwa Kidato cha 1, 2, 4 na 6;

(vii) itaandaa vitabu vya masomo ya hisabati na sayansi Kidato cha Pili katika mfumo wa kidijiti;

(viii) itachapa vitabu vya masomo ya awali ya ufundi (pre-vocational subjects) na moduli kwa wanafunzi wapya wa Mpango wa Elimu kwa njia Mbadala; na

(ix) itatathmini miswada ya vitabu na vifaa vya kielimu vinavyowasilishwa na wadau mbalimbali kwa lengo la kutumika katika shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha kuwa vifaa na machapisho husika yanaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya kielimu na maadili ya nchi yetu na itaendelea kununua na kusambaza vitabu katika maktaba 15 za jamii.

(x) itachapa na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuendana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 kwa shule 20,000 na vyuo vya ualimu 34;

(xi) itachapa na kusambaza vitabu 3,500,000 vya masomo ya ufundi, sayansi na hisabati kwa Kidato cha 1, 2, 4 na 6;

(xii) itaandaa vitabu vya masomo ya hisabati na sayansi Kidato cha Pili katika mfumo wa kidijiti;

(xiii) itachapa vitabu vya masomo ya awali ya ufundi (pre-vocational subjects) na moduli kwa wanafunzi wapya wa Mpango wa Elimu kwa njia Mbadala; na

(xiv) itatathmini miswada ya vitabu na vifaa vya kielimu vinavyowasilishwa na wadau mbalimbali kwa lengo la kutumika katika shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha kuwa vifaa na machapisho husika yanaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya kielimu na maadili ya nchi yetu na itaendelea kununua na kusambaza vitabu katika maktaba 15 za jamii.

114. Mheshimiwa Spika, mafunzo endelevu ni muhimu katika kuendeleza taaluma na kuimarisha utendaji kazi wa walimu, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu nchini. Hivyo, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itatoa mafunzo kwa walimu 13,784, maafisa elimu 488, wathibiti ubora 544, wakufunzi 100, wanafunzi 5,172 na walezi 100 wa skauti katika maeneo mbalimbali ikiwemo usawa wa kijinsia, masomo ya biashara na ufundi, ufundishaji wa elimu ya awali, utawala bora na menejimenti ya elimu, ushauri na unasihi, pamoja na utoaji wa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

115. Mheshimiwa Spika, Serikali, pia itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango na miongozo inayotolewa na Wizara ili kuhakikisha elimu ya msingi, sekondari inatolewa kwa ufanisi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;

(ii) itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa Kuwarejesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari shuleni;

(iii) itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa kwa shule za msingi, sekondari na vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi; na

(iv) itafanya ufuatiliaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilivyotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za Msingi 1,260 na Sekondari 45.

116. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji katika afua zinazopangwa na kutekelezwa kupitia miradi na programu mbalimbali inayotekelezwa katika ngazi zote za elimu ikiwemo ujenzi, ukarabati, mafunzo, uandaaji na uhuishaji wa mifumo, miongozo na nyaraka zingine za usimamizi wa utoaji wa elimu zinakuwa na thamani ya fedha iliyotarajiwa.

117. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafunzo ya uongozi na usimamizi wa elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi nchini itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tafiti tatu (3) katika maeneo ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa lengo la kutatua changamoto zinazojitokeza katika uongozi na usimamizi wa elimu nchini;

(ii) itatoa huduma ya ushauri wa kitaalamu kwenye maeneo sita (6) katika uongozi, usimamizi na uthibiti ubora wa shule ili kuwajengea uwezo wa kusimamia utoaji wa elimu; na

(iii) itaanza ujenzi wa ukumbi mtambuka katika Wakala wa Maendeleo ya Elimu- ADEM.

118. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza fursa za elimu kupitia vituo mbalimbali vya utoaji wa elimu kwa njia mbadala ili kuhakikisha kila mwanafunzi anakamilisha mzunguko wa elimu na kuimarisha huduma ya usimamizi wa elimu nchini, katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo:

(i) itawawezesha wasichana 3,000 walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali kupata elimu ya sekondari kwa njia mbadala;

(ii) itafanya utafiti wa kitaifa kuhusu hali ya kisomo na elimu kwa umma utakaoboresha utekelezaji wa mkakati wa kisomo na elimu kwa umma;

(iii) itatoa fursa za mafunzo ya kuwajengea ujuzi vijana walio nje ya shule kupitia Mpango wa Elimu Changamani (IPOSA) kutoka vijana 6,500 kwa mwaka 2024/25 hadi vijana 22,500 kwa mwaka 2025/26;

(iv) itaendesha Mitihani ya majaribio kwa wanafunzi waliopo katika vituo 191 vya Elimu kwa njia mbadala, ikiwemo wasichana walio katika mazingira magumu hatua ya I. Vilevile, itaendesha Tathmini ya Kitaifa ya Kidato cha Pili (NFTA) kwa wanafunzi 1,600 wa Elimu kwa njia Mbadala walio katika mazingira magumu;

(v) itaongeza fursa za utoaji wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 11,762 kwa mwaka 2024/25 hadi 15,000 kwa mwaka 2025/26; na

(vi) itajenga ofisi na madarasa katika mikoa ya Dodoma, Mbeya, Katavi na Mara na kufanya ukarabati wa miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika mikoa wa Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro.

119. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 2,000 watakaosoma Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum na kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu ikiwa ni moja ya jitihada ya kuondoa vikwazo vya kimfumo kwa kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji, mafunzo, uandaaji wa miongozo kwa ngazi zote za elimu.

120. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upimaji na tathmini ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Taifa itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea na upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,993,040 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Oktoba, 2025;

(ii) itaendelea na Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 1,086,107 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2025;

(iii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,339,988 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2025;

(iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 588,409 wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo mwezi Novemba, 2025;

(v) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 133,973 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2026;

(vi) itaendesha Mtihani wa Diploma ya Ualimu kwa watahiniwa 10,840 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2026;

(vii) itaendesha Upimaji wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi 1,998,400 wanaotarajiwa kufanya upimaji wa Darasa la Pili mwezi Oktoba, 2025;

(viii) itaongeza uwezo wa kuchapa Mitihani kwa kununua na kusimika mashine ya kisasa ya uchapaji na kuandaa Kiunzi cha Upimaji cha Taifa; na

(ix) itawajengea uwezo walimu 550 katika utekelezaji wa tathmini ya ndani ya shule.

121. Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza utekelezaji na uendeshaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ili kuhakikisha walimu wanaohitimu katika vyuo vinavyotoa mafunzo ya elimu ya ualimu vinavyotambulika na Serikali wanapata usajili utakaowawezesha kutambulika ndani na nje ya nchi pamoja na kuendeleza utaalamu wao. Aidha, bodi itawezesha usajili na uendelezaji wa

walimu wote walioajiriwa katika shule za Serikali na zisizo za Serikali.

122. Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itaboresha miundombinu katika vyuo vya ualimu nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaanza ujenzi wa nyumba tatu (3) za wakufunzi katika chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa. Vilevile, itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu katika chuo cha ualimu Mpwapwa na Kleruu;

(ii) itaanza ujenzi wa jengo la utawala katika vyuo vya ualimu vifuatavyo: Tarime, Kinampanda, Kitangali, Mpuguso, Shinyanga na Ndala na ujenzi wa miundombinu ya michezo katika chuo cha ualimu Dakawa na Butimba na mabweni ya wasichana katika vituo viwili vinavyotoa elimu kwa njia mbadala; na

(iii) itanunua na kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo 34 vya ualimu vya Serikali na itanunua na kusambaza vifaa vya maabara katika vyuo 13 vya ualimu vya Serikali.

123. Mheshimiwa Spika, itaratibu mashindano ya walimu kuhusu njia mbalimbali za ujifunzaji na ufundishaji kwa walimu wa sayansi wa sekondari na masomo mbalimbali katika shule za msingi kwa lengo la kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazosisitizwa katika mtaala ulioboreshwa. Aidha, mashindano haya ni njia mojawapo ya kutoa motisha kwa walimu katika kutumia mbinu sahihi za ufundishaji na ujifunzaji.

124. Mheshimiwa Spika, Serikali itawezesha ushiriki wa vijana wa rika balehe kushiriki mkutano wa pamoja kati ya Serikali na wadau na maadhimisho ya siku ya wasichana na wanawake katika sayansi yanayoadhimishwa kila mwaka Februari 11.

125. Mheshimiwa Spika, Serikali itaandaa Mpango wa Sekta ya Elimu wa Kukabiliana na Majanga na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, itazitambua shule zilizokabiliwa na majanga na zile

ambazo zipo kwenye hatari ya kukumbwa na majanga na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo.

126. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa elimu jumuishi na elimu kwa watu wazima kwa lengo la kujenga uelewa kwa watanzania kuhusu fursa mbalimbali za elimu zilizopo kwa makundi yote katika jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa elimu kwa wadau kuhusu Mwongozo wa Ujumuishi wa Matumizi ya Kidijiti katika Shule na Vyuo vya Ualimu; na

(ii) itajenga uelewa kuhusu haki na wajibu wa watu wenye ulemavu kupitia Maadhimisho ya siku ya watu wenye ulemavu duniani, wiki ya viziwi, siku ya fimbo nyeupe kwa wasioona, na siku ya breli na wenye ualbino.

127. Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya utafiti wa utekelezaji wa Mwongozo wa Urejeshaji wa Wanafunzi Shuleni. Utafiti huu utalenga kubaini changamoto zinazojitokeza katika mchakato wa urejeshaji wa wanafunzi waliokatisha masomo, athari chanya za utekelezaji wake, pamoja na mapendekezo ya kuboresha utekelezaji wa mwongozo huo.

128. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itafanya maadhimisho ya juma la elimu ya watu wazima kitaifa na itaendelea kuwezesha ushiriki katika michezo kwa wanafunzi wa vyuo vya ualimu, vyuo vya maendeleo ya wananchi na wafanyakazi kupitia Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA), Umoja wa Michezo wa Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) na Shirikisho la Vyama vya Michezo vya Shule za Sekondari Afrika Mashariki - FEASSA.

**e. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu**

129. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za Elimu ya Juu nchini kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuratibu udahili wa wanafunzi 150,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kujiunga na programu mbalimbali za masomo katika vyuo vya elimu ya juu;

(ii) itakagua asasi 10 zinazoratibu wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili zitakazokidhi vigezo au kuhuisha usajili. Aidha, itafanya tathmini ya maombi ya wanafunzi wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vikuu nje ya nchi kwa lengo la kuwapatia uhakika kwamba vyuo wanavyotaka kujiunga vina ithibati za mamlaka husika;

(iii) itakagua ubora wa vyuo vikuu 25 na kufanya tathmini ya mitaala 400 ya vyuo vikuu kwa lengo la kuipatia au kuhuisha ithibati kuendana na mahitaji ya soko la ajira;

(iv) itaanzisha programu mpya tatu (3) za kikanda zenye hadhi ya kimataifa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kampasi kuu na kampasi ya Mwanza. Programu hizo ni Bachelor of Engineering in Cyber Security, Bachelor of technology and laboratory science na Diploma in Leather Processing and Allied Technologies; na

(v) itafanya tathmini ya utambuzi wa maombi ya tuzo 5,000 za wahitimu zilizotolewa katika vyuo vikuu vya nje na kuzitambua zitakazokidhi vigezo.

130. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kutoa mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wenye sifa ili kuongeza fursa za elimu ya juu nchini kama ifuatavyo:

(i) itaongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu kutoka 245,314 mwaka 2024/25 hadi wanafunzi 252,773 (mwaka wa kwanza 88,320 na wanaoendelea 164,453) mwaka 2025/26;

(ii) itaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi 10,000 wa ngazi ya stashahada katika fani za kipaumbele ikiwemo Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;

(iii) itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 2,630 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi kupitia SAMIA Skolashipu ambapo kati ya hao wanafunzi wa mwaka wa kwanza 1,220, shahada za umahiri 80 na wanafunzi wanaoendelea 1,330; na

(iv) itaendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi hususan wanafunzi wa kike waliohitimu mitihani ya kitaifa ya kidato cha sita na shahada za awali kupitia Chuo Kikuu Dar es Salaam.

131. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mikopo iliyoiva yenye thamani ya Shilingi bilioni 210.2 kutoka sekta za umma, binafsi na zisizo rasmi kwa kuwatambua wanufaika wapya 40,000 na kufanya ukaguzi kwa waajiri 8,000 kuhusu umuhimu wa utii wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

132. Mheshimiwa Spika, Serikali itakamilisha mapitio ya tathmini ya majukumu na muundo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (Higher Education Students' Loans Board–HESLB) ili kutengeneza taasisi itakayowezesha uwepo wa uendelevu wa kutoa mikopo ya elimu ya juu kulingana na mahitaji.

133. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) itaendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(ii) itaendelea na upanuzi wa Hosteli za wanafunzi na uwekaji wa samani katika Hosteli ya Dkt. J.P.J. Magufuli (Blocks A na E) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iii) itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Magonjwa ya Moyo (Awamu ya II) katika Kituo cha Taaluma ya Afya cha Mloganzila;

(iv) itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuhudumia watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja pamoja na ujenzi mpya wa hosteli ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; na

(v) itaanza ujenzi na ukarabati na utoaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Elimu ya Juu - Zanzibar kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania.

134. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu katika Taasisi za Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itakamilisha jengo la kiwanda cha kufundishia katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na itaendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 katika Taasisi hiyo;

(ii) itakamilisha ujenzi wa majengo yafuatayo: jengo maalum la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STI) lenye maeneo matatu (3) ya atamizi litakalohudumia watumiaji 100; Kituo kimoja (1) cha Ubunifu chenye uwezo wa kuhudumia watu 150; maabara moja (1) ya Kifani "Prototyping" yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 50; chumba kimoja (1) kwa ajili ya makumbusho ya kisayansi chenye uwezo wa kuhudumia watu 200; chumba kimoja (1) cha maktaba chenye uwezo wa kuhudumia watu 50; chumba kimoja (1) cha Server; vyumba viwili (2) vya mikutano vyenye uwezo wa kuhudumia watu 400;

(iii) itakamilisha ukarabati wa majengo ya Tume ya Sayansi na Teknolojia; na ununuzi wa vifaa katika majengo husika; na

(iv) itaanza ukarabati katika vituo viwili (2) vya Umahiri na Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia (CEITT) ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya – (MUST).

135. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati katika taasisi 19 za elimu ya juu zinazotekeleza Mradi wa Elimu ya

Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi. Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa kumbi za mihadhara, madarasa, hosteli na ofisi.

136. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuendeleza elimu ya juu ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za Elimu ya Juu, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kukuza na kubiasharisha Lugha ya Kiswahili. Vilevile, itatoa ufadhili kwa wanafunzi wawili (2) raia wa Oman na wanafunzi watano (5) raia wa Hangaria kusoma katika vyuo vikuu vya hapa nchini kulingana na mikataba na utaratibu. Vilevile, itaimarisha uhusiano wa kiutendaji kati ya taasisi 15 za elimu ya juu na sekta binafsi/viwanda ili kuwezesha wanafunzi kupata nafasi za kujifunza kwa vitendo.

137. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na kuongeza idadi ya wanataaluma wenye sifa kwa kuwajengea uwezo watumishi wa taasisi za elimu ya juu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kuwawezesha watumishi 1,834 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi takribani 578 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya uzamivu na shahada ya umahiri.

138. Mheshimiwa Spika, vilevile, itaendelea kuimarisha Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati na maendeleo ya TEHAMA kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma ndaki ya Elimu. Vilevile, itaendelea kuadhimisha Wiki ya Elimu Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi zinazotekezwa na Wizara.

139. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwezesha taasisi 17 za elimu ya juu kutumia Teknolojia kidigiti katika kufundishia na kujifunzia pamoja na mifumo ya usimamizi na utoaji wa huduma. Aidha, itatengeneza mfumo wa kufundishia mtandaoni na kuandaa programu za ufundishaji kwa njia ya kielektroniki na kuboresha miundombinu ya mawasiliano, teknolojia na habari pamoja na elimu katika nyanja hiyo kwa wafanyakazi.

140. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi na walimu katika taasisi za elimu ya juu ikiwa ni jitihada za kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo vinavyoondoa usawa katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ushiriki wa viongozi wa elimu 420, watumishi 30, wanafunzi wenye ulemavu 20 na wasio na ulemavu 370 kutoka taasisi 10 za elimu ya juu kushiriki kongamano kuhusu elimu jumuishi ili kuongeza uelewa wa elimu jumuishi kwa jamii;

(ii) itatoa mafunzo kuhusu usaidizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum 205, wakutubi 19 na maafisa TEHAMA 19 kutoka taasisi za elimu ya juu;

(iii) itaimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kugharamia ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi 51 pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma ili kuhakikisha kuwa watu wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa za elimu; na

(iv) itatoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia saidizi kwa wanafunzi 100 na watumishi 35 wenye mahitaji maalum katika taasisi 19 za elimu ya juu.

141. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha masuala mtambuka ikiwemo mazingira, masuala ya kijinsia na elimu ya afya katika taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatoa mafunzo kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kwa washiriki 5,450 kutoka taasisi za elimu ya juu;

(ii) itawezesha mafunzo kwa taasisi 20 za elimu ya juu kuhusu masuala ya usalama wa mazingira na kijamii ili kuongeza uelewa wa utunzaji wa mazingira; na

(iii) itaendelea kuwezesha ushiriki katika michezo kwa wanafunzi na wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu kupitia

Shirikisho la Michezo Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (SHIMIVUTA) na Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma (SHIMUTA).

141. Mheshimiwa Spika, Serikali, itaendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Elimu ya Juu 2050 itakayotoa mwongozo wa mfumo wa elimu ya juu kulingana na mahitaji ya nchi.

**f. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchangia Upatikanaji wa Maendeleo Endelevu.**

143. Mheshimiwa Spika, ili kuendana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia na ubunifu kikanda na kimataifa, Serikali itaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996) ili kuwa na sera inayoakisi hali halisi na mahitaji ya sasa katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Vilevile, itafanya tathmini ya Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo 2010, Sera ya Taifa ya Bioteknolojia 2010 na Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia 2013 ili kubaini hali halisi ya utekelezaji wa sera hizo;

144. Mheshimiwa Spika, wabunifu na kazi za ubunifu ni chachu katika kuzalisha teknolojia mpya, kutatua changamoto za kijamii na kuchangia katika maendeleo ya nchi. Katika kutambua umuhimu huo, Serikali itaendelea kuwabaini na kuwaendeleza wabunifu wa kitanzania katika nyanja za sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kuratibu na kuwezesha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

145. Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali itaanza utekelezaji wa mfuko wa "SAMIA Innovation Fund" wenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.3 utakaotoa mikopo nafuu kwa wabunifu kwa lengo la kuendeleza na kubiasharisha ubunifu pamoja na kutoa fursa za ajira kwa watanzania kupitia kazi za ubunifu.

146. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa kazi za watafiti na kukuza ushindani wa kitaaluma, Serikali itaendelea kutoa tuzo yenye thamani ya Shilingi milioni 50 kwa utafiti utakaochapishwa katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa ili kuwahamasisha watafiti na wabunifu kuchapisha na kusambaza

matokeo ya kazi zao na kuweza kutumika na wananchi, watunga sera na watoa maamuzi kwa maendeleo endelevu.

147. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mara ya kwanza itatoa ufadhili kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika matokeo ya kidato cha sita kwenye mchepuo wa masomo ya Sayansi ili waweze kujiunga na masomo katika ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vikuu mahiri duniani kusomea taaluma za Data Science ikiwemo Artificial Intelligence (AI), Machine Learning (ML) na sayansi za mwelekeo huo. Program hiyo itaitwa Mama Samia Scholarship Extended for Data Science, Artificial Intelligence (AI) and Allied Sciences (Mama Samia 360 – DSP/AI+).

148. Mheshimiwa Spika, Lengo la programu ya Mama Samia 360 – DSP/AI+ ni kutengeneza wataalam mahiri katika masuala ya Data Science ili waweze kushindana na kufanya kazi popote duniani. Mkakati wa utekelezaji umegawanyika katika ngazi tatu kama ifuatavyo:

(i) Ngazi ya kwanza ni kuwajengea uwezo vijana waliomaliza kidato cha sita kupitia kambi maalum (Preparatory Camp) ili kuwaandaa kujiunga na vyuo vikuu mahiri duniani katika taaluma za Data Science kwa kupewa mafunzo na wataalam wabobezi kutoka sekta binafsi na wataalam wazawa wanaoishi nje ya nchi (diaspora). Mafunzo hayo yatatolewa kwa takribani miezi 10 na yatahusu: kujenga msingi katika matumizi ya kompyuta, programming na uchambuzi wa mifumo; soft skills ikiwa ni pamoja na uongozi; ufanisi wa lugha; uzalendo; na utamaduni wa nchi watakazokwenda kusoma. Aidha, washiriki watapata cheti cha ushiriki chenye hadhi ya kimataifa;

(ii) Ngazi ya pili ni kuwezesha vijana (waliopitia kambini) kupata udahili katika vyuo vikuu mbalimbali duniani na kuwasaidia kutafuta skolashipu katika sehemu mbalimbali;

(iii) Ngazi ya tatu ni kutoa ufadhili kwa vijana wenye Shahada ya Kwanza kwenda kuongeza ubobezi kupitia Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Indian Institute of Science and Technology kampasi ya Zanzibar.

149. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza nia ya kuongeza wataalamu wabobezi katika nyanja ya sayansi na teknolojia ya nyuklia, Serikali kupitia SAMIA Extended Skolashipu itaendelea kutoa ufadhili kwa Watanzania wenye ufaulu wa juu katika fani za Sayansi na Teknolojia ya Nyuklia kwa ngazi ya shahada ya kwanza ili kuweza kujiunga na masomo ya shahada za juu.

150. Mheshimiwa Spika, tafiti ni nyenzo muhimu katika kuongeza maarifa mapya, kuchochea maendeleo ya uchumi na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii. Serikali kwa kutambua umuhimu huo itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya kitaifa ya utafiti na ubunifu ili kuongeza ufanisi katika kazi za ubunifu na ubiasharishaji wa teknolojia na bidhaa zenye mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda;

(ii) itaimarisha kazi za utafiti katika taasisi za elimu ya juu na taasisi za kitafiti kwa kuendelea na miradi ya tafiti 130 na kuanza miradi mipya ya utafiti 155 katika maeneo ya kimkakati ikiwemo elimu, sayansi, teknolojia, ardhi, mazingira, mazao ya kilimo, sayansi ya jamii, uongozi, biashara, afya, misitu na uvuvi; na

(iii) itaendelea kuimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika kutatua changamoto za afya.

151. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha nchi inaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani pamoja na kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) itakamilisha mapitio ya Muundo wa Tume ya Taifa ya Sayansi naTeknolojia (COSTECH) kwa lengo kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa Tume hiyo na kuongeza mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(ii) itaendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA inayounganisha taasisi za Maendeleo ya Utafiti, Taasisi za Elimu ya Juu na mifumo ya uratibu wa utafiti na ubunifu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia;

(iii) itaendelea kufadhili tafiti 40 (mabadiliko ya tabia nchi 19 na uzalishaji wa viwanda 21) ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kuimarisha uwezo wa Taifa katika maendeleo ya viwanda, uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla;

(iv) itaendelea kugharamia vigoda viwili (2) vya utafiti pamoja na vituo vya umahiri katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili kuendelea kujenga mtandao wa kitaaluma katika maeneo husika; na

(v) itaendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Teknolojia 2050 inayojumuisha maeneo ya elimu, lugha, mawasiliano, maliasili, biashara, afya, kilimo, mifugo, uvuvi, haki za binadamu na maendeleo ya watu na TEHAMA ili kuimarisha mwelekeo wa kimkakati wa kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini.

152. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usambazaji wa maarifa, uhamasishaji wa mijadala ya kitaaluma na kuhakikisha matokeo ya kazi za utafiti yanatumika katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi kwa maendeleo endelevu ya Taifa, Serikali itachapisha machapisho 135 ya kitaaluma katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kueneza matokeo ya tafiti kwa jamii pamoja na kuandaa jarida la uongozi kwa lengo la kuongeza ujuzi kwa jamii. Aidha, itaongeza idadi ya majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 24 hadi kufikia 28.

153. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa kazi za ubunifu zinazofanywa na wabunifu wetu katika kuleta maendeleo yao na taifa kwa ujumla. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wa ndani ili kuimarisha kazi zao pamoja na

kuwaunganisha na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kukuza ubunifu wao kufikia hatua ya kuingizwa sokoni na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuboresha maisha yao kwa ujumla;

(ii) itawezesha idadi ya bunifu na teknolojia 13 zilizoendelezwa kuingia sokoni na hivyo kuongeza idadi ya bunifu na teknolojia zilizoingia sokoni kutoka 42 hadi 55;

(iii) itafanya ufuatiliaji wa ubunifu ulioendelezwa na ulioainishwa kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU);

(iv) itaboresha na kuongeza mahusiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi ili kuleta tija katika tafiti na shughuli mbalimbali za maendeleo; na

(v) itaendelea kuimarisha majukwaa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika ngazi ya Halmashauri.

154. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza maarifa ya watanzania ya utatuzi wa changamoto na kuongeza tija katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali kupitia Taasisi za elimu ya juu na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia itaendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itatekeleza miradi mipya 21 ya huduma za ushauri wa kitaalamu itakayowezesha kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa wadau takribani 2,000,000 katika nyanja za elimu, kilimo, utafiti, TEHAMA, mazingira, uongozi, udongo, kokoto na lami, maji, usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi na afya kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio ili kuongeza uzalishaji wenye tija;

(ii) itatoa huduma ya ushauri wa kitaalumu katika meneo matano (5) na kuanzisha mahusino na viwanda vitatu (3) ili kuimarisha uwezo wa rasilimaliwatu katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; na

(iii) itaendelea kutoa elimu ya ushirika ili kuchochea ari ya maendeleo ya sekta ya ushirika na jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika; Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania na Vyama vya Ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

155. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini kupitia Tume ya Nguvu za Atomu ili kudhibiti matumizi ya mionzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itakagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuimarisha usalama wa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla;

(ii) itapima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira ya vyanzo vya mionzi kwa lengo la kuwakinga na madhara yatokanayo na vyanzo vya mionzi sehemu za kazi;

(iii) itasimamia kituo maalumu cha kupima hewa katika anga kwa lengo la kuthibiti uchafuzi unaotokana na mionzi ili kuhakikisha hali ya usalama wa hewa katika anga;

(iv) itaendelea kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kwa lengo la kuhakikisha kuwa mabaki hayo yanadhibitiwa ili kuepusha madhara ya kiafya na kimazingira na kuiweka nchi katika hali ya usalama wa mionzi kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa; na

(v) itaendelea na ujenzi wa maabara za kanda za Tume ya Nguvu za Atomu katika Mkoa wa Mbeya na Mtwara kwa lengo la kusogeza huduma za udhibiti wa mionzi na teknolojia ya nyuklia kwa wananchi. Aidha, itaendelea na ujenzi wa maabara, ofisi na kituo cha mionzi katika kanda ya Dar es Salaam.

156. Mheshimiwa Spika, ili kuleta tija na ufanisi katika kukabiliana na tatizo la saratani nchini, Serikali itaendelea na utekelezaji wa

mradi wa kituo cha utafiti cha tiba za saratani na itaendelea kufanya utafiti na uchunguzi kwa kutumia teknolojia ya nyuklia.

**E. MPANGO WA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

157. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itaendelea kuratibu, kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa maeneo ya urithi wa dunia ili kuhakikisha kuwa maeneo yaliyopo katika orodha ya UNESCO pamoja na yale yanayotarajiwa kuingizwa yanaendelea kuhifadhiwa katika hali yake ya uasili na kuendelea kuzingatia vigezo vilivyowekwa na UNESCO;

(ii) itaendelea kuwa mjumbe kwenye kamati za kimkakati za UNESCO ili kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kulinda maslahi ya nchi katika duru za kimataifa;

(iii) itaongeza idadi ya maeneo ya urithi wa Dunia yanayotambuliwa na UNESCO kwa lengo la kuitangaza Tanzania na vivutio vyake vya asili kimataifa ili kukuza utalii wa kiutamaduni kutokana na vivutio vya asili; na

(iv) itatoa elimu kwa wadau na kuishauri Serikali kuridhia Mikataba ya UNESCO ambayo ina maslahi mapana kwa nchi.

**SHUKRANI**

158. Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa QS. Omary Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Daniel Elius Mushi na Dkt. Wilson Mahera Charles kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, ninaomba kutoa shukrani zangu kwa Kamishna wa Elimu,

Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi.

159. Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

160. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Ninaomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Cuba, Ethiopia, Finland, Hangaria, India, Israel, Italia, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

161. Mheshimiwa Spika, napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Aga Khan Education Services, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Christian Social Services Commission (CSSC), Comprehensive Nuclear–Test - Ban Treaty Organisation (CTBTO), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Global Partnership for Education (GPE), Human Development Innovation Fund (HDIF), Inter University Council for East Africa (IUCEA), International Atomic Energy Agency (IAEA), Japan International Cooperation Agency (JICA), Jumuiya ya Madola, Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), Plan International, Swedish International Development Agency (SIDA),

Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO) na United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF).

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26

162. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa kwa mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,436,428,405,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) Shilingi 688,614,234,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo Shilingi 635,249,992,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 53,364,242,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) Shilingi 1,747,814,171,000.00 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 1,186,987,965,000.00 ni fedha za ndani na Shilingi 560,826,206,000.00 fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

163. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 3,240,288,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni Shilingi 1,538,096,000.00 na Matumizi Mengineyo ni Shilingi 1,702,192,000.00

164. Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya Shilingi 2,439,668,693,000.00

165. Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

166. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara https://www.moe.go.tz

167. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mwenyekiti.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba taarifa yetu yote ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2025/2026. Hatua hii inazingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii ya kwanza inawasilisha rasmi taarifa hii katika hatua za Bunge kushughulikia hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, sehemu hii inaonesha namna taarifa ilivyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa za Kamati ikiwemo Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 142(b) inaonesha kuwa sehemu ya pili ya Taarifa hii inapaswa kutoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Kwa kuzingatia masharti hayo, sehemu hii itakuwa na maelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni Uchambuzi wa

Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025, sehemu hii inachambua mambo matano. Kwanza ni uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati; Pili, ni utekelezaji wa kazi zilizopangwa; Tatu, ni ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Nne, ni utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na Tano, ni upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huo utajenga vigezo vya kutumika kufanya tathmini ya uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi. Hatua hiyo ni ya muhimu katika uamuzi bora wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, lengo la kuripoti jambo hili ni kuliwezesha Bunge kujadili hoja iliyowasilishwa Bungeni ikiwa na kumbukumbu muhimu kuhusu ushauri uliotolewa mwaka wa fedha unaokwisha. Kufanya hivyo, kunaliwezesha Bunge kuwa na tathmini endelevu ya utekelezaji wa Wizara hii na mwenendo wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umefanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa, changamoto ya uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunza itatuliwe kwa kuongeza bajeti kwa ajili hiyo. Taarifa ya Waziri inaonesha kuwa ushauri huo ulizingatiwa kwa kuongeza kiasi cha shilingi bilioni 91.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Serikali kusikiliza na kuzingatia ushauri unaotolewa Bungeni inastahili kupongezwa. Ni hatua ambayo inafanikisha lengo la Serikali kuwezesha ustawi wa watu kwa kuzingatia ushauri wa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao ambao ni Wabunge. Ufafanuzi wa kina unapatikana katika Kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa kazi zilizopangwa. Maelezo ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yanapatikana katika Randama ya Fungu 46 – Wizara na Fungu 18 – Tume ya Taifa ya *UNESCO*. Uchambuzi wa taarifa hizo unaonesha kwamba: -

(i) Baadhi ya kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zinaendelea kufanyika hadi sasa kwa hatua yake endelevu;

(ii) Baadhi ya kazi zilizotekelezwa zilikuwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa rasilimali muhimu;

(iii) Sehemu kubwa ya kazi zilizotekelezwa zinaendelea na malengo yaliyopangwa yanatekelezwa na yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya mapato, uchambuzi na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia Februari, 2025 kiasi kilichokusanywa ni shilingi 377,423,172,771.9 sawa na 56%;

(ii) Mwenendo huu wa hali ya ukusanyaji wa mapato umekuwa kwa kiwango hicho au karibu na kiwango hicho kwa takribani miaka minne kuanzia 2021/2022 hadi 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo iliifanya Kamati kutathmini mwenendo huo kwa lengo la kubaini msingi wa hali hiyo. Jedwali Na. 2, linadhihirisha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi hicho kwa urahisi wa uchambuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha yafuatayo:-

(i) Mwaka 2021/2022 ambao ni wa mwanzo katika uchambuzi *(base year)* ukusanyaji ulikuwa wa kuridhisha kwa kuwa ulivuka nusu;

(ii) Miaka miwili iliyofuata, ukusanyaji ulikuwa na mwenendo unaoshuka hadi kufikia 47%;

(iii) Mwaka huu unaokwisha, mwenendo wa ukusanyaji umeanza kupanda ingawa bado siyo ishara ya kufikia lengo la makusanyo iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwa madhumuni ya usimamizi wa Kibunge na bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilitaka kufahamu hatua za utekelezaji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo kama ifuatavyo: -

(i) Mradi Na. 6350 – ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(ii) Mradi Na. 4382 – Ukarabati wa karakana za mafunzo, Hostel za wanafunzi, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*); na

(iii) Mradi Na. 4315 – mradi wa kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya mabadiliko ya Kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo inaendelea kutekelezwa ili kufikia malengo yaliyowekwa. Hata hivyo, kuna changamoto mbili zinazoikabili. Changamoto hizo ni kuchelewa kwa fedha za kugharamia miradi na kuwa nyuma ya ratiba. Maelezo kamili ya hali ya miradi yanapatikana katika Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya jumla ya upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo inaonesha kuwa ni ya kuridhisha. Taarifa kamili kuhusu taarifa hii, naomba urejee katika taarifa iliyoambatanishwa kiambatisho Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha, taarifa iliyotolewa kwenye Kamati ilibainisha mwenendo wa upokeaji kama inavyoonekana kwa muhtasari

kwenye Jedwali Na. 3. Uchambuzi wa taarifa hizo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopokelewa kwa ujumla ni 62% ikiwa ni karibu 67% ya kipindi cha utekelezaji;

(ii) Kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ni 56% tu.

(iii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 kilifikia asilimia kubwa zaidi ya asilimia za fedha ya matumizi mengineyo;

(iv) Uwiano wa bajeti ya mishahara na matumizi mengineyo wakati wa kupitisha bajeti kwa mwaka 2024/2025, unatofautiana na uwiano wa namna hiyo katika Taarifa za utekelezaji kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa kutumia mbinu ya ulinganisho kwa njia ya asilimia na uchambuzi wa mwenendo, mambo makuu yafuatayo yamewekewa mkazo ni: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; na

(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida *(Recurrent Expenditure)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya mapato, uchambuzi uliofanyika unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa asilimia 6.4 ikilinganishwa na mwaka 2024/2025;

(ii) Makadirio ya mapato kati ya Wizara na Taasisi zake yameongezeka kwa asilimia tofauti. Wakati Wizara ina ongezeko la 13.4%, taasisi zinaongezeko la asilimia 3.7;

(iii) Wakati ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2024/2025 ulionesha ugumu wa kufikia lengo, makadirio ya mapato yameongezeka kwa asilimia 6.4; na

(iv) Wakati bajeti ya matumizi ya Wizara hii imeongezeka kwa 24%, ongezeko la makadirio ya mapato haliendani na kiasi cha ongezeko la bajeti ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo, yanalenga kuwezesha gharama za utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Wizara hii. Uchambuzi umeonyesha mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti inayoombwa imeongezeka kwa takribani 32%.

(ii) Ongezeko la Bajeti hiyo limetokana na ongezeko kubwa la fedha za nje ambazo zimeongezeka kwa 90.3%.

(iii) Fedha za ndani zimeongezeka kwa 14.8%.

(iv) Utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 32% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo utegemezi ulikua ni 22.2%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsri ya matokeo ya uchambuzi huo inaonesha kuwa juhudi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan zimeongeza imani ya wabia wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya matumizi, ili kuliwezesha Bunge kufanyia kazi makadirio hayo inavyostahili, Kamati imeweka muhtasari wa uchambuzi wa fedha hizo katika Jedwali Na.5. Uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(ii) Ongezeko hilo linaonesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unatarajiwa kuboreshwa kwa kuzingatia uzoefu wa mwenendo huo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(iii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Taifa ya *UNESCO*, Fungu 18, imeongezeka kwa 12.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ni kuhusu maoni na ushauri wa Kamati. Maoni ya Kamati yanatokana na uchambuzi ulioripotiwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii. Maoni hayo ni kama fuatavyo: -

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kunaathiri malengo na madhumuni ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka huo.

(ii) Mtiririko wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya ukamilishaji wa vyuo 64 vya Elimu na Mafunzo Stadi *(VETA)* unachangia kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi huo.

(iii) Upungufu wa walimu wa Fani za Mkondo wa Amali na Somo la Elimu ya Biashara unachangiwa na kukosekana kwa mikakati maalum ya kuwapata walimu wa Amali na Fani ya Biashara.

(iv) Upungufu wa fedha katika vyuo vya ualimu unaathiri mafunzo ya ualimu yanayoendana na mtaala mpya.

(v) Ongezeko la wanafunzi linalosababisha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ufikie 1:3 au 1:5 unaweza kurekebishwa na kuwa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja iwapo fedha za uchapaji zitapatikana kulingana na mahitaji.

(vi) Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia vya kisasa, unaweza kuathiri lengo kuu la elimu nje ya mfumo rasmi unaotekelezwa kupitia Taasisi ya Elimu ya watu wazima kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(vii) Motisha na maslahi bora kwa makamu wakuu wa vyuo vikuu vya umma ni jambo muhimu kutokana na umuhimu wa majukumu yao.

(viii) Utaratibu uliopo wa *capitation grants* wa shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa ajili ya uthibiti ubora kupitia Fungu 56 Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa shule za msingi na sekondari unaoathiri utendaji kazi na ufanisi wa Wathibiti Ubora. Aidha, mgawanyo wa majukumu unatambua jukumu la udhibiti ubora kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushauri wa Kamati. Kwa kuzingata maoni ya Kamati ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu mambo manane yaliyotajwa hapo juu Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

(i) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, zitolewe kwa ukamilifu kabla ya tarehe 30 Juni, 2025. *(Makofi)*

(ii) Wizara ya Fedha ijitahidi kadri inavyowezekana kuwezesha mtiririko mzuri wa fedha kwa ajili ya uwezeshaji wa ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* ambavyo ni vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha mkoa.

(iii) Wizara ya ELimu Sayansi na Teknolojia iandae mikakati maalum ya kuwapata walimu wa Amali na Fani za Biashara.

(iv) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya vyuo vya ualimu ambavyo vitatoa na kuandaa mafunzo ya ualimu yatakayoendana na mtaala mpya.

(v) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuandaa walimu wa masomo ya amali ili kuwawezesha wahitimu wa mafunzo ya amali kusoma kozi hizo na kuajiriwa kama walimu. Aidha, mikakati itakayowawezesha walimu kupitia vyuo vikuu mbalimbali nchini iendelee kutekelezwa.

(vi) Serikali iendelee kutenga fedha za uchapaji wa vitabu kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja. Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafute uwezekano wa kusambaza machapisho ya kieletroniki *(e-books)* kwa baadhi ya ngazi za elimu ili kupunguza gharama za uchapaji na kuondoa nakala mango na pia kuhifadhi mazingira.

(vii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae mikakati ya kununua na kusambaza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia masomo yote ikiwemo ujasiriamali, stadi za maisha na ufanisi mbalimbali. Lengo liwe kuwajengea uwezo wa kujifunza maarifa mapya kwa namna bora.

(viii) Serikali ichukue hatua madhubuti ya kushughulikia maslahi ya Makamu Wakuu wa Vyuo vya Umma nchini na kuhakikisha kuwa wanapata stahiki zao kulingana na vyeo vyao.

(ix) Serikali ihamishe *capitation grants* ya shilingi 1000 kwa mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari ambayo inatolewa kila mwaka kwa ajili ya uthibiti ubora, kutoka Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambalo halihusiki na udhibiti ubora na kupeleka Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambalo ndiyo linahusika na masuala ya uthibiti ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa malezi, ushauri, miongozo na kwa namna ambavyo umekuwa ukituongoza humu ndani kwa viwango, *speed and standards*. Tunakushukuru na tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niliruhusu nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Spika wa

viwango vya juu sana. Hivi juzi baadhi yetu sisi Waheshimiwa Wabunge tulikuwa pale Mbeya tumeona namna ambavyo Wanambeya wanaendelea kumhitaji Dkt. Tulia, na wamesema bado wanaye kwa muda mrefu sana. Tunampongeza na tunamwambia Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha,nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni yao, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Mbunge, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na msaidizi wake, Mheshimiwa Omary Shaban Kipanga, Mbunge, Naibu Waziri; na Profesa Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii; Dkt. Wilson Mahera, Naibu Katibu Mkuu; Profesa Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji, viongozi na wakuu wa taasisi zote katika Wizara hii kwa ushirikiano ambao wameutoa kwa Kamati katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Tanga kwa kunivumilia katika kipindi chote ambacho nimekuwa katika majukumu ya Bunge na majukumu ya Kamati hadi kufikia hii leo. Mwenyezi Mungu awabariki sana akina mama wa Mkoa wa Tanga na aendelee kuwapa imani kubwa juu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili liijadili, liikubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2025/2026. Hatua inazingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufatilia mtiririko wa Taarifa hii, naomba kubainisha muundo wake ambao umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge. Kwa kufanya hivyo, vigezo vilivyozingatiwa katika uandishi wa Taaarifa hii vimebainishwa na uonesha uhalali wa uchambuzi, maoni na ushauri unaotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) **Sehemu ya Kwanza** inaeleza msingi, mbinu na wigo wa kazi ya Kamati katika uchambuzi wake;

(ii) **Sehemu ya Pili** inaeleza matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi;

(iii) **Sehemu ya Tatu** inahusu maoni, ushauri na hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi

### 1.3.1 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Taarifa hii ni Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Februaari, 2023. Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imeweka ufafanuzi wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo kamati hii. Kifungu cha 6(7) (a) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 118(5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, umenipa nafasi hii adhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge.

### 1.3.2 Mbinu Zilizotumika

**Mheshimwa Spika,** ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii inabinisha mbinu zilizotumika. Madhumuni ya kuonesha mbinu ni kuipa taarifa hii msingi wa

kuwa rejea madhubuti ambayo inakidhi vigezo vya uadilifu uliozingatiwa na kupata maoni na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi, Kamati ilitumia mbinu zilizojumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Njia kuu iliyotumika ni ulinganisho wa maudhui na hali halisi. Kwa kufanya hivyo, imekuwa yenye msingi na ushauri unaozingatia hali halisi kiutekelezaji.

**1.3.3 Wigo na mipaka ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** wigo na mipaka ya maudhui ya taarifa hii umetokana na kazi za Kamati zilizoainishwa katika Kanuni za Bunge. Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 unajikita kwenye malengo yaliyokuwa yamepangwa, ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa upande wa Mwaka 2025/2026, uchambuzi unagusa vipaumbele vya Wizara, makadirio ya mapato na matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** mambo yote nje ya maeneo niliyoyataja hayatakuwa sehemu ya Taarifa hii. Lengo ni kuzingatia masharti ya Kanuni ya 71(1) ya Kanuni za Bunge kuhusu mambo yasiyoruhususiwa kuzungumzwa wakati wa hoja hii. Kwa ujumla wigo na mipaka hiyo ni muhimu na unafanikisha azma ya Bunge kuendeshwa kwa taratibu bora na madhubuti.

**1.4 Majumuisho ya Sehemu**

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya yote katika sehemu ya kwanza, Taarifa imetoa ombi la kuwasilisha rasmi taarifa hii katika hatua za Bunge kushughulikia hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pamoja na hilo, sehemu hii imeonesha ilivyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa za Kamati ikiwemo Kamati hii. Kanuni iliyozingatiwa ni Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** misingi iliyotajwa kwenye sehemu ya kwanza ni Kanuni ya 137 iliyoanzisha Kamati na kufafanua

majukumu yake kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Vilevile Kanuni ya 118 inayohusu taratibu za kushughulikia makadirio ya mapato na matumizi na Kanuni ya 142 inayohusu muundo wa Taarifa zimerejewa kwa Kanuni hizo, makadirio haya yalifanyiwa uchambuzi, mapema asubuhi, Taarifa imewekwa mezani na sasa inasomwa rasmi.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 (b) inaonesha kuwa sehemu ya pili ya Taarifa hii inapaswa kutoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati kwa kuzingatia masharti hayo, sehemu hii itakuwa na maaelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(ii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo ulifanyika kwa ulinganisho kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) na 117 (2) za Kanuni za Bunge. Hivyo, uchambuzi huo unajenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** lengo la uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti limeelezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni hiyo, lengo ni kufanya ulinganisho na makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Tafsiri yake ni kuwa uzoefu wa utekelezaji utumike kujenga maoni kuhusu makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni hayo, sehemu hii inachambua mambo matano ambayo ni: -

(i) Uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizopangwa;

(iii) Ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(v) Upatikanaji wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo utajenga vigezo vya kutumika kufanya tathmini ya uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi. Hatua hiyo ni ya muhimu kwa uamuzi bora wa Bunge.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuonesha uwajibikaji Bungeni, sehemu hii inaripoti kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa kamati. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, tarehe 07 Mei, 2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo makuu kumi (10) kuhusiana na Wizara hii. Ushauri huo ulitolewa katika Kikao cha Ishirini cha Mkutano wa kumi na Tano wa Bunge wakati Bunge lilipopitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.1

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kuripoti jambo hili ni kuliwezesha Bunge kujadili hoja iliyowasilishwa Bungeni likiwa na kumbukumbu muhimu kuhusu ushauri uliotolewa Mwaka wa Fedha unaokwisha. Kufanya hivyo kunaliwezesha Bunge kuwa na tathmini endelevu ya utekelezaji wa Wizara hii na mwenendo wa sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

[1] Taz. Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge tarehe 07 Mei, 2025,

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umefanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa, changamoto ya uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunza itatuliwe kwa kuongeza bajeti kwa ajili hiyo. Taarifa ya Waziri ilionesha kuwa ushauri huo ulizingatiwa kwa kuongeza kiasi cha Sh. bilioni 91.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Aidha, Sh. Bilioni 21.3 zinaongezwa kwenye bajeti kwa Mwaka 2025/2026 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo 65 vya VETA. Taarifa zaidi ilionesha kuwa Sh. Bilioni 7 zinatengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo mitambo na mashine.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri mwingine umeanza kuzingatiwa na upo katika mchakato maalumu. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa vigezo vya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu vifanyiwe mapitio kwa lengo la kuwa na vigezo visivyosababisha malalamiko na vyenye tija katika azma ya Taifa. Majibu ya Serikali yameonesha kuwa ushauri huu umezingatiwa kwa kiasi kikubwa, kufikia hatua ya kusubiri maoni ya wadau. Taarifa ilionesha kuwa Serikali imekamilisha mapitio ya muundo na utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Aidha, Serikali imeboresha vigezo vya utoaji wa mikopo ambavyo vitaanza kutumika kuanzia Mwaka wa Fedha 2025/2026 baada ya kuridhiwa na wadau.

**Mheshimiwa Spika,** hatua ya Serikali kusikiliza na kuzingatia ushauri unaotolewa Bungeni inastahili kupongezwa. Ni hatua ambayo inafanikisha lengo la Serikali kuwezesha ustawi wa watu kwa kuzingatia ushauri wa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ufafanuzi wa kina kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, Kiambatisho Na. 02 kinaeleza zaidi. Lengo la ufafanuzi huo ni kubainisha namna Serikali ilivyozingatia na hatua iliyofikiwa.

**2.2.2 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa**

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lilipopitisha na kuidhinisha bajeti ya Wizara hii, lilizingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha na kiwango cha utekelezaji kilichofikiwa. Lengo ni kulijulisha Bunge matokeo ya utekelezaji wa bajeti katika kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yanapatikana katika Randama ya Fungu 46 – Wizara na Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO. Uchambuzi wa taarifa hizo unaonesha mambo yafuatayao:-

(i) Baadhi ya kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2024/2025 zinaendelea kufanyika hadi sasa kwa kuwa ni endelevu;

(ii) Baadhi ya kazi zimetekelezwa zikiwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa Rasilimali muhimu;

(iii) Sehemu kubwa ya kazi zilizotekelezwa zinaendana na malengo yaliyokuwa yamewekwa.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa kazi zinazoendelea ni kazi ya utekelezaji Sera na Mitaala, mapitio ya sheria zinazohusu utoaji wa elimu na mafunzo nchini pamoja na uandaaji wa miongozo inayohusika. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 ilizinduliwa tarehe 01 Februari, 2025. Aidha, Mikutano mbalimbali na vyombo vya habari ni miongoni mwa njia zilizotumika kutoa elimu kwa umma kuhusu sera ya taifa ya Elimu na Mafunzo pamoja na mitaala ya ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa kazi zilizokabiliwa na changamoto ni utekelezaji wa mpango wa fursa na

kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na ufundi stadi) katika shule za sekondari na vyuo vya amali. Taarifa ya Serikali ilionesha kuwa, kazi hiyo ilikabiliwa na uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri hususani katika masomo au fani za sayansi, hisabati na mafunzo ya amali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizo, kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2024/2025 zimetekelezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa ili kuwa na mwendelezo mzuri wa kazi hizo, upo umuhimu wa kutatua changamoto zinazohusika.

### 2.2.3 Ukusanyaji wa Mapato


**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo kawaida ya bajeti kuwa na pande mbili. Mapato na matumizi, Bunge lilipitisha makadirio ya mapato ya Wizara hii. Kwa madhumuni ya uwajibikaji Kibunge, Kamati ilitaka kufahamu ukusanyaji wa mapato yaliyoidhinishwa. Muhtasari wa taarifa za ukusanyaji wa mapato unaonekana katika Jedwali Na. 1 na picha ya hali halisi inatolewa kwenye Chati Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---:|---:|---:|
| Idara/Vitengo | 9,700,537,000.00 | 6,301,274,501.06 | 64.96 |
| Taasisi | 667,598,605,074.83 | 371,121,898,270.84 | 55.59 |
| **Jumla** | **667,299,142,074.83** | **377,423,172,771.90** | **56** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Chati Na. 1: Taswira ya Uwiano wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2024/2025**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa mwenendo huo wa ukusanyaji wa mapato unaonesha yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia Februari, 2025 kiasi kilichokusanywa ni Sh. **377,423,172,771.9** sawa na **asilimia 56;**

(ii) Mwenendo huu wa hali ya ukusanyaji wa mapato umekuwa kwa kiwango hicho au karibu na kiwango hicho kwa takriban miaka minne kuanzia 2021/2022 hadi 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo iliifanya Kamati kutathmini mwenendo huo kwa lengo la kubaini msingi wa hali hiyo.

**Jedwali Na. 2**, linadhihirisha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi hicho kwa urahisi wa uchambuzi.


**Jedwali Na. 2 Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Kipindi cha Kuanzia mwaka 2021/2022- 2024/2025**

| MWAKA | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 555,043,008,495.63 | 350,484,167,565.79 | 63 |
| 2022/2023 | 642,667,620,483.06 | 338,199,478,541.42 | 53 |
| 2023/2024 | 679,362,572,548.64 | 318,339,539,882.24 | 47 |
| 2024/2025 | 667,299,142,074.83 | 377,423,172,771.90 | 56 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Kamati 2021/2022 – 2022/2023 na Randama ya Wizara 2024/2025*

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuchambua mwenendo wa makusanyo, **chati Na. 2** inatoa taswira halisi.

**Chati Na. 2 Mwenendo wa Ufikiaji wa Lengo la Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 -2024/2025**




**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha yafuatayo: -

(i) Mwaka 2021/2022 ambao ni wa mwanzo katika uchambuzi (base year) ukusanyaji ulikuwa wa kuridhisha kwa kuwa ulivuka nusu;

(ii) Miaka miwili iliyofuata, ukusayaji ulikuwa na mwenendo unaoshuka hadi kufikia **asilimia 47;**

(iii) Mwaka huu unaokwisha, mwenendo wa ukusanyaji umeanza kupanda ingawa bado si ishara ya kufikia lengo kwa kipindi kilichobaki.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unatoa misingi ya kuzingatia katika uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kuna dalili kuwa lengo lililopangwa ama halikuwa halisi au ukusanyaji haukufanyika kwa ufanisi lakini kwa kuwa hali imekuwa hivyo kwa zaidi ya miaka miwili, kuna umuhimu wa kufanyia kazi lengo la makusanyo linalowekwa kwa Wizara hii.

**2.2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya usimamizi wa Kibunge wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilitaka kufahamu hatua za utekelezaji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu miradi hiyo ni: -

(i) Mradi Na. 6350 – ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam;

(ii) Mradi Na. 4382 – Ukarabati wa karakana za mafunzo, Hostel za wanafunzi, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Teknolojia Dar es salaam (DIT); na

(iii) Mradi Na. 4315 – mradi wa kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya mabadiliko ya Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** miradi hiyo inaendelea kutekelezwa ili kufikia malengo yaliyowekwa hata hivyo kuna changamoto mbili zilizobainika. Changamoto hizo ni kuchelewa kwa fedha za kugharamia miradi na kuwa nyuma ya Ratiba. Maelezo kamili ya hali ya miradi yanaelezwa katika Kiambatisho Na. 01.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya jumla ya upatikanaji wa fedha za kugharimia miradi ya maendeleo inaonesha kuwa nzuri. Taarifa ya Waziri ilionesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 64 ya fedha zote za miradi. Uchambuzi zaidi ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya upokeaji wa fedha za kugharamia miradi imekuwa nzuri kutokana na mchango wa fedha za nje kuliko fedha za ndani;

(ii) Upokeaji wa fedha za ndani hauoneshi mwenendo mzuri hadi kufikia mwezi Februari, 2025 fedha zilizopokelewa ni asilimia 55 tu.

(iii) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi hiyo inaonekana kuwa nzuri pamoja na changamoto za upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa kuchelewa na usimamizi kutowezesha uzingatiaji wa ratiba ya miradi zinafaa kufanyiwa kazi. Aidha, uzoefu kuhusu changamoto hizo na masuala mengine kuhusu usimamizi wa miradi ni mambo ya kuzingatiwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026.

### 2.2.5 Mwenendo wa upatikanaji wa fedha

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 lilipitisha kiasi cha Sh. 637,287,706,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida

(recurrent expenditure). Lengo la kiasi hicho lilikuwa ni kuwezesha ugharamiaji wa uendeshaji wa Wizara na mishahara ya watumishi. Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati ilibainisha mwenendo wa upokeaji kama inavyoonekana kwa muhtasari kwenye Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3 Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Elime, Sayansi na Teknoloja**

| AINA YA MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 85,225,031,000.00 | 368,412,483,674.74 | 63 |
| Mengineyo | 52,062,675,000.00 | 29,382,258,159.78 | 56 |
| **JUMLA** | **637,287,706,000.00** | **397,794,741,834.52** | 62 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi taarifa hizo unaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopokelewa kwa ujumla ni **asilimia 62** ikiwa ni karibu **asilimia 67** ya kipindi cha utekelezaji;


(ii) Kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ni **asilimia 56** tu.

(iii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 kilifikia asilimia kubwa zaidi ya asilimia za fedha ya matumizi mengineyo;

(iv) Uwiano wa bajeti ya mishahara na matumizi mengineyo wakati wa kupitisha bajeti kwa Mwaka 2024/2025, unatofautiana na uwiano wa namna

hiyo katika Taarifa za utekelezaji kama inavyoonekana katika **Chati Na. 3**.

**Chati Na. 3 Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2024/2025 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya hali hiyo ni kuwa fedha za uendeshaji zimekuwa changamoto. Kwa kuwa hadi mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopatikana ni asilimia 56 tu, ni wazi kuwa kwa kipindi cha Februari hadi Juni, 2025 uendeshaji utasuasua. Kamati ina maoni kuwa jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi.

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni 117 (2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti kwa Kamati kulinganisha utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka unaoisha na makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Kwa kuzingatia masharti hayo, sehemu hii inafanya uchambuzi unaozingatia ulinganisho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutumia mbinu ya ulinganisho kwa njia ya asilimia na uchambuzi wa mwendo, mambo makuu yaliyowekewa mkazo ni: -

(i) Makadiirio ya mapato kwa mwaka 2025/2026;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya matumizi ya kawaida (recurrent expenditure).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo unajenga msingi wa ushauri wa Kamati na ni taarifa muhimu kwa uamuzi wa Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa sababu hiyo, ufafanuzi unatolewa kama ifuatavyo: -

**2.3.1 Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika,** hotuba ya Waziri iliyowekwa mezani mapema asubuhi ya leo kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (3) ya Kanuni za Bunge imetaja kiasi cha fedha kinachokadiriwa kuwa mapato. Kiasi hicho ni sawa na kiasi kilichoelezwa kwenye Kamati. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya uchambuzi wa kiasi hicho kwa njia ya ulinganisho kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 04.

**Jedwali Na. 4 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elime, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026**

| CHANZO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAKADIRIO 2025/2026 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **WIZARA** | 9,700,537,000.00 | 8,402,257,000.00 | 1,298,280,000.00 | **13.4** |
| **TAASISI** | 677,299,142,074.83 | 702,105,622,789.63 | 24,806.480,714.83 | **3.7** |
| **JUMLA** | **667,598,605,074.83** | **710,507,879,789.63.** | **42,909,274,714.8** | **6.4** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanyika unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yameongezeka kwa **asilimia 6.4** ikilinganishwa na Mwaka 2024/2025;


(ii) Makadirio ya mapato kati ya Wizara na Taasisi ake yameongezeka kwa asilimia tofauti. Wakati Wizara ina ongezeko la **asilimia 13.4**, taasisi zinaongezeko la **asilimia 3.7**;

(iii) Wakati ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka 2024/2025 ulionesha ugumu wa kufikia lengo, makadirio ya mapato yameongezeka kwa **asilimia 6.4**

(iv) Wakati bajeti ya matumizi ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 24**, ongezeko la makadirio ya mapato haliendani na kiasi cha ongezeko la bajeti ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, uchanganuzi huo unaonesha pia uwiano wa mchango wa mapato ya Wizara na taasisi zake kama inavyoonekana katika **Chati Na. 4**.

**Chati Na. 4 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri ya uchambuzi huo, ni wazi kuwa uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka wa Fedha halikuzingatiwa. Kwa sababu hiyo Kamati ina maoni kuwa, ni vema upangaji wa bajeti uwe ukizingatia uzoefu unaopatikana kwa Mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, uhalisia wa vyanzo vya mapato usipozingatiwa, ukusanyaji wa mapato utatofautiana na lengo linalotokana na makadirio.

**2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya bajeti ya maendeleo yanalenga kuwezesha gharama za utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Wizara hii. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kama ilivyo kuwa kwa mwaka 2024/2025 **Fungu 18 Tume ya Taifa ya UNESCO** halitekelezi mradi ya Maendelo. Fedha zote za miradi ya Maendeleo chini ya Wizara hii linakadiriwa katika **Fungu 46 kwa ajili ya WIzara na Taasisi zilizo chini yake**. Uchambuzi umeonyesha mambo yafuatayo;-

(i) Bajeti inayoombwa imeongezeka kwa takribani **asilimia 32.**

(ii) Ongezeko la Bajeti hiyo limetokana na ongezeko kubwa la fedha za nje ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 90.3.**

(iii) Fedha za ndani zimeongezeka kwa **asilimia 14.8**.

(iv) Utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **asilimia 32** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo utegemezi ulikua ni **asilimia 22.2.**

**Mheshimiwa Spika**, tafsri ya matokeo ya uchambuzi huo inaonesha kuwa juhudi za Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zimeongeza imani ya wabia wa maendeleo katika utekelezaji wa Miradi. Hata hivyo iwapo fedha hizo hazitopatikana, yamkini miradi hiyo itakwama.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo Mheshimiwa Waziri aliweka mezani hotuba yake inayoonyesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba jumla ya shilingi **2,439,668,693,000** Kati ya fedha hizo **shilingi 691,854,522,000** ni makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mafungu mawili, **Fungu -46 Wizara** na **Fungu 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO**. Ili kuliwezesha Bunge kufanyia kazi makadirio hayo inavyostahili, Kamati imeweka muhtasari na mchanganuo wa fedha hizo katika **Jedwali Na 5**.

**Jedwali Na. 5 Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026 | % ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 585,225,031,000 | 635,249,992,000 | 9 |
| Kawaida | 52,062,675,000 | 53,364,242,000 | 3 |
| Maendeleo | 1,328,042,674,000 | 1,747,814,171,000 | 32 |
| **JUMLA** | **1,965,330,380,000** | **2,436,428,405,000** | **24** |

***Chanzo:*** Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio hayo yameongezeka kwa **asilimia 8.1** ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(ii) Ongezeko hilo linaonesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unatarajiwa kuboreshwa

kwa kuzingatia uzoefu wa mwenendo huo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(iii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Tafa ya UNESCO (Fungu 18) imeongezeka kwa **asilimia 12.4**

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri ya matokeo ya uchambuzi huo inaonesha kuwa majukumu ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* yamepewa kipaumbele zaidi ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha majukumu ya Wizara na Taasisi zake yamezingatiwa kwa kipaumbele zaidi ya ilivyokuwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 142(c) ya Kanuni za Bunge, inafanya hitimisho baada ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati. Kwa ujumla, sehemu hii inachukua matokeo ya uchabuzi kwenye sehemu ya pili iliyozingatia msingi wa Taarifa kama ulivyofafanuliwa kwenye Sehemu ya kwanza.

### 3.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kamati yanatokana na uchambuzi ulioripotiwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii. Moni hayo ni kama fuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zlizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kunaathiri malengo na madhumuni ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka huo.

(ii) Mtiririko wa fedha kutoka HAZINA kwa ajili ya ukamilishaji wa vyuo 64 vya Elimu na Mafunzo Stadi

(VETA) unachangia kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi huo.

(iii) Upungufu wa walimu wa fani za Mkondo wa Amali na somo la elimu ya Biashara. Unachangiwa na kukosekana kwa mikakati maalum ya kuwapata walimu wa Amali na fani ya Biashara.

(iv) Upungufu wa fedha katika vyuo vya ualimu unaathiri mafunzo ya ualimu yanayoendana na mtaala mpya.

(v) Ongezeko la wanafunzi linalosababisha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ufikie 1:3 hadi 1:5 unaweza kurekebishwa na kuwa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja iwapo fedha za uchapaji zitapatikana kulingana na mahitaji.

(vi) Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia vya kisasa, unaweza kuathiri lengo kuu la elimu nje ya mfumo rasmi unaotekelezwa kupitia Taasisi ya Elimu ya watu wazima kwa kushirikina na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

(vii) Motisha na maslahi bora kwa Makamu wakuu wa vyuo vikuu vya umma ni jambo muhimu kutokana na majukumu wanayotekeleza.

(viii) Utaratibu uliopo wa *Capitation grants* wa **shilingi 1000** kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kupitia **fungu 56** TAMISEMI kwa shule za msingi na sekondari unadhohofisha utendaji na ufanisi wa Wadhibiti Ubora. Aidha, mgawanyo wa majukumu unatambua jukumu la wadhibiti ubora kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**3.3 Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingata maoni ya Kamati ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu mambo manane niliyoyataja hapo juu Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa ukamilifu kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

(ii) Wizara ya Fedha ijitahidi kadri inavyowezekana kuwezesha mtiririko mzuri wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ambavyo ni vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha Mkoa.

(iii) Wizara ya ELimu Sayansi na Teknolojia iandae mikakati maalum ya kuwapata walimu wa amali na fani ya Biashara.

(iv) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu ambavyo vitatoa na kuandaa mafunzo ya ualimu yatakayoendana na Mtaala mpya.

(v) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuandaa walimu wa masomo ya amali ili kuwawezesha wahitimu wa mafunzo ya amali kusoma kozi hizo na kuajiriwa kama walimu. Aidha mikakati ya kuwaendeleza walimu kupitia vyuo vikuu mbalimbali nchini iendelee kutekelezwa.

(vi) Serikali iendelee kutenga fedha za uchapaji wa vitabu kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwiano wa kitabu na mwanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). Aidha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafute uwezekano wa kusambaza machapisho ya kieletroniki yaani (*e-books*) kwa baadhi ya ngazi za elimu ili kupungiza uchapaji wa nakala Mango na pia kuhifadhi Mazingira.

(vii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae mikakati ya kununua na kusambaza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia masomo yote ikiwemo ujasiriamali, stadi za maisha na ufanisi mbalimbali.

Lengo liwe kuwajengea uwezo wa kujifunza maarifa mapya kwa namna bora.

(viii) Serikali ichukue hatua madhubuti ya kushughulikia maslahi ya Makamu Wakuu wa Vyuo vya Umma nchini na kuhakikisha kuwa wanapata stahiki zao kulingana na vyeo vyao.

(ix) Serikali ihamishe ***capitation grants*** ya **shilingi 1000** kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kwa mwaka, kutoka **Fungu 56 - TAMSEMI** ambalo halihusiki na udhibti ubora na kupeleka Fungu 46 - Wizara ya ELmu, Sayansi na Teknolojia, ambalo linahusika na udhibiti ubora.

**3.4 Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Musa Ramadhani Sima, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Dr. Thea Ntara, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Ester Edwin Maleko, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Kassim Ali Khamis, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Mwanakhamisi Kassian Said, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb - Mjumbe

16. Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wasaidizi wake, Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Naibu Waziri; na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Dkt. Wilson Mahera, Naibu Katibu Mkuu – Elimu, Prof. Daniel Mushi - Naibu Katibu Mkuu - Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Idephonce. Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI WAKAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
12 Mei, 2025

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni Wawakilishi wa *TENMET*, *UNICEF*, *SIDA*, Benki ya Dunia *(World Bank), UNESCO* na *FCDO*, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Vicent Laswai, mmiliki wa Hoteli ya *Kibo Palace, Kibo Home* na mdau wa elimu. Karibu sana Mzee Laswai, wewe ni mtu muhimu sana Tanzania. Karibu sana. Umeweza kujenga hoteli nzuri, lakini ume-*maintain standards* za Kimataifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ajiandae Mheshimiwa Profesa Muhongo.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika Hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wiki mbili zilizopita nilitoa mchango kuhusu mageuzi ya mfumo wa ufundishaji katika vyuo vikuu. Leo nataka nihitimishe hoja yangu kwa kuzungumzia ufundishaji katika shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakubaliana nami kwamba, katika shule zetu, hasa za msingi, kuna msongamano mkubwa sana wa wanafunzi katika madarasa. Kwa uzoefu wangu wa ualimu hata kama mwalimu ungekuwa hodari kiasi gani, hakuna mwalimu ambaye anaweza kufundisha darasa lenye zaidi ya wanafunzi 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo hili, naomba nipendekeze jambo moja ambalo halina gharama kwa Serikali. Jambo hilo ni kwamba katika shule ambazo kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani, walimu wakuu wa shule wapewe maelekezo maalum ya kuwagawa wanafunzi katika makundi mawili makubwa kama ninavyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la kwanza liwe na wanafunzi wa darasa la kwanza, la pili na la tatu. Hawa waingine madarasani kwa utaratibu wa kawaida kuanzia saa moja mpaka saa nne kamili, wasome masomo kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la pili lenye wa wanafunzi wa darasa la nne, tano na sita, hawa wawekwe kwenye ukumbi mkubwa wa mikutano, huko waoneshwe filamu mbalimbali za kujifunza Kiingereza, Sayansi, wafanye midahalo, majadiliano, drama, michezo ya ndani, mashindano ya usanifu na ubunifu na utengenezaji wa vitu mbalimbali. Itakapofika saa nne na nusu, wabadilishane.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale walioko katika ukumbi wa mikutano, wataingia darasani kama kawaida kuanzia saa nne na nusu mpaka saa saba kamili watakapomaliza masomo na wale waliokuwa madarasani, waendelee na utaratibu wa kufanya shughuli mbalimbali nje ya mitaala, kama nilivyopendekeza hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mantiki ya kupendekeza jambo hili? Elimu yoyote iliyo bora na inayotakiwa kukidhi mahitaji ya mwanafunzi ni lazima ijielekeze kumkuza mwanafunzi katika maeneo matatu ya msingi. La kwanza, uwezo wa akili kufikiri, sisi walimu tunaita *cognitive domain*. Uwezo wa kukuza maadili mema, tabia njema na mitazamo ambayo tunaita *affective domain*. Tatu, ni kukuza uwezo wa michezo na kufanya kazi mbalimbali za mikono. Hii ndiyo elimu iliyokamilika, jambo ambalo silioni likifanyika katika shule za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kasoro nyingine ninayoiona kwenye mfumo wetu wa elimu, watoto wanapomaliza masomo ya siku na kurudi nyumbani, wanapewa kazi nyingi za nyumbani na wazazi wao kutakiwa wawasimamie. Hoja yangu ni, tupunguze kazi nyingi nyumbani. Kama kuna ulazima wa kuwapa wanafunzi kazi, tuwape kazi zenye lengo la kupima uwezo wa ufahamu na udadisi badala ya kukariri majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wengine wanakwenda mbali zaidi, wanawapeleka watoto wa shule za msingi kwenye masomo ya ziada. Hili ni jambo la hatari sana katika makuzi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sayansi ya ukuaji wa watoto inasema hivi, "mtoto chini ya umri wa miaka 15 ubongo wake unakuwa dhaifu sana. Huwezi kumudu kusoma mambo mengi kwa wakati mmoja. Unataka kutunzwa na kulelewa kwa umakini wa hali ya juu sana." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko mwanafalsafa mmoja mwenye busara aliwahi kusema, "kusoma sana, hasa kwa watoto wadogo, kunadumaza akili na uwezo wa kufikiri." Prof. Howard Gardner wa Chuo Kikuu cha Harvard Marekani katika kitabu chake maarufu *"Friends of Mine, Theory of Multiple Intelligences"*, aliwahi kusema, malezi na mifumo ya shule inadumaza uwezo wa watoto kufikiri na vipaji vingine vya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, akasema, "mkazo mkubwa sana wa malezi, wazazi na walimu ni kusoma, kuandika na kuzungumza peke yake." Vipaji vingine havipewi uzito unaostahiki. Mimi nimekuwa nikijiuliza hivi, kwa nini wazazi wetu ambao walikuwa hawajui kusoma na kuandika na walikuwa masikini wa kutupa, wametulea sisi tukafikia hatua hii tuliyonayo katika mazingira haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tuna elimu ya kutosha na uwezo mkubwa sana wa kiuchumi hatuwezi kulea watoto kama wazazi wetu. Kwa nini? Kwa sababu mifumo ya malezi, mifumo ya elimu imedumaza haya mambo. Darasani watoto wetu hawapewi nafasi ya kutosha kujifunza stadi za maisha na stadi za kazi. Nyumbani, mkazo mkubwa kama nilivyosema, kusoma, kuandika hakuna kucheza, wanafungiwa mageti. Huwezi kutayarisha vijana imara kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malezi ya watoto ni kama vile unavyotunza mimea. Leo ukichukua mimea miwili inayofanana, ya aina moja, mmoja unapanda kwenye ndoo unauweka sebuleni na mwingine unauchukua unaupanda shambani, baada ya miezi sita ukitembelea, ule wa sebuleni utadumaa, ule wa shambani utakuwa imara sana. Kwa nini? Kwa sababu mazingira magumu yanatengeneza vitu imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, mmea ukiwa shambani unajenga uwezo wa kuhimiLi hali ya hewa, mvua, jua, na wadudu waharibifu. Sasa sisi wazazi na walimu wa leo, watoto wetu wanalelewa na televisheni na dada wa kazi muda wote. utatengenezaje vijana makini na imara kwa utaratibu kama huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanafundishwa mambo ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na maisha wanayoyaishi. Wanafundishwa mada nyingi kupita kiasi, mambo ambayo wao wenyewe wangejifunza katika vitabu vyao na kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano hapa. Kwenye somo la Hisabati, walimu wanatumia muda mwingi sana kufundisha kukokotoa namna ya kutafuta *square roots* na *quadratic equation*. Sasa najiuliza, ni nini uhusiano kati ya *quadratic equation* na maisha halisi ya mwanadamu? Wale wa Kemia wanafundishwa *periodic table*. Ni nini uhusiano wa *periodic table* na maisha ya kawaida ya mwanadamu? Mimi siuoni. Kwa mawazo yangu, walimu walitakiwa kuwaeleza wanafunzi, nini umuhimu wa *periodic equation* katika maisha ya kawaida ili waone uhusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, watoto wanapoingia kidato cha nne, wanatakiwa kufanya uchaguzi wa kuchagua masomo watakayobobea mbele ya safari. Sasa uchaguzi huu siyo jambo rahisi sana, wanapaswa kuangalia malengo yao, wanapaswa kuangalia vipaji vyao, wanapaswa kuangalia uwezo wao wa kumudu masomo watakayoyachagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mnasaba huu, basi napendekeza, sioni kama kuna umuhimu kwa mwanafunzi ambaye anatamani kufanya kazi ya upishi au ufundi kutakiwa kujiunga na kidato cha tano na sita badala ya kwenda shule ya ufundi. *Udongo upate, ulimaji.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la busara, mtoto anapenda michezo. Badala ya kumpeleka kwenye *academy* ya michezo anatakiwa kwenda kidato cha tano na sita. Mimi naona kama ni kuwapotezea muda, na kwa bahati mbaya sana vipaji vina muda, muda ukipita vipaji vya mwanadamu vinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana au wanafunzi ambao wanatamani kusoma masomo ya utaalamu kama vile Udaktari, Sheria, Ufamasia, Sayansi ya Kilimo, na Ualimu. Hawa ni lazima wafuate utaratibu wa kawaida wa kwenda kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa maoni yangu masomo ya kidato cha tano na sita yana uhitaji wa kufanyiwa mapinduzi ya hali ya juu sana. Utaratibu huu wa sasa hautusaidii kuwatengeneza vijana mahiri sana. Kwa maoni yangu, badala ya kuendelea kuwafundisha vijana masomo ya jumla jumla, wafundishwe masuala ya ujuzi na utaalamu ili waweze kuoanisha nadharia waliyojifunza kidato cha nne na hali halisi ya mafunzo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wenye asili ya Kiasia, wanatupatia funzo kubwa katika hili jambo. Watoto wao wanapomaliza kidato cha nne wanapelekwa katika vyuo ambavyo vinatoa mafunzo ya utaalamu katika kiwango cha diploma ili wajifunze ujuzi wa kazi. Huko wanajifunza sayansi ya kilimo, utaalamu wa masuala mbalimbali, udaktari, ufamasia ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nahodha, kengele ya pili. Kwanza nikushukuru kwa mchango mzuri sana.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Nikuombe mengine ambayo hujayasema umwandikie Mheshimiwa Waziri ili ayachukue na iwe *recorded*

kwenye *Hansard*. Mheshimiwa Profesa Muhongo, wajiandae Mheshimiwa Prof. Shukrani pamoja na Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hii Wizara muhimu kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Ndugu zangu Wabunge, hii Wizara ndiyo roho ya nchi, na ni lazima tuipitishe. Vilevile umuhimu wake ni kwamba inatutoa kwenye dira iliyokwisha inatupeleka kwenye dira ya 2025 – 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo Jimbo langu. Sisi Musoma Vijijini, tuko mbele kabisa kwenye kutekeleza haya mabadiliko yanayofanywa Wizarani. Kwanza, Mheshimiwa Profesa na timu yake wanafanya kazi nzuri sana. Ukweli ndiyo huo. Nimemsikiliza anayoyasema na mengine, nami ndio nataka kuchangia hapa, tutaongezea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Musoma Vijijini kwa kusema darasa la mwisho la shule ya msingi, ni darasa la sita na kwamba wote watasoma mpaka kidato cha nne. Sisi tunaendelea kujenga kila kijiji kiwe na sekondari moja, ndivyo tunavyokwenda. Hivi juzi, mwaka huu tumefungua sekondari nne. Salamu zangu ziende Wizarani, lakini sana kwa Mheshimiwa Rais, tunafungua sekondari nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa aendelee kwa sababu vilevile tunamuenzi aliyekuwa Gwiji la Kiswahili Nchini, Profesa David Massamba, tumempatia sekondari yake. Tulianza kujenga kwa fedha kidogo, lakini Wizara na Serikali imetusaidia. Kwa hiyo, Musoma Vijijini tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika mambo ambayo kidogo yanatoka jimboni na yanashika Taifa zima, ni kuhusu hali ya elimu nchini kwetu. Maana ya hali ya elimu tuna vitu vinne vya msingi hapa, navyo ni suala la ufundishaji, suala la ujifunzaji, uelewa, na ufaulu. Vyote vinne ni lazima viende pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vinne kwenda pamoja sisi tumelisaidia Taifa, Musoma Vijijini, tumefanya mjadala kwa ngazi ya mkoa, halafu mimi mwenyewe nilikaa na ma-*head masters* wangu wote, na juzi tumefanya kwenye ngazi ya halmashauri, na hiyo ripoti nitawapatia Wizara ya Elimu, TAMISEMI, na Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili hii bajeti iende vizuri, namwambia *webmaster* aiweke kwenye tovuti ya jimbo kuanzia Jumatano, siyo leo. Kwa hiyo, hayo sina sababu ya kuyaongea, mtayapata huko, na yote yanafanana fanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote aliyoyaongea hapa Mheshimiwa Waziri namwomba sana, sisi Tanzania tumefanya vizuri kwenye nchi zinazoendelea na ndiyo maana tumepata fedha nyingi kutoka *World Bank*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri asisahau ile *SDG No. 04* (*Quality Education for All by The Year 2030)* ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri unakuja. Cha kwanza, ni ujenzi wa shule zetu kwa sasa. Dira yetu ya Maendeleo inaanzia mwaka huu. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na wanaonisikiliza, ikifika Juni mwezi ujao Watanzania tutakuwa milioni 70.55. Eneo letu la ardhi (Tanzania Bara na Visiwani) ukiliweka pamoja ni *kilometre square* 947,303, kwa hiyo, inamaanisha kwamba *population density,* yaani watu wanaoishi kwenye *kilometre square* ni watu 75 kwa mwaka 2025, tukifika mwaka 2050, Watanzania tutakuwa 137. Eneo la nchi yetu litakuwa hilo hilo, *population density* itakuwa ya watu 155 kwa *kilometre square* moja. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Elimu, na TAMISEMI, ujenzi wa shule ni lazima ubadilike. Ni lazima twende kwenye kujenga ghorofa sasa, twende juu kwa sababu ardhi haitatosha. Hilo ni pendekezo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni lazima tujue kuwa elimu ni ajira. Sasa hivi duniani kuna upungufu wa wafanyakazi wengi sana. Nikichukua *World Health Organisation* (Shirika la Afya Duniani), linasema ikifika mwaka 2030 upungufu wa wataalamu wa afya Duniani utakuwa 10,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukua Taifa kubwa kiuchumi duniani, Marekani, leo hii wana upungufu wa watu milioni 3.5 kwenye mambo ya uzalishaji viwandani na mambo ya sayansi na teknolojia. Nikichukua Ujerumani ambayo ndiyo ina uchumi mkubwa kwa nchi za Ulaya, leo hii wanapungukiwa watu 200,000 kila mwaka kwenye maeneo ya *engineering, IT,* na *construction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wizara ya Elimu ni lazima iweke maanani kwenye mitaala yetu kwamba elimu ni ajira. Nilishaongea hapa, na huwa sipendi kurudia yale yale. Nikasema watu kufanya kazi nje wanaleta fedha, imekuwa ni bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, elimu ni uchumi. Uchumi wa dunia wa sasa tukichukua *GDP* ya nchi zote duniani ni trilioni 116. Mwaka 2050 wakati tunamaliza Dira yetu mpya ya Maendeleo, uchumi wa dunia utakuwa trilioni 228; na kuna aina ya viwanda na biashara ambazo zitakuwa *engine* ya uchumi wa dunia toka sasa mpaka mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano hapa, kwanza ni *e-commerce (electronic commerce)* yaani biashara ya kidigitali. Mwaka 2022 mapato duniani yalikuwa trilioni nne, na mwaka 2040 biashara ya *e-commerce* mapato duniani yatakuwa trilioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili, nimemsikia Mheshimiwa Waziri Profesa anaongea, na aweke mkazo kweli kweli hapa kuhusu *Artificial Intelligence*. Sasa *Artificial Intelligence, software* na *services,* mwaka 2022 mapato yalikuwa bilioni 85 duniani, lakini mwaka 2040 mapato yatakuwa trilioni 4.6. Maana yake ni nini? Ni lazima Tanzania tuwekeze kwenye *science, technology*, na *Mathematics*. Sasa Tanzania tufanyaje? Nitatoa mapendekezo yangu, mengine ameyataja, mimi naongezea tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kama tunataka kwenda hivyo na hizo kazi duniani tuzipate, ni lazima sekondari zote Tanzania ziwe na maabara. Hii aichukue kama ambavyo wanajenga kwa nguvu maeneo mengi wanasahau kujenga maabara. Huu ndiyo msingi wa sayansi, ni lazima ufanye *practicals* toka *form one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili, Sekondari zote nchini ziwe na maktaba zenye kompyuta za kati. Inamaanisha kwamba ndugu zangu siku hizi vitabu vinatolewa bure. Sasa kama vinatolewa bure, ni lazima uweze kunyonya hivyo vitabu kupitia kwenye Kompyuta. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa na maktaba zenye vitabu na kompyuta ili vijana waweze kupata vitabu vya bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la tatu, kwa kuwa tumesema kwamba elimu ya nchini Tanzania itakuwa kidato cha nne. Ni lazima tuanze kuongeza kidato cha tano na cha sita, na tutaongeza kwa uwiano kwamba, kwenye kila Sekondari tano, tuweke *High School* moja ya Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mimi wa Musoma Vijijini ambaye sasa hivi nina sekondari 32, ninapaswa kuwa na *High Schools* sita za Masomo ya Sayansi. Hizi *high schools* tuachane na zote kukaa Wizara moja, hatutaenda kasi. Ni lazima tuzishushe kwenye halmashauri, ni lazima sasa *high schools* ziweze kusimamiwa na halmashauri zetu ndipo tutaweza kupata wasomi wengi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika na Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, pendekezo la nne, tujenge *technical colleges* za aina kama ilivyokuwa *Dar Tech*. Mnajua, *VETA* mtu anafanya kitu *mechanically*, anatengeneza kitu, lakini *technical college* mtu anauliza hata na sababu kwa nini hiki anakitengeneza? Kwa hiyo, kuna utofauti mkubwa sana. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *technical colleges,* na hizi tuzifunge kwenye sheria zisibadilishwe kama ilivyobadilishwa ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la sita, tuwe na wanafunzi wengi. Nimemsikia Profesa anasema, ila tuongeze wanafunzi wengi wanaokwenda kusoma nje, na tunachagua vile vyuo vizuri, siyo kuhesabu tu huko nje, vyuo vizuri. Nadhani Wizarani wanavifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri hapa, India inafanya maajabu na tunapeleka watoto kusoma India na China na bado

wao wanawapeleka kusoma nje. Angalia mwaka 2016 India ilikuwa na wanafunzi 440,000 wanaosoma nchi za nje mwaka 2023. Wamekuwa na wanafunzi zaidi ya milioni 1.4. Kwa hiyo, nasi tupeleke wanafunzi nje. Hawa wa India wanaosoma Ujerumani, 60% wanafanya shahada za *engineering* na mambo ya *Technology*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa kwa mchango mzuri. Kengele ya pili tayari, ushauri wako uandike ili Mheshimiwa Waziri aweze kuupokea na Serikali iweze kupitia.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuna wageni ndani ya Bunge:

Wageni wa Meshimiwa Profesa Mkenda. Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Umma na Binafsi, karibuni. *(Makofi)*

Wakurugenzi wasaidizi, wakuu wa taasisi zilizo chini na Wizara na maafisa kutoka Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Wadau wa maendeleo wa sekta ya elimu kutoka taasisi za Fedha; *CRDB, NMB, TCB,* na *NBC,* karibuni. *(Makofi)*

Wadau wa elimu kutoka taasisi za dini na binafsi, karibuni. *(Makofi)*

Madiwani wawili na Katibu wa UWT Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Bodi ya *Mkenda Cup* ikiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Themistocles Masae. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Viongozi wa CCM Wilaya ya

Mafia Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Mohamedi Faki Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mafia, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, wanafunzi kutoka Taasisi ya Teknolojia *Dar es Salaam Campus* ya Mwanza. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 100 na walimu watano wa Shule ya Sekondari ya Dkt. Samia kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Manya, jiandae Mheshimiwa Malleko.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na kama alivyoleta hoja ya kupewa fedha zinazofikia shilingi trilioni 2.4 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara hii, kadiri nitakavyochangia naunga mkono hoja, lakini nikisema kwamba kama ingewezekana basi tutakapokuja kwenye mchakato wa mwisho wa bajeti, bado anahitaji fedha kwa sababu ya mambo mapya na mazuri ambayo tumeyakubali na kuyaanzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaala unawataka wanafunzi wasome masomo ya amali. Ni hitaji la sasa baada ya nchi kufanya tathmini na kuona kwamba wanafunzi wetu wanamaliza vyuo na shule bila kuwa na ujuzi na kingi wanachokipata ni nadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri ni kwamba mwelekeo huu tunauchukua ukiwa ni mchakato ambao umekuwa ni jumuishi. Watu wengi wametoa maoni na wote tukafikia mahali tukakubali kwamba uelekeo huu ndiyo tunaoutaka kama nchi na kwa jinsi hiyo sitegemei tena kuweze kuwa na kupinduka pinduka hapo mbele kidogo. Tumekubali kwamba ndiyo uelekeo wetu, basi twende na uelekeo huo hata kama kutakuwa na mabadiliko, ni mabadiliko ndani ya uelekeo tuliouchukua kama nchi ili tusije kuwa tunakwenda mbele, tunarudi nyuma kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja yangu ninaijenga kwamba ili tuweze kupata wahitimu ambao tunawakusudia katika uelekeo wetu huu mpya na ndiyo maana nikasema yawezekana tukahitaji bajeti zaidi katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza natamani sisi kama nchi tujifunze kwa nchi ambazo zimefanya vizuri zaidi katika mwelekeo huu huko nje ya dunia. Unapopitia katika watu waliofanya vizuri zaidi hutaacha nchi ya Finland, Canada, na China, waliofanya vizuri katika upande wa mtaala huu wa amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukitaka tujifunze kwa waliofanya vizuri, maana ili ufanikiwe *learn from the best,* huo ndiyo unapaswa kuwa ndiyo uelekeo, yaani huwezi ukataka kuanzisha kitu kizuri halafu usijifunze, *just learn from the best. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuanza vizuri bila unyonge, bila udhaifu, hoja yangu na pendekezo langu ni kwamba walimu watakaofundisha mtaala mpya wasiwe walimu ambao hawakufunzwa vizuri. Wakiwa ni walimu ambao wametokana na mtaala wa zamani, lakini ukawa-*remodel* kidogo tu watapeleka ujuzi wao wa zamani katika mtaala mpya. Kwa hiyo, lazima tuwape mafunzo ya muda mfupi, na ya muda mrefu kwa wale ambao wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ushirikiano wetu, na hizo nchi ambazo tutaziainisha, aina ya mafunzo, na muda wa mafunzo waende wakapikwe vizuri. Wakishaiva, warudi ili *cream* ya kwanza ya watoto wetu katika mtaala huu wawe wamepikwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tutahitaji kujenga karakana, maabara na *studio* kwa ajili ya mafunzo hayo. Nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amedokeza jinsi ambavyo karakana hizi, maabara hizi na *studio* hizi zitajengwa. Sasa hoja yangu hapa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, siku za karibu ni mtakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *video clip* ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ambayo alionesha kwamba tulikuwa na madereva waliomaliza Chuo chetu cha Usafirishaji (*NIT),* wamefunza vizuri, walipokwenda kupata kazi nje wakakuta teknolojia imebadilika, wakashindwa kuendesha, lakini kwa hapa ni madereva walioiva vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapojenga karakana, maabara, na *studio* hizi lazima tuzingatie teknolojia ya sasa ili tusije tukakuta kwamba tunaanzisha mtaala wa amali, halafu tukaenda kuwafunza vitu vya kizamani ambavyo kumbe haitoleta tofauti na *VETA* zilizopo. Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo la kuwa tunajifunza teknolojia za zamani yawezekana pia ndiyo shida inayopatikana katika vyuo vyetu vikuu, kwa sababu tuna maabara za zamani, hatujawa-*equip* watu wetu kwa teknolojia za kisasa. Kwa hiyo, unakuta kwamba hata sayansi, *engineering*, *ICT*, na *medicine* bado tunakwenda kwa teknolojia za kizamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni eneo ambalo kama Taifa na ukiangalia *ICT* inakua haraka sana kiasi kwamba muda wetu ambao huwa tunaweka kwamba tutafanya *review* ya mitaala baada ya miaka mitano upande wa *ICT* unakuta umebaki nyuma nyuma kabisa. Maana ndani ya miaka mitano hata *laptop versions* zinakuja aina tatu ndani ya miaka mitano; wewe unatumia ya zamani unajikuta ukiwa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo lazima kama Taifa tuwe na *alert* kwamba teknolojia inabadilika sana, hivyo lazima katika vyuo vyetu tusiendelee na mwendo ule wa zamani tukajikuta kumbe kinachotokea nje ya nchi sisi bado tuko nyuma. Ili hili liwezekane, ni kweli kwamba lazima kila wakati wataalamu wetu waende waka-*brush* nje ya nchi kuona kwamba kinachobadilika kule, hapa pia kinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ili tuweze kufanya vizuri bado hatuna muunganiko mzuri baina ya Wizara, Taasisi za Serikali, sekta binafsi na vitu vinavyofunzwa kule vyuoni. Kwa hiyo, unakuta wanafunzi wanasoma hiki, katika sekta binafsi watu wanafanya hiki, halafu hatuwapi muda mzuri wa kwenda kujifunza kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ndani ya nchi hii tumekuwa na miradi mingi ya ujenzi wa *SGR*, maji, bwawa la umeme, ujenzi wa meli, na ujenzi wa barabara. Sasa jiulize ni wanafunzi wangapi ambao huwa wanapata *access* ya kuwa *interns* katika miradi hii mikubwa? *Hardly no*. Kwa hiyo, tunatamani kwamba kuwe na muunganiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachokifanya Wizara fulani, basi kiwe *reflected* katika mafunzo ambayo watoto wetu wanayapata kule vyuoni na wanawezaje kufanya hivyo? Ni kuwaongezea bajeti. Wakati mwingine watoto wanatamani kwenda kufanya *internship* au kwenda kufanya mafunzo ya vitendo, kinakuja kikwazo kimoja kinaitwa bajeti ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi upo, wanafunzi wapo radhi lakini chuo au taasisi husika haiwezi kuwapeleka pale kwa sababu bajeti ni ndogo. Aliyepaswa kukaa wiki nane anaambiwa sasa wewe kulingana na bajeti wanafunzi mmekuwa wengi, utakaa wiki mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo, tunakuja hatu-*impact* ujuzi ambao ulikuwa unakusudiwa, na ndiyo maana nikatangulia kusema kwamba yawezekana tukahitaji *more budget* mahali hapa kwa sababu kama tunataka watu bora, lazima ni wale ambao pia wanapata mafunzo na muda wa *intern* au *practical training* wa kutosha kwa bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tunaipongeza Serikali yetu kwamba imeweza kufanya watu wengi wakapata *access* na elimu ya juu kwa kutoa mikopo na Bodi ya Mikopo imeendelea kufanya vizuri. Hata hivyo, tunatamani watafiti wa mambo ambao wanatafiti changamoto zilizo katika jamii yetu ya

Kitanzania, lakini Serikali haitoi ufadhili kwa Shahada za Uzamili hapa nchini. Kwa hiyo, mara nyingi *product* ya watu wote unaowaona aliyesoma *Masters* na *Ph.D* ni zao la miradi ya wafadhili kutoka nje au alipata *scholarship* akaenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wewe una changamoto katika jamii yako ya Kitanzania, lakini hupeleki fedha ili kuwaandaa hawa watafiti ambao ni ngazi ya *Masters* na *Ph.D,* sasa unakuta wale wafadhili wanaotaka ku-*fund* wanapoleta miradi hapa nchini, wana ajenda yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, japo ndiyo watakwambia kwamba unajua lazima tu-*align* na malengo ya *SDG* na yale ya kwenu, lakini mara nyingi wana ajenda yao. Sasa sisi kama tuna ajenda yetu kama nchi, kwa nini tusitenge fedha katika maeneo maalumu, tukasema kwamba tunahitaji suluhisho katika eneo fulani na kwa jinsi hiyo tunatamani kwamba tuweze kuwapa wanafunzi wa *Masters* katika maeneo husika ili hao sasa waweze kufanya mafunzo hayo ya uzamili, baadaye walete suluhisho la changamoto zilizo katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, matokeo ya tafiti zao yaweze ku-*inform policy* yaani mara nyingi sera zetu hazitokani na utafiti mkubwa uliyofanywa na watu wetu. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo nadhani pia lazima tukubaliane kama Taifa ili tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliongea Mheshimiwa Prof. Muhongo alipokuwa anachangia kwamba mara nyingi tunapopeleka watu nje ni kwa sababu tu ya *opportunity* imepatikana katika nchi husika, siyo kwa sababu ya malengo yetu kama Taifa kwamba tunatamani kupata watu gani? Lazima tuwe *objective* katika eneo hili, kwamba tunatamani watu fulani, utaalamu fulani. Sasa huo tunaanda watu, na tunawasiliana na nchi husika ili tuwapeleke watu katika kufanya utaalamu husika, siyo kwa sababu rafiki yetu India ana *opportunity* 10 au mko wapi 10 mwende India.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa ni kengele ya pili. Nikupongeze kwa mchango mzuri, mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa. Nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Prof. Mkenda pamoja na Mheshimiwa Naibu wake Mheshimiwa Kipanga bila kumsahau Katibu Mkuu, Prof. Nombo na wataalamu wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa muda, naomba niende moja kwa moja kwenye zile mada ambazo nilikuwa nimekusudia kuzisemea siku ya leo. Nikianza na bajeti, nilikuwa naishauri sana Serikali kuangalia ni namna gani inaweza kuongeza bajeti ya sekta ya elimu ili iweze kufikia 15% ya Bajeti ya Taifa ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Wizara hii imebeba majukumu mengi na majukumu ya kimkakati ya kumwondoa na kumkomboa mwananchi au Mtanzania kutoka katika ile hali yake ya kutokuelewa jambo fulani na kumfundisha ili tuweze kuendana na soko la sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hii ya Bajeti, wakati anasoma Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 16 aligusia suala la kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali,

ufundi na ufundi stadi katika shule za sekondari na vyuo vya ufundi. Mimi ninataka kuongeza hapo ushauri wangu, kwamba hili jambo ni jema sana kwa nchi yetu kwa sababu jambo hili linaenda kuwa nyenzo muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi, na pia kuwezesha vijana wetu kuweza kujipatia kipato na zaidi kuweza kushindana katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kuishauri Serikali ione ni namna gani na njia bora zaidi ya kuweza kuimarisha mafunzo haya hasa kwa kutuambia ni namna gani imejiandaa kwa ajili ya kuwa na vifaa, lakini na wataalamu ili hili lengo letu liweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejiandaa tayari kwa ajili ya kujenga shule hizo za amali, na kuboresha vyuo vile vya *VETA*. Je, ni namna gani sasa tunaweza kupata vifaa vya kujifunzia tena vifaa vya kisasa na wataalamu ambao wataendana na teknolojia ya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nilisemee kwa sasa, je, bajeti yetu inaenda vipi kuiangalia na kuwa na mkakati, yaani iwe ni bajeti ya kisekta katika Wizara hizi za kisekta ambazo zinahusiana na elimu? Ni namna gani itakuja na mpango madhubuti wa kuweza kuajiri walimu wa kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zimejengwa, zipo za kutosha tunamshukuru Mungu, lakini ni namna gani ya kuweza kupata walimu au kuajiri walimu wa kutosha? Kwa sasa wanaajiriwa kwa mwaka walimu 10,000 mpaka 15,000. Tukienda kwa mtiririko huu tutamaliza zaidi ya miaka 15 tukiwa bado hatujaweza kuikamilisha changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali ione ni namna gani wataweza kujitahidi ajira zitolewe kwa mwaka 40,000 mpaka 45,000 ili tuweze kuondoa tatizo hili katika kipindi cha miaka mitano au miaka sita ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kushauri kwa wakati huu ni kuhusu uwiano wa kitabu

kimoja kwa mwanafunzi mmoja. Tunaishukuru sana Serikali imeweza kupigania jambo hilo, lakini sisi tunaomba kushauri kama Kamati, Serikali ione namna gani basi itatenga bajeti ya kutosha pamoja na kusambaza vitabu hivi kwa wakati, kwa sababu jambo la kutenga bajeti ni lingine lakini kuhakikisha vitabu vinawafikia wanafunzi kwa wakati ni jambo lingine, na ni bora zaidi. Nilikuwa naishauri Serikali ione ni namna gani vitabu vitawafikia wanafunzi kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iendelee kuangalia ni namna gani itaendelea kuchapisha vitabu kwa wakati, lakini kulingana na mahitaji, na wakati huo huo tuendelee kuangalia ni namna gani tutaenda kuwa na vitabu au kufundisha kidigiti ili kupunguza namna ile ya kwenda kuchapisha kitabu kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kusisitiza kwa mchango wangu wa leo ni namna Wizara hii itaweza kuangalia ni namna gani tunaweza kuifanya lugha ya alama kuwa ni somo la lazima shuleni na katika vyuo kwa kila mwanafunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Kenya na *South Africa* na baadhi ya shule wameanza kufanya jambo hili. Jambo hili linasaidia kuweza kuwasiliana na ndugu zetu hawa kwa sababu unakuta wakati mwingine inakuwa ni vigumu sana kwa sababu tunasema ni elimu jumuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapokuwa ni elimu jumuishi, na hawawezi kuwasiliana na watu hawa inakuwa ni shida. Kwa hiyo, inapendekezwa kwamba Lugha ya Alama ifanywe kwamba kuwa somo la lazima shuleni ili watu wengi zaidi wawe wanajua namna gani ya kuwasiliana na ndugu zetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nilitaka kuishauri Serikali kwa siku ya leo ni namna gani ya kuongeza ruzuku ili kuweza kuwapatia mabinti wa kike taulo za kike, kwa sababu imekuwa ni changamoto kubwa sana ambayo

inawafanya mabinti wengi mpaka sasa kushindwa kwenda shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie ni namna gani inaweza kutenga bajeti kwa ajili ya kusaidia mabinti zetu hawa kupata taulo za kike? Pamoja na hayo, kuna vituo ambavyo ni vya kuimarisha utambuzi na upimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri hivi vituo viwekwe kwenye kila halmashauri ili kuweza kusaidia walimu kutambua wale wanafunzi wenye matatizo kwa sababu kuna wakati mwingine wanafunzi wana matatizo ya kusikia, lakini hawajafanyiwa upimaji na utambuzi mapema, kwa hiyo, inakuwa ni changamoto kwa mwalimu kuweza kumfundisha kwa namna na yeye alivyo. Kwa hiyo, inakuwa inawawia vigumu wanafunzi hawa kuweza kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Jioni tutaanza na Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Simon Songe, Mheshimiwa Chikota, Mheshimiwa Mulugo, na Mheshimiwa Jesca.

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nilishamwita Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Simon Songe na Mheshimiwa Chikota.

Mheshimiwa Manyinyi hayupo, karibu Mheshimiwa Simon.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazoendelea kufanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anazoendelea kufanya kwenye Wizara hii ya Elimu pamoja na wasaidizi wake akiwemo Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu Prof. Nombo. Nampongeza sana na tunaendelea kumwombea katika kazi anazofanya za kuhakikisha elimu katika Taifa letu inaendelea kuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kuwapongeza watumishi wa Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa ambazo wanafanya tukiamini kabisa kwamba elimu itaendelea kuimarika kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maeneo mawili ambayo nataka nichangie jioni hii. Eneo la kwanza, naendelea kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuja na hoja kubwa kuanzia mwaka 2023 ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi ambavyo vinaendelea kujengwa katika wilaya zetu. Nakiri hata Busega

tayari tumepata chuo hiki ambacho sasa kinaendelea kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, na Mheshimiwa Waziri kwa kazi ambayo inaendelea kwenye majimbo yetu. Walianza na vyuo 29 na hapa katikati walikuwa na vyuo 64 *plus one* kwa maana ya 64 katika wilaya zetu na kimoja katika Mkoa wa Songwe kule kwa Mheshimiwa Hasunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili pamoja na kuwa ujenzi unaendelea, lakini hapa katikati ulikuwa unasuasua. Mwaka 2022/2023 tulipitisha hapa bajeti ya kupelekewa shilingi bilioni 100 katika Wizara yetu ya Elimu, lakini mpaka tunapozungumza hapa, zimeshapelekwa shilingi bilioni 74.6, bado shilingi bilioni 25.4 ambazo hazijapelekwa kwenye Wizara yetu ya Elimu ili kufanya utekelezaji wa ujenzi wa *VETA* hizi kwa awamu ile ya kwanza kwa maana ya majengo tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha, bahati mbaya siwaoni hapa, lakini naomba sana Serikali kuchukulia maanani kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapelekwa kwa watu wetu hawa wa Wizara ya Elimu ili ujenzi wa *VETA* sasa uendelee kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *objectives* za ujenzi wa *VETA* hizi ni nzuri sana, kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata mafunzo ili waweze kujiajiri na waweze pia kuajiriwa. Wanafunzi mbalimbali ambao wanatamani kwenda kwenye hivi vyuo ni wengi ambao bado hawajapata nafasi ya kwenda kwenye vyuo kwa sababu ya uchache wa vyuo vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muda mwafaka sasa Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba inapeleka fedha hizi shilingi bilioni 25.4 zilizobaki ili Wizara ya Elimu iweze kukamilisha hatua ya kwanza ya majengo tisa ili yaweze kukamilika katika maeneo yetu. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Fedha ipeleke fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, nimeona amesema kwenye hii bajeti kwamba kuna

mwendelezo wa awamu ya pili ya majengo mengine nane kama sikosei. Niendelee kuiomba Serikali na niendelee kuiomba Wizara ya Fedha, watakapopitisha bajeti hii, basi wapelekewe. Nia yetu ni kuona watoto wanapata sehemu ya kwenda kusoma ili wapate ajira na waweze kujiajiri, hao ambao tutakuwa tumewapangia kwenye vyuo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru chuo kikikamilika kwa wakati ili wananchi wa Jimbo la Busega waweze kukitumia chuo hiki ambacho Mama Samia amewapa kwa ajili ya huko baadaye waweze kupata sehemu ya kupata elimu. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Wizara ya Fedha ipeleke fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, hapo hapo kwenye eneo la *VETA*, sijajua ni namna gani Mheshimiwa Waziri amejipanga kupata wataalam, kwa sababu tunaamini vyuo hivi 64 vitakamilka, lakini vinaweza vikakamilika na vikakosa wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo lingine la pili ni kwa namna gani wanaenda kuandaa wataalam ili waje wahudumie vyuo vyetu kuhakikisha kwamba wanaenda kuwafundisha hawa Watoto? Ni eneo mojawapo ambalo pia lazima tulichukulie maanani ili tunapoenda, tuhakikishe vyuo hivi vimekamilika kwa maana ya majengo, basi na wataalam wawe tayari ili waweze kwenda kuwafundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona tusiishie hapo. Kwenye eneo la vifaa, pia sasa hivi tunaweza kuwa tunasema majengo, kumbe mpango wa ununuzi wa vifaa ukachelewa. Ni vizuri zaidi mpango huu na wenyewe ukaendana kama tunavyoenda kujenga majengo, na pia twende kwenye hatua ya pili ya ununuzi wa vifaa ili majengo yanapokamilika na vifaa viwe tayari ili watoto wetu waweze kupata sehemu ya kusoma, na majengo haya yasiendelee kuwa majengo tu, bali yapate vifaa ambavyo vinahitajika katika maeneo yetu ya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo lingine la pili ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumzia kwenye bajeti yake,

naomba Wizara ya Fedha iweke kipaumbele kwa sababu majengo yameshaanza, na vyuo hivi vimeshaanza kupata majengo, sasa yatakapokamilika, ni vizuri yapate vifaa, walimu wapatikane, ili tuweze kuhudumia vizuri majengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni la mtaala mpya. Tumeona mwaka 2024 tumepitisha mtaala mpya ambao sasa elimu ya msingi itaishia darasa la sita, na ninafikiri itakuwa mwaka 2027 kama sikosei, lakini mwaka huo kutakuwa na darasa la sita na hapo hapo kutakuwa na darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu, sijaona mpango ni kwa namna gani madarasa haya mawili yote watakwenda kuya-*accommodate* mwaka 2028. Mpango huu unatakiwa uanze sasa. Tunavyozungumza nilitamani kuona kuna mpango wa namna gani madarasa mawili haya kwa mwaka mmoja 2028 yatakapokuwa yanaingia *form one* tuwe tayari na miundombinu ya kuwatosheleza watoto watakaoingia kupitia haya madarasa mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni eneo mojawapo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* kesho, natamani kumsikia akizungumzia ni kwa namna gani wamejiandaa kuhakikisha kwamba tunapofika mwaka 2028 haya madarasa yote mawili yatakuwa *accommodated* kuhakikisha kwamba miundombinu ipo, na ni salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye eneo hili la kubadilika kwa mtaala, nimeona tutakapoingia huku sekondari kwa maana ya kidato cha kwanza, wanafunzi watakuwa na *option* mbili, mwingine ataenda kusoma masomo haya ya kawaida kwa maana ya *Physics, Chemistry* na mambo mengine, lakini kuna wengine ambao wataenda kwenye *vocational training skills* pale pale kwenye shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni zuri, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa maana ya Katibu Mkuu kwa kazi kubwa waliyofanya ya mtaala. Wasiwasi wangu kwa hao watoto ambao watakwenda kusoma *skills* za *vocational*

*training* kwenye sekondari, sijaona mpango ambao amekuja nao wa kitu kinaitwa maabara, wanaita wataalam *training factory. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo *training factory* itawasaidia watoto kama ambavyo tumekuwa tukiwasaidia watoto wanaosoma *Physics* wanapata darasa lao la *practical*, wanaosoma *Chemistry* wanapata darasa lao la *practical* na wanaosoma *Biology* wanapata darasa la *practical.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatamani sasa watoto wetu ambao wataenda kwenye *skills* za *vocation* kwenye sekondari zetu, pia tuwe na darasa lao la *practical.* Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tunapeleka vifaa kwa ajili ya *training factory* na vifaa hivi, basi vinaweza kugawanywa katika shule zetu za kata na ikionekana bado tunasuasua, basi tuanze hata kwenye shule mojawapo kwenye tarafa ili tuweze kuwasaidia watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kwenye eneo hili la *training factory* ni lazima tuangalie, kulingana na uzalishaji wa mazao ya kilimo kwenye eneo husika, tuhakikishe kwamba tunaenda kwenye eneo la kilimo, kwa maana ya Simiyu, sasa tunazungumzia pamba, ni *training factory* zipi ambazo zitaendana na uzalishaji wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda huko kwenye chai, tukienda huko kwenye kahawa, twende huko kwenye nini, tuhakikishe kwamba watoto hawa wanapokuwa wanajifunza, wakati hawa watu wa *Physics* wanaenda kwenye *practical,* hata hawa watu wa *skills* za *vocation,* waende kwenye *practical* yao ili anapomaliza *form four* awe na kitu ambacho anaweza kwenda kufanya kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sasa ndiyo itakuwa tija kwa mtaala mpya ambao tumeutengeneza na ndiyo itakuwa tija kwa namna gani tumewekeza kwa hao watoto ili tuone mabadiliko chanya kwa Watanzania wetu na watoto wetu katika hali nzima ya ufaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimesikia kengele, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota, jiandae Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo Mezani kwetu. Niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Mkenda; Naibu Waziri; Katibu Mkuu, Prof. Nombo; Naibu Makatibu Wakuu; Kamishina wa Elimu; na Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizopo kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya kwenye sekta hii ya elimu. Tumeona bilioni nyingi za fedha zinakwenda katika programu zetu hizi zilizopo katika *level* ya shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mradi wa *BOOST* kuna bilioni za fedha zinakwenda kule. Tuna mradi wa *SEQUIP* kwa elimu ya sekondari, lakini kwa elimu ya juu tuna mradi wa *HEET*. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji huo mkubwa ambao anaufanya kwenye sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha Waziri kimejaa takwimu, tena zenye matumaini makubwa sana kwa nchi yetu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. Mchana huu nimepitia kitabu hiki mara mbili, nikaona kwamba yale yaliyomo yakipata fedha kutoka Wizara ya Fedha, basi tutakuwa tumeingia kwenye hatua nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu Wizara ya Fedha kama walivyosema wenzangu, tutoe fedha ambazo zimeombwa na Mheshimiwa Waziri ili wakatekeleze yale ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna matumaini mengi kwenye taarifa hii, nimekuja na mengi ya kupongeza na kushauri. Kwanza, kwa miaka mitatu hivi tulikuwa tunazungumzia Chuo Kikuu; *University College* ya Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema kwamba wakati wa miaka 2000 tunapotekeleza mipango mikubwa ya elimu, ule Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MEM)* na ule Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MES),* kulikuwa na andiko lilitolewa pale kwamba ili kukabiliana na changamoto ya walimu wa sayansi, vyuo vitatu vibadilishwe, badala ya kupewa mafunzo ya ngazi ya kati, basi iwe sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Ualimu Dar es Salaam, Chuo cha Ualimu Mkwawa na Chuo cha Ualimu Mtwara.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitekeleza vyuo viwili, *DUCE* ilianza pale Dar es Salaam tukaona Mkwawa nayo ilibadilishwa, lakini Mtwara ikawa kimya. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba ile *document* ambayo kwa miaka 20 haikutekelezwa, sasa anaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa, sasa Chuo cha Ufundi Mtwara na Chuo cha Ualimu Mtwara vitabadilishwa sasa na kuwa *University College* ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya. Tunamshukuru sana kwa usikivu, tunaishukuru timu ya wataalam, Prof. Nombo na timu yake kwa kusikiliza kile ambacho tumekuwa tunakisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu sasa kwa sababu vyuo hivi viwili majengo yake yamechakaa, havina majengo ya kutosha, na tumeona kwenye bajeti wamesema wametenga fedha kwa ajili ya kuongeza majengo na vifaa kwa vyuo hivi ili sasa viwe kama sehemu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na *specifically* kwa ajili ya kuandaa walimu kwa ajili ya ule Mkondo wa Amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna kitu kinaitwa *skill over effect.* Kila palipo na chuo kikuu lazima majirani zake waathirike.

Kwa hiyo, nina ushauri kwamba, Profesa na timu yake watengeneze programu za muda mfupi hasa za kutoa ujuzi na maarifa kwa vijana na wakazi wa maeneo yale ili nao wapate ufundi ambao utatolewa wakati wanatayarisha wale walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, ni matarajio yetu sasa shule ambazo zipo katika maeneo hayo zinufaike kama sehemu ya *training,* kwamba kwenye *block teaching,* shule za jirani za amali zinafaidika na kile kitakachopikwa kwenye vyuo hivi viwili vya Mtwara kawaida na Mtwara Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakushukuru kwa kusikiliza kilio chetu na ninamtakia kila la heri katika utekelezaji na nimwahidi Wabunge wa Mtwara tutampa *support* katika utekelezaji wa kufanya mabadiliko hayo makubwa ya kubadilisha vyuo hivyo viwili kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia kule Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, kama walivyosema wenzangu, tumeshaanza kutekeleza mtaala mpya kwa maana ya utekelezaji wa Sera yetu ya Elimu ya Mwaka 2014, lile Toleo la 2023 tunafanya mambo mengi katika utekelezaji wa mtaala huu ikiwemo ongezeko la miumdombinu na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapoanza utekelezaji wa mtaala huu, vilevile tujikite au tujitayarishe na namna ya upimaji wa mtaala huu. Upimaji ni sehemu muhimu sana, kwa sababu mtaala wetu ni *competence based,* hatutarajii upimaji wetu uwe kama tulivyofanya kwenye mtaala uliopita. Kwa hiyo, naomba tufanye matayarisho, na upimaji siyo suala la bahati mbaya ni suala ambalo linahitaji matayarisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, walimu katika ngazi zote watayarishwe namna ya kuwapima wanafunzi wao, walimu wa awali, walimu wa shule za msingi na walimu wa sekondari, lazima watayarishwe namna ya kutayarisha yale maswali kwa sababu tunatarajia upimaji wetu ujikite kwenye ujuzi na ufundi na siyo kumbukumbu ya kile alichojifundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mitihani yetu mingi sasa hivi ukiipitia inamtayarisha mtoto kukariri ili kesho akayamwage kwenye chumba cha mtihani. Hatutarajii kwamba upimaji tutakaokwenda nao uwe wa namna hiyo. Ni lazima Baraza la Mitihani lifanye *review* ya utayarishaji wa mitihani yake ili tupate mitihani ambayo kweli ina lengo la kupima kile ambacho tunakikusudia, lakini tukifanya mitihani kama mazoea, kwa kweli hatutapata kile ambacho tunakitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata muda wa upimaji hatutarajii unapotaka kupima ujuzi na ufundi aliyoupata mtahiniwa ukatumia dakika 40 kwenye chumba cha mtihani. Haiwezekani unapotaka kupima ujuzi na ufundi, ukatumia masaa mawili ukapima mwanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima tufanye *review* tuangalie sasa tutawapima vipi wanafunzi wetu au wahitimu wetu katika ngazi mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya tatu ni *in service training,* yaani mafunzo kazini kwa walimu wetu. Hiki ni kitu muhimu sana. Mafunzo kazini yana faida kubwa sana. Nitataja faida tano tu. Faida ya kwanza ni kukuza utendaji. Unapompa mafunzo mapya, basi unaimarisha utendaji wa yule mtumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, mtumishi anapata maarifa mapya, mwalimu anaongezewa maarifa, lakini unakuza uhusiano wa kupata marafiki wapya wakati wa *training*. Vilevile, unaongeza ufahamu wa kile unachokifahamu. Pia cha tano, hakuna *in service training* ambayo inakwenda bure, inaongeza kipato kwa mtumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, nimeona hapo *figure* ambazo amezitoa katika kila ngazi. Kwa kuwa walimu ni jeshi kubwa na sehemu kubwa ya watumishi wa umma ni walimu, basi lazima tutafute fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo kazini ya walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwekeze mafunzo kazini kwa walimu. Walimu lazima wapate taarifa na maarifa mapya. Tusipofanya hivyo tutakuwa na walimu ambao sio wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mulugo amerudi, kwa hiyo, ataanza yeye halafu atakuja Mheshimiwa Jesca, halafu Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara hii. Huwa nasema miaka yote kwamba Wizara ya Elimu ni Wizara yangu. Naomba ku-*declare interest* kwamba mimi mwenyewe ni Mwalimu, na uhai wa maisha yangu yote kwa kweli yametokana na Wizara ya Elimu. Nimeishi kama Mwalimu na vilevile nimeshawahi kutumika kama Naibu Waziri wa Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nichangie tu kwamba cha kwanza naomba niipongeze sana Serikali kupitia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo tunaendesha elimu yetu nchini na namna ambavyo Serikali imewekeza sana kwenye Wizara hii ya Elimu. Hata huko TAMISEMI tumeona mambo yanavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mkenda pale, na ndugu yetu Naibu Waziri pale kwa namna ambavyo sasa hivi wanaiendesha Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa mhanga mkubwa sana na matamko ya huko nyuma tulivyokuwa tukienda, lakini hii miaka miwili nimekuwa naona tumeacha kabisa matamko matamko ya Wizara ya Elimu, sasa hivi yamepungua. Kila tunapofikia Januari unaona kuko salama, tunapofikia Julai kwenye mihula, tuko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi huko tunaokuwa tunaishi na watoto huko na tunaishi na walimu, nami ni kiongozi wa shule za *private* hapa nchini, na-*declare* kabisa kwamba sasa hivi kuna amani na ndiyo maana mnaona hata leo watu wa *TAMONGSCO* hapa hawapo, watu wa TAPIA hapa hawapo, ni kwa sababu huko kwetu tayari kuna amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimwia Profesa Mkenda pamoja na Katibu Mkuu, na Naibu Waziri, na viongozi wote ambao wapo pale Wizarani. Sasa hivi wanashirikisha na wanatusikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kilikuwa ni kilio cha mara kwa mara toka mwaka 2010, tunalia hapa kwamba jamani hebu mwashike shule za *private* na sisi shule za Serikali tukae pamoja tuweke mtaala pamoja. Tunashangaa nchi inakwenda pamoja, kwa sasa tunawafundisha watoto wetu pamoja. Watoto wetu wote wanasoma huko, kwa hiyo, lazima twende pamoja. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tukisimama hapa, tuko na akina Rweikiza hapa, na akina Marehemu Ester Mahawe, yaani tunakuwa tumekasirika kasirika hivi, Waziri alikuwa hatuangalii vizuri. Leo hii Mheshimiwa Waziri nampita tunasalimiana, tunaongea jambo linaeleweka; namshauri anasikia; Mheshimiwa Naibu Waziri tunakunywa naye chai pale tunashauriana, tunasikilizwa, mpaka nao wenyewe wanatushauri na sisi tunasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapokwenda kwenye Sera Mpya ya Elimu, naona kabisa tuko pamoja. Mheshimiwa Waziri siku moja tulikaa wote pale kantini nikawa najaribu kumpa mawazo ya namna kwamba hizi shule za *private* kama ambavyo nimesema, sasa hivi shule nyingi zimekosa wanafunzi huko kwa sababu ya elimu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bure inakwenda huko na wazazi wana-*opt* huko na kwa sababu tuna walimu wazuri Serikalini, tuna vitabu vizuri, tuna mtaala mzuri naye anasimamia

elimu vizuri. Kwa hiyo, wazazi wengi wana-*opt* kwenda huko. Vilevile, madarasa ambayo yamebaki *empty* kuna madawati yapo huku, kuna walimu vilevile wapo. Hebu warudi sasa wageuke nyuma waweze kurudi huku sasa waanze kujaza watoto kule kwa sababu ni jambo dogo tu kufanya *calculation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna-*calculate* kwamba hii shule ina madarasa labda 10, walimu kadhaa mnaweza aidha mkanunua au mka-*share* na yule mmiliki wa shule mkafanya ili mambo yaende, kuliko kila siku tunapeleka fedha kwa ajili ya kujenga tu kumbe kuna shule nyingine bado ziko tu ambazo zimekaa *empty* na mambo yanaweza yakaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu nimeona wamechangia hapa kuhusu hii Sera Mpya ya Elimu ya mwaka 2014 mpaka sasa. Nataka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunaanza mfumo wa MEMKWA, MMEM na MMES, mimi nakumbuka nilikuwa Mwalimu na nilikuwa *headmaster* wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulihangaika sana na namna ya kuanza, lakini leo hii tunaona matunda ya MEMKWA, tunaona matunda ya MMES tunaona matunda ya MMEM. Hata hii Sera Mpya tunapokwenda, baada ya miaka 10 ijayo tutakuja kuona mambo yatakavyokuja kuwa mazuri baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kama Serikali haiwezi kwamba siku moja hii tayari itakuwa imeweza kwenda kule Chunya ikaweka madarasa yote yana Amali, iende Bukoba ikaweke madarasa yote ya Amali, ije Dodoma kwa wakati mmoja, hapana. Ndiyo maana Serikali imetoa fedha, kila mkoa tumepata shule moja kwa jili ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wabunge wote hapa mnahakikisha kwamba kila mkoa Mheshimiwa Rais ametoa fedha ili kila mkoa uwe na shule moja kwa ajili ya elimu ufundi kwa ajili ya Amali. Kwa hiyo, tunakwenda huko na baadaye tutakwenda sasa kila wilaya ipate hiyo shule na baadaye kila kata kama ambavyo tumekwenda kwenye MMES na MMEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwe wavumilivu, mambo haya yanaenda pole pole na ndiyo maana nilikuwa nimesema kwamba hata kwenye shule za *private* tupeni uhuru twende benki. Mkituhakikishia nyie kwamba sisi twende benki tukakope vifaa, tukakope mashine, watu wa *carpentry,* watu wa nini, twendeni huko tukakope mafundi umeme na tujenge vifaa vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishaweka kwenye shule, je mtatuletea watoto ili watoto wale waweze kusoma haraka kuliko tunavyoweza kuchelewachelewa hivyo wakati tuna uwezo sisi wa kufanya vitu kama vile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye shule yangu Mheshimiwa Waziri alishawahi kunishauri kwamba, "njoo Wizarani tukupe barua uende ukakope hela benki, ukienda *CRDB* wanakupa hela shilingi bilioni moja, unaenda kununua vifaa kwa ajili ya watoto wako wa chekechea wale, *nursery* mpaka huko *primary* ili waweze kuanza kufundisha elimu ya Amali." Hata hivyo, sasa hivi tunaogopa kwa sababu hawajaturuhusu bado na hata akiniletea watoto, atashangaa baadaye wamehama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuhakikishiwe kwamba tukifanya hivyo tunaweza tukapata wanafunzi ili tuendelee kuwafundisha. Ni Watanzania wote kwa pamoja tusaidiane kama ambavyo sasa hivi wanatusikia, nasi tusikiwe kwamba tuanze kusaidiana. Sasa shule za *private* zipewe uhuru, tuletewe wanafunzi, sisi tuwafundishe kwa sababu sisi walimu tunao na mambo yataenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri kuhusu masuala ya *VETA* yanafanana fanana na elimu ya ufundi hii. Kule Jimboni Songwe mimi nimepewa *VETA* mwaka huu sasa ni wa tatu tunajenga, lakini iko *very slow*. Tunaona yaani fedha haziji mpaka wameezeka tu, lakini haijaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri angeweza kunisaidia, tupate fedha kidogo kwenye bajeti yake

hii, angalau basi na sisi tuanze kwa sababu naona wilaya nyingine *VETA* zimeanza, lakini kule Songwe kwa kweli bado kunasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa nimetoka kantini kule, kuja kumpongeza tu Mheshimiwa Waziri namna ambavyo ameituliza Wizara ya Elimu. Yaani sikuwa na chochote, ndiyo maana unaona naongea hapa kwa kumpongeza tu na Naibu wake. Kwa kweli Wizara imetulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena, Wizara ya Elimu sasa imetulia na nchi nzima inisikilize na walimu wenzangu wa shule za *private* wanisikilize; Katibu Mkuu, Kamishna wa Elimu, mzee nani pale Wizara wameituliza, na hii yote ni kwa sababu walitusikiliza ushauri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulimwambia Mheshimiwa Waziri sasa hivi hakuna kutoa waraka wowote bila Waziri kuuona. Huyu ni mwanasiasa, anajua nchi ilivyo huko nje. Kamishna anapotoa waraka wowote; sijui watoto wasilale kwenye mabweni, mabasi sijui nini, yaani kulikuwa kama vile kuna vurugu vurugu hivi, kila mtu anajichukulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaja nikamwambia, "Mheshimiwa Prof. Mkenda, wewe ndio Waziri wa Elimu. Tutakuwa tunakusema wewe kumbe wanaharibu watu wako wa chini." Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ashike hiyo kamba na ninamwombea Mungu kule Rombo wamrudishe aendelee kuwa Waziri wa Elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilimwita Mheshimiwa Manyinyi, alikuwa hayupo, amerudi. Kwa hiyo, anaendelea Manyinyi halafu ataingia Mheshimiwa Jesca.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hii Hotuba ya Waziri wa Elimu. Naendelea sana kuishukuru Serikali yangu kwa namna ambavyo imejitahidi sana kufanya mambo makubwa na mazuri hasa katika huu upande wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka michache tu iliyopita tulikuwa na changamoto kubwa kwenye shule za sekondari, tulikuwa na changamoto kubwa kwamba wanafunzi wengi walikuwa wanafaulu lakini hakukuwa na vyuo. Pia kulikuwa na changamoto kubwa hata katika mikopo. Sasa ukiangalia katika hiki kipindi mambo mengi sana yameboreshwa na vijana wetu wengi sasa wanasoma vizuri zaidi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunakoenda sasa walau hata yale matumaini makubwa yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu sasa, baada ya kuwa wanafunzi wengi wanaweza kusoma mpaka wakamaliza vyuo vikuu, changamoto kubwa ambayo iliyopo ni ya ajira. Leo ukiangalia watoto wengi wanamaliza vyuo, akishamaliza mzazi unakuja tena kupata mzigo mkubwa wa kumpatia ajira kwa sababu hizo ajira zenyewe hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo kibaya zaidi unakuta kwamba nafasi za ajira zinatoka, lakini wale wahitaji ni zaidi ya 5,000 au 10,000 lakini nafasi zenyewe ni nafasi 500 au1000. Kwa hiyo, hapo napo sasa imekuja kupatikana changamoto nyingine kubwa ambayo tunadhani na yenyewe itaendelea kutusumbua kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu sisi Wabunge kazi yetu ni kushauri, basi nashauri katika baadhi ya maeneo katika hiki kipindi tuone ni namna gani tunaweza kuwasaidia vijana wetu hasa wale wanaomaliza vyuo, na baada ya hapo sasa wanakaa nyumbani wakiwa wanahangaika kila siku na bahasha kwa ajili ya kutafuta kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa elimu, kwa bahati nzuri kwa Tanzania kama nchi sisi ndiyo waasisi wakubwa wa lugha ya Kiswahili, na lugha ya Kiswahili ni kati ya lugha ambayo sasa inakua kwa kasi na nchi nyingi zinaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, leo katika utafiti tu mdogo wa haraka haraka hata kwa wenzetu wa nchi jirani, wao ndio wanaweza kutumia fursa hiyo ya kutoa walimu

wengi kwenda kwenye nchi za wenzetu kwa ajili ya kufundisha Kiswahili. Leo unaposema unataka labda nchi nyingine ziweze kujifunza Kiswahili, wanahitaji tu vitu vichache sana. Watu wengi wanahitaji ajue kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia suala la kusoma na kuandika ni suala ambalo halihitaji Mwalimu aliyesomea Kiswahili *per-se* na kwa sababu halihitaji Mwalimu aliyesomea Kiswahili *per-se* kumbe sasa walimu wetu wote wale ambao ni ma-*graduate* katika masomo mbalimbali yawe ya Kiingereza, Historia na masomo yote hayo, bado anaweza kufundisha somo la Kiswahili ilimradi yeye alisomea Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, leo tukiamua, ninaamini kwamba tunaweza tukapeleka watu wengi zaidi duniani, na vijana wengi zaidi tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda kwenye nchi yoyote ile, nenda hata Ufaransa; kwa bahati nzuri sisi kama Tanzania tunazo Balozi mbalimbali katika nchi mbalimbali. Sasa leo tukiamua tu kwamba kila nchi ambayo tuna Ubalozi nayo, ambao wanahitaji kujifunza Kiswahili, tunaweza tukawaambia zile Balozi zetu watenge tu pale vyumba vichache, halafu tukawa na walimu pale na hao walimu tukajaribu kutangaza, watu wakafahamu kwamba tunafundisha Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini kwamba kwanza watu wengi watapenda kujifunza Kiswahili kwa sababu watakuwa wanajifunza tu katika muda labda wa saa mbili kwa siku na kwa sababu ni Kiswahili cha kusoma na kuandika ambacho ndicho watu wengi wanakipenda, basi kwa hiyo, itatupatia nafasi kubwa sana ya sisi kupata wanafunzi wengi katika hivyo vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, kwanza tutapata mapato kama nchi. Pili, ni kwa sababu sasa vijana wetu wengi wako huko duniani na wanafundisha Kiswahili, tafsiri yake ni kwamba watakuwa wamejipatia ajira. Kwa hiyo, tunadhani kwamba hilo nalo ni mojawapo ya eneo ambalo tukilitumia vizuri

tunaweza vijana wetu wengi ambao wanakaa bila kazi wakaweza kupata ajira na maisha yao yakaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, eneo lingine tunadhani sasa ni wakati muafaka ambapo tungeshusha nguvu zaidi kwenye hivi vyuo vya kawaida ambavyo ndivyo vina watumishi wengi. Yaani leo ukiwa na watoto wawili, mmoja amemaliza chuo kikuu amesoma *sociology*, mwingine amemaliza tu kidato cha nne akaenda *VETA*, yule wa *VETA* bado kwako au yeye mwenyewe anaweza kuendesha maisha zaidi kuliko yule wa chuo kikuu, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, yule wa chuo kikuu maana yake ni kwamba mpaka apate ajira ile aliyoisomea ndipo maisha yaweze kuendelea, lakini kile tu kitendo cha kujiona amesoma amefika chuo kikuu maana yake kila mara anaanza kufikiria namna ya kupata ajira. Kwa hiyo, tunadhani leo tukiendelea kuimarisha vyuo kama hivi vya *VETA* pamoja na hivi vyuo vidogo vidogo vya ufundi vinaweza vikasababisha watu wetu wengi zaidi wakapata ajira. Vyuo vya kilimo, Vyuo vya mifugo vitasaidia kuliko hali hii tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda tu kwa wenzetu hapo Kenya wana vile vyuo vya ujasiriamali, huu ufundi mwingi mwingi wanafanya na kwa kweli unakuta wanakutengenezea vitu vingi na vizuri, lakini wanaita Juakali. Sasa Juakali kama hizo ukiangalia kwa majirani zetu, vimewapatia ajira kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumbe hata kwenye nchi yetu kama hii Tanzania tukiendelea kuzisaidia akina *SIDO* zetu, tukasaidia na hivyo vyuo vingine, kwa hiyo tafsiri yake ni kwamba vijana wengi zaidi wataweza kujiajiri na maisha yao yakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali tuliyonayo sasa hivi ni kwamba tuna kundi kubwa la vijana wana elimu nzuri wame-*graduate* lakini kila siku wanatembea na bahasha wanatafuta kazi. Kutokana na hali hiyo, maana yake ni kwamba vijana wetu wanaendelea kusota badala ya kuwasaidia katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca, wajiandae Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Getere.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nami moja kwa moja naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Pia, napongeza kwa Sera ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 ambalo tunaendelea nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeendelea kuwa na sera mbalimbali za elimu tangu tulipopata uhuru na lengo la kubadilisha sera zile kila wakati ilikuwa ni kuendana na wakati na mabadiliko ya wakati huo, lakini pia kupata tija kutoka kwenye elimu kutokana na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1962 tulikuwa na Sera ya Elimu ambayo lengo lake kubwa ilikuwa ni kuangalia baada ya kupata uhuru, kuna nafasi nyingi ambazo zilikuwa zimeachwa wazi. Kwa hiyo, ilitakiwa kuandaa Watanzania haraka ili kuweza ku-*feed* nafasi hizo. Hilo lilifanyika kwa kuanzisha *program* mbalimbali ikiwepo kuanzisha madarasa kufika mpaka nane, lakini baadaye kuongeza masaa ya kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda kwa 1967 tukaona kwamba elimu tuliyokuwanayo bado ilikuwa ina misingi ya kikoloni. Kama tunavyojua, elimu ya kikoloni ilikuwa ni kwa ajili ya kupata maslahi ya kikoloni. Wao walianzisha elimu kutokana na wao walivyokuwa wanataka kwa kuzingatia maslahi yao, na sisi tukataka tuzingatie maslahi ya Taifa letu. Tukaanzisha elimu iliyoendana na Sera yetu ya Ujamaa na Kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, zimekuja sera nyingi na *program* nyingi za elimu na mwisho tumekuja na hii sera ambayo tukonayo sasa hivi ya 2014 ambayo hii nayo ilionekana ina upungufu kutokana na kutokuwa na walimu wa kutosha,

mazingira ya ufundishaji na kujifunzia kutokuwa bora, na pia kutokuwa na udhibiti wa ubora katika elimu yetu na kuwa na elimu ambayo haiendani na soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetengeneza sera nyingine ambayo kwanza tunaipongeza Serikali kwa sababu katika mazingira ya kujifunza na ujifunzaji kuna mambo makubwa yamefanyika kuhakikisha kwamba tunapata shule za kutosha na pia tunapata miundombinu mingine ya shule za kutosha, kuhakikisha kwamba tunaleta *motivation* kwa watumishi kwa kuajiri walimu wa kutosha na kuboresha maslahi ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba wana malalamiko makubwa ya mishahara, kupandishwa madaraja na stahiki za wafanya kazi. Haya yote Serikali imeyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nilitaka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Elimu maana yake ni mchakato unaohusisha mtu kupata ujuzi na maarifa, maadili na mtazamo. Sasa kwenye Taifa letu tume-*concentrate* sana kwenye ujuzi na maarifa, hatuangalii maadili na mtazamo (*attitude* za watu) na hii ndiyo inayotupa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mheshimiwa Mbunge aliyetoka, hii inatupa shida, mtu kufikiri kwamba akipata elimu lazima aajiriwe au akipata elimu lazima apate kazi. Sasa hii iko kwenye *package* ya Mheshimiwa Waziri na kwenye hii Sera ya 2014 Toleo la 2023 wewe kama Wizara ndiyo msimamizi wa uendeshaji wa elimu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunatamani tuone Wizara inasema nini katika suala linalohusu maadili na linalohusu mtazamo. Tunawajengeaje watoto wetu mtazamo chanya kwamba elimu ni nini? Tunawajengeaje watoto wetu maadili chanya hata wakipata kazi waweze kuwa na tija kama ambavyo sera yenyewe inasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto kwenye mifumo yetu ya elimu. Kwanza katika usimamizi, lazima tukubaliane kwamba elimu kama mchakato wa kupata ujuzi, maarifa, maadili na mtazamo unahusisha mfumo wa shule ulio rasmi ambao Waziri anausimamia lakini na mfumo usio rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea watoto hawa wapate maadili kutoka kwenye vyombo na taasisi nyingine pia, lakini leo hii, mfumo wa elimu umechukua muda mrefu kwa mtoto wetu. Watoto hawana muda, na vipindi vingine hatuwaachii, hatuna zile taratibu nzuri za kuwaachia ili kuruhusu taasisi nyingine zipate muda wa kupandikiza kitu kwa hawa watoto wetu ikiwemo taasisi za kidini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii watoto wakiwa likizo wanakwenda *tuition*, wakiwa shuleni Jumamosi na Jumapili wanakwenda *tuition*. Makanisa hayapati muda wa kuwafundisha hawa watoto imani zilizo sahihi; misikiti haipati muda wa kuwafundisha hawa wototo imani zilizo sahihi, *as a result* tunapata wasomi ambao wanafikiria ili akae kwenye cheo, lazima aroge; ili akae sijui kwenye nafasi ya biashara, lazima afanye mambo ya kikatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima sasa Wizara ya Elimu ituletee ratiba na ituambie; Mheshimiwa Nahodha alisema kwamba mtoto naye akifundishwa sana inaonekana pia hawezi kuelewa, hivyo unamletea *problem* ya afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati lazima tukubaliane, watoto wanatakiwa sasa wakajifunze masomo ya darasani na wakati huu tuwaachie wafanye masomo mengine ili kuwajengea mtazamo na maadili. Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni lazima tukubaliane, kuna *informal education* tuliyokuwa tunapata iliyokuwa nzuri. Tulipata kwenye unyago wakati huo, leo hii katika mfumo wa elimu ambao tunakaa nao muda wote...

**MHE. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** ...watoto wetu wanapata wapi mafunzo yale ya kujitambua kama mama? Kujitambua kama baba na kujua wajibu wao?

**MHE. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana msemaji anayezungumza sasa hivi, na hasa anaposema kwamba, tuangalie elimu inayotoka kwenye maeneo mengine. Kama dini zifundishwe, lakini nimtahadharishe kwamba, siyo dini zote zinatoa maarifa yanayofaa kwa watoto. Kwa mfano, kuna mtu anasema kabisa, anakwenda pale Kanisani au sehemu ya dini anasema yeye ni Mungu. Sasa dini hizi pia, tuangalie ni dini gani zinafaa kwa watoto wetu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, taarifa hiyo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipokea taarifa yake. Kama ilivyo kwamba, tunaposema imani, tunajua zipo imani potofu na siyo imani za kidini tu, hata hizo imani nyingine za kienyeji, zipo nyingine ambazo pia ni potofu. Kwa hiyo, naamini kabisa kwa namna Profesa alivyo makini, tunafahamu ni imani ipi tunayoiongelea kwa watoto wetu ili wajitambue, wajue na wawe na maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, hawa watoto tunataka wa-*acquire* ujuzi na maarifa. Sehemu kubwa ambayo inatumika, kiungo kinachotumika kwao katika kupata ujuzi na maarifa ni kichwa, na afya ya akili. Kwenye shule zetu watoto hawa wanapataje *skills* au wanafundishwaje kuwa na afya ya akili?

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kabisa kwamba, kuwa na afya ya akili, kwanza mtu yeyote mwenye afya ya akili,

ndiye mwenye uwezo wa kuzalisha vizuri, kupambana na changamoto, kusaidia jamii yake na kujitambua. Sasa, haya ni mambo ya muhimu kwa watoto wetu kuanzia ngazi ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona kabisa katika masuala ya ukatili wa kijinsia mambo mengi yamegundulika shuleni. Watoto wetu wanakwenda shuleni wana *stress* nyingi sana kutoka kwenye familia. Kule shuleni wakifika kuna chombo gani kinakaa kuwaangalia wale watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna watoto wengine wanazaliwa na ulemavu. Kutokana na taasisi zetu zilizopo, wengine wanashindwa kuwatambua toka huku chini. Anapofika shule, tuna kitu gani pale shuleni ambacho anaweza akaenda akatambuliwa? Mimi ninafikiri ni wakati sasa umefika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba robo dakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wakati umefika, tuanzishe *clubs* za *mental health* shuleni, ili watoto wetu wapate kuwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hii inatakiwa itolewe kwa usawa. Tumejenga shule za bweni za watoto wa kike, tunataka tujenge shule za bweni za watoto wa kiume. Wakati ule wa Sera ya Elimu tulikuwa tunajenga shule mbili mbili; ya kike na ya kiume.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulikuwa tuna Iringa *Girls* na tulikuwa na...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, najua una midadi. Mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mchungahela, Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Kapufi ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunipa fursa hii ya kupumua na kuweza kuendeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunivumilia nikitoa huduma hii kwa wananchi wangu. Halikadhalika, nawashukuru wananchi wangu kwa kuniunga mkono wakifahamu kabisa kuwa, napambana kwa ajili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia mambo mawili. Kwa kuanzia, kama walivyofanya wenzangu, naanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada zake kubwa sana katika eneo la elimu. Kipekee pia, nampongeza Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Prof. Mkenda, kwa kweli amefanya kazi kubwa ya ku-*transform* elimu kutoka tulikokuwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu anaweza kupinga kwenye hili kwamba, sasa hivi tuko katika mazingira ya mapinduzi makubwa kabisa ya elimu, lakini pamoja na pongezi hizi zote na kazi kubwa iliyofanyika, bado tunayo ya kusemea, kwa maana ya mambo ambayo tunatamani yafanyike, ili mapinduzi haya yaende kwa umakini kabisa, na yawe *very successful.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira yetu yanatofautiana, kwa maana ya mazingira ya jimbo, mazingira ya mikoa, halikadhalika mazingira ya wilaya na hata mazingira ya kata. Kuna maeneo ambayo yanahitaji sana huduma hii ya elimu, na kuna maeneo ambayo tunasema kwamba, yana afueni. Kwa mfano, tukichukulia maeneo ya vijijini, ni maeneo ambayo yanahitaji sana huduma ya elimu. Tunahitaji sana kutoa kipaumbele katika maeneo haya, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mazingira yaliyokuwepo bado yamesababisha wananchi wa vijijini kupata elimu isiyotosheleza, kwa maana watu wengi wanakosa kuwa na

elimu stahiki. Pia, wale wachache wanaopata, bado wanashindwa kuitumia elimu hiyo katika kufanya maendeleo ya hali halisi ya pale walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sera za Elimu ni lazima uzingatie haki za binadamu kwa maana elimu ni haki ya msingi kabisa na Kikatiba na ni haki ya binadamu. Hivyo, kila mtu anastahili kupata elimu kwa kiwango cha juu kabisa, na hii ndiyo itasababisha kwamba, haki imetendeka kwa wananchi wote katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumefanyika jitihada kubwa ya kupeleka miundombinu kadha wa kadha, lakini kama nilivyosema katika maeneo ya vijijini, kwa mfano ukichukulia katika eneo langu, kwenye jimbo langu, bado nina uhitaji mkubwa wa elimu, hususan elimu ya sekondari na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba kwa sasa hivi ukizungumzia kwenye kata, takribani kata zote za Jimbo la Lulindi kuna shule za sekondari. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo, lakini ninachoongelea hapa ni kwamba, kuna baadhi ya kata zina vijiji zaidi ya 11, kwa maana, bila shaka kata hizi zinahitaji kuwa na shule mbili za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukichukulia Kata ya Mkululu ni kata ambayo inastahili kuwa na angalau shule mbili za sekondari. Halikadhalika, ukienda kwenye Kata ya Mchauru kuna hali hiyo, na ukienda Kata ya Mbuyuni, maeneo haya ni maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji viko mbalimbali sana. Kutoka eneo moja kwenda kutafuta elimu inachukua umbali mrefu kweli kweli, ili ufike. Kwa mfano, ukitoka kule Namtona uende ukaitafute Nakachereni iliko, ni takribani zaidi ya kilometa saba; lakini ukitoka Namtona kwenda kuitafuta Sekondari ya Lupaso iliko, ni takribani kilometa 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia mazingira hayo, watu wengi sana, kwa maana ya vijana na watoto,

wanakatishwa tamaa kwenda kusoma huko. Kwa hiyo, angalau tukiweka shule maeneo ya karibu wataweza pia kusogea hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuunganisha hilo pia, ningetamani tuwe na upendeleo mahususi kabisa katika shule hizi za vijijini. Kuwe na mabweni katika shule zote za sekondari kwa sababu, umbali ulioko unawafanya watoto kushindwa kabisa kwenda kutafuta elimu, ni mbali. Kwa hiyo, kukiwa na mabweni itawashawishi watoto wengi kupata elimu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna uduni wa elimu inayotolewa pale, ambao unatokana na hali halisi, mojawapo ikiwa ni uchache wa walimu waliopo. Kwenye jimbo langu kumekuwa na changamoto kubwa sana ya walimu, ambayo nimekuwa nikiizungumzia hapa Bungeni mara kwa mara, lakini haijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu unakuta mwalimu yuko mmoja tu na hiyo ni shule ya sekondari au unaweza ukakuta walimu wako wawili tu na wanatakiwa wafundishe kuanzia *form one* hadi *form four,* lakini hata kwenye shule za msingi hali iko hivyo hivyo, kuna changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili alichukulie kwa umuhimu mkubwa kabisa katika Jimbo langu la Lulindi. Kuna changamoto kubwa nilishazungumza hapa mara kwa mara, natamani atakapokuja ku-*windup a*nieleze una mkakati gani maalumu kabisa kwa niaba ya Jimbo la Lulindi? Ni kwa jinsi gani tunaweza tukaondokana na hii adha ya uchache wa walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, nashauri suala la ujenzi wa nyumba za walimu lingeweza kusaidia sana kwa kiasi kikubwa walimu ambao wanakuja wasiondoke, kwa maana ya kutaka kuhama kukimbia mazingira mabaya; wangeweza kushawishika kuishi. Kwa hiyo, nashauri sana, hizi shule za vijijini angalau basi kuwe na nyumba za walimu kwa kuanzia, ili walimu wanavyokuja waweze kuwa wana sehemu za kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, natamani sana kuwe na *bonus* maalumu ya ufundishaji vijijini. Mwalimu wa kijijini asilipwe sawa na mwalimu wa mjini. Mwalimu wa kijijini alipwe mshahara mkubwa, ili kumshawishi yule mtu anayetaka kukimbia aendelee kubaki kule kwa sababu ya mshahara. Eneo hilo ninafikiri lingeweza kutusaidia pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine natamani kushauri kwamba, kuwe na upendeleo maalumu kabisa kwa wale wanaoomba kutoka katika maeneo ya vijijini. Kukiwa na watu wanaomba kutoka vijijini, basi wapewe upendeleo wa kwanza kabisa kuajiriwa kuliko hawa wa mjini kwa sababu, mazingira yao yako tofauti na mazingira yao, ingeweza kusaidia sana wao kuendelea kukaa kule vijijini badala ya kukimbilia mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getere atakuja baadaye kidogo, Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa Hassan Zidadu ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake yote, lakini niendelee kumpongeza Rais wetu kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye eneo la elimu jumuishi. Tukizungumzia suala la elimu jumuishi, ni elimu ambayo kwa ujumla wake inahitajika isimwache mtu nyuma. Mimi nimejaribu kupitia Taarifa ya Waziri, nimeona amezungumzia masuala yote hayo yanayogusa elimu jumuishi. Nikilisema hilo, maana yake ni kwamba tunakwenda kuwalenga watu wenye mahitaji maalumu. Watu hawa ni sehemu ya jamii yetu, hatuwezi tukashiriki elimu kwa mapana yake wakati wao tunawatenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sura hiyo nikijielekeza, kwa mfano, kwenye eneo la mikopo ya elimu ya juu, nimeona kwa kuanzia kulikuwa na shilingi bilioni 787.4 kwa mwaka 2024/2025

kutoka shilingi bilioni 570 ya mwaka 2021/2022 ambapo wanafunzi walitoka 177,925 mwaka 2021/2022 hadi 248,000 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukisema suala hilo la mikopo ya elimu ya juu, ningetamani, nikirudi kwenye *point* yangu ya elimu jumuishi, tunapokutana na watu wenye mahitaji maalumu katika eneo hili la mikopo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, tuje na upendeleo kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni anapokwenda kushiriki mkopo wa elimu ya juu na ukiangalia mahitaji ya mtu huyu, angeweza kupata hata ruzuku kwa sababu, ana mahitaji ya ziada. Kwa hiyo, tunapomweka kwenye kundi moja, na sisi tusiokuwa na mahitaji maalumu naona hapo Serikali inatakiwa tupaangalie kwa namna ya pekee, nashauri kama ni ruzuku au *scholarship,* kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la elimu jumuishi, kwenye suala la vifaa saidizi, watu wenye mahitaji maalumu, kwa maana ya vifaa saidizi, wenzetu hawa nimejaribu kupitia hapa, wanakutana na changamoto kubwa. Mathalan kiti-mwendo ni kati ya shilingi za Kitanzania 600,000 hadi 1,200,000. Kuna kifaa cha masikio, ni kati ya shilingi 800,000/= hadi 3,500,000. Vifaa ni ghali mno, na kama kweli tunahitaji watu hawa washirikishwe katika suala zima la kupata elimu na mahitaji mengine ya namna hiyo, Serikali iangalie namna ambayo ama kutakuwa na msamaha wa kodi, hasa kwa maana ya vifaa hivi ambavyo vinakuwa ni ghali mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, kuna suala zima la eneo la utambuzi na upimaji wa *total.* Nikilisema hili, na Waziri anisaidie hapa, Wizara itusaidie katika eneo hilo. Leo utakutana na mtoto darasani anaweza akaonekana labda ni mkorofi, hataki kusikiliza au mambo ya namna hiyo, lakini kimsingi kumbe mtoto huyu ana tatizo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo la upimaji na utambuzi wa watoto, suala hili natamani isiwe tu ni Wizara ya

Elimu peke yake, inaweza ikashirikisha Wizara ya Afya na watu wengine wa namna hiyo, ili tutakapombaini mtoto katika hatua za mwanzo, itakuwa ni rahisi kupunguza madhara huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu labda hata uelewa wake darasani ni mdogo, ukifikiri labda akili yake ni ndogo, *no!* Kumbe kuna tatizo la msingi. Kwa hiyo, vituo hivi vya upimaji, ninashauri viendelee kwenda mpaka katika ngazi za halmashauri zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, naomba kuhusu lugha ya alama. Tukizungumzia lugha ya alama, watu wanaweza wakaona hili ni jambo la namna gani? Lugha hizi kwa ujumla wake zikafundishwe kama yalivyo masomo mengine yoyote katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili, ni muhimu kweli kweli, mtu mwingine anafikiri kwamba, hizi lugha za alama ni kwa ajili tu ya watu wenye ulemavu. Iko katika sura hii, mtu mwenye ulemavu anaweza akahitaji kwenda kupata huduma za kifedha, labda benki, mtu mwenye ulemavu anaweza akahitaji kwenda kupata huduma *TRA*, mwenye ulemavu anaweza akaenda katika maeneo yote hayo na kuhitaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa isije ikawa labda tunamhitaji tu awepo mwalimu au mtu mwingine wa namna hiyo. Ikiwa sote tumebahatika kuzijua lugha za alama inakuwa ni msaada mkubwa mno kwa sababu, inafika mahali ni uhitaji. Nimezungumzia habari ya elimu jumuishi. Ni uhitaji kama ulivyo uhitaji mwingine wowote. Leo nimejaribu hata kutoa mfano mmoja mdogo, japo hilo linatakiwa liende mbali zaidi, kwa maana ya utaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka hata *Traffic Police* anavyokusimamisha hivi, halafu anaelekeza hivi, ametumia alama. Sasa tunatakiwa twende mbali zaidi katika masuala mengine ambayo yatafanya hawa wenzetu nao waone

wamejumuishwa katika shughuli zetu za kila siku. Naomba hiyo lugha ya alama, nimesema, tuiweke kwenye sura hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba kuna suala la akili mnemba *(Artificial Intelligence)*. Wenzetu wenye ulemavu, kwa maana ya elimu jumuishi, tunasemaje katika eneo hilo na tunawashirikishaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuone kwamba, dunia tunayokwenda sasa hivi hatuwezi tukakwepa suala la elimu hiyo ya *Artificial Intelligence* (akili mnemba) au *whatever* lugha yoyote ambayo inaweza ikazungumzwa hapo. Kwa hiyo, isiwabague watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nilikuwa naomba nihitimishe. Ninafarijika, nimeona tunazungumzia changamoto za mdondoko wa vijana, lakini kwa maana ya changamoto hii tumeambiwa kuna ujenzi wa shilingi bilioni 28.7 wa shule saba za kanda ambapo shule hizo zitasaidia hasa watoto wa kiume. Ni katika mwendelezo wa Serikali kukabiliana na suala zima la mdondoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii, mgeni wa Mheshimiwa Prof. Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Maulid Mwatawala, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Elimu Tanzania, karibu. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 80 na walimu watatu wa Shule ya Msingi Silvio Pasquali ya Mafinga kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 207 na walimu saba wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Ahsanteni hongereni sana, mmependeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hassan Zidadu jiandae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, jiandae Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, tuko hapa tunachangia Wizara yetu ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta mapinduzi makubwa mno katika elimu nchini. Sisi sote tunatambua ni namna gani alivyoleta mapinduzi juu ya suala hili la elimu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru na kumpongeza sana Waziri wa Elimu, kwa kweli anastahili pongezi na anastahili sifa. Amefanya kazi kubwa sana katika Wizara hii na ameleta mapinduzi makubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Adolf Mkenda kwa kweli anastahili pongezi kubwa. Pia namshukuru na kumpongeza Naibu Waziri QS Kipanga, naye pia amekuwa madhubuti katika kumsaidia Waziri wetu wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru na kumpongeza tena Katibu Mkuu wa Wizara hii Profesa Carolyne Nombo, amefanya kazi kubwa sana, tangu ameingia katika Wizara hii tunaona Wizara imetulia mno. Vilevile nawapongeza wataalam wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tunaishukuru Serikali katika Jimbo letu la Tunduru, tumepata shule mpya nne kwa awamu hii ya mama yetu mpendwa, ambapo kwa muda mfupi tumepata shule kubwa nne ambazo mpaka sasa zinafanya kazi vizuri. Tunashukuru na kuipongeza Serikali kwa namna ilivyotuletea zile shule kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nayo maombi machache katika shule ile. Natambua kuwa Wizara ya Elimu inasimamia elimu, lakini majengo yako chini ya Wizara ya TAMISEMI. Kwa hiyo, naomba, Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na TAMISEMI, basi tuweke mkakati wa kuhakikisha kuwa zile shule zote za sekondari tulizozipata ziwe na mabweni kwa ajili ya wanafunzi ama hosteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Kwa mfano, Shule ya Sekondari ya Kungu pale Nakayaya, watoto wengine wanaosoma pale wanatoka kilomita nane, wengine wanatoka kilomita tano, wengine kilomita nne. Wakati mwingine wale watoto ni wa kike, kwa hiyo, kutoka asubuhi kwenda shuleni na kurudi jioni inakuwa ni ngumu sana. *Otherwise* ni lazima wazazi wawatafutie vyumba ili waweze kupanga na hatimaye kuondoa usumbufu wa kwenda na kurudi shuleni. Sasa hii inaleta shida kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana kwamba shule zile zipatiwe hosteli ili wanafunzi waweze kulala pale pale shuleni na wapate utulivu ili waweze kupata elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunazo shule za sekondari pale ambazo hazina uzio. Kuna Shule ya Wasichana ya Sekondari ya Masonya haina uzio na ipo katikati ya mji, upande mmoja ni mji na upande wa pili ni mashamba; kuna mikorosho. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba sisi kwetu tumezungukwa na hifadhi. Sasa wakati mwingine simba wanakuja pale shuleni, fisi pia wanakuja shuleni ilihali shule ile ni ya wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna changamoto nyingi. Kuna changamoto za wanyama na pia kuna changamoto ya vijana wale wanaotamani sketi, kwa maana ya wale wanafunzi wa kike huwa wanasumbuliwa sana. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na TAMISEMI tuzipatie uzio Shule ya Sekondari ya Masonya na Shule ya Sekondari ya Nakapanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nizungumzie suala la Tawi la Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Nimesimama hapa leo hii kwa mara ya pili ama ya tatu, kama sikosei, nazungumzia suala hili la Tawi la *SUA* pale Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu tuliuanza tangu mwaka 2018, leo hii tunazungumza miaka saba sasa imepita, lakini bado hatujakamilisha kupata chuo na wanafunzi waendelee kupata mafunzo yao pale ya kilimo kwa muda wote. Isipokuwa mpaka sasa wanafanya *practice* kwa siku 14 kwa kila mwaka. Yaani kila mwaka wanakuja wanafunzi kutoka Sokoine na maeneo mengine wanafundishwa pale kwa siku 14 tu, baada ya siku 14 wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa pale kulikuwa na majengo ambayo yametolewa na halmashauri, majengo hayo ni yale ambayo yalikuwa yameachwa na wakandarasi wa barabara. Pia, tulitoa mashamba ekari 500; na wale wenye mashamba waliridhia kukiachia chuo; na baada ya hapo wakaambiwa wasiyaendeleze. Kwa bahati mbaya sana hakukuwa na mthamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye katika hali ya kutafuta mthamini na watu wamekaa kwa muda mrefu baada ya kuona mashamba yale hayaendelezwi, chuo hakiendelei wakaamua kuyatwaa tena yale mashamba na kufanya shughuli zao za kilimo. Baadaye, baada ya kuomba sana, ndipo *SUA* wakatupatia 18,800,086,690 kwa ajili ya kufanikisha kupata hati ya eneo lile la Tawi la *SUA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ataona, kwamba kwa miaka saba yote, na mchakato ule tulivyouanza mpaka hivi sasa kitu pekee tulichokifanikisha ni kuwa na mchakato wa kupata hati peke yake, ili kuweza kuweka majengo pale, kwa maana ya kwamba Serikali haiwezi kuwekeza eneo ambalo halina hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza, kwamba kama hati peke yake tumechukua miaka saba vipi, majengo yenyewe yatakamilika kwa miaka mingapi? Hilo ni swali ambalo najiuliza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba baada ya kupatikana fedha ile ya hati, mthamini amekwenda, amefanya uthamini wake na watu ambao wanahitaji kulipwa pale mpaka sasa kutoka kwenye ekari 500 zimebaki ekari 300 tu peke yake, lakini zile ekari 300 zinao watu ambao wanadai fidia, na fidia yake siyo chini ya shilingi milioni mia tatu na kitu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala hili kwake ni dogo sana. Shilingi milioni mia tatu na kitu, kwamba halmashauri imeshindwa kulipa! Namwomba atuisaidie Halmashauri ya Tunduru kuweza kulipa fidia ya watu wale ili eneo lile lipatikane na hatimaye hati ikamilike na baada ya hapo tuweze kukamilisha chuo kile cha kilimo na tuweze kupata tija ya elimu ya kilimo kwenye Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna Mheshimiwa Waziri anavyoweza kufanya kazi na jinsi alivyoleta mapinduzi makubwa kwenye Wizara hii, jambo hili ni dogo sana, haliwezi kumshinda. Shilingi milioni 300 ni ndogo sana katika Wizara hii. Naomba sana sana sana atusaidie katika jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nimalizie na suala la *VETA*. Kwenye wilaya yetu sisi hatuna chuo kabisa na Tawi hili la *SUA* ndilo ambalo lilikuwa linakuja sasa kutuamsha na kutufumbua. *VETA* pale majengo ya awali yalianza kwa *speed* kubwa sana, na Wanatunduru walifurahi kweli kweli kuona sasa watoto wao wakimaliza elimu hawatakwenda mbali kupata elimu yao ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpaka sasa, baada ya yale majengo ya awali kuanza, yamefika sehemu yamesimama, hakuna kinachoendelea. Tunatambua Serikali inafanya kazi kubwa sana, ina mambo mengi na miradi mikubwa inatekeleza, lakini tunaomba ichukulie mkazo kwa umuhimu wa peke yake ili tuweze kusukuma ile *VETA* ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rwamlaza, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Kanyasu wajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache juu ya hoja ya Bajeti ya Wizara ya Elimu iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameonesha utashi wa kisiasa kuhusu utoaji wa elimu katika nchi yetu. Hakuna kipingamizi au maneno yoyote tunayoweza kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli shule nyingi sana zimejengwa katika nchi yetu kipindi hiki. Zaidi shule za watoto wa kike zimejengwa kila mkoa. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Rais wetu kwa kuliona hili, na kwa kweli apate maua yake. Unapomsifu mtu, tunasifu na uwezo wake, tunamsifu pia kuwa ni mwanamama kwamba kwa kweli amejitahidi sana kuhakikisha nchi yetu, watoto wetu wote wanaweza kupata nafasi ya kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza katika mdondoko wa wanafunzi *(dropout)*. Nimesoma katika Randama ya Wizara ya Elimu ya Bajeti ukurasa wa 18, wamejitahidi kutuonesha takwimu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Randama hiyo mnasema mwaka 2020/2025 wavulana 5,613 na wasichana 10,239 ambayo inaleta karibu wanafunzi 15,800 wameweza kurejea katika mfumo rasmi wa elimu, lakini ukienda TAMISEMI sasa, wao wanasema 2023/2024 wana wanafunzi wavulana 76,125 na wasichana 72,218 ambayo inakuja takribani 16,000 hawa wamedondoka, ndiyo mdondoko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakuja *NECTA;* wao wanasema 2022/2023 wana wanafunzi 503,094 ambao hawakumaliza mitihani yao. Sasa nataka niiulize Serikali, kwamba

je, kwa takwimu hizi ambazo zinatoka kwao, zinatoka TAMISEMI na *NACTE,* ni kipi kipo sahihi? Napenda niishauri Wizara ya Elimu, kwamba wafanye utafiti sasa ili wahakikishe kwamba tunajua ukubwa wa tatizo hili. Jambo hili wasilipuuzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ni kwamba, Mheshimiwa Rais wetu amejitahidi kujenga shule, kwa hiyo, nchi ina-*invest* kwenye elimu, halafu kuna watoto ambao wanapotea huku hatujui hata mahali walipo. Hawafanyi mitihani, hawamalizi shule wasichana kwa wavulana; na wao huku kwenye randama wamesema wavulana ndio wengi. Kwa hiyo, ni lazima tufanye utafiti, waje na jibu ili wapate takwimu, waweze kupanga mkakati ulio rasmi wa kuweza kukabiliana na janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimetazama katika mpango wao wa bajeti, hakuna mahali ambapo wamegusia, yaani tuseme kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri hana kitu chochote alichotuwekea kwamba, je, mwaka huu kama walisema mwisho ni shilingi milioni 15, je, sasa hivi hii bajeti ambayo ni ya mwaka 2025 wameweka wanafunzi wangapi ambao watarejea? Kwa hiyo, tungetaka kujua kwamba watarejea wangapi ili tuone kwamba tunaweza kupunguza hili tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua hii takwimu ya TAMISEMI ni wanafunzi zaidi ya laki moja na arobaini na kitu. Ukitoa hiyo kumi na sita tuna wanafunzi 120,000 ambao hawamalizi shule, wanatoweka mitaani na hatujui mahali waliko ilhali tuna-invest na tunaweka watoto wetu. Je, baada ya miaka 10 ni kitu gani tutakachokuwa nacho?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwamba, wahakikishe kuwa wanafanya utafiti, wanahakikisha kuwa tunaweza kumaliza hili tatizo la wanafunzi wetu kutomaliza shule. Ukizingatia kwamba, tunapo-*discuss* bajeti hapa ni kwamba, tunaangalia mipango yetu ya nchi, na mipango hii tunaitafsiri katika fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kwamba, bajeti haipaswi kumwacha mtu nyuma. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba

watu wote wanakuwa *included,* bajeti inawaunganisha kwa pamoja, mipango yetu inawafanya na wao wafaidi bajeti yetu ambayo tunapitisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda niliongelee ni kuhusu walimu. Ni kweli kuwa tuna uhaba mkubwa wa walimu, lakini sitaongelea uhaba. Nitakachoongea ni kuwa, ni kwa namna gani Serikali inaweza ikaandaa wanataaluma ya ualimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwalimu *professionally,* nilisoma kwenye chuo cha ualimu, nimepitia hatua zote. Najua mwalimu anavyoandaliwa. Unakwenda *block teaching* una mwalimu wako nyuma, unajifunza *methodology,* unajifunza vitu mbalimbali, unapikwa na baadaye unafanya mtihani, wanakupa *certificate* kwamba, sasa nenda unaweza kufundisha watoto wa umma. Ndivyo tulivyosoma na ndivyo tulivyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifundishwa mpaka *BBD,* inaitwa *blackboard what,* lazima ufunzwe hata namna ya kuandika ubaoni, unafundwa kila kitu. Sasa wanawaandaa walimu halafu wanawa-*dump.* Tunao watoto mtaani wa mwaka 2018 mpaka leo. Sasa wamemsomesha mtu, wamempa *certificate* anakwenda kuwa bodaboda, anakuwa kwenye vibanda vya fedha, anakuwa mama lishe kwa sababu lazima ajikimu. Halafu wanatangaza ajira, wanataka kumpa mtihani, upi? Ana *certificate* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi cheti changu cha ualimu ndicho kilichonipa ajira, kwa sababu nilipita chuoni wakaniambia kwamba sasa Conchesta unaweza kwenda kufundisha watoto wa umma. Sasa wamewapika, wamewaandaa, wanatupa taaluma ya ualimu mitaani, halafu wanawadhalilisha na kuwanyanyapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wao mtu akiwapa mtihani wataufanya sasa hivi? Hata wa darasa la saba watashindwa. Eeeh! Kwa hiyo, wasiwanyanyapae, waje na *certificates* zao, waliandaliwa kule. Hivi vyuo wanavidharau,

waweke mitaala ya bodaboda kule basi, waweke mitaala ya mama lishe. Wajue kwamba, walimu hawa wakishasoma watatoka huko watakwenda kuendesha pikipiki. Watakuja sasa utawaambiwa kwamba, umekuja tuambie gia ya pikipiki inawekwa namba ngapi ili kusudi tukupe ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali waache kupoteza taaluma ya wasomi hawa, walimu, wanawa-*dump* halafu wanasema kuna uhaba wa walimu. Wawatoe waje na vyeti vyao, wanalalamika. Unakwenda kumuuliza maswali gani? Mimi hata siyajui, labda wengine wanajua wanawauliza maswali gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wewe umesomeshwa na mwalimu wako halafu baadaye Mheshimiwa Prof. Mkenda unamwambia x + y au unamwambia nini? Yeye amesoma taaluma yake na amekabidhiwa cheti, halafu unamweka miaka sita, jamani, ni mtu gani huyo ambaye anaweza kukaa miaka sita bado anakumbuka alivyoambiwa uwe msafi darasani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kwa kweli silipendi sana. Kwa mawazo yangu mimi mwenyewe, napenda watoto waje, hakuna *interview.* Waje na *certificates* zao. Kama ni *certificate,* walifoji? Kama walimu wamewapika, wamepikwa wamekuwa walimu kama sisi, anakuja na *certificate,* ndiyo nyenzo ambayo inaweza kumfanya kuwa mwalimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, wajiandae Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ili nami nitoe maoni yangu katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia ongezeko kubwa sana la mikopo katika elimu ya juu na elimu ya kati. Pia kuondoa ada kwa masomo ya *advance,* kitu ambacho kimewezesha watoto wengi kuendelea kusoma masomo ya *advance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na wenzake wote Wizarani kwa kupeleka *VETA* pale Nyamongo. Nimeambiwa mpaka mwezi wa Saba inaweza ikawa imekamilika vizuri zaidi kwa majengo ya awali, ili wale vijana ambao wanafanya kazi ya uchimbaji, na wanaolima karibu na Mto Mara pale wapate *course* na waweze kufanya kazi za kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaomba Mheshimiwa Waziri waweke nguvu katika kile Chuo cha Kilimo Butiama ambacho kina heshima kubwa ya jina la Baba wa Taifa pale ili kiwe Chuo kamili kama ilivyo Chuo cha Sokoine na watoto wa Kanda ya Ziwa na maeneo mengine wapate hiyo taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Rais aliahidi pale Hospitali ya Kwangwa iunganishwe na utalaamu wa kidaktari na manesi ili wanapoenda pale kufanya kazi ya mafundisho pia wafanye kazi ya kuhudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mitaala hii, tumekuwa na mjadala mkubwa sana katika nchi yetu. Ukiangalia Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa, kwamba ni kweli kumekuwa na wanafunzi ambao wameenda vyuo vikuu, wamehitimu lakini wamekosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapambana hapa kusugua ubongo, kutafuta namna ambavyo tutafanya kupunguza *gap* kubwa ya ajira iliyopo Tanzania, watakaopata kazi ya ajira katika sekta mahsusi, sekta binafsi au wakajiajiri lakini wapate utalaamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja imejitokeza hapa asubuhi nataka niisemee kidogo, mimi ni Mwalimu wa Hesabu na *Chemistry*, kwamba *quadratic equation* haina maana. Ukiingia kwenye *google* sasa hivi hapo ulipo Mheshimiwa Mbunge wewe

andika tu hapo, "*use of quadratic equation in life,*" utakuja kuona ni vitu vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kwa watu ambao wameenda jeshini kitaaluma, *military bases* zile, ukitaka kufanya *projection,* unaipiga ndege imeruka hapo, uipige pale; ni lazima ufanye *projection* ya sayansi, na hiyo *equation* ni *quadratic equation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, watu ambao wamefika *NASA* kule Marekani, unazungumza kurusha *parachute satellite,* unazungumzia *quadratic equation applications,* zipo pale. Kwa hiyo, kuna vitu vingi, lazima hii tuisemee kwamba siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila wale ambao wanaweza kuisoma *quadratic equation* wakafaulu, waache waendelee; wale ambao wanataka kusoma Kiswahili na Historia waache waendelee; wale ambao wanasoma ili wapate ajira tu, waendelee. Hapa kuna taaluma, kuna fani na kuna watu waliobobea, hao tuwaache waende kwenye sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, huwezi kuniambia kwamba hakuna matumizi ya *periodic table; no periodic table no chemistry.* Huwezi kuzungumza *atomic nuclear* hapa, *atomic energy, nuclear energy* zile *elements* zimekuwa *raised accordingly to the increment of atomic number* na *atomic mass.* Huwezi kuzungumza *electrolysis* hapa, huwezi kuzungumzia habari ya umeme *positive and negative charges move,* hii ni *periodic* inafanya kazi tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii hizi taaluma za watu tuwaachie wengine waendelee. Tunapata shida kuwashawishi watoto wasome sayansi, watakimbia masomo. Nenda kwenye shule ukafanye *sampling* yoyote ile, wengi wanaenda kwenye *arts*.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri, sasa hivi pia imeibuka hoja kwenye taaluma hizi, tusichanganye habari. Kuna watu wanachangia sasa hivi hoja, wanazungumza upungufu wa

ajira *versus* taaluma, hapana. Vijana mtawaandaa duniani watapwaya sana. Ukienda kwenye vyuo vingine, hutaenda, na ukiacha sayansi kwenye ngazi ya chini, huko mbele ni shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, waache vijana wajaribu, wale wanaoweza kusoma *physics,* wanasoma *biology,* wasome *chemistry.* Mwili wa binadamu huu 96% una *carbon,* una *oxygen,* una *nitrogen,* una *hydrogen* humu ndani. Unawasha taa nyumbani ni *chemistry* ile, *bulb* ni *chemistry* ipo pale, *helium* ni *chemistry,* unazungumzia gesi ni *chemistry*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani haya mambo niseme kwamba siyo wote ni wanasiasa na sisi tuna taaluma zetu hapa tumetulia. Kwa hiyo, ukigusa kidogo, lazima tutatofautiana katika maeneo hayo ili turudishe watu kwenye msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuna hoja imejitokeza sasa hivi, nimeenda kwenye shule zangu kule, ni kweli wameanza utekelezaji wa mitaala mpya, lakini ataka kumwambia Profesa, kuna changamoto ya walimu waliobobea katika huu mtaala mpya, uelewa ni mdogo sana, na kuna upungufu mkubwa sana wa vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaambia mwaka 2024 kwamba kama ungeweza kufanya tathmini upya, kama unaweza kufanya wakati mmoja kuanza mtaala mpya, tuendelee; kama unadhani hatuwezi, mngefanya *sampling* baadhi ya shule muimarishe walimu wapatikane. Hapa amesema amefundisha walimu wa shule ya msingi na awali aah, fundisheni mpaka sekondari zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hata walimu wa masomo ya Kiingereza kwenye shule hawapo. Wanafunzi wana-*struggle*. Ametoka shule ya msingi, amesoma masomo yote Kiswahili halafu anaenda sekondari hana mwalimu wa *English,* halafu unataka aelewe masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye shule yangu, Jimbo zima mwaka 2024, watoto wa *form two* waliopata *division zero* 1,539 kwa mwaka mmoja. Ukienda *division four* ni wanafunzi 3,710 hiyo ni mwaka mmoja. Nenda miaka mitatu nyuma, kuna shida ya lugha ya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twendeni tukaandae walimu wanaojua Kiingereza na Kiswahili vizuri. Bora akosekane mwalimu wa hesabu, kwa muda atafundishwa hata mtaani, lakini lugha inafanya watoto wakose masomo na wanakimbia masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mmesema habari ya mimba, ongeza tena, kuna mimba, kuna kuolewa, kazi za majumbani na kushindwa kujua lugha. Mwalimu mwenyewe anayefundisha Kiingereza shuleni hajui Kiingereza. Mwanafunzi anashangaa mwanzo wa kipindi mpaka mwisho wa kipindi halafu unampa mtihani afaulu, hapo mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana Serikali ijipange kuandaa Walimu wazuri wa Kiingereza na ikiwezekana watoto kabla ya kuingia *form one* wafanye *orientation course,* kama vyuo vikuu wanafundisha *CR* siyo! Tumefundishwa zile. Kwa hiyo, hawa watoto wasaidiwe lugha ya mawasiliano na namna ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningetaka nione kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri, walitenga shilingi bilioni 17 ziende kwenye Taasisi ya Elimu ili kuchapisha, kusambaza na kuandika vitabu. Fedha imekaa TAMISEMI miezi mitano, imerudishwa Hazina. Kule Shule yangu ya Kubiterere, Nyagisya, Kimusi, na Nyabichune kuna kitabu kimoja cha *chemistry* tu cha mtaala mpya, halafu fedha imekaa miezi mitano!

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuelezeni ni nini kilitokea? Shilingi bilioni 17 haikufanya kazi ikarudi Hazina, watoto hawana vitabu, walimu hawana vitabu vya kufundishia. Halafu hawa watu wa TAMISEMI waliwachukulia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini fedha isitoke Wizara ya Elimu moja kwa moja wapeleke Taasisi ya Elimu waka-*print,* wakaandike, na wakasambaze? Kwanza shule unakuta ina upungufu wa walimu. Tarime Vijijini tuna upungufu wa walimu wa Sayansi 145, sasa hakuna mwalimu wa Sayansi, hakuna kitabu cha Sayansi, mwalimu hana, hata shule ya jirani huwezi kuazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani huu mtalaa hebu tujipange vizuri. Mambo ambayo tunaweza kuyatekeleza ndani ya uwezo wetu tuyafanyie kazi. Baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, sasa ungetupatia kabisa na *Newton's Law of Motion. (Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Eehee!

**NAIBU SPIKA:** Aaah, kaa chini! *(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni baharia, umesoma sayansi kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, halafu jiandae Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Tendega.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwenye Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Geita hasa Geita Mjini ni mashahidi. Tumeshuhudia ongezeko la shule nyingi za msingi, sekondari, pia Ujenzi wa Shule Maalum ya Wasichana *Geita Girls* ambayo imekamilika na sasa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kabla sijaendelea, namhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba hoja inayozungumzwa ya walimu ni tatizo kubwa sana, ingawa nadhani inawahusu sana TAMISEMI, lakini nina hoja mahsusi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule yangu moja ya *Shanta Mine* na shule nyingine ya Geita Sekondari kuna walimu wanajitolea pale wa Hesabu na masomo ya Sayansi na zilipotangazwa nafasi za ajira hawa walimu wakaenda kufanya *interview,* katika shule hizo. Katika shule hizo, nakuruhusu u-*google* ataona matokeo ya hizo shule ni *division one, division two* watoto wanafaulu masomo ya Sayansi na Hesabu, lakini hawa walimu walioenda kufanya *interview* wakafeli, *interview* ambayo wameletewa kutoka Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamefundisha watoto wanafaulu lakini wanafeli *interview* inayokuja kufanywa ili waweze kuajiriwa, sasa napata shida sana, amesema hapa mchangiaji wa kwanza na wa pili nini kinatokea hapa? Kwamba mwalimu ambaye anafundisha watoto wanafaulu, akija yeye kufanyiwa *interview* anafeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona wengi wanalalamika wanaona kama kuna upendeleo, kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kuangalia vizuri, lakini hilo pia litusaidie kwenda kwenye vyuo vyetu kuangalia pengine mahitaji ya walimu ya sasa na wanaoandaa mitihani ya *interview* hayafanani na walimu waliofundishwa zamani na hii ndiyo changamoto ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwa Mheshimiwa Waziri, ni mwaka 2024 wakati wa maonesho ya madini pale Geita, nashukuru sana alikuwepo Mheshimiwa Waziri pamoja na Mawaziri wengine karibu kumi. Maonesho yetu yalihudhuriwa na Mheshimiwa Rais na Wananchi wa Geita wanakumbukumbu na maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maombi ya wananchi wa Geita, tunaipongeza Serikali kwa ujenzi wa Chuo cha *VETA*.

Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia Chuo angalau kikakamilika na kimeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimweleza kwamba mwaka 2024 kilikuwa na upungufu mwingi, akaahidi atakuja. Nadhani muda upo, utakuja, lakini yapo maombi maalumu tuliyaleta wakati wa maonesho yale, tunataka Chuo chetu za *VETA* cha Geita Mjini kifundishe zaidi teknolojia ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunasema hivyo? Kwa sababu vijana wengi wanaozunguka maeneo yale wanatamani kufanya kazi kwenye maeneo ya madini. Wanatamani kufanya kazi ambazo zina uhusiano na shughuli za mitambo ya madini, shughuli za uchenjuaji wa madini, shughuli za uchimbaji wa madini, shughuli za utambuzi wa madini, na shughuli za ku-*process* madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natamani kuona kwenye bajeti hii, Mheshimiwa Waziri akiwa amechukua yale maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo wananchi wa Geita wanatamani kuyaona kwenye bajeti hii yakiwa yameingizwa kwenye bajeti yake, ikiwa ni pamoja na kukipa Chuo kile miundombinu na vifaa vya kutosha ili kiweze kutoa *product* ambazo zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema wakati ule kwamba ni kweli kilikamilika, lakini kilikamilika kwa zimamoto. Ukifika pale utaona ni chuo ambacho hakina vifaa vingi. Tunashukuru kimeanza, safari imeanza na ninaamini kitakamilika, lakini naomba Mheshimiwa Waziri afike akitengee fedha, kitakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye eneo hilo, changamoto ya ajira ni kubwa nchini. Hakuna Wizara nyingine naitazama ambayo itasaidia Serikali kumaliza changamoto hii. Ninalo wazo, badala ya kufikiri kupeleka *graduates* wakakae *VETA* mwaka mmoja, miezi sita, miezi mingapi tufikirie kuwa na *incubators.* Tuwe na *incubators* nyingi maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *incubators* zinaweza zikatengenezwa. Kwanza ziwekewe *resources*, pawe na *mentorship* ambayo ita-*focus* kwenye kukabiliana na tatizo tulilonalo sasa. Kwenye *incubators* unaweza ukatengeneza *entrepreneurs,* ukafanya *innovations,* ukafanya *technology* mbalimbali, lakini zikawa zime-*focus* jambo fulani mahsusi na kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *incubators* nyingi ambazo ziko huko duniani, zinasaidia sana kwenye kupunguza tatizo la ajira, hata kwenye *management* ya *talents* mbalimbali, unakuta kuna mtu ana *talent* ambayo badala ya kwenda chuo, anaweza kupelekwa kwenye *incubator* sehemu fulani na kwa muda mfupi akaweza kujitokeza na hivyo kuweza kumwajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maoni yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba katika eneo hilo badala ya kufikiria *graduates* wote Tanzania waanze kwenda *VETA* ama wapi, tufikirie namna ambavyo tutatengeneza *incubators* ambazo zitasaidia kupunguza tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo nataka kuzungumza kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba Wizara ya Elimu ilifuta Walimu wa *Grade* A. Ikasema, itakuwa na walimu waliomaliza *Form Six,* tena ikasema angalau *division one, two, three, ni* jambo jema kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huku chini kuna vyuo ambavyo mtu ana 'D' nne anaanza kusoma *certificate,* anasoma *diploma* anakwenda kwenye *NACTVET,* anakwenda anapata *diploma* baadaye ana-*graduate BBA,* halafu huyo mtu anakwenda kusoma *Post Graduate Diploma* ya *Education,* tunawaona wanaajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kupata ufafanuzi, tumefuta *Grade 'A'* ya walimu ambao wamefaulu *Form Four* ana masomo mazuri, ana *division three,* ana ngapi? Huku juu tunaelekea kupokea walimu waliopata 'D' nne ambao tu ana

*degree* ya *BBA* ya kuungaunga halafu akaenda kupata *Post Graduate Diploma* ya *Education* ili kwenda ku-*cover gap.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwachukue walimu hawa hawa kama tuna tatizo la masomo ya biashara, tukawapeleka *incubator,* tukawapeleka *short course,* waliosoma Kiingereza na masomo mengine, tukawapeleka kufundisha masomo ya biashara badala ya kuchukua mtu ambaye ukimtazama kama anavyosema Mheshimiwa Waitara hata anachokwenda kufundisha hakifahamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani utaratibu huu unaweza kutusaidia tukatoa *product* ambazo zimepata elimu ambayo kwanza ina viwango, lakini anayefundisha anajua anachokifundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Tendega, na Mheshimiwa Mkundi jiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuiongoza na kuisimamia hii Wizara ya Elimu. Nawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa ambayo yamepelekea kuufumua mfumo wa elimu hapa nchini na kuja na mitaala mipya ambayo tunaamini inaenda kukidhi mahitaji ya Taifa letu. Tunampa hongera sana kwa hayo maono mapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu, kwanza Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa jina peke yake, maana yake inazo kazi mahsusi kama tatu. Kazi ya elimu, kazi ya sayansi na teknolojia zake. Sasa elimu yetu hii lazima itupatie maarifa na ujuzi

utakaosaidia kubadilisha tabia zetu, kubadilisha mitazamo yetu ili iweze kuendana na mahitaji ya Taifa, mahitaji ya jamii na tuweze kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu yetu lazima iwaandae vijana wetu kujenga Taifa linalojitegemea. Hatuwezi kujenga Taifa linalojitegemea kama hatutakuwa na elimu madhubuti yenye kuwapatia maarifa na ujuzi utakaotuwezesha kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi hii inafanywa vizuri na tumeanza kuifanya vizuri lakini elimu yetu ndiyo inatakiwa kufanya kazi kubwa yaku-*support* sekta nyingine zote ili ziweze kuendelea na kutoa mchango mkubwa wa uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, viwanda vyetu tunavyotaka kujenga, iwe ni kilimo, iwe ni uvuvi, tunahitaji maarifa na ujuzi utakaosaidia kusukuma na kuchagiza kuhakikisha kwamba tunapata hayo maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi hii imeanza na inafanyika vizuri, nami nawapongeza, lakini tunalo eneo la Sayansi na Hesabu ambalo limekuwa ni changamoto kubwa. Mheshimiwa Waziri sasa hivi akienda katika maeneo mengi, akienda katika shule zetu kuanzia za msingi, sekondari na kuendelea, watoto wetu wanaogopa masomo ya Sayansi na Hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake hatuwezi kujenga nchi imara bila kuwa na sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, lazima tuwaandae watoto wetu kupenda masomo ya sayansi, kama tunasema sayansi hatuihitaji, maana yake hatutaki kuishi hapa duniani. Bila sayansi hatuwezi kwenda popote. Kwa hiyo, ni lazima tuwaandae vijana wetu kupenda masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni nini tufanye? Ukichukua kwa mfano kwenye hesabu, tatizo la hesabu ni nyepesi na vijana wanaweza kuzielewa, lakini kabla hawajaenda hata shuleni wameambiwa Hesabu ni ngumu, wameambiwa Sayansi ni ngumu. Ukitaka kuona hilo ni tatizo la saikolojia, wewe mpe mtoto

hesabu ndogo tu, mwambie mbili kuongeza kisanduku sawa sawa na sita kwenye kisanduku ni ngapi? Anasema hizo nyepesi sana, hizo nilisoma nyepesi sana. Sasa badilisha weka pale mbili kuongeza X sawasawa na sita, (2+X = 6) anasema hizo ngumu za 'X' sizijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unajua kwamba hapa watoto tatizo ni la kisaikolojia zaidi. Kwa hiyo, kumbe Hesabu ni ile ile, *formula* ni ile ile, lakini anaogopa akishaona 'X' akishaona 'Y' tayari hesabu imekuwa ngumu. Kwa hiyo, nadhani tujenge misingi ya vijana wetu kuweza kupenda hesabu na kupenda masomo ya Sayansi, hii itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji wataalamu mbalimbali. niliona mwaka huo wakati Mheshimiwa Waziri anahitaji walimu wa masomo ya sayansi, na walimu wa *physics. S*omo la fizikia walimu hawakupatikana wa kutosha. Sina takwimu sahihi, lakini niliambiwa hawajapatikana wa kutosha. Sasa hivi katika maeneo mengi tunatafuta walimu wa Fizikia hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunayo fursa hii, tuwaandae watoto kwenye masomo ya sayansi, tuandae watoto kwenye masomo ya Fizikia, tuandae watoto kwenye masomo ya Hesabu ili tuweze kujenga Taifa letu zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka kusema, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana, naishukuru sana Wizara, na ninamshukuru Mheshimiwa Rais, wametupatia zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kujenga Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kinaenda vizuri, kinajengwa vizuri, tunashukuru sana, lakini naomba kile Chuo cha *VETA* wakati kinajengwa, tunatamani kinapokamilika watoto wa Jimbo la Vwawa wa Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe kwa sababu ni Chuo cha Mkoa, basi na vifaa viwe vimefika ili waweze kupata ujuzi na maarifa mbalimbali yanayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo letu, sisi tunazo shule za sekondari. Kwa mfano, Wilaya ya Mbozi ni zaidi ya shule 75 za

sekondari. Tunazo shule za msingi za zaidi ya 108 kwenye Wilaya ya Mbozi, lakini ukiangalia wale watoto wote wanaomaliza kidato cha nne na Mheshimiwa Waziri hili ni tatizo kubwa na ni kazi ya Wizara yake kwamba, sasa hivi katika nchi nzima ukiangalia watoto wanaomaliza kidato cha nne, ni karibu shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa vyuo vyetu vya kati, vya juu na vyovyote vile kuchukua hao watoto pamoja na shule za kidato cha tano na sita haufiki zaidi ya 400,000.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, malizia.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba mweke mkakati hapo. Naomba kwa nusu dakika, tunaomba pale Ikunga wametenga eneo ekari tatu, wanaomba Chuo cha Elimu ya Juu au Chuo cha Elimu ya Kati, eneo lipo pale Nyimbili. Pia kuna eneo Kambi ya Vijana ya Sasanda, pana eneo. Pale Hasamba kuna maeneo tumeyatenga kwa ajili ya elimu. Mkoa wetu tunahitaji vyuo vya elimu ya juu ili viweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tendega, Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Issaay.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia katika bajeti ya hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo unaifanya, kwa kweli umejitahidi sana kuhakikisha tunakwenda na mafunzo ya amali na tunakuwa na wanafunzi ambao wanaweza kufanya kazi kwa mikono yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uthubutu mkubwa ambao ameufanya kwa kuhakikisha kwamba, tunakuwa na sera nzuri, lakini tunakuwa na mitaala ambayo itakuwa inalega ujuzi ambao wanafunzi wetu wataweza kuupata pale ambapo watafundishwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza, kwa kuwa na Vyuo vya *VETA* ambavyo vimeweza kuanzishwa na wanafunzi walio wengi watakwenda kule. Sasa, sambamba na kuwa na hivyo Vyuo vya *VETA*, ushauri wangu waende sambamba na kuandaa wakufunzi watakaokwenda kufundisha wanafunzi hao, ambao watakuwa wanaweza kufundisha kwa ubora kama ilivyokuwa hapo awali. Pia mweze kuendana na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana za vyuo vingi kutokuwa na vitendeakazi vya kufundishia hayo mafunzo ya amali. Sasa, katika bajeti yake naomba aweke bajeti maalum kwa ajili ya vitendeakazi pamoja na karakana ambazo zitatumika kuweza kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi ambao watakuwa wanafundishwa katika vyuo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii elimu ya amali inatakiwa kuwa elimu ambayo ni bora kabisa. Sasa, ombi langu wale wadhibiti ubora ambao wapo, kama mtaweza kuwawezesha ni kujumu la Serikali kuwawezesha wadhibiti ubora kwenda kufuatilia udhibiti ubora wa hiyo elimu inayotolewa, kwa sababu tutasema tuna hiyo elimu ya amali, lakini kama wadhibiti ubora hatutawawezesha ipasavyo, hatutawapatia fedha, tutakwenda kuwa na jambo lile lile, kwa sababu elimu ili iwe nzuri ni lazima kuwe na wadhibiti ubora wanaongalia *quality* yake kwamba hii elimu ni bora ama siyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na elimu ambayo ipo, lakini tukijipima na nchi nyingine ama na wengine tunaona kwamba bado hatujafikia na ndiyo maana Mheshimiwa Rais

akaamua kwamba tutengeneze mitaala yenye mafunzo ya amali ambayo yatatufikisha hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninasisitiza wadhibiti ubora waweze kuongezeka. Kwanza mwaajiri wa kutosha, mwaandae wa kutosha na waweze kupewa *tools* ambazo zitakwenda kuwasaidia katika kuhakikisha wanakwenda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende katika kipengele cha changamoto ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika bajeti zetu. Mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 Wizara ilikopa shilingi bilioni tano kwa ajili ya miradi minne ambayo ilikopea *SEQUIP, GPE-Lens* na *EASTRIP* ambayo ilitakiwa ifanyike, lakini kwa sababu tuliondoa hizo fedha hatukwenda kufanyia katika kazi hiyo, mwaka 2023/2024 tuliomba tena fedha tutakosa shilingi bilioni 124 na *point*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumekosa hizi fedha kwa sababu tulikopa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo, hatukuitekeleza ipasavyo, sasa tukaja tukaomba fedha tena tukanyimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikatai kuomba fedha na sikatai, lakini *CAG* ametuambia kwamba, wamebaini fedha hizo zilikwenda kutumika huko ambapo hawakuombea. Sasa kama siku nyingine tunataka kutumia hizo fedha, ni bora tukatumia fedha za ndani, lakini tusitumie hizo fedha kwa sababu zinakwenda kusababisha kukosa fedha hizo ambazo tulikuwa tunatakiwa tuzifanyie katika miradi ambayo tulikuwa tunaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuwa makini katika kuangalia namna hiyo, ili tuweze kupata fedha ambazo zinaweza kutusaidia. Kwa sababu sisi wenyewe hatuna bajeti ambayo inajitosheleza peke yake, tunategemea bajeti ya ndani na nje. Kwa hiyo, tunapoomba bajeti kwa kitu ambacho umekiombea, basi tupeleke malengo yetu kule tulikoombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii, tuna makubaliano ya bajeti za elimu katika ukanda wetu. Bajeti za elimu ziweze kufikia angalau 15% ya bajeti nzima ya Serikali. Kwa hiyo, tuna matarajio kwamba, Bajeti ya Serikali yetu nzima inaweza ikafikia shilingi trilioni 55. Sasa, bajeti iliyopita angalau tulipata shilingi 12.5%, lakini nimeona Mheshimiwa Waziri ameomba shilingi trilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaangalia katika ile 15% tutafikia asilimia ngapi? Utaona kwamba hata nusu tunaweza tusifikie ambayo inatakiwa. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hivyo tunavyokubaliana kikanda, basi bajeti zetu ziwe angalau zinafikia hapo ili tuweze kwenda sambamba, kwa sababu hapa umeeleza kwamba, kuna elimu jumuishi ambayo inatakiwa iwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo elimu jumuishi ina mambo ya akili mnemba, masuala ya watu wenye ulemavu na masaula mbalimbali ambayo yapo kwenye elimu jumuishi. Sasa, hayo yote yatahitaji fedha, kama haitatosha ina maana tutaweka kwenye bajeti, lakini utekelezaji utakwenda kuwa siyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tunapoangalia hizi bajeti na tunapoenda kwenye bajeti kuu, basi angalau isogee, ivuke, ifikie, hata kama haifiki, basi isiwe chini sana ya makubaliano ya kikanda ambayo tunakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni vitabu. Nawapongeza wameweza kuandaa, Taasisi ya Elimu imeandaa vitabu vya kutosha, lakini kumekuwa na changamoto. Hivyo vitabu havifiki kwa wakati, na huu ni mtaala mpya. Sasa kama ni mtaala ulioboreshwa au mpya, walimu wanakuwa bado hawajaweza ku-*capture* mambo yanayotakiwa, hawajafundishwa wote. Kwa hiyo, vitabu vinapochelewa haviendi sambamba na mtaala unavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali ipeleke mapema vitabu, mwaka unavyoanza na vitabu viwepo. Kama Taasisi ya Elimu inakosa fedha, basi iwezeshwe kusafirisha vitabu

viweze kwenda kwa wakati, wanafunzi wale waweze kupata vitabu waweze kuvitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi, jiandae Mheshimiwa Issaay.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Taifa letu lipo kwenye mkakati mkubwa wa kufanya mapinduzi makubwa ya kitaaluma na kielimu, ili tuweze kupata maendeleo ya kiuchumi, na hatuwezi kufikia maendeleo hayo bila kurudi kuimarisha sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022 kwa mujibu wa sensa, Tanzania ina watu zaidi ya milioni 60, lakini karibu zaidi ya 40% ya kundi hilo ni kundi la umri wa kati ambalo ni kundi la wazalishaji. Kama kundi hili tutalitumia vizuri linaweza kutusaidia kufanya mapinduzi makubwa sana ya kiuchumi. Sasa, ili tufikie huko ni lazima kundi hili litumike, lakini haliwezi kutumika bila kuandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimeona nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa sana uliofanyika kwenye sekta ya elimu. Nitakuwa sijatenda haki kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda, Naibu wake na timu nzima ya Wizara ya Elimu kwa namna ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko makubwa sana kwenye sekta ya elimu kwenye nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa sana suala la Elimu ya Amali, lakini sambamba na hilo, nilitamani niongelee eneo la *VETA*. Katika maeneo mengi kwenye mataifa mengi yaliyopata maendeleo na kufanya mapinduzi makubwa ya kiuchumi, mengi yametumia hizi *vocational training* kwa ajili ya kutengeneza wazalishaji mali kwenye viwanda na hatimaye kufikia maendeleo hayo ya kichumi. Kwa sababu tunapoanzisha *VETA* hizi, hata sisi kwetu hapa lengo la hizi *VETA* kwanza ni kuandaa utaalam,

kuchochea ujasiriamali, kuimarisha ajira na hatimaye sasa kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameonesha namna ambavyo wanafanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Ni jambo jema sana kwa sababu kupitia mapitio haya kama itafanyika vizuri, jambo hili litatoa mwelekezo mzuri wa namna ambavyo hivi Vyuo vya *VETA* vinaweza kutusaidia, kwa sababu kama Taifa, tumefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye ujenzi wa *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ninaamini tukifanya kama ambavyo tunatarajia, itatusaidia sana ku-*absorb* namba kubwa ya vijana kuingia kwenye taasisi hizi, wakapata uelewa na utaalam ambao utasaidia kufikia lengo letu la mapinduzi ya kichumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka nishauri mambo mawili kwenye eneo hili. Ni lazima kama lengo letu ni kufanya mapinduzi ya kiuchumi, ni lazima tuendane na teknolojia na mabadiliko yanayoendelea kwenye teknolojia, na kwa sababu hiyo, kama walivyosema wachangiaji kadhaa, uwepo wa vifaa vya kisasa vinavyoendana na mabadiliko ya kiteknolojia na sayansi kwenye vyuo hivi, ni jambo la msingi sana. Vile ambavyo tayari vimeshaanza, ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba, vinapatiwa vifaa. *(Makofi)*

Naibu Spika, vile ambavyo vinaendelea kujengwa, basi utaratibu wa kupata vifaa ni jambo la msingi sana, ili pale ambapo vinakuwa vimekamilika, basi vifaa hivyo vinapatikana. Nikitoa mfano, kwenye Jimbo langu la Ukerewe, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Wizara imetusaidia kujenga Chuo cha Ufundi cha *VETA* pale Ukerewe, lakini chuo hiki bado hakina vifaa. Walimu wanalazimika kuazima vifaa kwenye vyuo vya jirani ndiyo wafundishe watoto kwenye chuo kile. Kwa hiyo, ni muhimu sana vikapatikana vifaa *(machine tools)* zikawepo, ili watoto wanapoenda pale waweze kufundishwa na kupata kile ambacho tunakitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilipenda kushauri vilevile kama ambavyo baadhi wamesema, ni maandalizi ya wakufunzi kwenye vyuo hivyo. Ni muhimu sana tukapata wataalam, ili tunapokuwa tunapata watoto kuweza kupata elimu hii ya ufundi, basi wataalam wakufunzi wawepo kwa ajili ya kuwasaidia kuwa-*equip* watoto hawa na taaluma ile tunayoitarajia, mwisho wa siku tupate *products* ambazo zinaweza kutusaidia kwenye eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano, vilevile nashukuru kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kwamba wanaandaa wanafunzi 391 wanaopewa mafunzo kwa ajili ya kuja kufundisha, lakini kwangu naona kama hii namba ni ndogo kwa sababu Chuo cha *VETA* cha Ukerewe kina upungufu kwa mfano wa wakufunzi karibu tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiangalia na vyuo vingine nchi nzima bado mahitaji ni makubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana maandalizi ya wakufunzi hawa na hasa wenye uwezo na ujuzi wa kuwasaidia vijana wetu ikahitaji uwekezaji mkubwa, ili tupate wakufunzi wa kutosha watakaotusaidia kwa ajili ya kuandaaa vijana ambao kweli wanaweza kuwa *competent,* wakatusaidia kufanya mapinduzi hayo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kuchangia ni juu ya namna ambavyo tunaweza tukapata watoto wazuri wenye uelewa na uwezo wa kitaaluma. Moja kati ya changamoto tulizonazo kwenye Taifa letu, tunachukulia kirahisi sana suala la lishe kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku za karibuni kumekuwa na msisitizo kuhakikisha kwamba watoto wanapata chakula wanapokuwa shuleni. Bado kuna uelewa mdogo sana wa jamii yetu juu ya umuhimu wa kuhakikisha kwamba watoto wanapata lishe wakiwa shuleni. Matokeo yake pamoja na kwamba ni kweli Serikali haiwezi kutoa chakula kwa watoto wote, jamii imekuwa inashirikishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamii inaona kama jambo hili siyo la lazima na muhimu, lakini ni jambo ambalo linaathiri sana watoto wetu kukua kiakili, kuwa na uwezo wa ku-*absorb* kile ambacho wanapewa kama wanafunzi na hatimaye kuwa watoto ambao wanatoka wakiwa na uwezo wa kulisaidia Taifa, kwa sababu akili inakuwa haiwezi kuwa na nguvu ya uelewa kama ambavyo ingekuwa iwapo wangepata chakula shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali kupitia Wizara ikishirikiana na TAMISEMI itoe mwongozo, elimu au namna yoyote ambayo itafanya jamii ihamasike, ielewe nini umuhimu wa watoto wetu kupata chakula shuleni na hatimaye watoto wale wanapokuwa wanapata chakula, wanakuwa na uwezo wa kuelewa na kupata yale ambayo wanafundishwa na hatimaye Taifa linakuwa na *products* ambazo zinakuwa na uwezo kweli na nguvu na zinaweza zikasaidia Taifa letu kuleta maendeleo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Pondeza, jiandae Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, nilikuita lakini nilipoona haupo nikajua labda hukukaa kwenye kiti chako, basi endelea. *(Kicheko)*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, *mic* ilikuwa ina shida kidogo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kuungana na Watanzania wote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema nyingi katika nchi yetu, pia kwa baraka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii tena kwa ufupi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye hii Wizara na sekta ya elimu nchini. Amefanya kazi kubwa na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake; Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitazungumza maeneo machache. Eneo la kwanza ni la uboreshaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi Nchini na ikiwepo Chuo cha Tango *FDC* kule Mbulu. Kwanza, naishukuru Serikali kwa sababu tayari walishakarabati zaidi ya nusu ya majengo. Chuo kile kilikuwa cha enzi ya ukoloni, sasa hivi maeneo mengi katika majengo yamekarabatiwa na mengine yanayohitajika yamejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitatu sasa bado viporo vya majengo havijakamilishwa, na niseme, katika bajeti hii kwa fedha zile zilizotengwa, tuone namna ya kukamilisha yale majengo. Pia, kwa kuwa sisi hatukupata fursa ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*, tumeambiwa hivi Vyuo vya *FDC* vitakuwa *VETA B*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, naishauri Serikali *Tango FDC* ni chuo cha zamani hapa nchini na bahati nzuri kina rasilimali ya ardhi. Mheshimiwa Waziri anisikilize, nilienda na Naibu Waziri tukafanya ziara. Nilipomshawishi tubadilishe, Marehemu Olenasha aliniambia tunakuja na "Tanzania ya Viwanda", hatuwezi kubadilisha chuo hiki kuwa *branch* ya Chuo Kukuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwelewa wakati ule kwamba tunapokarabati, baadaye tutakuja kufanya maboresho. Pia tutaanzisha fani za kiufundi, kwa maana pengine kwenye sekta ya kilimo kwa sasa ina ekari karibu 400 ukitoa ya makazi ni ekari 200 za akiba zipo. Lakini katika mawazo yale ya awali ilikuwa tuwe na ranchi za ufugaji na pia tuwe na eneo lingine linalotumika kwa matumizi mbalimbali ya ufundi ikiwepo kwa maana ya ranchi za

kilimo, pia *demarcation* ya kilimo kwa maana ya mashamba darasa pia na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sasa hatujatumia hiyo rasilimali. Mheshimiwa Waziri, nadhani kama inawezekana, tunapoanzisha vyuo hivi vya *VETA* tukaacha zile *FDC,* bado hatujapata tija kamili katika eneo hilo kwa maana ya *FDC* kuleta tija nchini na malengo yaliyokusudiwa toka awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba, kama inawezekana, hawana trekta. Wana ekari 200, kilimo chenyewe hakina tija, ni kilimo kinachofanyika chini ya kiwango. Unaweza ukakuta pengine kwa ekari hawazalishi hata zile gunia 20 hadi 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna haja ya timu ya Mheshimiwa Waziri kufanya tathmini ya marejeo ya *FDC* nchi nzima ili kuona tija inayofanyika na mazoezi ya vitendo yanayofanyika kwenye vyuo hivyo nchini ili kuleta tija zaidi na namna ambavyo vijana hawa baadaye wataweza kutumia ujuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye eneo la elimu ya amali, naishukuru Serikali. Sasa hivi tunajenga shule ya amali kule Bunyoda, katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Jambo ambalo nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, ni kwamba, ujenzi huu wa shule ya amali tuangalie utaratibu unaowezekana wa kwamba tunajenga shule za amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie, je, wakati huu tunapojenga shule za amali kwa ajili ya ujuzi stadi pengine wa kutengeneza simu, kutengeneza vifaa mbalimbali na ujuzi wa mabomba na vitu kadhaa kama hivyo, hatuwezi kuwa tumekaa meza moja, yaani Wizara ya Elimu pamoja na Viwanda kwa maana ya *SIDO,* na pia Wizara nyingine mtambuka ili waje mezani kutambua namna ambavyo siyo kutengeneza tu vifaa kama ujuzi, na ubunifu unakuwepo wa kuwa na viwanda vidogo kupitia *SIDO*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo viwanda vidogo vitachochea kwa jinsi ambavyo malighafi zinakuwepo katika baadhi ya maeneo nchini ili walau vijana wanapojifunza na baadaye isiwe sisi ndio tunatengeneza simu kutoka nje, tunaunganisha umeme kwa kutegemea waya kutoka nje. Pia, kuna masuala kama mbegu na vitu gani ambapo kuna fursa kwenye maeneo hayo nchini, ili kwa pamoja Vyuo vya *FDC (VETA)*, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Elimu, na Wizara nyingine Mtambuka ili waje na mpango ambao unakuwa mwambata wa fani hizi mbili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda, niendelee pia kuona mchango mkubwa ambao Waziri ameutoa katika Wizara hii kwa maboresho haya ya shule ya amali. Tunaona shule zinajengwa, lakini tunakuta kwenye yale maeneo ambayo pengine shule tayari zimeshaanza kupokea watoto, hatujaandaa kama ni karakana ama shule hii tumeiandaa kwa mtaala upi? Kama ni mtaala wa sayansi, ama ni mtaala wa kilimo, ama mtaala wa aina gani? Kama ni karakana na vitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani katika bajeti zetu zinazokuja kuanzia mwaka huu, tuanze kufikiri shule zile zinapata vifaa vya kujifunzia, kwa maana ya fani iliyokusudiwa pale ili tuweze kuleta tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kwamba, katika eneo hili la vyuo vikuu, vijana wengi bado hawajapata mikopo na wanakuwa na mdondoko kwa maana ya kuahirisha masomo. Nadhani kuna haja ya Serikali kutazama upya, vijana wangapi nchini kwa mwaka wameshindwa kuendelea na masomo baada ya changamoto hii ya ada, ili kuona ni namna gani hao wote ambao wamekosa namna ya kuendelea na masomo kwa ajili ya ukosefu wa ada, tunawatafutia dirisha lingine la kutambua matatizo yao na namna ya wao kurudi kwenda kusoma, kwa sababu haki ya kuwasomesha na wajibu wa kuwahudumia kwa ada tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, nendeni kwenye takwimu zetu mtaona idadi kubwa ya vijana wengi wameshindwa

kuendelea na masomo kwa ajili ya ada, na kwa maana ya gharama ya vyuo vikuu. Ni kweli kuwa vijana wengi na hasa wale wananchi walioko kijijini, ama kwa taarifa zao kutokukaa vizuri ama kwa uwezo wetu mdogo wa Serikali, lakini kwa ujumla wao wameshindwa kuendelea na masomo. Hii sehemu itasaidia sana kutoa imani na pia kuleta ubunifu zaidi, lakini pia vijana hao kumaliza safari yao ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee tena kuangalia eneo hili la elimu maalum. Nawashukuru sana, Shule ya Msingi Endagikoti katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na maeneo mengine, mmefanikiwa kujenga mabweni ya watoto wa elimu maalum, lakini hatukuweza kuwapata walimu, hatukuweza kupata vifaa vya ufundishaji, na pia hatukuweza kupata pengine vifaa vingine pamoja na kuajiri watumishi wengine katika maeneo haya ya elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanafunzi wako bweni, lakini walimu wanalipwa pengine kwa kuchangia changia na wengine huwa hawapo, hivyo kukosa tija kwenye eneo hili la hao wanafunzi wa elimu maalum. Naomba kama inawezekana, kwa kuwa ninyi ni sera na wale upande wa elimu pengine ni TAMISEMI, lakini kwa namna ambavyo tayari tumejenga, Serikali ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga mabweni, tuna wanafunzi zaidi ya 40, lakini unakuta walimu wa fani hiyo hawapo, lakini pia unakuta vifaa hatujaweza kutafuta na tukapeleka pamoja na vifaa vingine mbalimbali, lakini pia na watumishi wasio walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafikiri kuna haja ya kutazama, je, tumejenga bweni?

*(Hapa kengele ilila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, malizia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga bweni, je, tija inapatikana na hao vijana wanapata

hiyo elimu? Kwa jinsi ambavyo tunaona, kazi kubwa imefanyika ni maboresho yanahitajika. Nawapa hongera Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Wizara itazame vyuo vya *FDC* kama vina tija na kwa namna gani tunavyoweza kuleta maboresho zaidi katika fani mbalimbali ya kuweza kuwapatia vijana wetu ujuzi wa kujiajiri huko baadaye na kwa namna ambavyo tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ussi Pondeza halafu Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi hii leo angalau nami niwe miongoni mwa ambao wataweza kuchangia Wizara yetu hii ya Elimu, katika bajeti yake ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mkenda, Naibu wake, na watendaji wake wakuu wote ambao wamekuwa ni msaada mkubwa kwao katika kuhakikisha wanayatekeleza yale ambayo watu wengi tumeyaishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nitakuwa na jambo moja au mawili, lakini sana nitakuwa na jambo moja. Nitajielekeza katika elimu ya vyuo vya amali ambayo ni sera mpya ambayo imeanzishwa kwa ubunifu wao hawa viongozi wetu, lakini nataka niipe nyama kidogo. Maagizo yao nayakubali *hundred percent*, lakini na maelekezo yao jinsi ambavyo wamekusudia kuifanya iwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwanzo, nachukua nafasi hii pia kuipongeza Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inaongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zaidi katika kuhakikisha vile ambavyo

vinapatikana kwa ajili ya kuinua elimu ndani ya Tanzania hii, lakini na sisi upande wa pili, basi vinatufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwapongeze Wizara hii ya Elimu katika Mradi wao wa *HEET*. Mimi natokea Zanzibar Jimbo langu la Chumbuni lakini ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ndiyo maana nimesimama kuelezea Sera hii ya Elimu ya Juu ambayo na sisi inatuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Wizara hii ya Elimu kwa kuweza kugawa miradi ile ya *HEET* ambayo imekuja kwa nafasi kubwa sana Zanzibar na italeta ufanisi mkubwa ikimalizika. Kama haitoshi, pia kuja kwa hii *HEET* imetoa upanuzi wa kiuchumi na zaidi katika elimu, kiasi ambacho mpaka wenzetu wa *UDSM* sasa hivi nao wameamua kuja Zanzibar na kufungua tawi lao katika maeneo ya Buyu na tumewapa eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wanaendelea na ujenzi na *Inshallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu watafanikiwa lile ambalo wanataka kulifanya, lakini na sisi kama Wazanzibar tutafaidika na uwepo wa *Campus* ile ndani ya Visiwa vyetu vile vya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Mheshimiwa Profesa Mkenda na QS Kipanga, lakini na timu yenu yote kwa kuweza kuyafanikisha haya. Tumekuwa tukipiga kelele sana, mimi mwenyewe nimekuwa nikimwuliza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa anakuwepo sana katika maswali, na nikitaka Mwongozo kwa hii miradi ya *HEET,* lakini namshukuru sana imeweza kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024 tumepata idhini ya dola milioni 21, kiasi ambacho siyo mchezo. Tunasema tunawashukuru sana, tunaipongeza sana Serikali hii inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije sehemu yangu ya pili ambayo nimekusudia. Sehemu yangu ya pili ni kuhusu hii Elimu ya Amali. Elimu ya Amali maana yake ni kuwafundisha wanafunzi

ambao tunao kuhakikisha wanajifunza, wanapata *skills* za kujitegemea; *which is* sawa. Ni jambo zuri, lakini nataka niishauri Serikali sehemu moja au mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuwa tuna maelezo mazuri katika makaratasi haya ya kuifundisha hii elimu yetu ya amali, lakini mpaka sasa hivi sina hakika kama tuna walimu wazuri ambao wanaweza kufundisha elimu ya amali kwa vitendo. Kwa sababu, elimu yetu hii ya amali maana yake ni elimu ya ufundi, yaani kwa Kiswahili cha haraka haraka, mambo mengi sana yanayopatikana ni ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivo, kwanza tunahitajika tuwe na walimu wenye *knowledge* ile ya kufundisha kwa vitendo, isipokuwa sasa hivi vyuo vya amali vipo vingi. Tunasema tunajenga vyuo 64 au 68 siyo haba, jambo siyo dogo, ni zuri, lakini je, tuna walimu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na walimu hao, jambo la pili tunatakiwa tuwe na maabara za kuwafanya watu waweze kusoma kwa vitendo. Elimu ya mafunzo ya amali eneo kubwa inasomeka kwa vitendo kuliko kwa nadharia. Walimu wengi ambao wapo katika hivi vyuo vya elimu ya amali, wengi wanakuwa na mafunzo yale ya nadharia, lakini siyo ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vinapatikana baada ya kuwa na walimu wenye *knowledge* ile na Serikali tukaamua kuweza kujitolea, kuhakikisha kabisa tuna mpango kazi wa kuhakikisha vyombo vinapatikana, maabara zinawekezwa, lakini na walimu wanapatiwa mafunzo ya kuhakikisha wanao uwezo wa kusomesha kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini ninasisitiza hii? Mwezi uliopita Serikali yetu ilipata; mnafahamu sasa hivi tuna ushirikiano na nchi hizi za *UAE* wakataka watu ambao wanaweza kuendesha magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kama mmeangalia wiki iliyopita tu, Qatar walitaka watu 75. Kufika kule yale magari yote *digital* na waliochukuliwa hapa wamefanyiwa mtihani *(vetting)*, wote wamesoma *NIT*, lakini karibu watu wote waliosoma wamesoma *NIT* wanafundishwa zile gia za hapa. Siku hizi kuna gari *digital*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamefika kule, na mnajua Waarabu wenzetu wananunua gari ya mwaka huu. Wamefika kule wanakuta kuna magari ya *digital*. Walikuwa 75, walio-*pass* watano, 70 wamerudi. Hao watano siyo kwamba wameingia moja kwa moja kuendesha, wameingia kusomeshwa sasa zile gari za *digital*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tusije tukawa na hii sera ambayo tunawasifu hapa muda wote, kila anayesimama, kwa ajili ya mafunzo ya amali, kwa sababu, mafunzo ya amali kwanza watu tukiwafundisha kuanzia sekondari na vyuo na ikiwa kuna vitu hivi, maana yake tayari tunawapa vijana ujuzi wa kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake nini sasa? Tukiwapa ujuzi wa kujitegemea maana yake hata ile *mindset* ambayo watu wengi wanajua, mimi nikisoma nikiwa na *degree* mbili lazima niajiriwe. Pia tangu yuko shule ameweza kupata ujuzi wa kutengeneza sabuni, mizinga ya nyuki na nini, au useremala, basi akimaliza hasubiri mpaka apate ajira rasmi ya Serikali au ya yale maeneo maalum. Atakwenda *direct* katika ile elimu ambayo ameipata shuleni wakati anasoma haya mafunzo ya amali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili pia nilikuwa nataka nilisisitize sana. Walimu kupewa uwezo, lakini na shule za amali ziwe na vitendea kazi ambavyo vitaweza kuifanya ile amali yenyewe iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda nichukue nafasi hii pia kukupongeza wewe Naibu Spika, jinsi ambavyo unatuongoza na hili suala letu la elimu nafikiri tunapata muda

mzuri wa kuchangia bila wewe kutusumbua wala kengele. Nawashukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Nianze kwa kuishukuru sana Serikali na kuipongeza hususan Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya kwenye Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda alitutembelea kule Ludewa kwenda kuangalia *VETA* ya Mkoa wa Njombe ambayo imeshakamilika na watoto wameanza. Kwa kweli niweze kuipongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, namshukuru Mheshimiwa Prof. Mkenda, siku ile niliomwomba vifaa, fedha kwa ajili ya samani za ofisi, viti, meza na mambo mengine na nimechungulia huku ninaona kama ametenga fedha. Kwa hiyo, namshukuru sana na ninaishukuru sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa miaka hii mitano Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye elimu ya awali, elimu ya msingi, na elimu ya sekondari. *Reforms* nyingi sana zimefanyika na maboresho makubwa ya miundombinu yamefanyika kwenye elimu ya msingi, sekondari, na ile elimu ya awali, hasa eneo la sekondari. Kwa kweli kazi kubwa sana imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza kwenye bajeti ya Waziri Mkuu na TAMISEMI na nikataja idadi ya shule ambazo Ludewa tumeweza kuzipata. Shule mpya za msingi mbili, shule za sekondari ambazo zimekamilika na kuanza nne, ikiwemo Shule ya

Amali ya Mkoa wa Njombe, ambayo ni *Njombe Technical School* ambayo imejengwa pale Mlangali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tuna kila sababu ya kuishukuru sana Serikali na tuweze kumwahidi Mheshimiwa Rais kwamba, kule Ludewa yeye hatumdai isipokuwa anatudai sisi tuweze kumpigia kura nyingi ili miradi mingine iweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda sasa kujikita kwenye elimu ya vyuo vikuu. Kutokana na maboresho makubwa sana ambayo yamefanyika kwenye elimu ya awali, msingi, na sekondari, sasa tunatarajia hii fujo itahamia kwenye elimu ya juu. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Mipango, waanze sasa kuweka mikakati ya kufanya *reforms* kubwa sana kwenye elimu ya juu, hasa elimu ya *diploma*, cheti na vyuo vikuu. Maeneo haya nayo yaweze kuangaliwa, tuangalie sera tuboreshe tuweze kujilinganisha na wenzetu ngazi ya Kikanda na Ngazi ya Kimataifa, tuone kwamba je, tunaenda sawasawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo nashauri tuliangalie zaidi, kwanza ni miundombinu kwenye vyuo vikuu. Sasa, mtoto asije akaenda kwenye chuo kikuu akaona hamna mazingira yaliyobadilika kutoka kule alikotoka. Lazima vyuo vikuu viweze kuboreshewa sana miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Serikali imefanya kazi kubwa, lakini kutokana na *reforms* kubwa zaidi ambazo zimefanywa na Serikali na fedha nyingi zaidi zilizofanywa huku kwenye elimu ya awali, msingi, na sekondari, sasa tunatarajia huku juu sasa ndiyo fujo inakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, na kwenyewe tuanze kujipanga sasa kuviwezesha vyuo vikuu kuhakikisha kwamba vinaweka miundombinu yake vizuri ya kujifunzia na kufundishia. Vilevile, lazima tuangalie ile *staffing*, tuangalie wale *professors*, je, tuna *Professors* wa kutosha? Kama hakuna, basi tuwe na mikakati kwa kushirikiana na Tume ya Mipango kuhakikisha kwamba

tunazalisha wanataaluma wa kutosha kwa ajili ya kufanya kazi kwenye vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuangalia hawa *Professors* wawe kwa kiwango cha kutosha, vilevile tuendelee kuangalia hata muda wa *professors* kustaafu. Nakumbuka kuna Mwalimu wetu mmoja hapo *UDOM* alikuwa anaitwa Kopoka, alistaafu akiwa bado ana uwezo mkubwa, ana nguvu, na alikuwa anaweza kuendelea kulisaidia Taifa letu, lakini unamlazimisha astaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuangalie vizuri hili eneo kwa sababu kuna bidhaa nyingine inavyozidi kukaa ndiyo inazidi kuwa bora. Nafikiri hata divai ya Dodoma ikikaa muda mrefu inakuwa bora zaidi. Kwa hiyo, hata *professors*, yaani jinsi wanavyokuwa wametumika muda mrefu, ndiyo wanapata uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine unakuta anachelewa kufikia hiyo ngazi ya kupata Uprofesa, halafu anatumikia kidogo anaambiwa astaafu. Kwa hiyo, tuendelee hapo, lakini vilevile tuwe na mikakati ya kupeleka hawa madaktari na wale wenye *Masters* kwenye masomo ya mbele zaidi ili tuweze kuwa na *staffing* ya kutosha kwa ajili ya vyuo vikuu vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie hata eneo la kuwezesha vyuo vikuu kifedha ili waweze kufanya tafiti nyingi zaidi, na zile tafiti zinaweza kuwa na manufaa pia kwa Serikali, wakashirikiana na Tume ya Mipango na Wizara mbalimbali. Hii itakuwa na manufaa makubwa sana kwa Taifa. Kwa hiyo, siyo vibaya tukiendelea kusimamia ile asilimia fulani ya pato letu la Taifa (mapato ya nchi) iende kwenye maeneo ya tafiti na tuweze kushirikisha vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tuangalie hata maslahi ya hawa watumishi wa vyuo vikuu ili kusiwe na wengi wanaokimbilia nchi nyingine kwa ajili ya kwenda kufanya kazi kwa kutafuta mafao mazuri zaidi. Tunatamani kuona hawa wahadhiri, maprofesa, madaktari, watoke maeneo mengine warudi vyuoni

kwenda kufundisha. Hili litawezekana tu iwapo Serikali itaongeza kulipa thamani eneo la taaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongea hapa Mheshimiwa Hasunga, amesema Sekta ya Elimu ndiyo inazalisha wataalamu kwa ajili ya sekta nyingine zote. Kwa hiyo, lazima tuangalie pia maslahi yao kuhakikisha kwamba watu wanatoka maeneo mengine na hawakimbii nchi yetu kwa ajili ya kwenda kufanya kazi maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, hata eneo la kusimamia maadili kwenye vyuo vikuu, kudhibiti rushwa, ili wale wanafunzi waweze kufundishwa kwa misingi ambayo inakubalika na waweze kupata elimu ile ambayo itawafanya wawe wabunifu, wawe na ujuzi wa kutosha, lakini siyo ile kufaulu kutokana na njia nyingine ambazo ni kinyume na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni eneo la mikopo ya elimu ya juu. Naipongeza sana Serikali. Nilikuwa naangalia ukurasa wa 35 Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa kwamba, "ongezeko la mikopo ya elimu ya juu kufikia shilingi bilioni 787.4 mwaka 2024/2025, kutoka shilingi bilioni 570 mwaka 2021/2022". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii kwa kweli ni mapinduzi makubwa sana, Serikali imeweza kuyafanya. Kwa hiyo, natoa pongezi nyingi na ninaipongeza pia kwa kuanzisha mikopo kwa wale wanaosoma ngazi ya cheti na *diploma*, hasa kwa kozi zile ambazo zina uhitaji mkubwa kwenye jamii na kwenye soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia wale watu wa Bodi ya Mikopo, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameongeza sana hizi fedha, vile vigezo vyao hasa vinavyowaondoa wale waliosoma shule binafsi kuanzia shule ya msingi na sekondari. Hii inaumiza watoto wengi ambao walipata ufadhili wa muda au walikuwa wana wazazi wenye uwezo, baadaye labda mzazi kafariki, sasa, wale wanaangalia historia badala ya kuangalia hali halisi ya mtoto wakati anaomba mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia hata kule Jimboni kwangu Ludewa, kuna watoto walikuwa wamesaidiwa na Ma-*father* (Mapadri) kwa ajili ya kwenda kusoma na walisoma shule binafsi, lakini baadaye wanavyokuja kuomba mikopo mfumo unawakataa. Kwa hiyo, naomba sana hili eneo tuweze kuliangalia vizuri ili watoto waweze kupata masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mwingine ameelezea hapa, Mheshimiwa Issaay, amezungumzia kwamba kuna watoto pia ambao wameshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mikopo. Serikali ingeshirikiana na Wakuu wa Wilaya katika eneo hili kuweza kuwatambua wale watoto ambao walisoma kidogo na kukatisha masomo yao kutokana na kukosa mikopo au kupata asilimia ambazo hazikuwawezesha waweze kubaki masomoni wakati wote. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga, kengele ilishalia mara ya pili, malizia. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Vilevile, naomba miundombinu ya barabara kwenye shule za sekondari. Serikali iangalie *checklist* hasa maeneo ya pembezoni, kwa sababu *TARURA* wanasema siyo barabara zao, halmashauri mapato hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kule Mundindi, kupeleka mtoto akipata dharura inakuwa changamoto. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanyie kazi na hili kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kupewa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, huyu ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge kwa michango mizuri. *(Makofi)*

Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wenu kwa kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais na kuyatekeleza kwa ubunifu na kwa weledi mkubwa sana. Hongereni sana! *(Makofi)*

Wizara hii sasa hivi imepata watu makini sana, ile migogoro ya kizamani zamani siku hizi hakuna tena. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.22 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 13 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*